

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Thelathini na Nne – Tarehe 25 Mei, 2017**

*(Bunge Lillianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae. Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI (K.n.y. MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE - MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII):**

Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MHE. SALMA M. MWASSA (K.n.y. MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MWENYEKITI:** Katibu, tuendelee.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 273

**Kuwawezesha Wajasiriamali kupata Mikopo**

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA** aliuliza:-

Wananchi wengi wajasiriamali huwa hawapati mikopo katika taasisi za fedha kwa sababu hawana uzoefu na ujuzi wa kutayarisha andiko la uchanganuzi wa miradi ya kibiashara, pia hawana mali ya kuwawezesha kuweka dhamana.

(a) Je, ni lini Serikali itaweka mpango madhubuti unaotekelezeka ili wananchi hao waweze kukopesheka?

(b) Je, Serikali haioni muda umefika sasa kuzitaka taasisi za fedha kupunguza masharti ya ukopeshaji ili wajasiriamali waweze kupanua miradi yao na kuwapatia ajira watu wengine?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mbunge wa Mtambwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inawawezesha wananchi ili waweze kukopesheka kupitia Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 na Sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Na. 6 ya mwaka 2004. Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imeainisha nia ya Serikali ya kuweka mazingira mazuri ya upatikanaji wa mitaji kwa kuboresha vyanzo vya akiba na kuchukua hatua za kuondoa vikwazo mbalimbali ili kuwezesha mablenki kukopesha kikamilifu amana zilizopo na kwa gharama nafuu kupitia vikundi vidogo vidogo na pia *SACCOS* na *VICOBA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na sera hii, mipango, miradi na mifuko kadhaa imeanzishwa na Serikali ili kuwezesha wananchi kukopa kwa urahisi. Aidha, Serikali inaendelea kusimamia mipango na mifuko ya uwezeshaji nchini na wananchi wengi wanaendelea kunufaika na mikopo inayotolewa ambayo ina masharti nafuu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wetu wa mablenki na taasisi za fedha kwa sasa unaendeshwa kwa utaratibu wa ushindani, hivyo viwango vya riba pamoja na masharti mengine huwekwa na taasisi husika ili kuhakikisha marejesho. Jukumu la Serikali ni kuweka mazingira mazuri kwa vyombo hivyo kuweza kutoa huduma kwa wananchi.

Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania kulingana na mazingira inaendelea kuangalia viwango vya riba kwa mablenki na taasisi za fedha ili ziweze kumudu kupata fedha kwa ajili ya kukopesha wajasiriamali kwa riba ndogo. Mfano, ni hatua ambayo imechukuliwa na Benki Kuu hivi karibuni ya kupunguza kiwango cha riba kwa mikopo yake kutoka 16% mpaka 12%.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa swali la nyongeza.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini msingi wa swali langu katika *introduction* nilikuwa nazungumzia wajasiriamali kuwa hawapati fursa hii ya kukopeshwa au kuweza kujua fursa kwa sababu hawana utaalamu na uzoefu wa kuandika andiko la miradi.

Sasa nataka kufahamu ni lini hasa Serikali itatoa maelekezo na utaalamu wa kuweza kuwafanya wale wenye nia na hamu ya kupata fursa hii kuweza kuitumia vilivyo na kwa kupata taaluma?

Pili, ni kweli kwamba kuna vikundi vingi tu ambavyo vinasaidia ama kwa kujichanganya katika *SACCOS* hizi au *VICOBA*, lakini kuna wajasiriamali mmoja mmoja ambao wangependa kutumia fursa hii ya kupata michanganuo na kuweza kupata fursa ya kukopa, lakini pia hawajawezeshwa, wala ile fursa ambayo ipo kiuchumi hawajaweza kuitumia vizuri, kwa sababu ile taaluma bado haijawafikia. Kwa hiyo, ni lini Serikali italeta taaluma hii ili watu wenye hamu na ari ya kuweza kutaka kujikwamua kiuchumi katika maisha yao, waweze kuipata fursa hiyo? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali la kwanza kwamba Serikali itatoa lini maelekezo ili wajasiriamali wengi waweze kupata elimu hii na wafahamu fursa zilizopo. Kwa taarifa tu ambayo napenda kumpatia Mheshimiwa Mbunge hapa ni kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu ndani yake lipo Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambao kazi yao kubwa kabisa ni kutoa elimu lakini vile vile kuwaandaa Watanzania kushiriki katika uchumi wa nchi yao kwa kuwatangazia fursa mbalimbali zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia, tayari tuna ma-*desk* katika kila Halmashauri kwa nchi nzima ambapo kuna Kamati ya Uwezeshaji ambapo wao sasa wanasaidia katika kuwapa wananchi elimu, lakini vilevile wananchi

wanapata fursa ya kufahamu fursa zilizopo za kiuchumi. Kwa hiyo, kupitia hiyo, ni rahisi wananchi wengi zaidi kuweza kupata elimu na kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuongezea tu, bado tumeendelea kufanya semina, makongamano na warsha mbalimbali za kuwafanya wananchi wetu wa Tanzania waelewe fursa zilizopo na watumie rasilimali zilizopo kwa ajili ya uchumi wa nchi yetu na tumefanya katika mikoa mingi na tumepata mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili la nyongeza, ameuliza kuhusu namna ambavyo Serikali inaweza ikawawezesha mjasiriamali mmoja mmoja naye akapata fursa ya kushiriki katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda nitoe taarifa katika Bunge lako Tukufu na ninyi Waheshimiwa Wabunge mnisikilize ili mwende mkawasaidie wananchi wenu, katika nchi yetu ya Tanzania tunayo mifuko 19 ya uwezeshaji ambayo inatoa ruzuku na mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mifuko hii ina ukwasi wa kiasi cha shilingi trilioni 1.3 ambayo ni fursa ya kipekee kwa sisi Waheshimiwa Wabunge kwenda kuwaelimisha wananchi wetu kuzitumia fursa hizi badala ya kutegemea Mifuko ya Maendeleo ya Vijana au Mifuko ya Maendeleo ya Akina Mama na mifuko mingine, lakini bado ziko fursa nyingi sana. Kuna watu wanaitwa *TFF (Tanzania Forest Fund)* ambao wenyewe wanatoa ruzuku kuanzia shilingi milioni tano mpaka shilingi milioni 50 katika vikundi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge wengine wote, naomba tuichukue hii kama fursa ya kwenda kuwaelimisha wananchi wetu watumie fursa hii kujinufaisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Mheshimiwa Shally Raymond, atafuatiliwa na Mheshimiwa Selasini.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Swali langu linahusu umbali wa wananchi hawa na benki zao. Kwa kuwa benki hizo zina nia nzuri ya kuwakopesha, lakini tatizo ni wananchi wanakoishi ni mbali na zile benki, kwa sababu benki nyingi zimefunguliwa mijini na nyingi zinafanya kibiashara zaidi.

Ni lini sasa Serikali itawasiliana na hizi benki zifungue matawi yao kule vijijini zikiwemo kule Mamba Miamba kule Same na kwingineko?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa tunashukuru sana kwa *concern* yake ya kuona kwamba wananchi wengi wanahitaji huduma hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kama Serikali hatua ambazo zinaanza kuchukuliwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba mablenki haya ya biashara yanakwenda kutafuta wateja maeneo ya pembezoni ili sasa watu wengi zaidi wapate fursa ya kuweza kupata huduma hizi za kifedha.

Kwa hiyo, naamini kabisa katika mipango ile ya Serikali ambayo mojawapo kubwa lililofanyika mwaka 2015 ni kuhakikisha kwamba fedha ambayo ilikuwa ni ya Mashirika ya Umma ambayo mablenki mengi walikuwa wanaitegemea, ilirudi Benki Kuu sasa ili mablenki waende kuwatafuta wateja wengi zaidi. Kwa kufanya hivyo pia itasaidia sana mablenki haya kwenda katika maeneo ya pembezoni ili kuwahudumia wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inalichukua hilo na kazi inaendelea kufanyika, kuhakikisha kwamba wananchi wengi wanapata huduma hii ya kifedha.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Katika jambo ambalo wanafunzi wetu wanahimizwa sasa hivi ni kuondokana na dhana kwamba elimu yao ni kwa ajili ya kujipatia ajira rasmi Serikalini na hivyo waingie katika mtazamo kwamba elimu itawasaidia kujijiri wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muktadha huo, benki ni chombo muhimu sana cha kuwasaidia vijana wetu wanapomaliza shule kuweza kukopa ili kufanya mambo mbalimbali kwa ajili ya kujijiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jambo linalowakwamisha ni dhamana. Vijana wetu wanaambiwa wapeleke hati za mashamba, majumba na vyombo visivyohamishika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itaiagiza Benki Kuu iweze kurekebisha sheria zake ili kuwasaidia vijana hawa wanaomaliza vyo viko waweze hata kutumia vyeti vyao kama dhamana kwa ajili ya kukopa ili waweze kupata fedha kwa ajili ya kuanzisha miradi mbalimbali ya kuwasaidia katika maisha yao? *(Makoff)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi. Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana. La kwanza, ni muhimu sana kutambua kwamba benki zetu zinafanya biashara. Ni lazima benki hizi zipate faida kama mfanyabiashara yeyote ili shughuli za benki hizi ziweze kuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba vijana wetu walioko shuleni wanakwamishwa na baadhi ya masharti ya mabanki yetu ikiwemo hili la dhamana ambalo Mheshimiwa Selasini anasema, lakini tumeanza kupiga hatua kuelekea huko ambako tunataka kwenda. Mathalani, vijana

walioko Igunga walipomaliza masomo yao Chuo Kikuu cha Sokoine, kitu cha kwanza walijiunga pamoja wakaunda kikundi wakakiandikisha na wakaanza shughuli yao katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya *CRDB* ni moja ya benki ambayo ilijitokeza na kuwakopesha kufanya shughuli zao. Kwa hiyo, pole pole tunakwenda kuangalia, ni vyombo gani ambavyo vinaweza vikatumika kama dhamana kulinda mabanki yetu yasipate hasara, lakini wakati huo huo kuwawezesha vijana wetu waweze kupata mikopo. Kwa hiyo, hilo ni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni muhimu sana niendeleo kusisitiza kwamba vyombo hivi sisi wenyewe tunao mchango. Mara nyingi baadhi ya wakopaji wanakuwa na historia mbaya, hawalipi. Sasa wasipolipa maana yake ni kwamba zile benki nazo zitapata hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu nao wakopaji wakalinda ile *credibility* yao, ndio, maana tulianzisha *Credit Reference Bureau* kuhakikisha kwamba wakopaji wanakuwa na historia ya ukopaji. Wale ambao wana rekodi nzuri vyombo vyetu vya fedha viko tayari kuwakopesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko benki ambazo sasa hivi zimeanza hata kutoa mikopo kwa watu wasio na dhamana. Zipo benki ambazo zinakopesha kwa mfano vikundi vya akina mama, ikiwemo *CRDB* na *NMB*, vikundi vya walemavu, bila dhamana lakini sharti ni kwamba kiwepo kile kikundi *credible* kimeandikishwa ili fedha zinazokopeshwa zisipotee. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Sasa namkaribisha Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi aweze kuuliza swali lake.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na kwa masikitiko makubwa sana naomba



Serikali inijibu swali langu namba 274 la mwananchi ambaye ameondoka jana kwenda kwenye matibabu nje ya nchi.

Na. 274

**Deni la Ujenzi wa Vituo vya Polisi Vilivyojengwa  
na Kampuni Al Batna**

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB** aliuliza:-

Kuna mjenzi aliyejenga Vituo vya Polisi kupitia Kampuni itwayo *Al Batna Building Co. Ltd.* Vituo alivyojenga ni Kituo cha Polisi Mkokotoni - Unguja na Kituo cha Polisi cha Madungu kilichoko Chakechake Pemba kwa gharama ya shilingi 223,440,000.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kulipa deni hilo tangu 2012 hadi leo hii?

(b) Je, Serikali inayo taarifa kwamba mwenye kampuni hiyo aliyejenga vituo hivyo amepata maradhi makubwa huku akihangaika kufuatilia haki yake hiyo bila mafanikio?

(c) Je, ni lini Serikali itamtembelea na kumpa pole kwa maradhi hayo mabaya yaliyompata?

**MWNEYEKI:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashimu Ayoub, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandarasi aliyejenga Kituo cha Polisi Mkokotoni kupitia Kampuni ya *Al Batna Building Co. Ltd.* alishalipwa shilingi za Kitanzania 560,000,000 na anadai shilingi za Kitanzania 525,000,000 ili kumalizia ujenzi katika kituo hicho. Deni hilo limehakikiwa na Mkaguzi Mkuu

wa Ndani na atalipwa mara fedha zitakapokuwa zimetolewa.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Serikali nitoe pole kwa mkandarasi wetu kwa maradhi yaliyompata na nimhakikishie kuwa deni lake atalipwa na Serikali iliamua kusitisha malipo kwa Wazabuni wote katika kipindi fulani kwa ajili ya kufanya uhakiki ili kuepuka kulipa madeni mara mbili.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, tutamtembelea kumpa pole baada ya kumalizika kwa Mkutano huu wa Bunge lako Tukufu kwa kadri ya upatikanaji wa nafasi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimwa Waziri wa Mambo ya Ndani. Mheshimiwa Jaku swali la nyongeza kama unalo.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa umakini wake, ufuatiliaji wake na utendaji wake na hasa kwa wapiga kura wake vilevile Jimboni kwake ingawa majukumu ni mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza kwa kukiri na hii ni mara ya pili kukiri, katika wakati wa bajeti na leo hii. Nafikira baada ya kupitisha bajeti yake ataniambia labda kesho au kesho kutwa tufuatane. Naomba kumwuliza maswali mawili madogo sana ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, zabuni zinafunguliwa na Serikali, izeje leo hii uhakiki ufanyike wakati mradi umeshafanyika na kukamilika karibu miaka mitano? *That is (a).*

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mhusika amemaliza kazi, kwa nini Serikali isimlpe fedha yake na uhakiki huo ufanyike kwa watendaji waliosimamia *tender* hizo ili kuwawajibisha? Hii ni sawa sawa na kumchukua kuku aliyechinjwa kisha akaliwa, ushahidi huwezi kuupata. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Jaku kwa kufuatilia masuala yanayohusu wananchi wake. Hili siyo jambo moja ambalo Mheshimiwa Jaku amefanya hivyo, nawaomba na Wabunge wengine tuige mwenendo wake. Panapotokea jambo linalohusu wapiga kura wake, Mheshimiwa Jaku huwa anafuatilia Ofisini, Wizarani na hapa Bungeni. Nampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba suala la uhakiki ni utaratibu ambao tulijiwekea Serikalini kwa ajili ya; moja, kuwa na uhakika wa madeni ambayo yanatakiwa kulipwa; pili, kuweka kumbukumbu sawa ili kuondokana na ulipaji wa madeni mara mbili. Hii ina faida pia hata kwa anayedai kuweza kuhakikisha kwamba haki yake haipotei. Kwa maana hiyo, kwa sababu ni utaratibu ambao una-*cut across* kwa wazabuni wote kwa madeni yote ya Serikali na *suppliers* wengine wote, ni lazima na sisi kama Wizara, ni lazima tufuate taratibu hizo kwa wazabuni wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa taratibu hizo zilishafanyika kama nilivyokwambia, sasa hivi ni suala tu la upatikanaji wa fedha. Sehemu kubwa ilikuwa ni kukubalika kwa deni hilo, kukubalika kwa kazi ambavyo hivyo vyote vimeshafanyika na tunampongeza kwamba amefanya kazi nzuri.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Rhoda Kunchela atafuatiwa na Mheshimiwa Mwakasaka na Mheshimiwa Flatei.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kumekuwa na upungufu wa vituo vya polisi nchini. Pamoja na changamoto hizo, lakini polisi hao wamekuwa na changamoto za kukosa magari na mafuta kwa ajili ya kulinda wananchi wetu kwenye maeneo yetu. Vilevile hivi karibuni polisi wamekuwa wakilalamika kwamba

magari hayana mafuta, kwa hiyo, wanashindwa kufanya doria kuzunguka kwenye maeneo korofi kwa ajili ya kuwalinda wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha sasa polisi hao wanapatiwa mafuta, lakini pia kuongezewa magari kwa ajili ya usalama wa Watanzania? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ingawa halihusiani sana na vituo vya polisi, tuendelee.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia jambo la sskari wetu. Niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba katika bajeti hii tuliyoupitisha, fedha zilizotengwa kwa ajili ya mafuta, doria pamoja na shughuli nyingine imeongezeka tofauti na iliyokuwa inatoka katika Awamu ya Kwanza ya mwaka wa fedha uliopita. Kwa maana hiyo, tutakuwa tumepunguza kwa kiwango kikubwa ukosefu wa mafuta katika shughuli zetu hizo za doria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016 tulipokea magari 77 kwa ajili ya askari wetu na kati ya mwezi huu mpaka mwezi wa saba tunatarajia kupokea magari mengine zaidi ya 200 na tutayagawa katika maeneo ambayo yana uhitaji mkubwa wa magari kwa ajili ya shughuli za doria ikiwemo Mikoa kama ya Kagera, Kigoma, Katavi pamoja na maeneo mengine ambayo yanahitaji doria na yanahitaji magari yawepo katika maeneo yale ikiwemo kwa ndugu yangu Mheshimiwa Nsanzugwanko na Mheshimiwa Bilago.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakasaka.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Tatizo la kutolipa wakandarasi au wazabuni katika sehemu mbalimbali za nchi hasa wale ambao wanatoa huduma kwenye vituo vya polisi limekuwa ni kubwa kwa

muda mrefu. Kwa mfano, mkoani Tabora kuna wazabuni wengi ambao wanaidai polisi malimbikizo ya muda mrefu ya huduma wanazotoa na hasa utengenezaji wa magari.

Kwa mfano Tabora yapo malalamiko ya muda mrefu ya mzabuni ambaye anatengeneza magari ya polisi hajalipwa sasa hivi ni zaidi ya miaka mitatu, anadai zaidi ya shilingi milioni 222. Sijui Mheshimiwa Waziri anazo taarifa hizi na kama hana, atasaidiaje mkandarasi huyu ambaye ndiye anatengeneza magari ya polisi pale Tabora Mjini alipwe fedha zake?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazo taarifa anazosisemea Mheshimiwa Mbunge. Nakumbuka nilivyotembelea Mkoa wa Tabora nililetewa jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu kwenye swali la msingi, ni utaratibu wa Serikali tulioweka wa kuhakiki kwanza madeni yote. Baada ya kuwa tumeshafanya uhakiki, yale madeni ambayo yamehakikiwa ndiyo yanalipwa kukiwa na kumbukumbu sawa za kazi iliyofanyika na fedha zinazodaiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, kwa jambo hili ulilolileta Mheshimiwa Mbunge, mhakikishie mtoa huduma huyo kwamba baada ya uhakiki huo ambao ulishafanyika nitawaelekeza watu wangu waweke kipaumbele katika kulipa madeni hayo ili kutokuwakwamisha wazabuni wetu kuweza kuendelea na shughuli zao na kutoa huduma hizo ambazo wametoa hata huko kwetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali ilitoa ahadi ya kujenga Kituo cha Polisi katika bonde la Yaeda Chini na muda umepita sasa na wananchi wanaibiwa mifugo na kutokea mauaji katika lile bonde.

Je, ni lini sasa Serikali itatekeleza ahadi ya kutengeneza Kituo cha Polisi ya Yaeda Chini? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Flatei jambo hili amelileta mara nyingi sana nami nampongeza kwa hamasa ambayo ameifanya Jimboni kwake kuhusu masuala haya ya ulinzi na usalama. Nilimhakikishia kwamba baada ya Bunge hili la Bajeti kuisha nitazungukia maeneo hayo ambayo kuna uhalifu umekuwa ukijitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuahidi kwamba punde tutakapoanza utaratibu wa ujenzi wa vituo hivyo, eneo lake ni moja ya eneo la kipaumbele kufuatana na uhalifu ambao umekuwa ukijitokeza katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye jibu nililojibu la masuala ya magari, Mheshimiwa Flatei pamoja na ndugu yake (pacha yake) Mheshimiwa Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, alikuja jana tu kusemea mambo ya aina hiyo yakihusisha pia na mambo ya magari.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Flatei pamoja na Mheshimiwa Issaay, niwahakikishie kwamba tutawapa kipaumbele kwenye vituo pamoja na upatikanaji wa magari kufuatana na jioografia ya Majimbo yao na Wilaya yao.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, Mbunge wa Ilege aulize swali lake.

Na. 275

## **Ujenzi wa Viwanda Vidogo na Vya Kati – Ileje**

**MHE. JANET Z. MBENE** aliuliza:-

Wilaya ya Ileje ni kati ya Wilaya zinazozalisha sana mazao mbalimbali ya nafaka, pia ina fursa nyingi sana za kilimo cha *cocoa*, *vanilla*, tangawizi, iliki na pilipili manga lakini hakuna viwanda vidogo na vya kati ili kuongeza thamani ya mazao hayo.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha viwanda vidogo hivyo ili kuongeza ajira kwa wananchi na pia mapato ya Serikali?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, Mbunge wa Ileje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza mkakati wa ujenzi wa viwanda, Mamlaka za Mikoa na Wilaya zimeelekezwa kutenga maeneo mahsusi kwa ajili ya kujenga viwanda vidogo, vya kati na vikubwa. Pia katika maeneo hayo, Mamlaka za Wilaya zinapaswa kutenga sehemu za hifadhi ya mazao au bidhaa na sehemu za masoko pale inapohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri za Wilaya pamoja na kutenga maeneo, zimehimizwa katika mipango yao ya maendeleo kuhusisha ujenzi wa miundombinu wezeshi na miundombinu saidizi katika maeneo hayo ya ujenzi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa nilizonazo ni kwamba Halmashauri ya Ileje imetenga mita za mraba 9,832 sawa na hekta 0.98 katika eneo la Itumba na mita za mraba 43,615

sawa na hekta 4.36 katika eneo la Isongole ambazo ni kidogo sana. Pia tathmini ya Wilaya moja, bidhaa moja (*ODOP*), ilionesha Ijeje inaweza kufanya vizuri zaidi katika zao la alizeti. Tathmini hiyo hiyo inaonesha Ijeje haijafikia kiwango cha kuzalisha *cocoa, vanilla*, tangawizi, iliiki na pilipili manga kwa kiasi cha kukidhi mahitaji ya viwanda vya kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wilaya ya Ijeje iko katika Mkoa mpya wa Songwe ambao kwa sasa hauna Meneja wa *SIDO*, Wizara imemwagiza Meneja wa *SIDO* Mbeya awasiliane na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ijeje ili watathmini fursa zilizopo na kusaidiana nao katika kuandaa mpango mkakati wa ujenzi wa viwanda vidogo ikiwa ni pamoja na mipango ya uzalishaji wa malighafi ya kutosha.

Aidha, Wizara inakamilisha mwongozo utakaotumika katika Mikoa na Wilaya katika kutenga maeneo, kuyaendeleza na kuhamasisha uwekezaji.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Janet Mbene, swali la nyongeza.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa jibu la Mheshimiwa Waziri lakini halijanipa faraja hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ijeje ina fursa nyingi, kuwa mazao mengine sasa hivi hayajajitosheleza, ni kwasababu hakuna masoko, lakini fursa zipo. Sasa hivi hayo maeneo tuliyotenga, nilimuita Meneja wa *SIDO* Mbeya, alikuwa hajawahi kufika Ijeje hata siku moja. Amekuja pale akatuambia tengeni eneo, hakutupa viwango, tutenge eneo kiasi gani? Hakutupa maelekezo yoyote. Miaka miwili imepita, wala hajarudi tena kuangalia kitu gani kinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna fursa kubwa sana ya viwanda vidogo vya usindikaji wa nafaka. Tunalima mahindi mengi, karanga nyingi na ulezi mwingi. Hivyo ni vitu ambavyo tunaweza kuanzia kwa sasa.



Mheshimiwa Mwenyekiti, mnaposema sisi tutayarisha miundombinu yote wezeshi, kwa uwezo gani wa Halmashauri zetu masikini watu wa pembezoni kama sisi? Nini maana ya ile Sera ya Kuendeleza Viwanda ya 1996 mpaka 2020 inayosema mtapeleka viwanda nchi nzima na mtakwenda mpaka maeneo ya pembezoni? Sisi ndio watu wenyewe wa pembezoni, mnakuja lini kutusaidia kuweka viwanda? Msituachie huo mzigo wa kutengeneza miundombinu, hatuna uwezo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, lini Mawaziri watakuja Ileje? Naomba Mheshimiwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo waje Ileje. Mkija mkajionea wenyewe hali halisi ndiyo mtajua majibu ya kutupa humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

**WAZIRI WA VIWANDA BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa na ninaweza kusikia uchungu alionao Mheshimiwa Mbunge kuhusu Wilaya yake na hasa kuhusu maeneo ya pembezoni. Nianze na lile swali ambalo ni rahisi. Nimeshapata mwaliko kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Katavi na Rukwa. Tarehe 6 Agosti, nitakwenda kutembelea mikoa hiyo tukiwa pamoja na shughuli za Nane Nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sera ya Viwanda *(Sustainable Industrial Development Strategy)* ya mwaka 1991 – 2020 katika jibu langu nimeeleza, tumegundua mwendo usio sawa katika viwanda vinavyoenea Wilayani. Kutokana na hiyo na kwenye jibu langu nimeeleza na kwenye bajeti yangu nimeeleza, ndiyo maana tunatengeneza mwongozo. Huo mwongozo utaweza kuwasukuma Watendaji wetu wafuate kama mwongozo unavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge, nikuhakikishie nitafanya kazi na wewe na kuhusu suala la tangawizi tuanze shughuli hapa. Nenda kamfuate Mheshimiwa Mama Kilango akueleze alifanyaje kufufua Kiwanda cha Tangawizi na amepata wapi zile pesa shilingi bilioni 1.7 za kuendesha kiwanda cha Same? Akuelekeze, tuanzie hapo. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Hawa Ghasia atafuatiwa na Mheshimiwa Goodluck Mlinga, Mheshimiwa Issaay na Mheshimiwa Mwijage.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuuliza swali moja la nyongeza kwa Mheshimiwa Mwijage. Mkoa wa Mtwara na hasa Manispaa ya Mtwara na Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara tayari tumeshatengeneza *Master Plan* na tumeshatenga maeneo kwa ajili ya viwanda. Tunayo *EPZA*, lakini tunayo maeneo ambayo hayahitaji fidia wala nini. Wizara yake inasaidiaje huo mkoa kuhakikisha kwamba na wenyewe unakuwa wa viwanda kwa sababu fursa zote zipo? Gesi, bandari, mazao kama korosho yapo. Je, Wizara yake ina mkakati gani wa kusaidia Mkoa wa Mtwara? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA VIWANDA BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo. Nina taarifa kwamba tarehe 2 Mei, 2017 *Master Plan* ya Mtwara ilikamilika. Kilichobaki au jukumu nililionalo na Wizara yangu ni kuendelea na jitihada za uhamasishaji. Nimeshaanza uhamasishaji Mheshimiwa Mbunge, juhudi zako za kunipa kwanja cha bure kwa ajili ya kujenga Kiwanda cha *Sulphur* siyo kwamba nimenyamaza, tunapambana kuweza kuwaleta hao wawekezaji. Niseme kilichobaki ni uhamasishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtwara naendelea kuhamasisha, iko kwenye ramani yangu, ni eneo ambalo liko tayari kwa ajili ya uwekezaji. Wawekezaji watakuja Mtwara.

**MWENYEKI:** Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wapogoro tunajulikana dunia nzima kuwa chakula chetu kikubwa ni wali na kambale, kwa kuwa Ulanga tunalima sana mpunga.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kujenga kiwanda ili sasa wakulima wasiuze mpunga wauze mchele ili kuwaongezea kipato? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA VIWANDA BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya kukoboa mpunga ni viwanda vidogo na viwanda vya kati. Ni viwanda vyenye thamani kati ya shilingi milioni tano mpaka shilingi milioni 200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakachofanya kwa ajili ya wajomba zangu, ni kuwahamasisha wananchi. Matajiri wa shilingi milioni 200 tunao, badala ya kuwekeza kwenye malori, ni kununua *dryer*. Nitoe taarifa, kwa nini mchele wetu wa Tanzania unakataliwa nje? Ni kwamba tunashindwa ku-*control moisture content*. Nimeshamweleza hata rafiki yangu pale Mheshimiwa anayependa kula sana pepeta, nimeshamweleza kwamba *control moisture content*. Kwa hiyo, *moisture content* inauzwa dola 50,000, kinu kinauzwa dola 100,000. Tunaweza kufanya hivyo.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nitasaidiana na wewe na tulishafika pazuri, sitaki kukurudisha kwenye historia; tutaweza kuhamasishana. Hivi viwanda vya shilingi milioni 200, shilingi milioni 300 au shilingi bilioni moja, msitafute wageni, tunavimudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango amezungumza hapa, ziko benki, tunavimudu na tutawasimamia. Ndio nyie wenye kuwekeza. Wale wengine watakuja baadaye, lakini watu wa kuwekeza ni sisi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Mboni, atafuatiwa na Mheshimiwa Aida.

**MHE. MBONI M. MHITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri swali la nyongeza.

Katika bajeti iliyopita Mheshimiwa Waziri alituahidi wananchi wa Jimbo la Handeni Vijijini kuweza kupata Kiwanda cha Matunda katika Kata ya Kwamsisi na mpaka hivi leo bado wananchi wa Jimbo la Handeni Vijijini wana matumaini makubwa na hakuna ambalo limefanyika. *(Makofi)*

Je, Mheshimiwa Waziri mko katika hatua gani ili kuweza kuwawezesha wananchi wa Jimbo la Handeni Vijijini kupata kile kiwanda ambacho mlituahidi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA VIWANDA BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo, Mradi wa Kiwanda cha Matunda Handeni bado upo. Mwekezaji ambaye anawekeza kiwanda, anayelima Bwana Roy Nightingale ameshaanza kuzalisha ndizi kwa ajili ya kiwanda hicho. Sasa ndizi zake zinauzwa kwenye Kiwanda cha Elven.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisamehe kitu kimoja, niwaelezee kiwanda cha *Elven*. Kiko kiwanda kinakausha matunda na matunda hayo yanauzwa Ulaya, kiko sehemu ya Bagamoyo juzi nimekikagua pamoja na Mkuu wangu wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania mpaka ninapozungumza hatuwezi kutosheleza kiwanda hicho kwa matunda. Kwa hiyo, wakati matunda yenu mtayauza Bagamoyo, Kiwanda chenu cha Nightingale, mwekezaji binafsi kinaendelea. Ni matatizo ya kifedha lakini nitaendelea kusimamia na wewe tushirikiane, kiwanda hicho ningependa kuona kinajengwa na kufanya kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwijage, halafu Mheshimiwa Aida. Naona mko *interested* na viwanda, kwa hiyo, maswali yanayofuata hayatakuwa na maswali mengi ya nyongeza.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa Mkoa wa Kagera una ardhi kubwa ambayo inatumika hata kwa kuingiza wafugaji haramu na majambazi na kwa kuwa wewe Mheshimiwa Waziri ni mzaliwa wa Mkoa wa Kagera.

Ni lini utaiona Kagera kuweka viwanda angalau vya kuchakata kahawa, majani na vyakula mbalimbali ili tukajivunia kwamba tumekuwa na Waziri wa Viwanda na Masoko? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi kabisa.

**WAZIRI WA VIWANDA BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unitendee haki. Naulizwa mara ya pili swali hili. Mimi ni muumini wa Muammar Gaddafi, alianza kujenga mbali na kwao, akamalizia kwao.

Kuhusu Kagera, *mapping* ya viwanda Kagera, naomba nitoe jibu. Kagera ina fursa ya kujenga viwanda vya maziwa. Kinachofanyika sasa, tunatafuta mwekezaji wa kuweka Kiwanda cha Maziwa ili sasa soko lije livute uzalishaji. Tulikuwa na ufugaji wa ng'ombe, hatukufanya vizuri, sasa tunatafuta wawekezaji waweke viwanda vikubwa vya maziwa, ni rahisi kwa uoto wa Kagera kuweza kufuga ng'ombe wa maziwa, mkapata maziwa na *by product*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikueleze, wapo vijana wajasiriamali na tumeshawaelekeza mahali pa kwenda kusudi waweze kujasiria. Shangazi usiwe na wasiwasi siwezi kuwa ngariba wa Kilwa. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Natumaini hawakuulizi tena swali hilo jinsi ulivyojibu kwa

msisitizo. Tunaendelea na Mheshimiwa Aida atafuatia Mheshimiwa Issaay na tunamalizia na Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mkoa wa Rukwa tunalima sana mazao ya chakula na sasa ni msimu wa mavuno... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naomba Waheshimiwa tumpe fursa aulize swali la nyongeza. Naona mmelifurahia. Naomba aulize swali la nyongeza tafadhali.

**MBUNGE FULANI:** *Order, order, order! Order please! Order!*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa mnapoteza muda. Mheshimiwa Aida endelea tafadhali. Nasema Mheshimiwa Aida uliza swali.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mkoa wa Rukwa tunalima sana mazao ya chakula na sasa ni msimu wa mavuno, lakini wananchi wa Mkoa wa Rukwa mpaka sasa hawajapata soko la uhakika la kuuza mazao yao wala kiwanda hakipo. Ni lini kiwanda kikubwa kitajengwa Mkoa wa Rukwa ili kiwanufaishe wakulima hao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi kabisa.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili swali limejirudia. Viwanda anavyovizungumza, Viwanda vya Asali, vya Ulezi, vya Mahindi ni viwanda vidogo, vya kati na viwanda vikubwa. Kiwanda alichokijenga Mheshimiwa Aeshi chenye thamani ya dola milioni za Kimarekani, ni kiwanda kikubwa.

Kwa hiyo, ninachokwambia, tuhamasishane sisi tujenge viwanda. Msitafute mtu kutoka nje aje achume sisi tumeshahangaika. Viwanda hivi vya shilingi milioni 400 au shilingi milioni 500 tunavimudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaeleze, itafika wakati tutaweza kulazimishana mtu asitoe mahindi Rukwa kuyapeleka Dar es Salaam, tengeneza *product*, *zi-brand*; *regional branding*. *Brand* unga wako kule upeleke mjini chakula, msipeleke ajira mjini. Ndivyo nilivyozungumza kwenye bajeti yangu na tukubaliane tuanze, hatujachelewa.

Mheshimiwa Aida, kiwanda kidogo cha shilingi milioni 500 unakimudu. Kama hujui fursa uliyonayo, njoo nikuelekeze namna ya kuzipata.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri inaonekana maswali kama yanajirejea. Naomba ungewajibu kwa ujumla ili wanufaike wote pamoja. Tuendeleo, tumalizie na Mheshimiwa Issaay na Mheshimiwa Dkt. Mary.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wilaya ya Mbulu ni miongoni mwa Wilaya kongwe hapa nchini. Wilaya hiyo kongwe huko mbele ilikuwa na kiwanda cha kutengeneza vigae vya kuezeka maghorofa na pia kulikuwa na kiwanda kilichokuwa kinamilikiwa cha kutengeneza chokaa na *gypsum powder*. Hivi sasa hivyo viwanda havifanyi kazi.

Je, ni lini Wizara itaenda Mbulu ili ikae na Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu na Halmashauri ya Vijijini waweze kufufua viwanda hivi ambayo vilianzishwa na wenzetu huko awali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Issaay, kuhusu vifaa vya madini ya ujenzi, kwa mamlaka niliyonayo namuagiza Mkurugenzi anayeshughulikia viwanda aandae safari ya wataalam kwenda kuangalia fursa zilizoko kule na awapeleke wawekezaji kule Mbulu kusudi mimi nikienda, niende kufungua na kuzindua kiwanda hicho.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mary na swali la mwisho litaulizwa na Mheshimiwa Bulembo.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Katika Wilaya ya Mbeya tumekuwa na viwanda vingi sana kama Kiwanda cha *Mbeya Textile, Hill Soap, Tanganyika Packers, Zana za Kilimo* na kadhalika na viwanda hivi ni vya muda mrefu sana vimekufa. Namuomba Mheshimiwa Waziri kwa kushirikiana na Msajili wa Hazina, anieleze ni lini na nini mkakati wa Serikali katika ufufuaji wa viwanda? Siyo ujenzi wa viwanda. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio. Natambua na kumbukumbu zinaonesha kwamba viwanda vingi vilivyopo Mbeya vilikufa na vilipokufa vilibinafsishwa na kupeleka miliki kwa watu wengine, watu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa ya awali kwamba *Treasury Registrar* kwa kushirikiana na Wizara za kisekta wanafuatilia ikihusisha uhamishaji wa miliki ambayo ni masuala ya kisheria kusudi waweze kuvirudisha hivyo viwanda kwenye wamiliki wapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwaeleze Waheshimiwa Wabunge, mtu aliyezuwa kitu kwa mkataba huwezi kumnyang'anya hivi hivi, labda tubadilishe matumzi ya sheria, siyo kitu rahisi.

Ningependa tuwanyang'anye mara moja, lakini siyo kitu rahisi. Tunachofanya zaidi pamoja na kuwanyang'anya, tunajaribu kuangalia namna gani rasilimali zile zinaweza kutumika kuzalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, kwa uelewa zaidi, someni *vision 2025* mjue kwa nini viwanda vilikufa? Vingine vilikufa kwa sababu pale vilipojengwa, havikustahili kujengwa.

**MWENYEKITI:** Subiri hapo hapo Mheshimiwa, tumalize na Mheshimiwa Bulembo.



**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Waziri kwa sababu nchi hii ina tatizo kubwa sana la sukari na katika Mkoa wa Kagera umesema tuanzishe viwanda vya maziwa, ukitoka pale Bulembo kwenda Busheregenyi, kwenda Msira kwenda Rugongo, kwenda sehemu za huko kama unaenda Kasharu; maeneo yale ni maeneo ya tingatinga kuweza kulima mashamba ya miwa na watu wajasiliamali wadogo wakaanzisha viwanda vidogo vidogo.

Ni lini unaenda Misenyi kukaa na wananchi? Ofisi yako ikawaambie kwa sababu uwezekano wa kupatikana miwa upo ili waweze kuanzisha viwanda vidogo vidogo? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namsukuru Mheshimiwa Bulembo. Hilo la kwenda Busheregenyi kwa bibi zangu halina mjadala, lakini napenda nikueleze kwamba ninaye mwekezaji sasa katika maeneo hayo ambaye anataka kuingia ubia na Jeshi la Magereza sehemu Kitengule, kushirikiana na Jeshi la Magereza kutumia uoto ule kuweza kulima miwa ya kuzalisha sukari. Kwa hiyo, tutalijadili mimi na pacha wangu, yule mwekezaji yupo *serious* anataka kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatafuta wawekezaji lakini Waheshimiwa Wabunge muelewe, mwekezaji humleti leo akaanza leo. Mkijua huo mchakato wa kuweza kuchukua ardhi mpaka kuzalisha, ndiyo maana nikaanzisha ule utafiti wa wepesi wa kufanya biashara. Ndiyo mambo ambayo tunayarekebisha na tutayarekebisha kusudi angalau wawekezaji wachukue muda kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala na Mheshimiwa Bulembo ni kwamba Busheregenyi mnaweza kupata huduma *Kagera Sugar* na mkapata huduma Magereza watakapokuwa wameanzisha kiwanda wale wawekezaji.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa kutuvumilia. Tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na hatutakuwa na maswali ya nyongeza.

Naomba sasa Mheshimiwa Lucy Simon Magereli, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 276

**Askari wa JWTZ Kutesa Raia**

**MHE. CECILIA D. PARESSO (K.n.y. MHE. LUCY S. MAGERELI)** aliuliza:-

Askari wa JWTZ wamekuwa wakijichukulia sheria mkononi kwa kutesa raia na saa nyingine Jeshi la Polisi. Matukio haya yamekuwa yakifanyika maeneo ya starehe, kwenye foleni za magari, mitaani na katika magari ya usafiri wa umma. Hivi karibuni Mkoani Tanga, kijana mmoja kondakta wa daladala alimzuia mtoto wa mwanajeshi kupanda daladala yake bila nauli, alikamatwa na kuteswa na wanajeshi ndani ya Kambi, kitu kilichopelekea kifo chake.

(a) Je, sheria ipi inawapa wanajeshi haki ya kutesa raia?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kukomesha hali hii?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Simon Magereli, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hakuna sheria yoyote inayowapa haki wanajeshi kutesa raia au kuvunja sheria.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio ya wanajeshi kushambulia raia au raia kushambulia wanajeshi mara nyingi yamekuwa yakijitokeza katika mazingira yanayohusisha kutofautiana kauli, ulevi, wivu wa kimapenzi na hata ujambazi. Hivyo katika kushughulikia hali hii, mara nyingi kesi hufunguliwa kwenye mahakama za kiraia na hukumu kutolewa kwa mujibu wa sheria zilizopo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hakuna mtu aliye juu ya sheria inashauriwa wanaokubwa na kadhia hii wapeleke mashtaka kwa mujibu wa taratibu zilizopo ili sheria ifuate mkondo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taratibu zilizopo za Jeshi letu la Ulinzi, afisa au askari anapopatijkana na hatia katika mahakama za kiraia na kuhukumiwa adhabu ya vifungo au nyinginezo, pia hupoteza sifa za kuendelea kulitumikia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. Aidha, maafisa na askari mara kwa mara wamekuwa wakiaswa kuishi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Magereli swali la nyongeza kama unalo.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi ni Mheshimiwa Paresso, kwa niaba ya Mheshimiwa Magereli.

**MWENYEKITI:** Haya, samahani, Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa ni ukweli kwamba hakuna aliye juu ya sheria lakini wakati mwingine wanajeshi wetu baadhi wamekuwa wakijiona kwamba wao ni *superior* kuliko watu wengine; je, Wizara ina mkakati gani wa kuendelea kutoa elimu ili wanajeshi hao wafuate sheria na kujenga mahusiano mazuri kati ya wananchi na jeshi?

Swali la pili, pia kumekuwa na mahusiano hafifu kati ya jeshi na wananchi hasa katika yale maeneo ambao yana migogoro ya ardhi. Je, Wizara sasa ipo tayari kuhakikisha migogoro hii inaisha kwa wakati ili mahusiano haya yaendelee kuimarika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa kutoa elimu upo. Wanajeshi mara zote wamekuwa wakikumbushwa kuishi vizuri na raia hususan wale wanaowazunguka katika makambi yao. Mara kwa mara zimekuwa zikichukuliwa hatua za kinidhamu ndani ya vikosi vyetu vya jeshi pale wanapokiuka utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tueleze vilevile kwamba sheria za nchi hii zinataka mtu anapohisi amevunjiwa haki yake, basi ana haki ya kwenda kushtaki. Kwa kuwa wanajeshi hawako juu ya sheria, sheria hufuata mkondo wake. Kwa hiyo, hilo lizingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mahusiano hafifu kwenye migogoro ya ardhi, hili napenda niliseme, kama tulivyoeleza wakati tunatoa bajeti yetu hapa, kwamba juhudi zote zinafanyika ili migogoro ya ardhi inayohusisha Kambi za Jeshi iweze kuisha. Yapo maeneo ambayo wananchi wamevamia maeneo ya jeshi, kwa hiyo, ni vizuri wananchi nao wakapewa elimu hiyo hiyo ili wasiweze kuvamia maeneo ya jeshi. Kwa yale maeneo ambayo jeshi imechukua haijalipa fidia, juhudi zinafanyika ili tuweze kulipa fidia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Jeshi la Ulinzi. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kuna swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza ambalo litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo mwenyewe.

**MWENYEKITI:** Yupo Mheshimiwa Rweikiza?

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Nipo.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Rweikiza tuendelee.  
(Kicheko/Makofi)

Na. 277

### **Kuzuia Uvuvi wa Samaki Wadogo – Ziwa Victoria**

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Serikali inazuia wavuvi kuvua samaki wadogo na hivyo nyavu zenye matundu madogo haziruhusiwi; katika Ziwa Victoria kuna samaki ambao kwa maumbile yao hawawezi kuwa wakubwa kama vile dagaa, furu na hata sato.

Je, Serikali haioni kuwa kwa kuzuia tu nyavu ndogo samaki hawa hawatavuliwa kamwe?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009 katika kulinda na kusimamia rasilimali za uvuvi ili ziwe endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha rasilimali za uvuvi zinavunwa katika njia endelevu bila ya kuathiri vizazi vyao, Serikali imepiga marufuku matumizi ya nyavu (*dagaa net*) zenye macho madogo chini ya milimita nane kwa uvuvi wa dagaa, badala yake nyavu zinazoruhusiwa kwa uvuvi wa dagaa ni kuanzia milimita nane hadi milimita 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa uvuvi wa sato na sangara, Serikali imekataza wavuvi kutumia nyavu za makila zenye ukubwa wa macho chini ya inchi sita ili kuvua samaki wakubwa tu. Aidha, samaki hao wanaweza kuvuliwa kwa kutumia mishiipi au nyavu za makila kuanzia inchi sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kuu la Serikali la kupiga marufuku matumizi ya nyavu zenye macho madogo ni kunusuru kizazi cha samaki kisipotee kwa kuepusha uvuvi wa samaki wachanga kwa manufaa ya kizazi kilichopo na kizazi kijacho. Hata hivyo, kulingana na sheria na kanuni hizo, samaki wa aina zote huvuliwa kwa kutumia nyavu zilizoruhusiwa kisheria na ndiyo maana samaki wa aina zote wanapatikana sokoni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rweikiza swali la nyongeza.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kuzuia uvuvi wa nyavu ambazo hazistahili, hazifai ni ni zuri na wavuvi hawa wanapokamatwa wanapata taabu sana, nyavu zinaharibiwa, wanakamatwa, wanawekwa ndani, na kadhalika, lakini hawa wavuvi hawajitengenezei nyavu hizi, wanazinunua madukani. Kwa nini wasikamatwe wale wanaozuza ili ziondolewe? (*Makofi*)

Swali la pili, kwa jinsi ninavyofahamu, Tanzania hakuna kiwanda cha nyavu, kama kipo hakifanyi kazi. Nyavu hizi zinatoka nje ya nchi, zinaagizwa nje ya nchi, zinaingia Tanzania na Wizara ipo. Kwa nini Wizara isizuie nyavu hizi ambazo haziruhusiwi zisiingie? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba siyo wavuvi pekee wanaolazimika kufuata Sheria ya Uvuvi kulingana aina ya nyavu wanayotakiwa watumie. Mtu yeyote yule ambaye anajihusisha na shughuli ambayo inapelekea kutumia nyavu ambazo hazitakiwi kutumika, anakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya mwaka 2003 na Kanuni zake 2009.

Kwa hiyo, mtengenezaji, msafirishaji, dalali, mtumiaji, mtu yeyote yule ambaye anaingia katika mfumo wa kuhakikisha kwamba nyavu hizo zinapatikana vilevile anakuwa ametenda kosa la kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge kwamba lengo la Serikali siyo kujaribu kuwabana na kuwaletea matatizo wavuvi, wao hasa ndio wanufaika wa kwanza na jitihada za Serikali za kulinda rasilimali za uvuvi kwa sababu tusipolinda, baadaye hawatakuwa na cha kuvua. Ndiyo maana tunasisitiza zitumike nyavu ambazo zitafanya uvuvi uwe endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pili, kwamba kwa nini tusizuie nyavu ambazo zinatoka nje, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tunazuia hata mwaka 2016 tulikamata nyavu pamoja na vifaa vingi ambavyo vilitoka China vilikamatwa bandarini na Serikali inaendelea kufuatilia mtu yeyote yule ambaye anaingiza nyavu ambazo haziruhusiwi.

Lakini vilevile lazima niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge changamoto iliyopo ni kwamba mara nyingine nyavu nyingine zinasokotwa kienyezi.

Kwa hiyo, watu wananunua nyuzi ambazo zinapatikana kwa ajili ya matumizi mengine halafu wanakwenda kutengeneza nyavu ambazo hazitakiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba tunadhibiti uingizwaji wa nyavu zile

lakini vile vile utumiaji wake katika maeneo mbalimbali nchini.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Kwa vile muda umebaki kidogo, nitatoa fursa kwa Mheshimiwa Mwakajoka na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali. Dhamira ya Serikali ya kuanzisha Benki ya Kilimo ilikuwa ni kuwainua wakulima nchini. Wakati Serikali inafikiria kuanzisha Benki ya Kilimo ilikubali kutoa mtaji wa shilingi bilioni 800, lakini fedha iliyotolewa ni shilingi bilioni 60 tu na benki hii imeshindwa kabisa kuwahudumia wakulima wa nchi hii.

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wakulima wanapata mikopo na wanalima kilimo chenye tija? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, hilo suala naona lipo nje kidogo kama utaweza kujibu, kama huwezi liache.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwakajoka, nafikiri limekaa sawa kwa sababu linaendena hasa na jitihada ya Serikali kujaribu kuwekeza na kuwasaidia wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba huko nyuma kulikuwa na jitihada kujaribu kuhakikisha kwamba Benki ya Maendeleo ya Kilimo inapata shilingi bilioni 800. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa benki hiyo imeweza kupata shilingi bilioni 246 tayari zimeshaingia benki na yote itaelekezwa katika kilimo ikiwa ni pamoja na kilimo cha mazao, uvuvi na ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge labda tukitoka hapa leo anione nimfahamishe taratibu za kuweza kupata hizo fedha kwa ajili ya wavuvi



wake. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba hizo fedha zimepatikana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mary, Mheshimiwa Hawa na Mheshimiwa aliyeko nyuma yake. Inaonekana hapa kuna wakulima wengi na wavuvi. Kwa hiyo, nitapunguza muda wa miongozo.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii. Naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Keissy kwamba Wilaya ya Hanang ina Ziwa Basutu na ina samaki wengi sana.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sikubali ni bwawa! (*Kicheko*)

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa hatuna polisi wa kutosha na ndiyo maana tunashindwa kudhibiti hawa wavuvi wanaotumia nyavu ndogo ndogo. Je, Serikali haioni kwamba itakuwa vizuri sana kuwahamasisha wananchi wa Tanzania kuanzisha mabwawa mengi ya kufugia samaki na wazungu wanaita *aqua culture* kama namna ya kuwafanya wavuvi wakawa na samaki wa kutosha na wakaacha kutumia nyavu ndogo ili waweze kuendelea kuishi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikiri kwamba Jimboni kwa Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu kuna uvuvi katika Ziwa Basutu ambao wananchi wake wanategemea sana na Serikali inatambua fika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nakubaliane naye kwamba kwa sasa jitihada kubwa duniani ni kuelekea kwenye uvuvi ambao tunaita ufugaji wa samaki (*aqua culture*) na tunatambua kwamba hata hapa kwetu, Serikali tayari imechukua jitihada za kutosha kuhahakisha kwamba

tuna-*diversify* sasa kutoka kwenye uvuvi wa kutumia maji kuelekea kwenye ufugaji wa samaki. Ndiyo maana kuna mikakati mbalimbali inaendelea. Kuna Waheshimiwa Wabunge wanafahamu kwamba sasa kuna ufugaji unaitwa ufugaji wa vizimba (*cage culture*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hata *aqua culture* sasa hivi Serikali inawezekeza katika ufugaji wa samaki kwa utaratibu wa *aqua culture* na tayari kuna vituo ambavyo vinazalisha vifaranga.

Kwa hiyo, kama kuna Mheshimiwa yeyote anataka kuwekeza au kusaidia wananchi wake wawekeze katika ufugaji wa samaki, awasiliane na mimi ili nimwelekeze pa kupata vifaranga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari kuna mradi mkubwa unaitwa *Sawfish* ambao unajaribu kuhahakisha kwamba tunaanchia nafasi, rasilimali zetu za uvuvi kwenye maji ya kawaida kwa kuweza kuwekeza kwenye ufugaji wa samaki kwenye nchi kavu. Kwa hiyo, tuna jitihada hizo ndani ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Naomba mwulize maswali kwa ufupi na Mheshimwia Naibu Waziri aweze kujibu kwa ufupi. Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante napenda kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inawapatia wakulima pembejeo kwa ajili ya kilimo na wafugaji hivyo hivyo. Kwa upande wa uvuvi Serikali mna mkakati gani wa kuhakikisha na wenyewe mnawawezesha badala ya kila siku kuchoma nyavu zao na kuacha wakiwa maskini? Mwisho, naipongeza timu yangu ya Yanga. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hilo la Yanga, sitalijibu, siyo sehemu ya swali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika ruzuku ya kilimo, wavuvi hawajasahauliwa. Wizara ina utaratibu ambapo inatoa ruzuku kwa wavuvi wanaotaka kununua injini za boti. Kwa hiyo, kama kuna Mheshimiwa Mbunge yeyote ambaye ana vikundi vyake vya wavuvi ambao wanataka kununua boti, Serikali inatoa ruzuku ya asilimia 40 kwa vikundi vinavyonunua injini za boti. Kwa hiyo, ruzuku ipo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaanza na Mheshimiwa hapa, halafu tutakuja huko. Mheshimiwa Maryam Msabaha na Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Wananchi wa Jimbo la Manyoni Magharibi ni wananchi ambao nao wanapenda kitoweo cha samaki. Kwa kuwa hatuna bwawa wala ziwa.

Je, Serikali iko tayari kushirikiana nami Mbunge wao na vikundi vya vijana na akina mama wa Itigi kuweza kuanzisha mabwawa ya samaki?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kusikia kwamba Mheshimiwa Mbunge anataka kuhamasisha vijana wake wa Jimbo la Manyoni Magharibi ili kuwekeza katika ufugaji wa samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimfahamishe tu kwamba Wizara iko tayari kushirikiana naye ili mradi afuate utaratibu ambao unatakiwa nao ni kwa kupitia Halmashauri ambayo yeye mwenyewe ni Diwani.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Maryam.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami naomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa vijana wengi wamekuwa wakijijiri kwa kupitia uvuvi wa bahari kuu, lakini vijana hawa hawana mitaji ya kuendeleza sekta hii ya uvuvi.

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha vijana hawa wanapatiwa angalau mikopo ya bei nafuu ili wapate kujiendeleza katika sekta hii ya uvuvi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi kabisa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vijana kufanya uvuvi katika bahari kuu, taarifa tulizonazo ni kwamba hakuna vijana wanaofanya uvuvi katika bahari kuu. Bahari kuu ni suala lingine, ni gumu kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na vijana wanaojishughulisha na uvuvi katika maji ya kawaida na maji ya Kitaifa tunafahamu. Zanzibar mradi wa *Sawfish* umetoa dola milioni 11 kwa ajili ya kuwezesha wananchi wajishughulishe na shughuli za uvuvi. Labda Mheshimiwa Mbunge tunaweza tukaonana tukitoka hapa leo nimhabarishe na nimpe taarifa vizuri zaidi ili aangalie namna ya kuwasaidia vijana wake wawekeze katika uvuvi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ndassa.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa Serikali imepiga marufuku...

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Ndassa ni mmoja tu humu ndani.

**MBUNGE FULANI:** Endelea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndassa, halafu Mheshimiwa Dau na Mheshimiwa huyo niliyemsahau, wa mwisho. Eeh, huyo! (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mtu amevaa Yanga humu, aone!

**MBUNGE FULANI:** Yanga oyee!

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kuna utaraibu mzuri wa kuzuia hizo nyavu zisizoruhusiwa, lakini samaki katika maziwa yetu; Ziwa Victoria kuna samaki aina ya sato, nembe, sangara na samaki wengine; lakini kuna utaratibu mzuri katika bahari yetu hasa uvunaji wa samaki aina ya kamba, kwamba wanavunwa baada ya muda fulani halafu wanasimama. Ili samaki hawa waweze kukua katika Ziwa Victoria; sato na samaki wengine; kwa nini sasa tusiwe na utaratibu wa kuzishirikisha nchi za Kenya, Uganda na Tanzania ili kusudi samaki hawa wawe na tija, badala ya kuvua samaki wadogo wadogo tuwe na muda wa kuwavuna? Ahsante.

**MBUNGE FULANI:** Yanga oyeeee!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Ndassa kwa sababu inaelekea ana ufahamu wa ndani kabisa kuhusiana na masuala ya uvuvi. Kimsingi Ziwa Victoria kabla ya miaka ya 1980 samaki aina ya nembe, furu na gogogo walianza kupotea, lakini siku hizi tayari wameshaanza kuonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la kusimamisha au kusitisha uvuvi katika Ziwa Victoria

majadiliano yanaendelea katika ukanda wetu wa Afrika Mashariki kuangalia kama hilo ni suala ambalo linaweza likafanyika. Kwa sababu kimsingi hata sisi Tanzania tukisimamisha leo wenyewe na wengine wakiwa wanaendelea, haitakuwa na faida kwa sababu samaki wale ni *migratory*. Ukifanya uamuzi katika nchi moja halafu wakaendelea kuvuliwa katika nchi nyingine, bado hautakuwa umepata nafuu yoyote. Kwa hiyo, majadiliano yanaendelea na utafiti vile vile unaendelea. Matokeo yakishatolewa, basi uamuzi sahihi utachukuliwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunamalizia na Mheshimiwa Dau na mwisho Mheshimiwa Gekul.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Umenisahau.

**MWENYEKITI:** Nimekusahau? Haya, tutamalizia na wewe basi Mheshimiwa. (*Kicheko*)

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa. Kwa kuwa Serikali imepiga marufuku uvuvi wa majongoo bahari Kisiwani Mafia; wakati huo huo majongoo bahari yanavunwa kule Zanzibar upande wa pili wa Muungano.

Je, Serikali sasa haioni ni wakati muafaka kuruhusu uvuvi wa majongoo bahari kuendelea Mafia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema kwamba uvuvi wa majongoo bahari umepigwa marufuku Mafia, kwa sababu kimsingi kwa namna ulivyokuwa unaendelea ulikuwa unaharibu sana matumbawe. Kwa sababu kuvua majongoo bahari inabidi uzame ndani uende kwenye mazalia ya samaki na ni lazima uingie kwenye miamba ndiyo uweze kuvua majongoo bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar wao wanaendelea kufanya, lakini nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba suala la uvuvi katika maji yale ya kawaida siyo suala la Muungano. Kwa hiyo, Zanzibar wanakuwa na sheria zao na sisi tuna sheria zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri anachosema Mheshimiwa Mbunge ni kwamba ni vizuri katika kujenga ule ushirikiano tuwe na maamuzi ambayo yanaweza yakafanana na hasa yale ambayo yanasaidia pande zote mbili kuendelea kuimarisha na kulinda rasilimali za uvuvi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul na Mheshimiwa Magdalena Sakaya wa mwisho, tumemaliza.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wavuvi wa Ziwa la Babati wamekuwa wakipata taabu sana kwa Ziwa Babati kufungwa miezi sita kwa mwaka ilhali wavuvi hawa wanategemea uvuvi katika kuendesha maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Waziri, yuko tayari kufika Ziwa Babati na kushauriana na watalaam wa Halmashauri ya Mji wa Babati ili kupata mbegu ya samaki ambayo itatumika kwa mwaka mzima badala ya kama ilivyo sasa ambapo wavuvi hao huvua kwa miezi sita tu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kama niko tayari kwenda Babati kwenda kuongea na Halmashauri kuhusiana na hili, mimi sina shida na niko tayari hasa tukiandamana na yeye mwenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba kufungwa mara kwa mara kwa Ziwa Babati ni utaratibu wa kawaida katika *small water bodies* yaani maji madogo. Kama usipodhibiti ni rahisi uvuvi ukafanyika na ukamaliza

kabisa bioanuwai iliyopo ya samaki. Kwa hiyo, ni uataratibu wa kawaida. Hata ukisikia Bwawa la Nyumba ya Mungu limefungwa, ni kawaida. Kwa hiyo, Serikali inafanya hivyo ili kuwasaidia wananchi wako wa Babati. Lengo siyo baya, lakini tunatambua kwamba tusipodhibiti baada ya muda hakutakuwa hata na samaki mmoja katika Ziwa Babati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini akitaka twende, tutaenda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Magdalena.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wananchi tunaowapa elimu kwa ajili ya ufugaji wa samaki katika maeneo mbalimbali, wamekuwa wanahamasika na wanajenga mabwawa ya samaki lakini wanakosa vifaranga kwa muda mrefu, zaidi ya miaka miwili mpaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani kuhakikisha maeneo yote ambayo tunatoa elimu ya ufugaji wa samaki, tunanunua mashine za kutosha za kutotoa vifaranga vya samaki ili wananchi wale waweze kupata vifaranga kwa urahisi, lakini kwa bei nzuri waweze kunufaika na ufugaji wa samaki maeneo wanayokaa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupitia Bunge lako Tukufu nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba hakuna ukosefu wa vifaranga vya samaki. Kwa sasa kama kuna mtu yeyote ambaye anataka vifaranga, awasiliane na Wizara. Kimsingi vifaranga vya samaki mbalimbali wanazalishwa katika vituo vyetu vya uvuvi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge kama wananchi wake wanataka kuwekeza katika ufugaji wa samaki, anione nimwelekeze namna ya kupata vifaranga vya samaki.



Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba hata kwenye Ziwa Victoria Serikali imejipanga, kuna mradi ambao tunauanza katika mwaka huu wa fedha unaokuja wa kuwekeza vifaranga vya zaidi ya milioni 50 katika Ziwa Victoria ili kuendelea ku-boost uzalishaji wa sangara na sato. Kwa hiyo, kama kuna upungufu wowote Mheshimiwa Mbunge anaweza akaniona.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri na pia ahsante kwa kutuvumilia. Wengi humu naona ni wakulima na wavuvi, lakini bahati mbaya sana kwa vile siwajui ni nani wavuvi na wakulima, kwa vile hata mtu ukiishi Pwani au Ziwani unaweza kuwa sio mvuvi. Kama mimi hapa, naishi Pwani lakini ni mkulima wa Karafu. Kwa hiyo, naomba mnisamehe sana kwa hilo. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza muda wetu wa maswali na ningetamani niwape wote nafasi ya kuuliza maswali, lakini muda hautoshi. Kwa hiyo, naomba nianze kutoa matangazo kwanza kwa wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni ambao wapo hapa ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni wa kwanza hao. Wageni wawili wa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Lukuvi, kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao ni Dkt. Yamungu Kayandabila ambaye ni Katibu Mkuu, Dkt. Moses Kusiluka ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, wameambatana na watendaji 108 kutoka Wizarani, pamoja na Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo. Karibuni sana watendaji wetu kutoka Wizara ya Ardhi. *(Makofi)*

Pia tunao wageni saba wa Mheshimiwa Lukuvi ambao ni Mheshimiwa Balozi Einar H. Jense, Balozi wa Denmark anayewakilisha Mabalazi wa Uingereza na Sweden pamoja na Mashirika ya Maendeleo ya *DFID, DANIDA* na *SIDA* ambao ni wafadhili wa mradi wa *Land Tenure Support Programme* ulio chini ya Wizara ya Ardhi. Wa pili ni Ndugu Suleiman Dabbas ambaye ni *Senior Technical Advisor*, Mradi

wa *Land Tenure Support Programme* ulio chini ya Wizara ya Ardhi; Ndugu Blandina Nyoni ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*); Dkt. Fredy Msemwa ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji Watumishi *Housing Company*. Ndugu Oscar Mgaya ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji Tanzania *Mortgage Refinancing Company* na Ndugu Germina Lukuvi ambaye ni Mke wa Mheshimiwa Lukuvi. Karibuni sana, hasa mke wa Mheshimiwa Lukuvi. (*Makofi/Vigelele*)

Pia tuna wageni 31 wa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Angelina Mabula, ambao ni viongozi na wachezaji wa timu ya *Mbao FC* kutoka Mwanza wakiongozwa na Ndugu Etienne Ndayiragije ambaye ni kocha mkuu. (*Makofi*)

Wageni 33 wa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira Mheshimiwa Antony Mavunde, ambao ni wachezaji wa timu ya *Young African* kutoka Jiji la Dar es Salaam, (*Makofi/Vigelele*)

**MBUNGE FULANI:** Simba pigeni makofi basi! Simba pigeni makofi!

**MBUNGE FULANI:** Simba oyeee!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walipiga makofi na kuimba Simba, Simba!*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Wachezaji hawa...

Samahani jamani Waheshimiwa Wabunge, washabiki wa Simba naomba mnyamaze! (*Kicheko/Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, timu hii bingwa mara tatu imeongozwa na Ndugu Salum Mkemi, Mjumbe wa Kamati ya Utendaji. Lazima niseme kwa vile timu hii tayari imeshapongezwa na *FIFA*. Hongereni sana. (*Makofi/Vigelele*)

**MBUNGE FULANI:** Najma na wewe mnazi kumbe!

**MBUNGE FULANI:** Rufaa vipi?

**MBUNGE FULANI:** Rufaa hamna?

**MWENYEKITI:** Ahsanteni kwa kufurahi. Na mimi nimefurahi, tunaendelea na wageni. (*Makofi/Vigelegele*)

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge waliokuja kutembelea Bungeni wakimemo wageni wawili kutoka Kata ya Ulanga alikoza kwa Mbunge wa Ulanga, karibuni sana wote.

Waheshimiwa Wabunge, tuna tangazo moja kutoka Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Wajumbe wa Kamati hii wanataarifiwa kuwa leo tarehe 25 Mei kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo saa 7.30 mchana katika Ukumbi wa *Utawala Annex, Dispensary*. Kwa hiyo, Wajumbe wote mnatakiwa kuhudhuria.

**MBUNGE FULANI:** Hatujaisikia hiyo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na mambo yetu, kwa vile muda wangu mkubwa mmeuchukua kwenye maswali ya kilimo, uvuvi pamoja na masuala mengine, sasa kabla sijaendelea na taratibu nyingine, Katibu naomba tuendeleo mara moja halafu niweze kumaliza.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo!

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vipi? Wanataka kutuharibia hawa! Hao wote Simba hao!

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo!

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo, mwongozo!

**MWENYEKITI:** Leo hamtaki Miongozo eeh! Haya, ahsanteni sana. Tuendeleo, Katibu. *(Kicheko)*

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali  
kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 – Wizara ya Ardhi,  
Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

**MWENYEKITI:** Katibu, kabla hatujamkaribisha Mheshimiwa Waziri, tulikubaliana pale naongeza maswali ili niondoe miongozo, mlikubali.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamkaribisha Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, naomba nimkaribishe Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu), ili aweze kuja kutoa Hoja ya Kutengua Kanuni, halafu tuendeleo na kazi zetu.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mwongozo, tulitaka tuichangie Yanga tukatwe posho.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo!

**MBUNGE FULANI:** Katoe ng'ombe wako.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Hoja ya Kutengua Kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya siku chache zijazo katika Mkutano wa Saba unaoendelea, waumini wa dini ya kiislamu wataanza mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhani ambapo katika kipindi hicho waumini hao hutakiwa kuswali na kufuturu ifikapo saa 12.45 jioni. *(Makofi)*

KWA KUWA, Kanuni ya 28 inayohusu muda wa Vikao vya Bunge inaelekeza kwamba Shughuli za Bunge zinapositishwa saa 7.00 mchana ni lazima ziendelee saa 11.00 jioni na kuahirishwa saa 1:45 usiku hadi siku nyingine inayofuata;

NA KWA KUWA, ili kuliwezesha Bunge kutekeleza shughuli zake bila kuingiliwa na uhuru wa kuabudu kwa Wabunge ambao ni Waumini wa Dini ya Kiislamu, Bunge linatakiwa kutafuta utaratibu utakaowawezesha Wabunge hao kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za Bunge na hapo hapo kuswali na kufuturu kwa wakati muafaka kwa mujibu wa taratibu za dini yao;

HIVYO BASI, ninaliomba Bunge lako liazimie kwamba, Kanuni ya 28 (2) na (4) itenguliwe ili katika Kipindi chote cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani Bunge likisitishwa saa 7.00 mchana lirejee tena saa 10.00 jioni na liendelee kukutana hadi saa 12.00 jioni litakapoahirishwa hadi siku inayofuata na hivyo kuwaruhusu Waheshimiwa Wabunge wa dini ya kiislamu kuweza kuendelea na shughuli zao kama ilivyo utaratibu wa dini yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hiyo, naomba sasa kutoa hoja.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono. Nashukuru sana, asanteni. Katibu, tuendelee.

## HOJA ZA SERIKALI

### **Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

**MWENYEKITI:** Tunaendelea sasa na Waziri wa Ardhi, aweze kuja kuwasilisha Taarifa yake. Karibu sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Lukuvi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA  
MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ingependeza ungemruhusu Mheshimiwa Zungu atoe Mwongozo wake wa Simba labda. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Yanga bado wapo hapa, nawapongeza sana kwa kazi kubwa waliyofanya, lakini pia nawapongeza *Serengeti Boys* na Simba tutawapongeza wakati ukifika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2016/2017 pamoja na ile ya Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi.

Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Fungu Namba 48 na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, Fungu Namba 3 kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile pamoja na hotuba hii, nimewasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Programu ya Miradi, ikijumuisha miradi iliyosimamiwa na Taasisi, Wakala zilizo chini ya Wizara pamoja na Taarifa ya Urasimishaji wa Makazi Nchini. Taarifa hizi mbili wameziweka kwenye *pigeon holes*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kutoa salamu za pole kwako na Bunge lako Tukufu kufuatia kifo cha aliyekuwa Spika wa Bunge la Tisa, Hayati Mheshimiwa Samuel John Sitta. Aidha, katika kipindi hiki tumewapoteza Wabunge wenzetu wawili ambao ni Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani - CCM; pamoja na Dkt. Ely Marko Macha, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum - CHADEMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa familia za Marehemu, ndugu na wote walioguswa na misiba hiyo. Vilevile nitumie fursa hii kuwapa pole Watanzania ambao wamefiwa na wependwa wao. Mwenyezi Mungu azilaza roho za Marehemu hao mahali pema peponi, Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki katika Mkutano wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kwa namna ya kipekee, naomba nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na viongozi wote wa Serikali kwa mafanikio makubwa yanayoendelea kupatikana katika Awamu ya Tano. Kwa kasi hii tunayokwendanayo ikichagizwa na kauli mbiu ya Hapa Kazi Tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa tukio la jana la kizalendo alilolionesha kwa ripoti iliyosomwa jana. Nina uhakika tutafikia dhamira ya Tanzania ya viwanda. Aidha, nawapongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Idd, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mbunge wa Jimbo la Kitope kwa mafanikio makubwa yanayoendelea kupatikana chini ya uongozi wao imara kule Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kukupongeza wewe Mwenyekiti wa Kikao cha leo, wewe binafsi na Naibu Spika, lakini pia nampongeza sana Mheshimiwa Spika na ninamtakia safari njema huko aliko, arejee salama. Nampongeza Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Mwansasu, kwa jinsi mnavyosimamia shughuli za Bunge hili Tukufu kwa umakini wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nawapongeza Wenyeviti wa Bunge lako Tukufu, Mheshimiwa Chenge, wewe Mwenyekiti uliyepo hapo, Mheshimiwa Azzan Mussa Zungu, Mbunge wa Ilala, ambao kwa nyakati tofauti mmekuwa mkiongoza shughuli za Bunge kwa ufanisi. Mwenyezi Mungu aendelee kuwaongoza na kuwapa nguvu, afya njema na hekima, ili mwendelee kutimiza jukumu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Juma Ali Juma kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani.

Aidha, nawapongeza Wabunge wapya walioteuliwa kuingia katika Bunge hili, Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi ambaye pia ameteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria; Mheshimiwa Alhaji Abdallah Majura Bulembo, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Lwakatara na Mheshimiwa Catherine Nyakao Ruge. Nawatakiwa kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake ambayo imeelezea utekelezaji wa malengo ya Serikali katika mwaka huu tunaoendelea nao na mwelekeo wa utendaji wa sekta mbalimbali pamoja na kazi za Serikali zitakazotekelezwa katika mwaka wa fedha ujao 2017/2018. Wizara yangu itayafanyia kazi yale yote yanayoihusu sekta ya ardhi ili kuhakikisha kwamba malengo ya Serikali ya Awamu ya Tano yanafikiwa.



Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee natoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mhandisi Atashasta Justus Nditije, akisaidiana na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Kemilembe Julius Lwota, pamoja na Wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano mkubwa na uzalendo waliouonesha katika kutafakari na kupitia shughuli mbalimbali za Wizara na kutushauri. Aidha, nampongeza pia Waziri Kivuli wa Wizara hii kwa ushirikiano mkubwa ambao wamekuwa wananipa wakati wote wa kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Kamati hii kwa uchambuzi makini walioufanya na ushauri waliotoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekezaji wa Mpango wa Bajeti wa mwaka 2016/2017 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 48 na Fungu Namba 3. Pia nawashukuru kwa maoni na ushauri waliotoa wakati Kamati ilipotembelea miradi na taasisi zinazosimamiwa na Wizara na kujadili masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya ardhi. Ushauri wao utaendelea kuzingatiwa wakati wote wa utekezaji wa majukumu ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani za pekee kwa Naibu wangu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Lubala Mabula, Mbunge wa Ilemela na kiongozi Mhamasishaji wa timu ya Mbao, tumeiona pale juu, kwa ushirikiano mkubwa na ushauri alionipa wakati wote wa utekezaji wa majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nawashukuru sana Katibu Mkuu Dkt. Yamungu Kayandabila, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Moses Kusiluka, Wakuu wa Idara, Kamishna, Msajili, Mkurugenzi wa Mipango Miji, Mkurugenzi wa Upimaji, Mkurugenzi wa Shirika la Nyumba, Mkurugenzi wa Shirika la *Watumishi Housing*, Wakala wa Taasisi zilizo chini ya Wizara yangu, pamoja na wadau mbalimbali wakiwemo wapima wote, viongozi wa makampuni binafsi ya kupima ardhi, ambao tunashirikiana nao katika kupima na kupanga ardhi

ya nchi hii na baadhi yao nawaona wako pale. Pia, viongozi wa Makampuni ya Kupanga Mipango Miji, ambao pia wamealikwa katika kikao hiki. Nawapongeza sana kwa ushiriki katika kutekeleza sera yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya ya utangulizi, naomba sasa nieleze kwa kifupi utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Takwimu za Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti zilizopo katika hotuba hii zinaishia tarehe 15 Mei.

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara yangu ilipanga kukusanya shilingi bilioni 111.77 kutokana na vyanzo vya mapato yanayotokana na kodi, ada na tozo mbalimbali za ardhi. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, Wizara ilikuwa imekusanya shilingi bilioni 80.52 sawa na 72% ya lengo. Aidha, katika mwaka wa fedha 2015/2016, mwaka mmoja nyuma, Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka tulikusanya shilingi bilioni 74.71 sawa na 107% ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 70. Ni matarajio yetu kwamba hadi kufikia Juni 17, lengo la kukusanya fedha zote shilingi bilioni 111.77 litafikiwa kwa kutekeleza Mpango Mkakati wa Wizara, kuna Jedwali Na. 1 ambalo linaonesha takwimu za makusanyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo nachukua nafasi hii kuwapongeza wamiliki wa ardhi waliolipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati. Aidha, nawataka wamiliki wote wa ardhi ambao hawajalipa kodi hiyo wahakikishe wanalipa kabla ya tarehe 30 Juni. Serikali itaendelea kuwachukulia hatua kali wamiliki wote ambao hawalipi kodi kwa wakati, ikiwa ni pamoja na kuwafutia miliki zao, kuwafikisha Mahakamani na kukamata na kuuza mali zao kwa ajili ya kufidia deni la kodi wanalodaiwa. Tukumbuke kwamba kodi hii ndio inayojazilisha bajeti kwa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016/2017 Wizara iliahidi kuhuisha viwango vya kodi ya ardhi kwa mashamba ya biashara yaliyopo nje ya miji yaliyomilikishwa chini ya Sheria Na. 4 ya mwaka 1999. Baada ya kupitia viwango hivyo,

Serikali inakusudia kuongeza viwango vya pango la ardhi kutoka shilingi 400 hadi shilingi 1,000 kwa ekari kwa mwaka kuanzia tarehe 01 Julai kwa mashamba ya biashara yaliyopimwa na kumilikishwa nje ya miji. Kiwango kinachotozwa leo cha shilingi 400 kwa ekari moja ni ndogo sana ikilinganishwa na thamani ya pamoja ya uwezo wa uzalishaji wa ardhi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa sina maana ya wakulima wadogo wadogo maskini wenye Hati za Kimila; wale wenye Hati za Kimila watatozwa sifuri sifuri, hawatozwi kodi yoyote. Haya ni mashamba ya katani, mashamba makubwa ya kilimo yanayotozwa shilingi 1,000 tu kwa ekari. Kama unavuna magunia 20 kwa mwaka, basi uilipe Serikali shilingi 1,000 kwa ekari, lakini wale masikini wengi waliopo na sisi tunaomiliki ardhi ekari 20, 30 kwa Hati za Kimila, hawatatozwa kodi yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwawezesha wananchi wengi kumiliki maeneo yao kwa gharama nafuu pamoja na kupanua wigo wa walipaji kodi, pango la ardhi, Serikali inatarajia kupunguza tozo (*premium*) kutoka 7% ambayo inatozwa sasa. Mtakumbuka hatukufikia malengo ya ukusanyaji wa kodi kwa sababu wananchi wengi sasa wanajenga katika viwanja ambavyo havikupangwa kwa sababu, tozo ile ya kuchukua hati ilikuwa kubwa sana, inawashinda. Hata hapa Dodoma watu wanashindwa. Unatakiwa kulipa mamilioni ili upate hati. Wawekezaji wetu wamekuwa wanashindwa wanaomba msamaha wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa tumeamua kuanzia tarehe 01 Julai tozo ya *premium* ambayo ilikuwa inatozwa 7.5% ya thamani ya ardhi itatozwa sasa 2.5% ambayo ni punguzo la 67%. Nia ya tozo hii kupunguzwa ni kuwawezesha wananchi wote waweze kumiliki mashamba yaliyopimwa na kupangwa, waweze kumiliki viwanja vilivyopangwa na kupimwa na hivyo katika miji kupunguza *squtter*, watu sasa wajenge katika viwanja vyenye hati. Kwa hiyo, tunapunguza hapa tozo ya *premium* kwa 67%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ada hii hutozwa mara moja tu wakati wa umilikishaji ardhi kwa mujibu wa Fungu la 31 la Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999. Kupunguzwa kwa kiwango hiki cha tozo la mbele, tutavutia wananchi wengi na wawekezaji wenye maeneo ya ardhi kujitokeza kwa wingi zaidi kupimiwa na kumilikishwa ardhi yao. Natoa rai kwa wananchi wote kutumia fursa hii ya punguzo la tozo ya mbele kupima na kumilikishwa maeneo yao na kulipa kodi stahili kila mwaka. Kupungua kwa kodi au tozo hii ambayo ilikuwa inaongeza gharama za viwanja kutawafanya watu wengi zaidi, hasa wa kipato cha chini, kumudu gharama za kumilikishwa viwanja na kutapunguza gharama za uwekezaji na za kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka ujao Wizara inatarajia kukusanya shilingi bilioni 112 kutokana na shughuli za sekta ya ardhi. Mapato haya yatatokana na vyanzo mbalimbali vya kodi na tunaamini sasa kutokana na punguzo la kodi, watu wengi sana watapenda kumiliki ardhi na hivyo tutaongeza na tutapanua wigo wa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016/2017 huu unaoisha, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 70.49 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 16.34 zilitengwa kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 28.85 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 25.30 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 15 Mei, Wizara ilikuwa imepokea na kutumia jumla ya shilingi bilioni 34.95 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo, sawa na 50% ya lengo la mwaka. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 13.21 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ambapo shilingi bilioni 2.28 zilitolewa kwa Halmashauri mbalimbali kwa ajili ya kuendeleza shughuli za sekta ya ardhi. Shilingi bilioni 14.11 ni fedha za mishahara na shilingi bilioni 7.63 ni fedha za miradi ya maendeleo; kuna jedwali Na. 2 kwenye kitabu chenu. (Makofi)

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2016/2017 kwa Fungu Namba 3, Tume ilikuwa na lengo la kukusanya shilingi milioni 775.25 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali ambavyo ni kodi ya pango la nyumba za Tabora na mauzo ya nyaraka za zabuni. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, Tume ilikuwa imekusanya shilingi milioni 531.66 sawa na 69% ya lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa ardhi nchini ni suala mtambuka kwa kuwa linahusisha mamlaka mbalimbali zikiwemo Halmashauri za Vijiji, Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa, Majiji na Wizara yangu. Pamoja na uwepo wa mamlaka hizi, Wizara imeendelea kupokea hoja ya malalamiko mbalimbali yanayohusiana na ardhi kutoka kwa wananchi ambayo kimsingi wangeweza kushughulikiwa katika ngazi za vijiji au Halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwakumbusha wananchi kutumia Ofisi za Halmashauri kwa ajili ya kutatua kero zao kabla ya kuwasilisha kero hizo katika ngazi ya Wizara. Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Wakuu wa Wilaya waliotenga muda wao kwa ajili ya kusikiliza na kutafuta ufumbuzi wa kero za wananchi zinazohusu masuala ya ardhi. Aidha, natoa rai kwa Wakuu wote wa Wilaya ikibidi kama nilivyoomba ninyi Wabunge siku moja hapa nilipokuwa najibu swali la nyongeza, hebu mpate muda mtembelee katika Masjala zetu za Ardhi zilizopo kwenye Halmashauri zetu kukagua ofisi hizo za Masjala za Ardhi katika Halmashauri kwa lengo la kuchukua hatua dhidi ya urasimu wa makusudi na uzembe kwa maafisa wanaochelewesha utoaji wa haki hasa hati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majalada yanakaa kwenye faili watu hawapati hati zao kwa zaidi ya miaka miwili, mitatu wakati Serikali imetangaza kila mmoja apate hati ndani ya mwezi mmoja. Kwa hiyo, tushirikiane katika kufanya ukaguzi wa kushtukiza katika Ofisi za Ardhi tuangalie yale mafaili yameficha hati, kuna watu mpaka wamesahau hati zao zimefichwa kwenye ofisi zile. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnaweza mtakatembea na Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya naomba muwe mnafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusogeza huduma za ardhi karibu zaidi na wananchi, Wizara imeboresha muundo wa ofisi za kanda kwa kuanzisha kanda mpya ya Simiyu, kupunguza na kuongeza mikoa katika baadhi ya kanda. Kwa hiyo, kuanzia tarehe 1 Julai, 2017, Ofisi za Ardhi za Kanda zitakuwa zikihudumia mikoa kama ifuatavyo. Kutakuwa na Kanda ya Dar es Salaam ambayo sasa itahudumia Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani; Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambayo itakuwa Mbeya itahudumia mikoa ya Mbeya, Njombe, Rukwa na Songwe; Kanda ya Kati hii Dodoma sasa itahudumia Mikoa ya Dodoma, Singida, Iringa na Morogoro; Kanda ya Kaskazini ambayo sasa itatoka Moshi inakuja Arusha, Ofisi ya Kanda inahama kutoka Moshi kwenda Arusha, itahudumia Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Manyara; Kanda ya Ziwa Mwanza itahudumia Mikoa ya Mwanza, Geita na Kagera; Kanda ya Magharibi Tabora sasa itahudumia Mikoa ya Tabora, Kigoma na Katavi; Kanda ya Kusini Mtwara itahudumia Mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma na Kanda Mpya ya Simiyu itakayokuwa Bariadi itahudumia Mikoa ya Simiyu, Shinyanga na Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha utoaji huduma, Wizara imeendelea kuimarisha Ofisi za Ardhi za Kanda kwa kupeleka wataalam wa kanda wa kada mbalimbali. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, Wizara imepeleka watumishi wa kada ya Wapima Ardhi na Wasajili katika Ofisi za Kanda ya Ziwa Mwanza; Kanda ya Kusini Mtwara na Kanda ya Magharibi Tabora. Aidha, vitendea kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na magari nane mapya tumeyakabidhi katika kanda zote lakini vifaa na vitendea kazi mbalimbali vimepelekwa kwenye kanda zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu tunaoanza mwezi wa saba, watumishi wa kanda ya Maafisa Ardhi, Wasajili wa Hati, Wathamini, Wapima Ardhi na Maafisa Mipango Miji watapelekwa katika Ofisi za Kanda zote. Lengo la hatua hii ni kuwawezesha wananchi kupata huduma mbalimbali za ardhi katika kanda badala ya kuzifuata huduma hizo Makao Makuu. Mwaka wa fedha ujao itakuwa ndiyo mwisho wa mtu yeyote kutoka katika pembe yoyote

ya Tanzania kuja kutafuta huduma katika Wizara. Kazi zote za kuidhinisha uthamini zitaishia kwenye kanda, kazi zote za kuthibitisha michoro ya upimaji zitaishia kwenye kanda, kazi zote za kupitisha mipango miji zitaishia kwenye kanda, hati zote zitasainiwa kwenye kanda na usajili utafanywa kwenye kanda. Kwa hiyo, Wizara hii inajimega kwenye kanda nane ambapo kila kanda ina uwezo wa kufanya kazi zote za ardhi bila kuchelewesha, hiyo itaanza tarehe 1Julai, 2017. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuvunjwa kwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu. Kwanza nampongeza sana Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuondoa kero hii na kwa kusikiliza kilio cha wananchi wa Dodoma na Watanzania wanaotaka kuwekeza Dodoma kwa kipindi kirefu. Kufuatia uamuzi wake na Serikali wa kuvunja CDA, kupitia Tamko la Rais, Tangazo Na. 213 la mwaka 2017, kazi za iliyokuwa CDA sasa zimehamishiwa rasmi Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma na zitafanywa kwa mujibu wa sheria kama Halmashauri nyingine zote zinavyoendesha shughuli za ardhi katika Tanzania hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia sasa wananchi wote wanaohitaji huduma za ardhi watapata huduma hizo kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma. Iliyokuwa Hati ya CDA ambayo walipewa ardhi yote ya Dodoma, Hati Na.4585DLR imefutwa. Kuanzia tarehe 1 Julai, 2017 wananchi wote waliokuwa wanamiliki ardhi kwa kupewa hati hafifu zile *lease* kwa mikataba ya pango la ardhi (*ground lease*) iliyokuwa inatolewa na CDA miliki zao zitahakikiwa na watamilikishwa ardhi yao kwa kupewa hati miliki (*title deed*) ambazo zitakuwa na umri wa miaka 99. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kila mmoja ambaye ana hati yake ya Dodoma atakuta tangu amepewa ilikuwa na miaka 33 leo imebaki miaka kumi aongeze 66, hii ni nyongeza ambayo imetolewa na Mheshimiwa Rais, kwa hiyo, kila hati yako ongeza miaka 66. Kila hati itaongezwa miaka 66 ili hati za Dodoma zifanane na hati nyingine zinazotolewa katika mahali pengine Tanzania na zitakuwa *title deed* ambazo sasa unaweza ukashirikiana na mwekezaji

wa nje akaja kuwekeza Dodoma kwa sababu sasa *TIC* atakuwa na uwezo wa kutoa *derivative right* Dodoma kitu ambacho hakuwa nacho. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, mageuzi haya sasa tutaanza kuona *direct foreign investiment* Dodoma na pia wananchi sasa wanaweza kukopesheka kwa sababu hati zao zitakuwa na umri mrefu ambao unaweza kuaminika katika mabenki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai kwa wananchi wote wanaomiliki ardhi Dodoma kuhakikisha wanalipa malimbikizo ya kodi ya pango la ardhi ili kuondoa usumbufu unaoweza kujitokeza wakati wa zoezi la kubadilisha hati ambalo tutaanza kulifanya tarehe 1 Julai, 2017. Kila mmoja mwenye *lease* atapewa *title deed* ya miaka 99 bila gharama yoyote. Mheshimiwa Rais amesema kazi hii ifanyike bila kuongeza hata shilingi moja. Watu watabadilishiwa hati zao kupewa hiyo miaka 99 bila kuongeza gharama hata shilingi moja, Serikali itagharamia kazi hii yote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tunafahamu kwamba kuna viwanja vilivyopimwa *CDA* hapa karibu 60,000 lakini hati zilizotolewa ziko 26,000 tu. Kwa hiyo, sisi tunajua wale *CDA* ya zamani iliyokuwepo watatuambia hivi viwanja 34,000 viko wapi mpaka kumekuwa na ukame wa viwanja wakati viwanja vilivyopimwa na kupangwa Dodoma ni 60,000 lakini vyenye hati ni 26,000, 34,000 viko kwenye maduka ya madalali na watu fulani fulani. Kwa hiyo, uhakiki utafanywa na kuhakikisha kwamba viwanja vyote 60,000 vinaingia mikononi mwa wananchi ambao wamekuwa wanahangaika kutafuta umilikishwaji wa ardhi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba maafisa wote wamsaidie Mkurugenzi wa Manispaa na wale wote watakaojiingiza katika udanganyifu kwa nia ya kudhulumu, kutapeli, kuficha au kuhodhi viwanja watachukuliwa hatua kali za kisheria. Nawatahadharisha tu rafiki zangu wafunge maduka yao ya kuuza viwanja sasa biashara imehamia sehemu mbaya zaidi. Kwa hiyo, watoe ushirikiano kwa Mkurugenzi na Wizara yangu iko tayari kushirikiana na



Halmashauri ili kuhakikisha kwamba masuala yote ya ardhi yanaenda vizuri kama yanavyoendesha katika maeneo mengine ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa pamoja na zoezi hili la kubadilisha hati za Dodoma, haki za wananchi na taasisi za fedha zinazohusiana na mikataba ya mapango iliyotumika katika dhamana kupata mikopo na miamala mingine iliyokuwa haijakamilika hazitaathirika na mabadiliko haya. Kuna watu tunajua wame-*mortgage*, *mortgage* mabenki hayatapata hasara. Tutafanya kazi vizuri ili mabenki yasipoteze haki yake kutokana na mabadiliko haya ya hati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia kuongezeka kwa majukumu katika Kanda ya Dodoma sasa, Wizara yangu itaongeza vitendea kazi na wataalam wa kada mbalimbali ili kuhakikisha kazi hizi za usimamizi wa kanda hii unaenda vizuri. Kwa hiyo, naomba tena nirudie wananchi wa Dodoma sasa mambo yenu yatakwenda kwenye Manispaa na yatasimamiwa chini ya Baraza la Madiwani, Madiwani ambao mmewachagua wenyewe kidemokrasia. Narudia tena kwa niaba yenu watu wa Dodoma na Watanzania kumshukuru tena Mheshimiwa Rais kwa kuamua jambo hili ambalo limedumu kwa muda mrefu sana kwa kuamua kurudisha madaraka ya usimamizi wa ardhi kwa wananchi kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa miliki. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara iliamua kuandaa hati miliki za ardhi 400,000 na kutoa hati za kimila 57,000. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017, Wizara imetoa hatimiliki za ardhi 33,979 na imeratibu uandaaji wa haki miliki za kimila 35,002. Aidha, Wizara imeandaa vyeti vya ardhi za kijiji, Jedwali Na. 4 linaonesha. Hatukufikia lengo lakini sababu ni nyingi, wananchi wengi tumegundua walikuwa wanashindwa gharama za kupima na kulipia hati zao. Ndiyo maana tumechukua hatua kupunguza tozo mbalimbali ili wananchi wengi waweze kumilikishwa katika mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutambua ushiriki wa wadau mbalimbali kwa mchango wao katika kuwezesha utoaji wa vyeti vya ardhi za vijiji na hati za haki miliki za kimila. Baadhi ya wadau hao ni MKURABITA; USAID; DFID; DANIDA na SIDA. Wengine ni *Oxfarm International Tanzania*; *Care International Tanzania*; *Ujamaa Community Resource Team*; *African Wildlife Foundation* na wengine wote ambao mtawakuta wamechapwa kwenye kitabu hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nawashukuru sana wadau wa maendeleo, leo tunaye Balozi wa Denmark hapa ambao wanatusaidia sana mradi wetu wa *Land Tenure Support Programme* amekuja kwa niaba ya wenzake, wanatusaidia sana katika mpango wa awali wa majaribio wa kupanga na kupima na kumilikisha ardhi yote katika Wilaya tatu za Mkoa wa Morogoro. Tunataka tuone ili baadaye tuweze kuwa na kigezo cha upangaji na upimaji wa ardhi ya nchi nzima. Nampongeza Balozi wa Denmark kwa kujitolea kuja Dodoma na kwa mchango wake wa kusaidia sekta ya ardhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri nchini itaandaa hati miliki 400,000, vyeti vya ardhi 1,000 na kutoa hati za kimila 57,000. Natoa rai kwa Halmashauri zote nchini kwa kuhakikisha kuwa zinamilikisha viwanja vyote vilivyopimwa na kuandaa hati ili wananchi waweze kuwa na miliki salama lakini waweze kuchangia kodi kwa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhakiki wa viwanja na mashamba; mwaka huu wa fedha, Wizara imechukua hatua ya kubatilisha miliki za viwanja 227 na mashamba 17 kutokana na ukiukwaji wa masharti. Viwanja na mashamba haya yapo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, Iringa, Kagera na Morogoro na mengine yako njiani. Najua kuna maeneo mengi ya Mlali, Muheza, Korogwe na kadhalika, yako mashamba mengi yameshahakikiwa lakini yako kwenye *process* ya kufutwa ili angalau wananchi wa wilaya zile ambao kwa muda mrefu wamekosa ardhi

waweze kumilikishwa ardhi hizi. Wale wote wenye taarifa nyingine ambazo wana mashamba ya namna hiyo tutaendelea kuwasiliana na tutatoa huduma ili kuhakikisha kwamba kila mwawanchi wa Tanzania anapata fursa ya kumiliki ardhi kwa maendeleo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri imefanya ukaguzi wa mashamba ya 121 yenye ukubwa wa ekari 552,139.21 yaliyopo katika Mikoa ya Tanga, Morogoro, Pwani, Njombe na Kagera na kuingiza taarifa zake katika kanzidata ya Wizara. Kati ya mashamba haya, 63 yameendelezwa na 58 yametelekezwa. Najua yako mengi lakini tutafika kila mahali kushirikiana na nyie Waheshimiwa Wabunge ili kuhakikisha haki ya wananchi wenu katika majimbo inapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utatuzi na udhibiti wa migogoro. Katika hotuba ya bajeti yangu mwaka wa fedha uliopita suala la migogoro ya ardhi liligusa hisia za Waheshimiwa Wabunge wengi na waliitaka Serikali kuwa na mkakati maalum wa kushughulikia suala hili. Kwa kutambua kuwa migogoro ya matumizi ya ardhi ni suala mtambuka, kama ambavyo mmeliona kwenye bajeti mbili zilizotangulia, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Takwimu iliunda Kamati ya kisekta ili kubaini aina na vyanzo vya migogoro na kupendekeza namna bora ya kutatua migogoro hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupokea taarifa ya Kamati, Serikali inafanya uchambuzi utakaowezesha kuchukua hatua ya kutatua migogoro hiyo. Ie taarifa niliyowapa mwaka jana mliyoainisha migogoro pamoja na taarifa mbalimbali ambazo zimewahi kutolewa na Tume zikiwemo zile za Kamati za akina Sendeka na nyinginezo zimechambuliwa na ziko kwenye taarifa hii. Sasa imebaki kwa sisi tuliounda ile Kamati kuchambua na kuipeleka katika ngazi za Serikali ili uamuzi ufanyike kwa mapendekezo ya Tume, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge kazi hiyo inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, safari hii tuna kitabu kingine ambacho kina uchambuzi siyo orodha ya migogoro, ni uchambuzi. Tupeni muda tukamilishe kama wenzangu walivyofanya, *I am sure*, mtaona matokeo hata kabla ya bajeti ijao. Tutaendelea na kasi ya utatuzi wa migogoro vilevile na tutaendelea kushirikiana na ninyi ili kuhakikisha kwamba migogoro yote ya ardhi katika miaka mitano ikiwa na ile ya mipaka mliyozungumza ya vijiji na hifadhi za misitu na wanyama, wakulima na wafugaji, tutashirikiana ili kuhakikisha inakwisha. Ni ngumu lakini wenzetu wa Kamati hii wametutafutia mwarobaini wa namna ya kushughulikia migogoro hii haswa ile ambayo inajulikana na ambayo Waheshimiwa Wabunge mmetupatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu ya Kuwezesha Umilikaji Ardhi. Wizara yangu inaendelea na utekelezaji wa Programu ya Kuwezesha Umilikishaji Ardhi (*Land Tenure Support Programme*) katika Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi Mkoani Morogoro chini ya ufadhili wa Serikali za nchi za Uingereza, Sweden na Denmark kupitia mashirika yao ya maendeleo ya *DFID*, *SIDA* na *DANIDA*. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara yangu iliahidi kuandaa hati kimila 50,000 katika vijiji 40 vya eneo la mradi na kujenga Masjala za Ardhi katika vijiji hivyo. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017, hati za kimila 11,403 zimeandaliwa katika vijiji saba vya Wilaya za Kilombero hati 8,303 katika vijiji vinne na Ulanga hati 3,100 katika vijiji vitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara yangu kupitia Programu ya Kuwezesha Umilikishaji Ardhi imepanga kufanya uhakiki wa vipande vya ardhi 80,000 na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 37; kujenga ofisi za ardhi katika Wilaya za Kilombero moja, Ulanga moja na Malinyi moja na kuandaa vyeti vya ardhi vya vijiji 15 katika Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi. Hapa tumeanza majaribio lakini lengo la mradi huu utakapokamilika ni ili tujifunze yaliyotokea na mafanikio tuweze kutumia kama *model* ya kufanya zoezi hili la kupanga, kupima na kumilikilisha nchi mzima.

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Kwa hiyo, narudia tena kuwapongeza wadu wetu wa maendeleo na wananchi wa wilaya hizi tatu kwa ushiriki wao katika kutekeleza mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usajili wa hati miliki. Mwaka 2016/2017, Wizara yangu ilipanga kusajili hati miliki na nyaraka za kisheria 450,500 kati ya hizo 400,000 ni hati miliki, 2,500 hati za kumiliki sehemu ya jengo yaani *unit title* na nyaraka za kisheria 48,000. Hadi kufikia tarehe 15 mwezi huu, hati miliki pamoja na nyaraka za kisheria 79,117 zimesajiliwa. Kati ya hizo hati miliki ni 32,178. Naomba Waheshimiwa Wabunge mwende kwenye kitabu chetu muangalie Jedwali Na. 7A, 7B na 7C yanaonyesha kazi mbalimbali za usajili wa nyaraka ambazo zimefanywa kupitia kanda zetu nane ambazo zinafanyakazi ya usajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara inakusudia kusajili hati miliki na nyaraka za kisheria 453,000; kati ya hizi, hati za kumiliki ardhi ni 400,000, hati za kumiliki sehemu ya jengo (*unit title*), leo mwananchi anaweza akamiliki kaghorofa ndani ya jengo lenye gorofa 50 na akapewa hati yake sawa na mtu anayemiliki ardhi ya chini. Kwa hiyo, hizi hati za namna hiyo za *unit title* mwaka huu tunatarajia tutazitoa 3,000 na nyaraka nyingine za kisheria 50,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu teknolojia ya habari, katika mwaka wa fedha uliopita, Serikali iliahidi kuanza ujenzi wa Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi (*Integrated Land Management Information System-ILMIS*). Katika kutekeleza ahadi hii, Serikali imetekeleza na imeingia mkataba wa mkandarasi (*JGN F*) ambao *consultancy* wao tunao hapa wa kujenga mfumo huo. Mkataba huo ulisainiwa tarehe 8 Julai, 2016. Kazi ya ujenzi wa mfumo ilizinduliwa rasmi tarehe 26 Agosti, 2016 na mkandarasi tayari ameanza kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na ujenzi wa mfumo huu, Serikali imekamilisha ujenzi wa jengo la Kituo cha Taifa, tumejenga Kituo cha Taifa cha Taarifa za Ardhi na ufungaji wa baadhi ya vifaa umekamilika. Kwa hiyo,

tutakuwa na kituo kimoja ambacho kitatunza taarifa zote za ardhi za nchi mzima. Ukiingia pale Dar es Salaam kwenye Ofisi ya Makao Makuu lipo jengo pale ambalo limewekwa vifaa vya kisasa ambavyo sasa taarifa zote za ardhi zinaweza zikapatikana za nchi mzima kwa kuunganishwa ndani ya jengo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha ujao, Wizara itanza kutoa hati za kielektroniki katika Manispaa za Kinondoni na Ubungo. Kwa awamu ya pili, mfumo huu utaunganishwa katika Wilaya zote. Mfumo tumefunga Dar es Salaam tunafanya majaribio Kinondoni na Ubungo baada ya hapo sasa tuta-*hook* na Wilaya zote za Halmashauri za Tanzania kupitia kile kituo ambacho kimejengwa Dar es Salaam. Kwa hiyo, awamu ya kwanza katika Bunge lijalo Mungu akipenda inawezekana tukaonyesha hati ya elektroniki ikoje na pengine wale ambao wanamiliki ardhi katika Wilaya za Ubungo na Kinondoni watakuwa wameshaziona wenyewe kwa sababu tutafanya mabadiliko ya hati ili watu waweze kupata hati ya usalama zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara iliahidi kukamilisha usimikaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Kuhifadhi Kumbukumbu na Kukadiria Kodi ya Ardhi (*Land Rent Management System-LRMS*) katika Halmashauri 17 zilizobaki kati ya 14. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kazi hii imefanyika vizuri katika Halmashauri kumi na Halmashauri Halmashauri saba saba zilizobaki ambazo ni Buhigwe, Nanyamba, Momba, Madaba, Mbogwe, Buchosa na Mpimbwe zitafanyiwa kazi katika mwaka ujao wa fedha, lakini nyingine zote kumi zimeshawekewa mfumo huo. Wizara itaendelea kuboresha ili kuhakikisha kwamba ukusanyaji wa kodi unakwenda vizuri na mifumo hii inawekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uthamini wa mali; katika mwaka 2016/2017 Wizara iliahidi kuandaa na kuidhinisha taarifa 32,500 za uthamini wa kawaida na fidia ka matumizi mbalimbali. Hadi 15 Mei, 2017, Wizara iliidhinisha taarifa za uthamini 8,725 ambapo taarifa 97 ni uthamini wa fidia, 8,628

ni uthamini wa mali kwa madhumuni mbalimbali kama vile rehani, dhamana ya mahakama, bima, mirathi na mgawanyo wa mali na wana ndoa. Jedwali Na. 8A na 8B linaonyesha maeneo mbalimbali ambayo tathmini imefanywa na yamepitia kwa *Chief Valuer*. Mwaka ujao wa fedha, Wizara inatarajiwa kuandaa na kuidhinisha taarifa 35,000 za uthamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda kuutarifu umma na kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwamba kufuatia ile sheria iliyotungwa na Bunge mwaka huu na kuanza kutumika kwa Sheria ya Uthamini na Usajili ya Wathamini Na. 7 ya mwaka 2016 iliyotungwa mwaka jana, taarifa zote za uthamini zinapaswa kuidhinishwa sasa na Mthamini Mkuu wa Serikali. Kuna baadhi ya taarifa zamani zilikuwa hazipitii kwa Mthamini Mkuu wa Serikali na kwa mwaka ujao wa fedha tunaweka Manaibu Wathamini Wakuu wa Serikali kwenye Kanda kama mlivyotunga sheria ili kuhakikisha kwamba wanasimamia suala hili vizuri. Huu ndiyo mwarobaini wa wathamini ambao walikuwa hawatendi haki kwa maskini, huu ndiyo mwarobaini wa sheria. Kwa hiyo, sasa inatakiwa kila tathmini lazima ipitie kwa Mthamini Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za upimaji na ramani. Kwa mwaka huu wa fedha 2016/2017, Wizara iliahidi kuendelea kuhakiki na kuandaa ramani za mipaka na wilaya mpya kwa mujibu wa matangazo ya Serikali iliyoanzisha wilaya hizo. Wizara imekamilisha uhakiki na uandaaji wa ramani za mipaka tano ambayo ni Nyang'wale, Geita, Bukombe, Mbogwe na Chato. Katika mwaka ujao, Wizara itahuisha ramani ya msingi kwa uwiano wa moja kwa 50,000 kwenye miji 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imebaini kuwepo kwa baadhi ya taasisi binafsi zinazojihusisha na uandaaji wa ramani na kuziuzaa bila idhini ya Wizara, jambo hilo ni kosa kisheria. Baadhi ya ramani hizi hazitoi taswira sahihi ya mipaka na hasa mipaka ya nchi yetu na nchi jirani. Natoa onyo kwa wote wanaojihusisha na shughuli hizo waache mara moja

vinginevyo Wizara haitasita kuwachukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kuafikisha mahakamani. Ramani hizi nyingine zimekuwa zinatumika hata kwenye mashule kupotosha vijana wetu ukweli halisi wa mipaka ya nchi yetu. Ramani ya mipaka halisi ya Tanzania ni kama inavyoonekana ndani ya kitabu changu cha bajeti ukurasa wa 156.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipaka ya kitaifa. Katika mwaka wa fedha huu tunaoendelea nao 2016/2017, Wizara iliahidi kuanza kazi ya upigaji picha za anga katika mpaka wa Tanzania na Kenya, kule wanakotoka akina Mheshimiwa Selasini, wenye urefu wa kilometa 756. Upigaji wa picha za anga kwenye mpaka huo umekamilika. Vilevile uhakiki wa ubora wa picha hizo umefanyika na kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka ujao wa fedha, Wizara itaendelea na uimarishaji wa mpaka wa Tanzania na Kenya ikiwa ni pamoja na utengenezaji wa ramani za msingi pamoja na kupima kipande cha mpaka kuanzia Ziwa Victoria hadi Ziwa Natron chenye urefu wa kilometa 240. Aidha, majadiliano kati ya Tanzania na Zambia na Tanzania na Uganda kwa ajili ya kuimarisha mipaka yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upimaji wa viwanja na mashamba. Katika mwaka 2016/2017, Serikali iliahidi kuidhinisha ramani za upimaji zenye viwanja 200,000 na mashamba 400. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, ramani za upimaji zenye jumla ya viwanja 118,502 na mashamba 374 zillidhinishwa. Katika mwaka wa fedha ujao, Wizara itaidhinisha ramani za upimaji zenye jumla ya viwanja 200,000 na mashamba 400.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu pia Wizara iliahidi kusimika na kupima alama za msingi za upimaji yaani *control points* ambazo zinatumika na wapima wote 200. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017, Wizara ilikuwa imesimika alama za msingi 154 katika Halmashauri za Manispaa 44 kama kiambatanisho kinavyoonyesha yaani Morogoro 44, Dodoma 60, Manispaa 30, Halmashauri ya Wilaya alama zinaonekana



kule. Alama hizi ni nyongeza kati ya alama za msingi zilizosimikwa katika mfumo mpya kusaidia shughuli za wapimaji hapa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka ujao, Wizara itasimika alama za msingi 200 kwa ajili ya kusaidia upimaji katika Halmashauri mbalimbali nchini. Alama hizi tunaziweka kwa sababu tunanunua vifaa vipya vya upimaji ambavyo haviwezi kupima bila kuwa na alama hizi ambazo zitaunganisha masafa na *satellite* ili kurahisisha upimaji. Kwa hiyo, alama hizi tunaziweka nchi nzima. Pia tuna mpango wa kununua vitu kama vile *drones* kwa ajili ya upigaji picha za anga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara yangu imekamilisha kusimika mtandao mpya wa alama za msingi kwa ajili ya shughuli za upimaji wa ardhi, uchoraji wa ramani unaoendelea na mifumo ya kisasa ya upimaji wa ardhi. Tanzania inakuwa nchi ya kwanza Afrika Mashariki na Kati na ya pili Kusini mwa Jangwa la Sahara baada ya Afrika Kusini kuwa na mtandao wa aina hiyo. Uwepo wa mtandao huu utasaidia kuharakisha mchakato wa upimaji kila kipande cha ardhi nchini Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtandao huu una jumla ya alama 686 katika madaraja tofauti kama inavyoonekana katika ukurasa 157, mtaona kuna vidoti doti vingi sana, kuna alama nyingine ndogo na nyingine kubwa lakini alama hizi zote zimewekwa katika maeneo yote ya Wilaya na kwenye kitabu change yameonyeshwa katika ukurasa 157 na mchanganuo wa alama hizo za msingi umefafanuliwa vizuri kwenye kitabu.

Kwa ufupi ni kwamba alama 16 zinazoonyeshwa katika nyota ya rangi ya njano hutumika kwa ajili ya kuunganisha mitandao ya Tanzania na ile ya kimataifa. Sijui kama mbali kule mnaona, lakini kwenye kitabu ukurasa 157 inaonekana. Alama 72 za daraja la kwanza zinazoonyeshwa kwa rangi nyekundu, alama hizi hutumika kuzalisha alama ya daraja la pili pamoja na kusaidia kuhuisha mifumo ya

upimaji iliyopo sasa ya upimaji ardhi kwenda katika mfumo wa kisasa. Alama 600 ni daraja la tatu na hutumika kwa ajili ya shughuli za kawaida za upimaji wa viwanja na mashamba, barabara na kadhalika. Alama hizi zinaonyeshwa kwa miduara ya rangi ya kijani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kupima kila kipande cha ardhi, katika mwaka wa fedha ujao, tena mapema, Wizara yangu kupitia mradi wa *Private Sector Competitive Project* itanunua vifaa vya kisasa kabisa vyenye ufanisi mkubwa katika upimaji wa ardhi. Vifaa hivyo vimegawanyika katika makundi matatu. Kundi la kwanza ni vifaa 27,000 vitakavyopima moja kwa moja, vifaa hivi vitawekwa kila mkoa na kwenye kanda vitakuwa vinawasiliana moja kwa moja na *satellite* ambapo mpima wa kawaida yeyote awe wa Serikali au mtu binafsi mwenye *GPS* za kisasa anaweza kuvitumia vifaa hivi kwa ajili ya upimaji wa ardhi kwa wigo wa kilometa 30 kutoka kifaa chake kitakapokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya faida ya vifaa hivi ni uwezo wa kuchukua vipimo vya aina nyingi kisayansi ambavyo vinaweza kutumika kwa matumizi ya aina mbalimbali ikiwemo tathmini ya matetemeko ya ardhi, kwa sababu hivi vifaa vinakuwa vimeunganishwa na mitandao; utabiri wa hali ya hewa; mawasiliano ya simu na shughuli za madini. Aidha, ili kuwezesha wataalam wetu kutumia mfumo huu wa kisasa, Wizara yangu itanunua *GPS* za kisasa 54 ambazo zitasambazwa mbili kila mkoa kwa ajili ya kusaidia shughuli za upimaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi la pili vifaa vya kisasa vya upimaji (*RTK GPS*) ambavyo vina uwezo wa kupima katika umbali wa kilometa 15 mpaka 30 kutoka sehemu inayoanzia kipimo yaani *total station* tofauti na vipimo vinavyopima kilometa moja mpaka tatu kama *total station*. Vifaa hivi vinachukua vipimo vya haraka zaidi, sekunde tano hadi dakika mbili ikilinganishwa na vifaa vinavyotumika sasa ambavyo huchukua mpaka nusu saa kuchukua vipimo. Aidha, vifaa hivi vinahitaji watu wawili tu kufanya kazi ya

upimaji ikilinganishwa na vifaa vinavyotumika sasa vinavyohitaji watu zaidi ya watano ili kufanya upimaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika awamu ya kwanza tunanunua vifaa 29 vya aina hii, tumeshatangaza *tenderna supplier* atavileta wakati wowote. Vifaa hivi tutavigawa katika Ofisi zetu za Kanda. Tukimaliza kugawa kwenye awamu hii ya Kanda, Halmashauri zinaweza zikaazima pale, lakini tunaendelea na awamu ya pili ambapo tunanunua vifaa hivi na kuvipeleka kwenye Halmashauri zote Tanzania. Napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Halmashauri ya Ilemela wao wenyewe wamefika mbele kidogo wameshanunua aina ya vifaa hivi *set mbili kwa own source*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na vifaa hivi, tutanunua *total station* 43, *computer* 90 pamoja na *printer* za kisasa 66 ambazo tutazigawa katika kanda na kila mkoa. Jitihada hizi zinalenga kuongeza ufanisi katika kupima na kupanga miji yetu. Tunapeleka hizi *computer* ili kuondoa urasimu wa utengenezaji wa *deed plan*, kwenye hati zenu mtakuta teknolojia ya zamani kuna kipande cha karatasi kama ya bluu hivi ambayo ukipima kiwanja katika kona ya Tanzania kile ki-*deed plan* lazima kitengenezwe Dar es Salaam. Sasa mwaka ujao wa fedha tunanunua hivi vifaa ili kila Halmashauri iwe na uwezo wa kutengeneza *deed plan* pale pale. Hii ni kwa sababu nayo imekuwa inachelewesha upatikanaji wa hati na inaongeza gharama. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa hivi vya *RTK* tutavinunua awamu ya pili kupeleka kila Halmashauri. Tunajua uwezo wa wapima wetu hawajasomea vitu hivi, Wizara itaendesha mafunzo ya kuhakikisha kwamba wapima wote wa wilaya zote wanafundishwa namna ya kutengeneza *deed plan* pale wilayani na namna ya kutumia vifaa hivi vya *RTK* vya kisasa ambavyo tunataka virahishe shughuli za upimaji na kurahisisha upatikanaji wa hati kwa wakati na kupunguza gharama za upimaji. Leo upimaji unafanywa kwa gharama kubwa sana ni kwa sababu ya vifaa na usumbufu mkubwa wa upimaji, unahitaji watu wengi na muda ni mrefu

lakini kwa vifaa hivi, kifaa kimoja kinapimwa na watu wawili na kinapima umbali wa zaidi ya kilometa 30 kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto ya kuandaa ramani (*deed plan*) ambayo katika mwaka huu wa fedha tumeamua sasa zitakuwa zinatayarishwa kwenye Halmashauri na kwenye Kanda badala ya kutayarishwa Wizarani. Msishangae Waheshimiwa Wabunge mtakuta mambo haya ni makubwa yanahitaji mabilioni ya fedha. Mradi wa *ILMIS* na ununuzi wa vifaa vyote hivi na magari haya hamtaona kwenye vitabu hivi, ni mradi unaoendelea, tumeanza nao mwaka juzi na fedha tunazo ndiyo maana tunajitapa hapa kwamba tutafanya. Mnaweza kuona tuna shilingi bilioni 68 lakini fedha za kununua vifaa hivi tunazo zaidi ya shilingi bilioni 15 au 20 ambapo tunaenda kwa awamu kulingana na Sheria ya Manunuzi. Kwa hiyo, fedha ya kufanya haya yote ya ununuzi wa vifaa hivi tunazo tayari ambazo sasa zinasimamiwa na Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya upangaji wa miji na vijiji, mpango kabambe yaani *master plans*; katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara iliahidi kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Mwanza na Arusha kukamilisha mipango kabambe ya majiji haya.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mipango hiyo imekamilika na Mungu akipenda tutaizindua rasmi mwezi Agosti mwaka huu. Aidha, Wizara iliahidi kushirikiana na Jiji la Mbeya, Manispaa ya Moshi, Bukoba, Mpanda, Lindi na Halmashauri ya Mji wa Babati kuandaa mipango kabambe ya miji hiyo. Utayarishaji wa mipango kabambe ya miji hiyo ipo katika hatua mbalimbali za uandaaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wizara iliahidi kuidhinisha mpango kabambe wa Majiji ya Dar es salaam, Mwanza, Arusha, Tanga, Manispaa ya Iringa, Musoma, Tabora, Mtwara, Sumbawanga, Songea, Singida, Tabora pamoja na Miji ya Bariadi, Kibaha na Korogwe. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017 mipango kabambe ya Manispaa za

Musoma na Mtwara imekamilika na imezinduliwa, mipango kabambe iliyobaki iko katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifungua katika kitabu changu hiki Jedwali Na.10 mtakuta Wilaya zenu zote ambazo zinashiriki katika mipango ya *master plan* ziko katika hatua mbalimbali na yote itakamilika katika mwaka huu wa fedha ili kuwezesha sasa miji yetu yote iwe kitovu cha maendeleo, iwe imepangika vizuri, iwe salama na watu sasa waweze kutengeneza mipango ya kina, wapime viwanja, wapange vizuri ili watu waweze kujenga kwenye viwanja vilivyopimwa. Kwa hiyo, mkitaka kujua ni Wilaya gani tutashirikiana kutengeneza *master plan* someni Jedwali Na.10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha ujao, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri husika itakamilisha mipango kabambe ya Majiji ya Dar es Salaam na Tanga, Manispaa ya Singida pamoja na Miji ya Ifakara, Mahenge, Malinyi, Bariadi, Kibaha na Korogwe. Aidha, Wizara itaendelea kupokea na kuidhinisha mipango kabambe kadiri itakavyopokelewa kutoka Mamlaka za Upangaji na sasa mipango hii itaidhinishwa kwenye kanda, haitakuwa na lazima ya kuja Dodoma moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuisitiza kuwa Halmashauri zote nchini zitenge fedha ya kuwezesha kuandaa mipango kabambe ili kuwa na majiji na miji iliyopangwa. Aidha, Halmashauri zihakikishe kuwa uendelezwaji wa mji unazingatia mipango kabambe husika kwa lengo la kuepuka ukuaji holela wa miji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, urasimishaji wa makazi; kwa kushirikiana na Mamlaka ya Upangaji, Serikali itaendelea na awamu ya kurasimisha makazi na kuzuia ujenzi holela. Mwaka huu wa fedha Wizara iliahidi kuendeleza urasimishaji makazi 6,000 katika Kata za Kimara na Salanga kule Dar es Salaam. Aidha, Wizara iliahidi kushirikiana na Halmashauri za Manispaa Sumbawanga, Singida, Musoma, Kigoma Ujiji, Lindi na Tabora kurasimisha makazi 3,000. Pia hadi tarehe 15 Mei, jumla ya makazi 4,333 kati ya 6,000 yalirasimishwa na

uchongaji wa barabara zote umefanyika katika Manispaa ya Ubungo na kazi inaendelea, tutamaliza mapema mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha pia Wizara yangu iliahidi kuendelea kutekeleza programu ya urasimishaji na kugawa miongozo ya urasimishaji 97 ya sekta ya ardhi katika Halmashauri 12 za Mwanza, Musoma, Kigoma Ujji, Tabora, Lindi, Nzega, Singida, Iringa, Mbeya, Tunduma, Sumbawanga na Mtwara. Aidha, michoro ya urasimishaji katika Halmashauri mbalimbali yenye jumla ya vipande vya ardhi 53,764 iliidhinishwa. Pia utafiti wa awali ulifanyika katika Halmashauri sita za Musoma, Kigoma Ujji, Singida, Tabora, Sumbawanga na Lindi umeonyesha maeneo jumla ya makazi 50,200 ambayo maeneo yote haya tutafanya urasimishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Halmashauri waliofanya vizuri katika zoezi la urasimishaji. Najua Wilaya ya Nyamagana wanaendelea vizuri sana, Wilaya ya Ilemela wanaendelea vizuri, Tunduma pale wamechonga mpaka na barabara, Wilaya ya Mtwara, Musoma, Geita na Halmashauri mbalimbali mtaona kwenye kiambatanisho ambao kwa mwaka huu wa fedha watazalisha viwanja zaidi ya 50,000 kwa zoezi la urasimishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, watu ambao walikuwa wanaitwa wamekaa kwenye makazi yasiyo salama yaani *squatter* sasa wanarasimisha wanakaa katika makazi yaliyo rasmi. Hii ni heshima, Watanzania hawa wamewekeza katika maeneo hayo, wanayo haki ya kupata hati kama watu wengine na kupata miundombinu katika maeneo yao. Kwa hiyo, Halmashauri zote Tanzania tunaomba zichukue fursa hii na kurasimisha. Hawana dhambi hawa watu wanaokaa kwenye *squatter* na haikuwa kosa lao, kwa hiyo, Serikali tumeamua kurasimisha ili wapate faida ya rasilimali walizowekeza katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya ujenzi wa viwanda. Katika kushiriki kutimiza azma ya Serikali ya kujenga

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

uchumi wa viwanda, jumla ya hekari 83,080 zimeainishwa katika maeneo ya mipango kabambe katika Halmashuri 14 nchini kwa ajili ya ujenzi wa viwanda, Jedwali Na.12 linaonyesha. Hii ni ongezeko la hekari 19,050 ikilinganishwa na maeneo yaliyoainishwa mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Ujenzi na Uendelezaji Mji wa Kigamboni, kwa Mheshimiwa Dkt. Ndugulile. Pamoja na juhudi zinazofanywa na *KDA* katika kuendeleza Mji wa Kigamboni, kumekuwa na maoni ya baadhi ya wadau wakiongozwa na Mbunge wao Dkt. Ndugulile na Kamati vilevile kwamba majukumu ya *KDA* yatekelezwe sasa na Halmashuri ya Manispaa ya Kigamboni badala ya Wizara ya Ardhi. Hivyo, Serikali inafanyia kazi maoni haya ambayo yameendelea kutolewa vilevile na Kamati yetu ya Ardhi tangu mwaka jana na mwaka huu. Kwa hiyo, Serikali inayafanyia kazi maoni haya ikiwa ni pamoja na kuitisha kikao cha mwisho cha wadau katika mwezi huu ili kuhakikisha kwamba jambo hili linafanikiwa.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Dkt. Ndugulile ikifika wakati wa shilingi usikamate hata senti moja kwa sababu haya ni maoni yako na wadau wengine wa Mkoa wa Dar es Salaam, haya ni maoni yenu tunayafanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 03, mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji. Tumefanya vizuri mwaka uliopita, tumeandaa matumizi ya ardhi ya wilaya tano na vijiji 1,500 kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, Tume imewezesha kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi vijiji 91 katika Wilaya 23. Kazi imefanyika kwa kushirikiana na wadau hao nilikuwa nawataja mwanzo na wanapatikana kwenye kitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2017/2018 Tume itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuongeza kasi ya kupanga matumizi ya ardhi nchini kufikia lengo la vijiji 1,500 na Wilaya tano kwa mwaka. Ili kuweza kufikia lengo hili na kutatua changamoto mbalimbali zinazokabili upangaji, natoa rai kwa sekta binafsi na wadau

mbalimbali wa maendeleo washirikiane na Tume ili kuongeza kasi ya upangaji wa matumizi ya ardhi ya vijiji na wilaya kuondoa migogoro. Aidha, kwa mara nyingine tena nazikumbusha Halmashauri za Wilaya kutenga bajeti yao kwa ajili ya kupanga na kutekeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi ili kupunguza migogoro katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya nyumba. Mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kufuatilia maendeleo ya sekta ya nyumba. Mwamko wa taasisi za fedha kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba umeongezeka mwaka hadi mwaka. Hadi sasa jumla ya benki 28 zimeshatoa mikopo ya nyumba yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 416. Serikali imekuwa ikitoa fedha kupitia Taasisi ya *Tanzania Mortgage Refinancing Company* ili kuziwezesha benki kutoa mikopo ya nyumba kwa wananchi. Hadi sasa zaidi ya wananchi 1,210 wamefaidika na mikopo yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 126.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali kupitia Benki Kuu inatoa mikopo ya nyumba ya taasisi ndogondogo za fedha (*micro financing*) ili zitoe mikopo ya uendelezaji kwa nyumba yenye masharti nafuu kwa wananchi wa kipato cha chini. Hadi sasa wananchi 574 wamefaidika na mikopo hiyo ambayo jumla ni zaidi ya shilingi bilioni tisa. Nawapongeza sana viongozi wa Taasisi ya *TMRC* ambao wako hapa, akina Mgaya na wenzao kwa usimamizi wa kazi hii. Tutaboresha zaidi ili twende kwa kasi. (*Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Mikopo ya Nyumba za Watumishi kwa mwaka huu watumishi 80 wamepatiwa mikopo ya jumla ya shilingi milioni 743. Vilevile katika kipindi hicho, Wizara imekusanya marejesho ya jumla ya shilingi milioni 500.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii vilevile kuwapongeza *Watumishi Housing* kwa hatua waliyochukua ya kushirikiana na Mamlaka ya Elimu kujenga nyumba 240 za walimu katika shule na kata 102 ambazo zimekamilika nyumba 102, katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani, Tanga, Simiyu, Shinyanga, Dodoma, Singida, Morogoro



na Dar es Salaam. *Watumishi Housing* wanafanya kazi nzuri, wamejenga majengo sehemu mbalimbali kama Dar es Salaam, Morogoro na maeneo mengine, ni taasisi iliyoanzishwa juzi juzi kwa hiyo tuiunge mkono iweze kushirikiana vizuri katika kupanga na kujenga majengo haya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika la Nyumba, katika hotuba yangu ya mwaka huu, suala la ujenzi wa nyumba wa gharama nafuu liligusa hisia za Waheshimiwa Wabunge wengi na waliitaka Serikali kuangalia upya suala hili. Wizara yangu imeendelea kuhimiza Shirika la Nyumba kuweka kipaumbele katika ujenzi wa nyumba za gharama nafuu na kuzihamasisha Halmashauri kulipatia shirika ardhi nafuu ya kujenga nyumba hizi. Aidha, taasisi na Halmashauri zimeelekezwa na Serikali kuweka miundombinu ya umeme, maji na barabara katika maeneo yaliyojengwa nyumba za *National Housing* ili kupunguza gharama za ujenzi wa nyumba hizo. Hadi sasa shirika limekamilisha ujenzi wa miradi ya nyumba za gharama nafuu 14 yenye nyumba 492. Aidha, jumla ya miradi 25 yenye jumla ya nyumba 4,129 itaendelea kujengwa. Kati ya hiyo miradi 14 ni ya nyumba za gharama nafuu yenye jumla ya nyumba 1,002.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ili kumwezesha mwananchi wa kawaida asiyemudu gharama za ununuzi wa nyumba kwa mkupuo, Shirika limeweka utaratibu wa mpangaji mnunuzi (*tenant purchase scheme*) ambayo itaanza kutumika kwa nyumba za gharama nafuu. Utaratibu huu unatoa fursa kwa mwananchi kulipa tu asilimia 20 ya bei ya nyumba na kiasi kilichobaki kitalipwa kama kodi ya pango kwa kila mwezi kwa kipindi cha miaka kumi, baada ya miaka kumi ya pango la nyumba kumalizika mwananchi atakabidhiwa hati na funguo na kumilikishwa nyumba hiyo ambayo aliipata kama mpangaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaondoe hofu kwamba endapo mpangaji atafariki akiwa katika zoezi hili, warithi wake wataruhusiwa kuendelea kulipia pango na hatimaye kumilikishwa nyumba hizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa shirika limekamilisha ujenzi wa miradi 29 kati ya 54 iliyokuwa inatekelezwa. Miradi hiyo ni ya nyumba za gharama nafuu, gharama ya kati na majengo ya biashara na ya matumizi mchanganyiko yenye jumla ya nyumba 1,686.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuunga mkono uamuzi wa Serikali wa kuhamishia rasmi Makao Makuu Dodoma, Shirika limetoa kipaumbele katika ujenzi wa nyumba za makazi kwa ajili ya watumishi na wananchi wengine watakaohamia Dodoma. Mwaka huu wa fedha unaoendelea shirika limeendelea kukamilisha nyumba za awamu ya kwanza 300. Aidha, katika mwaka ujao shirika litakwenda awamu ya pili ya ujenzi katika eneo la Iyumbu na kukamilisha utaratibu wa kupata ardhi katika maeneo mengine ya Mji wa Dodoma tukiwa na lengo la kujenga nyumba angalau zisizopungua 1,500 katika Mji wa Dodoma ili kurahisisha wananchi wengi, hata Wabunge, kuweza kumiliki na kupata nyumba hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauzo ya makusanyo ya kodi ya nyumba; hadi tarehe 15 Mei, shirika lilikuwa limekusanya jumla ya shilingi bilioni 39 kutoka kwenye mauzo ya nyumba. Aidha, katika mwaka huu wa fedha, shirika linatarajia kukusanya kodi ya pango kiasi cha shilingi bilioni 86.39.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za kisheria. Wizara yangu imeendelea kusimamia sekta ya ardhi kwa kuzingatia sheria zilizopo. Kwa mwaka 2016/2017, Wizara iliahidi kuandaa mapendekezo ya kutunga/kuhuisha sheria zinazohusu sekta ya ardhi. Kazi hiyo imefanyika katika kipindi hiki na kutunga Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini Na.7 ya 2016 ambayo ilianza kutumika rasmi tarehe 01, Januari baada ya kutangaza kwenye Gazeti la Serikali Namba 01, tarehe 06 Januari, 2017. Aidha, ili kusimamia na kuendeleza sekta ya miliki, kuhuisha utaratibu wa utoaji ardhi na kusimamia mawakala wa ardhi, Wizara yangu imeandaa Rasimu ya Muswada wa Sheria ya Usimamizi na Uendelezaji wa Miliki, Sheria ya Utoaji wa Ardhi na Fidua na Sheria ya Mawakala wa

Ardhi ili kupunguza dhuluma ya mawakala wa ardhi wanaouza nyumba za maskini bila utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Wizara imeandaa Rasimu ya Tafsihi ya Kiswahili ya Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Na. 02 ya Mwaka 2002 ili wananchi wengi waweze kuisoma na kuipitia. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara itakamilisha Rasimu ya Muswada wa Sheria ya Usimamizi na Uendelezaji wa Miliki. Haya yamekuwa maombi ya muda mrefu kwamba tuanzishe chombo kitakachosimamia uendelezaji wa miliki, sasa kinakuja kwa sheria itakayoletwa hapa Bungeni mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekamilisha mapitio ya Sera ya Ardhi ya mwaka 1995 na kuandaa rasimu ya marekebisho yake, tumeshirikiana na wataalam wengi wa ndani. Lengo la maboresho haya ni kuimarisha usalama wa miliki; kuboresha mazingira ya uwekezaji katika sekta ya ardhi; kudhibiti migogoro ya matumizi ya ardhi pamoja na kuhakikisha kwamba kila kipande cha ardhi kinapangwa, kupimwa na kupilikishwa. Sera ni ya mwaka 1995, ndiyo maana tumefanya uhuishaji mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2016/2017 Wizara iliahidi kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2000 na kuandaa Sera ya Nyumba ambayo haikuwepo. Kazi hii inaendelea vizuri na nawaahidi kwamba mwaka huu wa fedha tutakamilisha kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za utawala; Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya utendaji wa kazi kupitia Kituo cha Huduma ya Mteja (*Customer Care Centre*) kilichopo pale Kanda ya Dar es Salaam ilipokuwa Wizara. Kituo kimewezesha kuhudumia wananchi 88,400 ambao ni sawa na wastani wa wateja 2,100 kwa wiki na wateja 442 kwa siku ikilinganishwa na wastani wa 420 kwa siku katika mwaka uliopita. Nawakaribisha wote wenye matatizo ya Dar es Salaam mfike ilipokuwa Wizara pale chini muangalie ile *Customer Care*, pale sasa wananchi wote wanahudumiwa bila mizengwe, bila umaarufu wala bila pesa. Ni kituo

ambacho kinasaidia sana kupunguza migogoro hasa ya Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto na mikakati ya kukabiliana nazo. Mwaka wa fedha 2017/2018, hotuba yangu imeainisha mikakati mbalimbali itakayotekelezwa ili kukabiliana na changamoto ikiwa ni pamoja na kasi ya ongezeko la idadi ya mifugo ikilinganishwa na upatikanaji wa ardhi iliyopangwa na kupimwa. Ili kukabiliana na changamoto hiyo yafuatayo yatafanyika:-

(i) Kuimarisha Ofisi za Kanda kwa kupeleka wataalam wa kada zote na vifaa vya kutosha vikiwemo vifaa vya kisasa vya upimaji na uchapaji wa ramani pamoja na magari ya kisasa ili kuongeza kasi ya kupanga, kupima na kumilikisha kama inavyooneka kwenye kurasa za kitabu.

(ii) Kujenga uwezo wa Idara za Ardhi za Halmashauri kwa kuwapelekea vifaa vya kisasa na mafunzo ya uandaaji wa *deed plan* ili kuharakisha zoezi la upimaji na utoaji wa hati.

(iii) Kupunguza gharama za upatikanaji wa hati kwa kupunguza tozo ya *premium* kutoka asilimia 7.5 hadi 2.5. (*Makofi*)

(iv) Wizara itaangalia pia namna nzuri ya matumizi ya tozo ya *deed plan*, *survey fee* na *application fee* inayotozwa wakati wa umilikishaji ikiwezekana ibaki katika Halmashauri inayomilikisha ili kusaidia kuboresha huduma ya ardhi.

Vilevile *survey fee* ya shilingi 50,000 isitozwe kwa mwananchi ambaye amegharamia mwenyewe upimaji. Hakuna sababu mtu kugharamia upimaji halafu tena mnakuja kumtoa shilingi 50,000. Kwa hiyo, tunatoa Waraka kwa Halmashauri zote zisiendelee kutoza shilingi 50,000 kwa kila hati kama *survey fee* kwa wananchi ambao wamegharamia wenyewe upimaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na mikakati hiyo, najua bado katika miji, hasa maeneo mbalimbali wapo watu wanaojifanya madalali na kuuza nyumba za wananchi wanyonge kwa nguvu za fedha, udanganyifu kwa kutegea siku za sikukuu na siku za mwisho wa wiki, wanauza nyumba za maskini bila kufuata taratibu za mnada na wanawapanga wanunuzi wanaowauzia kwa bei za kidhalimu. Wizara yangu ipo katika mchakato wa kutunga sheria ya kukomesha udhalimu huu, ndiyo maana tunatunga sheria ya kuwaratibu madalali na kutaja sifa zao. Watu wanadhulumiwa sana kwa kivuli cha mahakama, wanatangaza mnada siku ya Ijumaa saa nane, benki inakuja na dalali na dalali anakuja na mnunuzi, watu wamelia sana. Kwa hiyo, mwaka huu Bunge mtatunga sheria hii iwe kiama cha hawa majambazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wale wote wanaoingia katika sekta ya ardhi kwa ajili ya kutakatisha fedha chafu tutawabainisha wote na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria. Nawaonya wale wote mnaopitapita katika kona mbalimbali za nchi na kupora na kuhodhi ardhi vijijini na mijini, mnawanyanyasa wananchi kwa kutumia vibaya sana amri za mahakama, sheria zitazingatiwa, tutawafuata kila kona na kurudisha ardhi kwenye mikono ya Serikali, hasa za vijiji kwa matumizi ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wananchi wachache sana Tanzania hii ambao wanamiliki ardhi kubwa kuliko wengi na kila ardhi nzuri ya Tanzania wanataka wamilikishwe wao. Juzi nimekwenda Lindi nimefuta, kuna mtu mmoja anamiliki hekta 4,000 za *beach* yote ya Mkoa wa Lindi kwa kubadilishana na kujenga *dispensary*. Kwa hiyo, nawaonya watu wote wanaofikiri hatuwajui, hata Dar es Salaam, kuna watu wamehodhi eka 200, 500 hawazitumii na ndiyo maana nimeagiza mwaka huu tutaanza kuwatoza kodi watu wote wanaomiliki ardhi mjini hata kama hawajapima kwa sababu wanaitia hasara Serikali. Hawataki kupima kwa sababu wanajua watalipa kodi ya ardhi kila mwaka na watakapouza watalipa *capital gain*, kwa hiyo, wanaacha bila kupima lakini wanauza vipandevipande. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiwa na ardhi mjini eka 200, 500 hulipii kodi na mjini hakuna mashamba sisi tumesema hiyohiyo tutaorodhesha utalipa kodi yetu, ukitaka ukapime tukupe hati ulipe kodi kihalali, vinginevyo kama unafikiri umekwepa kulipa kodi kwa kutokuipima safari hii itakula kwako, tutaoroshesha tuitambue na tutaifuatilia. Ikikaa zaidi ya miaka sita hujaendeleza tunakunyang'anya hata kama haina hati.

Kwa hiyo, zoezi hili ni jema, kwa sababu kuna watu wamefuga ardhi lakini wanauza kila siku, hawalipi *capital gain* kwa sababu *capital gain* inanza kutathminiwa kwa mtu aliyemilikishwa kwa hati, ukiwa umejamilikisha tu hivihivi hutozwi *capital gain*. Kwa hiyo, hawa wanaiibia Serikali kinyemela ndiyo maana tumesema tutasajili ardhi zote kubwa kubwa wanazomiliki. Kuna watu Kigamboni wa ekari 5,000, 10,000, 30,000 Dar es Salaam za nini, halafu hampimi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumalizia hotuba yangu kwa kuwashukuru kwa dhati wadau wote wa sekta ya ardhi ikiwa ni pamoja na Serikali za Vijiji, Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa za Majiji.

Vilevile napenda kuishukuru Benki ya Dunia, wahisani wote wakiwemo Uingereza, Denmark, Sweden, Japan, China, India, Korea Kusini na Marekani. Wizara yangu inatambua na kuthamini michango inayotolewa na wadau wote wa sekta ya ardhi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana watumishi wote waaminifu wa sekta ya ardhi waliopo kwenye Halmashauri zetu mbalimbali kwa kutekeleza vizuri majukumu yao. Ninyi Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, leo kidogo kwenye sekta ya ardhi kuna nidhamu ukilinganisha na miaka ya nyuma, kwa hiyo, wapo watu wanaojenga nidhamu hii, naomba niwashukuru sana, si wote wabaya. Wale wabaya tutaendelea kushirikiana kuwaainisha ili wawe wazuri wahudumie watu bila kishawishi chochote. (Makofi)

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Kwa mwaka ujao wa 2017/2018 Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri zote kutayarisha mipango ya kuendeleza miji na vijiji, kusimamia upangaji, upimaji, urasimishaji, umilikishaji wa ardhi, usajili wa hati ili kuwezesha kuwepo kwa usalama wa miliki. Natoa rai kwa mamlaka na asasi mbalimbali pamoja na wadau wote wa sekta ya ardhi kutoa ushirikiano ili kuhakikisha kuwa inaziwezesha sekta zote kufikia malengo ya kumletea Mtanzania maendeleo ya kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya mapato, mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara inatarajia kukusanya jumla ya shilingi 112,050,000,000 kutokana na kodi, tozo na ada mbalimbali zinazotokana na shughuli za sekta ya ardhi kwa kutekeleza mikakati ambayo imeainishwa kwenye hotuba yaungo kwenye kitabu hiki ambacho mmpewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu ninayoelezea katika hotuba hii kwa kipindi cha mwaka 2017/2018 sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu Ijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 48, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na Fungu 03, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi kama ifuatavyo:-

(i) Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Mapato ya Serikali shilingi 12,050,000,000; Matumizi ya Kawaida - Matumizi ya Mishahara shilingi 18,484,916,852; Matumizi Mengineyo shilingi 24,770,166,074 na jumla ndogo shilingi 43,255,082,926. Aidha, Matumizi ya Maendeleo - fedha za ndani shilingi 16,400,000,000; fedha za nje shilingi 9,000,000,000 na jumla ndogo shilingi 25,400,000,000 na jumla kuu ni shilingi 68,655,082,926.

(ii) Fungu 03 - Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi - Matumizi ya Mishahara shilingi 1,135,550,000; Matumizi Mengineyo shilingi 979,821,822 na jumla kuu ya fedha zote zilizoombwa katika Fungu 48 na Fungu 03 ni shilingi 70,770,454,748.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba hii, yapo majedwali ambayo yanafafanua kwa kina utekelezaji wa majukumu, randama na pia vimeambatanishwa vitabu viwili ambavyo mtavikuta kwenye *pigeonhole* vya taarifa ya utekelezaji wa majukumu ambavyo ni sehemu ya hotuba yangu. Naomba taarifa hizo zichukuliwe, ikiwa ni vielelezo vya hoja hii. Hotuba hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Wizara kwa anuani ya [www.ardhi.go.tz](http://www.ardhi.go.tz) pamoja na kukumbuka vile vinyonyo nilivyowapa mwaka jana ambavyo vina taarifa zaidi ya 175, mtaendelea kuzitumia kwa miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamaliza hotuba hii, naomba nimshukuru sana mke wangu ambaye mmemuona pale, Germina na watoto wangu ambao wamenijenga muda wote ili kuhakikisha kwamba natekeleza majukumu yangu vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara wote na watumishi wote wa sekta hii waliopo nchi nzima.

Nawashukuru sana ninyi Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano ambao mmenipa kila mara tunapokutana, naomba muendeleo kunipa ushirikiano huu kwa sababu sekta ya ardhi ni ngumu na ni yetu wote. Tutaendeleza kasi ya kutembea zaidi kwenye majimbo yenu mwaka huu ili tushirikiane katika kutatua kero papo kwa papo zinazowakabili wananchi. Tutaendeleza moto wa Wizara yetu wa kuwahudumia na kuhudumia wananchi bila ubaguzi wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaambia tu Waheshimiwa Wabunge, tumehamia Dodoma, ofisi yetu ipo kwenye Jengo la *CAG Office*, ghorofa ya sita. Waheshimiwa Wabunge wote wenye kero mbalimbali wameagizwa na wananchi wao wafike ofisini, tuna uwezo wa kutatua kero nyingi hapahapa, sio lazima sana mshike shilingi hapa lakini tuna uwezo wa kutatua tukitulia. (*Makofi/Kicheko*)



*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia kila la heri Waheshimiwa wote ambao wanaingia kwenye Mfungo wa Ramadhani Jumamosi na naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Jenista Mhagama lakini alikosea mistari miwili hokusoma, kwamba alikuwa anapenda muunge mkono kwamba hata Bunge lenyewe hoja hii iishe mapema ili wananchi waislamu wakajitayarisha, ili wanaofunga wakajitayarisha kwa ajili ya maandalizi ya Mfungo wa Jumamosi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja imeungwa mkono, baada ya hapo narudia tena kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa mambo ya jana, naamini wote mtaniunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI, MHESHIMIWA WILLIAM V. LUKUVI (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18**

**A: UTANGULIZI**

1) ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2016/17 pamoja na ile ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Fungu Na. **48** na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi,

Fungu Na. 3 kwa mwaka wa fedha 2017/18. Vilevile, pamoja na hotuba hii nimewasilisha taarifa ya utekelezaji wa programu na miradi ikijumuisha miradi inayosimamiwa na taasisi, wakala zilizo chini ya Wizara pamoja na taarifa ya urasimishaji wa makazi nchini.

2) **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote naomba kutoa salamu za pole kwako na Bunge lako Tukufu kufuatia kifo cha aliyekuwa Spika wa Bunge la Tisa hayati Samuel John Sitta. Aidha, katika kipindi hiki tumewapoteza wabunge wenzetu wawili ambao ni Mhe. Hafidh Ally Tahir aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani (CCM) pamoja na Mhe. Dkt. Elly Marko Macha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA). Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa familia za marehemu, ndugu na wote walioguswa na misiba hiyo. Vilevile, nitumie fursa hii kuwapa pole Watanzania ambao wamefiwa na wapendwa wao. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amen.

3) **Mheshimiwa Spika**, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki katika Mkutano wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kwa namna ya kipekee naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na viongozi wote wa Serikali kwa mafanikio makubwa yanayoendelea kupatikana katika Serikali ya Awamu ya Tano. Kwa kasi hii tunayokwenda nayo ikichagizwa na kauli mbiu ya "**Hapa Kazi Tu**", nina hakika tutafikia dhamira ya Tanzania ya viwanda. Aidha, nawapongeza kwa dhati Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mhe. Balozi Seif Ali Idd, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mbunge wa Jimbo la Kitope kwa mafanikio makubwa yanayoendelea kupatikana chini ya uongozi wao imara.

4) **Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii pia kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.) kwa jinsi mnavyosimamia shughuli za Bunge hili Tukufu kwa umakini wa hali ya juu. Vilevile, ninawapongeza Wenyeviti wa Bunge lako Tukufu Mhe. Andrew John Chenge (Mb.), Mhe. Najma Murtaza Giga (Mb.) na Mhe. Azzan Mussa Zungu (Mb.) ambao kwa nyakati tofauti wamekuwa wakiongoza shughuli za Bunge kwa ufanisi. Mwenyezi Mungu aendelee kuwaongoza na kuwapa nguvu, afya njema na hekima ili muendelee kutimiza jukumu hili.

5) **Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mhe. Juma Ali Juma kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani. Aidha, ninawapongeza Wabunge wapya walioteuliwa kuingia katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ni Mhe. Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, ambaye pia ameteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria; Mhe. Alhaji Abdallah Majura Bulembo, Mhe. Anne Kilango Malecela, Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mhe. Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare na Mhe. Catherine Nyakao Ruge. Ninawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yenu.

6) **Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia fursa hii kumpongeza Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake ambayo imeelezea utekelezaji wa malengo ya Serikali katika mwaka wa fedha 2016/17 na mwelekeo wa utendaji wa sekta mbalimbali pamoja na kazi za Serikali zitakazotekelezwa katika mwaka wa fedha 2017/18. Wizara yangu itayafanyia kazi yale yote yanayoihusu sekta ya ardhi ili kuhakikisha kwamba malengo ya Serikali ya Awamu ya Tano yanafikiwa.

7) **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee natoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Mhandisi Atashasta Justus Nditiye (Mb.) akisaidiwa na Makamu Mwenyekiti Mhe. Kemirembe Rose

Julius Lwota (Mb.) pamoja na Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano mkubwa na ushauri wao ambao unaiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, nawashukuru kwa uchambuzi makini walioufanya na ushauri walioutoa wakati wa kupitia taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2016/17 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu Na. **48**, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu Na. **03**, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa mwaka wa fedha 2017/18. Ninawashukuru kwa maoni na ushauri waliotoa wakati Kamati ilipotembelea miradi na taasisi zinazosimamiwa na Wizara na kujadili masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya ardhi. Ushauri wao utaendelea kuzingatwa wakati wote wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu.

8) ***Mheshimiwa Spika***, ntoa shukrani za pekee kwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhe. Dkt. Angeline Sylvester Lubala Mabula (Mb.) kwa ushirikiano mkubwa na ushauri anaonipa wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yangu. Pia, ninawashukuru Katibu Mkuu Dkt. Yamungu Kayandabila; Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Moses Kusiluka; Wakuu wa Idara na Vitengo, Shirika la Nyumba la Taifa, Wakala na Taasisi zilizo chini ya Wizara yangu pamoja na watumishi wote wa sekta ya ardhi katika ngazi zote kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao. **Nawakumbusha watumishi wote wa sekta ya ardhi nchini kutimiza majukumu yao kwa weledi na kwa kuzingatia sera, sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo na itakayokuwa inatolewa ili kuboresha utoaji wa huduma za sekta ya ardhi.**

9) ***Mheshimiwa Spika***, baada ya maelezo ya utangulizi, naomba sasa nieleze kwa kifupi utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/17, na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/18. Takwimu za taarifa ya utekelezaji wa bajeti zilizopo katika hotuba hii zinaishia tarehe 15 Mei, 2017.

**B: MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2016/17 NA MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2017/18**

10) *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza majukumu, Wizara imeendelea kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa II wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17- 2020/21); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020; Mpango Mkakati wa Wizara (2012/13-2016/17); Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995; Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 pamoja na miongozo mbalimbali ya Serikali.

**Mapato na Matumizi ya Fedha: Fungu 48 (Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi)**

**Ukusanyaji wa Mapato**

11) *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara ilipanga kukusanya Shilingi bilioni **111.77** kutokana na vyanzo vya mapato yanayotokana na kodi, ada na tozo mbalimbali za ardhi. Hadi tarehe 15 Mei, 2017, Wizara ilikuwa imekusanya Shilingi bilioni **80.52** sawa na asilimia **72** ya lengo. Aidha, katika mwaka wa fedha 2015/16 Wizara ilikusanya Shilingi bilioni **74.71**, sawa na asilimia **107** ya lengo la kukusanya Shilingi bilioni **70.00**. Ni matarajio yetu kwamba hadi kufikia Juni 2017, lengo la kukusanya Shilingi bilioni **111.77** litafikiwa kwa kutekeleza mpango mkakati wa Wizara. **Jedwali Na. 1** linaonesha hali ya makusanyo. **Nachukua fursa hii kuwapongeza wamiliki wa ardhi waliolipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati. Aidha, nawataka wamiliki wa ardhi wote ambao hawajalipa kodi hiyo wahakikishe wanalipa kabla ya tarehe 30 Juni, 2017. Serikali itaendelea kuwachukulia hatua kali wamiliki wote ambao hawalipi kodi kwa wakati ikiwa ni pamoja na kuwafutia miliki, kuwafikisha mahakamani, na kukamata na kuuza mali zao.**

12) *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2016/17 Wizara iliahidi kuhuisha viwango vya kodi ya ardhi kwa mashamba ya biashara yaliyoko nje ya miji yaliyomilikishwa chini ya Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999.

Baada ya kupitia viwango hivyo, Serikali inakusudia kuongeza viwango vya pango la ardhi kutoka Shilingi **400/=** hadi Shilingi **800/=** kwa ekari kwa mwaka kuanzia Julai, 2017 kwa mashamba ya biashara yaliyopimwa na kumilikishwa nje ya miji. Kiwango kinachotozwa sasa cha Shilingi **400/=** kwa ekari moja bado ni kidogo sana ikilinganishwa na thamani pamoja na uwezo wa uzalishaji wa ardhi husika.

13) ***Mheshimiwa Spika***, ili kuwawezesha wananchi wengi kumiliki maeneo yao kwa gharama nafuu pamoja na kupanua wigo wa walipaji wa kodi ya pango la ardhi, Serikali inatarajia kupunguza tozo ya mbele (*premium*) kutoka asilimia **7.5** hadi asilimia **2.5** ya thamani ya ardhi kuanzia Julai, 2017. Ada hii hutozwa mara moja tu wakati wa umilikishaji ardhi kwa mujibu wa fungu la 31 la Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999. Kupunguzwa kwa kiwango cha tozo ya mbele kutavutia wananchi wenye maeneo ya ardhi kujitokeza kwa wingi zaidi kupimiwa na kumilikishwa ardhi yao. **Natoa rai kwa wananchi wote kutumia fursa hii ya punguzo la tozo ya mbele kupima na kumilikishwa maeneo yao na kulipa kodi.**

14) ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara inatarajia kukusanya Shilingi bilioni **112.05** kutokana na shughuli za sekta ya ardhi. Mapato hayo yatatokana na vyanzo mbalimbali vya kodi ya pango la ardhi, ada na tozo mbalimbali za ardhi. Lengo hili litafikiwa kwa kutekeleza mikakati ifuatayo:-

i) Kuongeza kasi ya kurasimisha maeneo yasiyopangwa mijini;

ii) Kuimarisha mifumo iliyopo ya utunzaji wa kumbukumbu za ardhi;

iii) Kuendelea kupima maeneo mapya pamoja na kukamilisha upimaji na umilikishaji wa viwanja katika maeneo ambayo upimaji wake haujakamilika;

iv) Kuhimiza wamiliki wote wa ardhi nchini kulipa kodi ya ardhi kwa mujibu wa sheria na kuwachukulia hatua wadaiwa sugu ikiwemo kuwafikisha mahakamani;

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

v) Kushirikisha sekta binafsi katika upangaji na upimaji wa ardhi ili kuongeza idadi ya viwanja na hivyo kuongeza wigo wa mapato;

vi) Kuanza kutoza kodi ya pango la ardhi kwenye maeneo ambayo hayajapimwa mijini; na

vii) Kurahisisha ulipaji wa kodi ya pango la ardhi kwa kuwawezesha wananchi kufanya

i) malipo kwa kutumia mitandao ya simu na kuongeza idadi ya benki za kukusanya kodi.

### Matumizi

15) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni **70.49** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni **16.34** zilitengwa kwa ajili ya mishahara; shilingi bilioni **28.85** kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni **25.30** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017, Wizara ilikuwa imepokea na kutumia jumla ya shilingi bilioni **34.95** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo, sawa na asilimia **50** ya lengo la mwaka. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni **13.21** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ambapo shilingi bilioni **2.28** zilitolewa kwa halmashauri mbalimbali kwa ajili ya kuendeleza shughuli za sekta ya ardhi, shilingi bilioni **14.11** ni fedha za mishahara na shilingi bilioni **7.63** ni fedha za miradi ya maendeleo (**Jedwali Na. 2**).

### Mapato na Matumizi ya Fedha: Fungu 03 (Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi)

#### Ukusanyaji wa Mapato

16) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Tume ilikuwa na lengo la kukusanya shilingi milioni **775.25** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali ambavyo ni: kodi ya pango la nyumba za Tabora na mauzo ya nyaraka za

zabuni. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017, Tume ilikuwa imekusanya shilingi milioni **531.66** sawa na asilimia **69** ya lengo.

## Matumizi

17) *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2016/17, Tume iliidhinishiwa Shilingi bilioni **1.75** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi milioni **845.28** zilitengwa kwa ajili ya mishahara na Shilingi milioni **901.62** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017, Tume ilipokea jumla ya Shilingi bilioni **1.16** sawa na asilimia **66** ya fedha iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi milioni **494.04** ni matumizi mengineyo sawa na asilimia **55** ya fedha zilizoidhinishwa na Shilingi milioni **665.47** ni fedha za mishahara.

## HUDUMA ZA MAENDELEO YA ARDHI

18) *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara yangu iliendelea kutoa huduma za ardhi kwa wananchi. Huduma hizo ni pamoja na utoaji wa hatimiliki za ardhi; hati za hakimiliki za kimila; uthamini; usajili wa hati, nyaraka na miamala ya ardhi; kushughulikia migogoro ya ardhi kiutawala na uhakiki wa milki. Pamoja na shughuli hizi, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri nchini imeendelea kuhimiza wananchi kuzingatia masharti ya umiliki wa ardhi na kuchukua hatua dhidi ya ukiukwaji wa masharti hayo, mathalan; kutoendeleza ardhi, kuendeleza ardhi kinyume na masharti na kutolipa kodi ya pango la ardhi. Aidha, Wizara iliendelea kuimarisha kumbukumbu za ardhi na kutoa ushauri kuhusu masuala mbalimbali ya ardhi nchini.

### Usimamizi wa Ardhi

19) *Mheshimiwa Spika*, usimamizi wa ardhi nchini ni suala mtambuka kwa kuwa linahusisha mamlaka mbalimbali zikiwemo Halmashauri za Vijiji, Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa, Majiji na Wizara yangu. Pamoja na uwepo wa mamlaka hizi, Wizara imeendelea kupokea hoja na malalamiko mbalimbali yanayohusiana na ardhi kutoka kwa wananchi ambayo kimsingi yangeweza kushughulikiwa



katika ngazi za vijiji au halmashauri husika. **Napenda kuwakumbusha wananchi kutumia ofisi za Halmashauri kwa ajili ya kutatua kero zao kabla ya kuwasilisha kero hizo katika ngazi ya Wizara.**

### **Kuimarisha Huduma katika Ofisi za Ardhi za Kanda**

20) **Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha utoaji huduma, Wizara imeendelea kuimarisha Ofisi za Ardhi za Kanda kwa kupeleka wataalam wa kada mbalimbali. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017, Wizara imepeleka watumishi wa kada ya wapima ardhi na wasajili katika ofisi ya kanda ya Ziwa (Mwanza), kanda ya Kusini (Mtwara) na Kanda ya Magharibi (Tabora). Aidha, vitendea kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na magari mapya nane (8) vimepelekwa katika kanda zote nane (8). Katika mwaka wa fedha 2017/18, watumishi wa kada ya maafisa ardhi, wasajili wa hati, wathamini, wapima ardhi na maafisa mipangomiji watapelekwa katika ofisi za kanda zote. Lengo la hatua hii ni kuwawezesha wananchi kupata huduma mbalimbali za ardhi katika kanda badala ya kuzifuata huduma hizo Makao Makuu ya Wizara.

21) **Mheshimiwa Spika**, katika kusogeza huduma za ardhi karibu zaidi na wananchi, Wizara vilevile imeboresha muundo wa ofisi za kanda kwa kuanzisha kanda mpya ya Simiyu, kupunguza na kuongeza mikoa katika baadhi ya kanda. Kuanzia Julai, 2017 Ofisi za Ardhi za Kanda zitakuwa zikihudumia mikoa kama ifuatavyo; **Kanda ya Dar es Salaam** (Dar es Salaam) itahudumia mikoa ya Dar es Salaam na Pwani; **Kanda ya Nyanda za Juu Kusini** (Mbeya) itahudumia mikoa ya Mbeya, Njombe, Rukwa na Songwe; **Kanda ya Kati** (Dodoma) itahudumia mikoa ya Dodoma, Singida, Iringa na Morogoro; **Kanda ya Kaskazini** (Arusha) itahudumia mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Manyara; **Kanda ya Ziwa** (Mwanza) itahudumia mikoa ya Mwanza, Geita na Kagera; **Kanda ya Magharibi** (Tabora) itahudumia mikoa ya Tabora, Kigoma na Katavi; **Kanda ya Kusini** (Mtwara) itahudumia mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma na **Kanda ya Simiyu**

(Bariadi) itakayohudumia mikoa ya Simiyu, Shinyanga na Mara.

### **Kuvunjwa kwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (CDA)**

22) **Mheshimiwa Spika**, kufuatia uamuzi wa Serikali wa kuvunja CDA, kufutwa kwa hatimiliki ya ardhi ya CDA na kuhamishia shughuli zake katika Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma, kuanzia sasa wananchi watamilikishwa ardhi kwa kupewa hatimiliki za muda wa miaka 99. Wamiliki waliokuwa na mikataba ya pango la ardhi (*ground lease*) iliyotolewa na CDA watahakikiwa na kumilikishwa upya kwa kupewa hatimiliki ya miaka 99 bila kulipa tena gharama za umilikishaji. Hata hivyo, kabla ya kumilikishwa watapaswa kulipa malimbikizo ya kodi ya pango la ardhi. Aidha, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa haki za wananchi na taasisi za fedha zinazohusiana na mikataba ya pango iliyotumika kama dhamana kupata mikopo na miamala mingine iliyokuwa haijakamilika hazitaathirika na mabadiliko haya.

23) **Mheshimiwa Spika**, kuanzia sasa wananchi wote wanaohitaji huduma za ardhi watapata huduma hizo kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma na hati zitatolewa na Ofisi ya Kanda ya Kati. Kufuatia kuongezeka kwa majukumu katika kanda hiyo, Wizara itaongeza vitendea kazi na wataalam wa kada ya maafisa ardhi, wasajili wa hati, wathamini, wapima ardhi na maafisa mipangomiji.

### **Utoaji Milki za Ardhi**

24) **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri na sekta binafsi imeendelea kuhakikisha kuwa kila kipande cha ardhi nchini kinapangwa, kupimwa na kumilikishwa. Halmashauri mbalimbali kwa kushirikiana na sekta binafsi zimekamilisha miradi ya upimaji wa viwanja katika miji mbalimbali nchini (**Jedwali Na. 3**). Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara yangu itaendelea kuhimiza ushiriki wa sekta binafsi katika kupanga na kupima ardhi ili kuongeza kasi ya utoaji wa milki za ardhi nchini. Ushiriki

wa sekta binafsi utaongeza fursa za ajira, kuongeza mapato ya Serikali yatokanayo na kodi ya pango la ardhi na kukuza pato la Taifa.

25) **Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa Sera na Sheria za Ardhi, Wizara inaratibu utoaji wa vyeti vya ardhi ya vijiji, hati za hakimiliki za kimila, hatimiliki za ardhi, kutoa elimu kwa wananchi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali na kutatua migogoro kwa njia za kiutawala. Katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara iliahidi kuandaa hatimiliki za ardhi **400,000** na kutoa hati za hakimiliki za kimila **57,000**. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017 Wizara imetoa hatimiliki za ardhi **33,979** na imeratibu uandaaji wa hati za hakimiliki za kimila **35,002**. Aidha, Wizara imeandaa vyeti vya ardhi ya kijiji **505 (Jedwali Na. 4)**. Napenda kutambua ushiriki wa wadau mbalimbali kwa mchango wao katika kuwezesha utoaji wa vyeti vya ardhi ya kijiji na hati za hakimiliki za kimila. Baadhi ya wadau hao ni; MKURABITA, USAID, DFID, DANIDA na SIDA. Wengine ni *Oxfam International Tanzania, Care International Tanzania, Ujamaa Community Resource Team, African Wildlife Foundation, Eco Village Adaptation to Climate Change in Central Tanzania, Tanzania Natural Resource Forum, SNV Netherlands Development Organization* na HakiArdhi.

26) **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri nchini itaandaa hatimiliki za ardhi **400,000**, vyeti vya ardhi ya vijiji **1,000** na kutoa hati za hakimiliki za kimila **57,000**. Aidha, ili kuwawezesha wananchi wengi kupata hatimiliki za ardhi, Wizara inakusudia kupunguza tozo ya mbele ambayo hutozwa wakati wa kumilikisha ardhi kutoka asilimia **7.5** mpaka asilimia **2.5** ya thamani ya ardhi. **Natoa rai kwa Halmashauri zote nchini kuhakikisha kuwa zinamilikisha viwanja vyote vilivyopimwa na kuandaa Hati ili wananchi waweze kuwa na miliki salama.**

### **Kamati za Ugawaji Ardhi**

27) **Mheshimiwa Spika**, Wizara inalo jukumu la kuteua wajumbe wa Kamati za Ugawaji Ardhi katika

Halmashauri baada ya kupokea mapendekezo kutoka katika halmashauri husika. Kamati hizi ni muhimu katika kusimamia ugawaji wa ardhi nchini ili kuepuka ugawaji ardhi usiozingatia sheria ambao wakati mwingine husababisha migogoro ya ardhi. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara yangu imeidhinisha uteuzi wa Kamati za Kugawa Ardhi katika Halmashauri **19**. Halmashauri zilizohusika katika uteuzi ni Jiji la Arusha, Manispaa ya Moshi, Manispaa ya Tabora, Manispaa ya Kigoma, Mji wa Ifakara, Wilaya ya Arusha, Simanjiro, Kongwa, Mpanda, Kasulu, Mwanaga, Siha, Chalinze, Mafia, Mkalama, Urambo, Bunda, Buhigwe na Itigi. Uteuzi huu umefanya jumla ya Halmashauri **102** kuwa na Kamati za Kugawa Ardhi, kati ya Halmashauri 184 zinazotakiwa kuwa na kamati hizo (**Jedwali Na. 5**). **Nazikumbusha Halmashauri ambazo bado hazina Kamati za Ugawaji wa Ardhi kuwasilisha mapendekezo ya wajumbe wa Kamati hizi kwa ajili ya uteuzi.**

28) ***Mheshimiwa Spika***, Wizara yangu pia inasimamia shughuli za Kamati ya Taifa ya Ugawaji Ardhi ambayo, pamoja na majukumu mengine, huidhinisha maombi ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji. Katika mwaka wa fedha 2016/17, Kamati hii ilipitia maombi **46** na kuidhinisha ugawaji wa viwanja **40** na mashamba **6** ya uwekezaji kwa ajili ya matumizi ya kilimo, biashara, hoteli, makazi ya zaidi ya familia moja na viwanda (**Jedwali Na. 6**). **Natoa rai kwa Halmashauri zote nchini zishirikiane na Kituo cha Uwekezaji Tanzania ili kuharakisha maombi ya wawekezaji. Uhakiki wa Viwanja na Mashamba**

29) ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara iliendelea kuhakiki viwanja na mashamba nchini ili kubaini ukiukwaji wa masharti ya umiliki. Kutokana na uhakiki uliofanyika, Wizara imechukua hatua ya kubatilisha milki za viwanja **227** na mashamba **17** kutokana na ukiukwaji wa masharti. Viwanja na mashamba haya yapo katika mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, Iringa, Kagera na Morogoro.

30) **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara imeshughulikia maombi ya kuhawilisha mashamba yenye ukubwa wa jumla ya hekta **25,259** yaliyopo katika wilaya ya Rufiji mkoani Pwani ili kuwezesha uwekezaji wa kilimo cha miwa kwa ajili ya uzalishaji wa sukari. Ardhi ya mashamba yaliyobatiliswa na yaliyohawilishwa itasaidia kupatikana kwa ardhi ya kutosha kwa ajili ya uwekezaji mkubwa utakaowezesha uzalishaji wa malighafi za viwanda. Aidha, Wizara yangu imepanga na kupima ardhi yenye ukubwa wa hekta **433** katika eneo la Pembamnazi lililopo Manispaa ya Kigamboni kwa ajili ya matumizi ya viwanda. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara yangu itaendelea kuongeza hazina ya ardhi kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo uwekezaji mkubwa katika sekta ya viwanda ili kufanikisha azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuwa na Tanzania ya viwanda.

### Usimamizi wa Ardhi ya Uwekezaji

31) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara iliahidi kufuatilia uwekezaji na uendelezaji wa mashamba na viwanja na kuweka taarifa hizo kwenye kanzidata. Hatua hii inalenga kuwa na kumbukumbu sahihi za ardhi ya uwekezaji iliyoendelezwa na kubaini iwapo inatumika kwa malengo yaliyokusudiwa. Mpaka sasa Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri imefanya ukaguzi wa mashamba ya uwekezaji **121** yenye ukubwa wa ekari **552,139.21** yaliyopo katika mkoa ya Tanga, Morogoro, Pwani, Njombe na Kagera na kuingiza taarifa zake katika kanzidata ya Wizara. Kati ya mashamba haya, **63** yameendelezwa na **58** yametelekezwa. Kwa mashamba ambayo hayajaendelezwa, hatua za kisheria zinaendelea kuchukuliwa. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu itafanya uhakiki wa mashamba ya uwekezaji nchini.

### Utatuzi na Udhhibiti wa Migogoro ya Matumizi ya Ardhi

32) **Mheshimiwa Spika**, katika Hotuba ya bajeti ya Wizara ya mwaka wa fedha 2016/17 suala la migogoro ya

ardhi liligusa hisia za Waheshimiwa Wabunge wengi na waliitaka Serikali kuwa na mkakati maalum wa kushughulikia suala hili. Kwa kutambua kuwa migogoro ya matumizi ya ardhi ni suala mtambuka, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Takwimu iliunda kamati ya kisekta ili kubaini aina na vyanzo vya migogoro na kupendekeza namna bora ya kutatua migogoro hiyo. Baada ya kupokea taarifa ya kamati, Serikali inafanya uchambuzi utakaowezesha kuchukua hatua ili kutatua migogoro hiyo. Aidha, migogoro mingine ilitatuliwa kupitia mikutano niliyofanya na wananchi katika ziara nilizofanya sehemu mbalimbali nchini. Kadhalika migogoro mingine ilitatuliwa kwa kushughulikia malalamiko yaliyowasilishwa Wizarani na kwenye ofisi za kanda.

### **Mfuko wa Fidia ya Ardhi**

33) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, nililiarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara inakamilisha uundaji wa Bodi ya Mfuko wa Fidia kwa mujibu wa Kifungu Na. 173 cha Sheria ya Ardhi (Sura 113) na Kanuni zinazosimamia Mfuko wa Fidia za mwaka 2001. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Bodi hii imeshaundwa rasmi baada ya Mwenyekiti na wajumbe wake kuteuliwa. Bodi ya Mfuko wa Fidia itaratibu shughuli zote za ulipaji wa fidia nchini zitakazofanywa na Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea, Wakala, Mikoa na Halmashauri ili kuondoa kero kwa wananchi ikiwemo kuchelewa kulipwa fidia, kupunjwa au kutolipwa fidia. Wizara yangu itaandaa na kusambaza mwongozo wa namna ya shughuli za mfuko wa fidia zitakavyofanyika.

### **Programu ya Kuwezesha Umilikishaji Ardhi**

34) **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inaendelea na utekelezaji wa Programu ya Kuwezesha Umilikishaji Ardhi (**Land Tenure Support Programme**) katika Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi mkoani Morogoro chini ya ufadhili wa Serikali ya nchi za Uingereza, Sweden na Denmark kupitia

Mashirika yao ya Maendeleo ya DFID, SIDA na DANIDA. Katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara yangu iliahidi kuandaa Hati za Hakimiliki za Kimila **50,000** katika vijiji **40** vya eneo la mradi na kujenga masjala za ardhi katika vijiji hivyo. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017 Hati za Hakimiliki za Kimila **11,403** zimeandaliwa katika vijiji **7** vya Wilaya za Kilombero (hati **8,303** katika vijiji **4**) na Ulanga (hati **3,100** katika vijiji **3**).

35) **Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa Programu hii Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji **18** imeandaliwa katika Wilaya za Kilombero (**8**) na Ulanga (**10**). Aidha, alama za msingi za upimaji (*control points*) **54** zimesimikwa ili kuwezesha upimaji wa mipaka ya vijiji na hatimaye vipande vya ardhi ambavyo vitaandaliwa hati za hakimiliki za kimila. Alama hizo zimesimikwa katika Wilaya za Ulanga (**16**), Kilombero (**26**), Malinyi (**10**) na Mufindi (**2**). Vilevile, mipaka ya vijiji **52** imepimwa katika wilaya za Kilombero (**30**), Ulanga (**19**) na Malinyi (**3**). Kutokana na upimaji huo jumla ya vyeti vya ardhi ya vijiji **45** vimeandaliwa na kutolewa. Vilevile, ili kuwa na mazingira bora ya kuhifadhi kumbukumbu za ardhi, Wizara imehamasisha ujenzi na ukarabati wa masjala za ardhi na ofisi za vijiji katika vijiji **61** katika wilaya za Kilombero (vijiji **28**), Ulanga (vijiji **18**) na Malinyi (vijiji **15**).

36) **Mheshimiwa Spika**, ili matokeo ya utekelezaji wa Programu yawe endelevu hususan baada ya Programu kukamilika katika Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi, Wizara imekuwa ikishirikiana kikamilifu na Halmashauri za Wilaya tajwa pamoja na vijiji katika utekelezaji wa Programu. Aidha, wataalam wa Halmashauri za Wilaya pamoja na Kamati za Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi ya Kijiji na Kamati za Uhakiki za Vijiji wamejengewa uwezo katika kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji na kupima vipande vya ardhi ili kutoa Hati za Hakimiliki za Kimila.

37) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara kupitia Programu ya Kuwezesha Umilikishaji Ardhi imepanga kufanya uhakiki wa vipande vya ardhi **80,000** na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **37**; kujenga

ofisi za ardhi katika wilaya za Kilombero (1), Ulanga (1) na Malinyi (1); na kuandaa vyeti vya ardhi vya vijiji 15 katika wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi.

### Usajili wa Hati Miliki na Nyaraka za Kisheria

38) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17 Wizara yangu ilipanga kusajili Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria **450,500** kati ya hizo **400,000** ni Hatimiliki, **2,500** Hati za kumiliki sehemu ya jengo na Nyaraka za Kisheria **48,000**. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017 Hatimiliki pamoja na Nyaraka za Kisheria **79,117** zimesajiliwa. Kati ya hizo Hatimiliki ni **32,178** na nyaraka nyingine za kisheria **46,939**. Nyaraka **29,304** zimesajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Ardhi (Sura 334) na Hati za Umiliki wa Sehemu ya Jengo **1,343** zimesajiliwa chini ya Sheria ya Umiliki wa Sehemu ya Jengo (Sura 416) (**Jedwali 7A**). Aidha, Nyaraka za Kisheria zipatazo **16,975** zimesajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka (Sura 117) (**Jedwali 7B**) na nyaraka **660** zilisajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Rehani ya Mali zinazohamishika (Sura 210) (**Jedwali 7C**).

39) **Mheshimiwa Spika**, wananchi wanahamasishwa kupima maeneo yao na kupata hatimiliki. Hati hizi zina umuhimu mkubwa ikiwemo kuwahakikishia usalama wa miliki zao na pia zinaweza kutumika kama dhamana za mikopo katika taasisi za fedha. **Ninawahimiza wananchi kufanya uhakiki kwenye Ofisi ya Msajili wa Hati kila wanapokusudia kufanya miamala inayohusu ardhi ili kuepuka utapeli.**

40) **Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii kuwahamasisha wananchi kuona umuhimu wa kusajili nyaraka mbalimbali za kisheria kama vile nyaraka zinazotoa mamlaka, mabadiliko ya majina, wosia na mikataba ya mikopo. Nyaraka hizi husajiliwa katika Ofisi za Msajili wa Hati kwenye kanda husika. Hatua hii itasaidia kuhakikisha usalama wa nyaraka hizo na kurahisisha upatikanaji wa nyaraka husika pindi zinapohitajika kwa matumizi mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara inakusudia kusajili hatimiliki na nyaraka za kisheria **453,000**. Kati ya hizi, hati za kumiliki ardhi



ni **400,000**, hati za kumiliki sehemu ya jengo **3,000** na nyaraka za kisheria **50,000**.

### **Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)**

41) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Serikali iliahidi kuanza ujenzi wa Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi (*Integrated Land Management Information System-ILMIS*). Katika kutekeleza ahadi hii, Serikali imeingia mkataba na mkandarasi (IGN FI) wa kujenga Mfumo huo. Mkataba huo ulisainiwa tarehe 5 Julai, 2016. Kazi ya ujenzi wa Mfumo ilizinduliwa rasmi tarehe 26 Agosti, 2016 na mkandarasi tayari ameanza kazi. Sambamba na ujenzi wa mfumo huu, Serikali imekamilisha ukarabati wa jengo la Kituo cha Taifa cha Taarifa za Ardhi (NLIC) na ufungaji wa baadhi ya vifaa umekamilika. Kukamilika kwa mradi huu kutaboresha utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka za ardhi, kurahisisha utendaji kazi, kuharakisha huduma za utoaji wa milki na kuongeza mapato ya Serikali. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara itaanza kutoa hati za kielektroniki katika Manispaa za Kinondoni na Ubungo.

42) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara iliahidi kukamilisha usimikaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Kuhifadhi Kumbukumbu na Kukadiria Kodi ya Ardhi (*Land Rent Management System-LRMS*) katika Halmashauri 17 zilizobaki kati ya 184. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kazi hii imekamilika katika Halmashauri 10 na inaendelea katika Halmashauri saba (7) zilizobaki ambazo ni Buhigwe, Nanyamba, Momba, Madaba, Mbogwe, Buchosa na Mpimbwe. Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara itaendelea kuboresha Mfumo wa Ukusanyaji wa Kodi ya Pango la Ardhi ili uweze kuongeza ufanisi katika makusanyo ya kodi, umilikishaji ardhi na usajili wa hati.

### **Uthamini wa Mali**

43) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara iliahidi kuandaa na kuidhinisha taarifa **32,500**

za uthamini wa kawaida na fidia kwa matumizi mbalimbali. Hadi tarehe 15 Mei, 2017 Wizara iliidhinisha taarifa za uthamini **8,725** ambapo taarifa **97** ni uthamini wa fidia na **8,628** ni uthamini wa mali kwa madhumuni mbalimbali kama vile rehani, dhamana mahakamani, bima, mirathi na mgawanyo wa mali kwa wanandoa (**Jedwali Na. 8A & 8B**). Taarifa hizi ni kwa ajili ya matumizi ya utozaji ada na ushuru wa Serikali unaotokana na uthamini. Aidha, Wizara ilishiriki kufanya uthamini wa fidia katika baadhi ya miradi ya kitaifa ikiwemo upanuzi wa viwanja vya ndege Dodoma, Kigoma na Chato; upanuzi wa eneo la Ikulu - Chamwino na utwaaji wa eneo la mradi wa gesi asilia eneo la Likong'o mkoani Lindi. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara inatarajia kuandaa na kuidhinisha taarifa **35,000** za uthamini. **Napenda kuutarifu umma wa Watanzania kwamba, kufuatia kuanza kutumika kwa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini Na. 7 ya mwaka 2016, taarifa zote za uthamini zinapaswa kuidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali.**

### **Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya**

44) *Mheshimiwa Spika*, Wizara yangu kwa mujibu wa Sheria ya Mahakama za Ardhi Na.2 ya mwaka 2002 ina jukumu la kuanzisha na kusimamia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwa lengo la kupokea, kusikiliza na kutatua migogoro ya ardhi nchini. Katika mwaka wa fedha 2016/17 Wizara yangu imefungua Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya katika wilaya za Kilindi, Lushoto na Kiteto hivyo kufanya jumla ya mabaraza yanayofanya kazi kuwa **53** kwa nchi nzima. Katika mwaka wa fedha 2016/17 Wizara iliahidi kushughulikia mashauri **13,590** yaliyokuwepo na ambayo yangefunguliwa. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017 jumla ya mashauri **40,135** yalishughulikiwa ambapo kati ya hayo mashauri **18,571** yaliyamuliwa (**Jedwali Na.9**). Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara itaendelea kushughulikia mashauri yaliyobaki na yatakayofunguliwa.

45) *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2016/17 Wizara iliahidi kuendelea kuboresha utendaji kazi wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwa kuongeza

idadi ya ofisi za Mabaraza na kuyapatia vitendea kazi muhimu. Aidha, Wizara iliahidi kuanzisha Mabaraza mapya katika Wilaya tano (5) ambazo ni Lushoto, Bagamoyo, Kiteto, Kasulu na Kibondo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Mabaraza ya Wilaya za Kilindi, Kiteto na Lushoto tayari yameanza kufanya kazi. Kwa Mabaraza ya Bagamoyo, Kasulu na Kibondo majengo yalikuwepo, tathmini ya gharama za ukarabati zimeshafanyika na ukarabati ukikamilika mabaraza hayo yataanza kufanya kazi. Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara yangu inatarajia kuzindua Mabaraza ya Wilaya za Kongwa, Mwapwa na Urambo. Hadi sasa Mabaraza **39** bado hayajazinduliwa kutokana na ukosefu wa majengo na samani. **Natoa wito kwa Halmashauri za Wilaya kutoa majengo yanayoweza kutumika kwa shughuli za Mabaraza bila kuhitaji gharama kubwa za ukarabati.**

## HUDUMA ZA UPIMAJI NA RAMANI

### Huduma za Ramani

46) **Mheshimiwa Spika**, mojawapo ya majukumu ya Wizara yangu ni kutayarisha ramani za msingi ambazo ni chanzo muhimu cha taarifa zinazohitajika katika kubuni na kutayarisha mipango ya maendeleo kwa sekta mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara iliahidi kuendelea kuhakiki na kuandaa ramani za mipaka ya wilaya mpya kwa mujibu wa Matangazo ya Serikali yaliyoanzisha wilaya hizo. Wizara imekamilisha uhakiki na uandaaji wa ramani za wilaya mpya tano (5) ambazo ni Nyang'hwale, Geita, Bukombe, Mbogwe na Chato. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara itahuisha ramani za msingi za uwiano wa 1:50,000 kwenye miji 50.

47) **Mheshimiwa Spika**, Wizara imebaini kuwepo kwa baadhi ya taasisi binafsi zinazojihusisha na uandaaji wa ramani na kuziua bila idhini ya Wizara yangu, jambo ambalo ni kosa kisheria. Baadhi ya ramani hizi hazitoi tafsiri sahihi ya mipaka na hasa mipaka ya nchi yetu na nchi jirani. **Natoa rai kwa wote wanaojihusisha na shughuli hizo waache mara**

**moja vinginevyo Wizara haitasita kuwachukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kuwafikisha mahakamani.** Ramani ya mipaka halisi ya Tanzania ni kama inavyoonekana nyuma ya kitabu hiki.

### **Mipaka ya Ndani ya Nchi**

48) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17 Wizara iliahidi kukamilisha uhakiki wa sehemu ya mpaka wa Hifadhi ya Ngorongoro wenye urefu wa kilomita **83.6** kwa kushirikiana na wadau wengine. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kazi hii imekamilika. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais- TAMISEMI; Wizara ya Maliasili na Utalii; Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi na Hifadhi ya Mamlaka ya Ngorongoro na Hifadhi ya Serengeti, inaendelea kuainisha mipaka ya ushoroba wenye ukubwa wa kilomita za mraba **2,500** katika pori tengefu la Loliondo wilayani Ngorongoro.

### **Mipaka ya Kimataifa**

49) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara iliahidi kuanza kazi ya upigaji picha za anga katika mpaka wa Tanzania na Kenya wenye urefu wa kilomita **756**. Upigaji picha za anga kwenye mpaka huo umekamilika. Vilevile uhakiki wa ubora wa picha hizo umefanyika na kukamilika. Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara itaendelea na uimarishaji wa mpaka wa Tanzania na Kenya ikiwa ni pamoja na utengenezaji wa ramani za msingi pamoja na kupima kipande cha mpaka kuanzia Ziwa Victoria hadi Ziwa Natron chenye urefu wa kilomita 240. Aidha, majadiliano kati ya Tanzania na Zambia na Tanzania na Uganda kwa ajili ya uimarishaji wa mipaka yanaendelea.

### **Upimaji wa Viwanja na Mashamba**

50) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Serikali iliahidi kuidhinisha ramani za upimaji zenye viwanja **200,000** na mashamba **400**. Hadi kufikia 15 Mei, 2017, ramani za upimaji zenye jumla ya viwanja **118,502** na

mashamba **374** ziliidhinishwa. Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara itaidhinisha ramani za upimaji zenye jumla ya viwanja **200,000** na mashamba **400**.

51) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17 Wizara iliahidi kusimika na kupima alama za msingi za upimaji (*control points*) **200**. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017, Wizara ilikuwa imesimika alama za msingi **154** katika Halmashauri za Manispaa ya Morogoro (**44**), Dodoma (**60**), Manispaa ya Ubungo (**30**) na Halmashauri ya wilaya ya Buchosa (**20**). Alama hizi ni nyongeza katika alama za msingi zilizosimikwa katika mfumo mpya kusaidia shughuli za upimaji hapa nchini. Katika mwaka 2017/18 Wizara itasimika alama za msingi **200** kwa ajili ya kusaidia upimaji katika halmashauri mbalimbali nchini.

52) **Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na changamoto ya kuandaa ramani hati (*deed plan*) ambazo ni muhimu katika kuandaa hatimiliki. Katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara yangu imeboresha utaratibu wa kuandaa ramani za hati. Kuanzia sasa ramani hizo zitaandaliwa kwenye ofisi za kanda za ardhi ili kurahisisha na kuharakisha uandaaji wa hatimiliki. Aidha, Wizara itatoa mafunzo kwa warasimu ramani (*cartographers*) wa halmashauri ili ramani hati ziandaliwe katika ngazi ya halmashauri kwa lengo la kupunguza urasimu, muda na gharama za kuandaa hatimiliki.

**Upimaji wa Ardhi Chini ya Maji**

53) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara yangu iliahidi kuanza kazi ya upimaji ardhi chini ya maji katika bandari ya Tanga. Wizara kwa kushirikiana na Jeshi la Wanamaji la India, Mamlaka ya Bandari na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) Kikosi cha Wanamaji imekamilisha upimaji chini ya maji katika bandari ya Tanga.

### **Kujenga uwezo wa kupima ardhi nchini**

54) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara yangu kupitia mradi wa *Private Sector Competitiveness Project* (PSCP) itanunua vifaa vya kisasa

vyenye ufanisi mkubwa katika upimaji wa ardhi. Vifaa hivyo vitapelekwa katika ofisi za kanda ili kurahisisha upimaji na pia itatoa mafunzo kwa wataalam wa upimaji watakaotumia vifaa hivyo. Vifaa hivyo vimegawanyika katika makundi matatu, kundi la kwanza linajumuisha vifaa vinavyopima mfululizo ili kupata takwimu za hali ya nchi (*Continuous Operating Reference Stations CORS*), kundi la pili ni vifaa vya upimaji wa ardhi vinavyotumia simu na interneti (RTK- GPS), na kundi la tatu ni vifaa vya kuchora ramani (*digital photogrammetric workstations*).

### Utayarishaji wa Ramani Picha

55) **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imekamilisha uandaaji wa Ramani Picha (*orthorectified image*) za Jiji la Dar es Salaam. Ramani picha hizo zitatumika katika ujenzi wa Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi (ILMIS). Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara itatumia ramani picha hizo katika kuhuisha ramani za msingi, kubuni na kuandaa mipango mbalimbali ya maendeleo katika Jiji la Dar es Salaam.

### Halmashauri ya Taifa ya Wapima

56) **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kupitia Halmashauri ya Taifa ya Wapima na Wathamini imeendelea kusimamia maadili ya taaluma ya wapima ardhi na wathamini nchini. Katika siku za karibuni kumekuwa na wimbi kubwa la watu wasiosajiliwa kujihusisha na shughuli za upimaji ardhi na uthamini na kuwa chanzo cha migogoro ya ardhi nchini. Ili kukabiliana na tatizo hili, Wizara yangu imechukua hatua kwa kufanya uhakiki wa makampuni ya upimaji na wapima ardhi wa makampuni hayo. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017 Halmashauri ilikuwa imesajili makampuni **67** ya upimaji ardhi na **58** ya uthamini nchini. **Natoa wito kwa umma kutumia makampuni na wataalam waliosajiliwa.**

## HUDUMA ZA UPANGAJI MIJI NA VIJJI

57) *Mheshimiwa Spika*, kuratibu na kusimamia upangaji na uendelezaji wa miji na vijiji ni mojawapo ya majukumu ya Wizara yangu. Utekelezaji wa jukumu hili unalenga kuwa na makazi yaliyopangwa, kuhifadhi mazingira na uhakika wa uwekezaji katika ardhi.

## Mipango Kabambe ya Uendelezaji Miji (*Master Plans*)

58) *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara iliahidi kushirikiana na Halmashauri za Jiji la Mwanza na Arusha kukamilisha mipango kabambe ya majiji hayo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mipango kabambe hiyo imekamilika. Aidha, Wizara iliahidi kushirikiana na Jiji la Mbeya, Manispaa za Moshi, Bukoba, Mpanda na Lindi na Halmashauri ya Mji wa Babati kuandaa mipango kabambe ya miji hiyo. Utayarishaji wa mipango kabambe ya miji hiyo ipo katika hatua mbalimbali za uandaaji. Vilevile, Wizara iliahidi kuidhinisha mipango kabambe ya majiji ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Tanga; Manispaa za Iringa, Musoma, Tabora, Mtwara, Sumbawanga, Songea, Singida pamoja na Miji ya Bariadi, Kibaha na Korogwe. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017, mipango kabambe ya Manispaa za Musoma na Mtwara imekamilika na kuzinduliwa rasmi. Mipango kabambe iliyobaki ipo katika hatua za kukamilishwa na kuidhinishwa (**Jedwali Na.10**).

59) *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri husika itakamilisha mipango kabambe ya majiji ya Dar es Salaam na Tanga; Manispaa ya Singida pamoja na miji ya Ifakara, Mahenge, Malinyi, Bariadi, Kibaha na Korogwe. Aidha, Wizara itaendelea kupokea na kuidhinisha mipango kabambe kadri itakavyopokelewa kutoka Mamlaka za Upangaji. **Naendelea kusisitiza kuwa Halmashauri zote nchini zitenge fedha ya kuwezesha kuandaa mipango kabambe ili kuwa na miji iliyopangwa. Aidha, Halmashauri zihakikishe kuwa uendelezaji miji unazingatia mipango kabambe husika kwa lengo la kuepuka ukuaji holela wa miji.**

## Usanifu na Uendelezaji wa Miji

60) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2016/17, Wizara iliahidi kupokea, kukagua na kuidhinisha jumla ya michoro ya mipangomiji **2,000** kutoka Mamlaka za Upangaji. Jumla ya michoro ya Mipangomiji **1,428** ilipokelewa kutoka halmashauri mbalimbali nchini. Kati ya hiyo, michoro **1,029** yenye jumla ya viwanja **401,607** iliidhinishwa na kuhifadhiwa. Michoro **399** ilirudishwa katika Halmashauri husika ili ifanyiwe marekebisha. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara inatarajia kupokea, kukagua na kuidhinisha jumla ya michoro ya mipangomiji **2,000** kutoka mamlaka za upangaji.

61) **Mheshimiwa Spika**, Wizara iliahidi kukamilisha Mpango wa Uendelezaji upya eneo la Kurasini katika Jiji la Dar es Salaam. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Mpango huo umekamilika na eneo linatumika kwa shughuli zinazohusiana na bandari. Kadhalika kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji iliahidi kutangaza vituo vya huduma pembezoni mwa miji katika miji ya Mwanza, Arusha, Musoma, Mtwara, Iringa, Shinyanga, Singida, Songea, Tanga, na Tabora. Hadi tarehe 15 Mei, 2017 jumla ya vituo **30** vilikuwa vimetambuliwa kwa mchanganuo ufuatao: Mwanza (**2**), Arusha (**3**), Musoma (**3**), Mtwara (**4**), Iringa (**3**), Shinyanga (**4**), Tabora (**6**) na Kibaha (**5**).

## Usimamizi na Udhhibiti wa Uendelezaji Miji

62) **Mheshimiwa Spika**, mabadiliko ya matumizi ya ardhi, mgawanyo wa mashamba na viwanja unalenga kutumia ardhi na miundombinu kwa ufanisi, kuruhusu uwekezaji mpya na kuongeza thamani ya ardhi. Katika mwakawafedha 2016/17 Wizara kwa kushirikiana na halmashauri nchini iliendelea kusimamia na kudhibiti uendelezaji wa miji na kupunguza matumizi kinzani. Katika mwaka huu wa fedha, Wizara yangu ilipokea jumla ya maombi **334** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi, na mgawanyo/muunganiko wa viwanja na mashamba kutoka Halmashauri mbalimbali nchini. Maombi **187** yaliidhinishwa,



maombi **49** yalikataliwa kutokana na kutokidhi vigezo, maombi **29** yalirudishwa katika halmashauri husika kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho mbalimbali na maombi **69** yapo kwenye hatua za uhakiki.

63) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara yangu itaanza kuidhinisha maombi ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi, mgawanyo wa viwanja na mashamba katika ofisi za kanda ili kusogeza huduma karibu na wananchi. Vilevile, Wizara yangu inatarajia kuandaa mwongozo wa kuziwezesha mamlaka za upangaji nchini kusimamia na kudhibiti uendelezaji wa miji katika ngazi za Halmashauri, Mitaa na Vijiji ili kuwa na miji endelevu na kupunguza migogoro ya ardhi.

### Urasimishaji wa Makazi Holela Mijini

64) **Mheshimiwa Spika**, kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji, Serikali inatekeleza kwa awamu Programu ya Taifa ya Kurasimisha Makazi na Kuzuia Ujenzi Holela Mijini (2013 – 2023). Katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara iliahidi kuendelea na urasimishaji makazi **6,000** katika Kata za Kimara na Saranga katika Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo. Aidha, Wizara iliahidi kushirikiana na Halmashauri za Manispaa za Sumbawanga, Singida, Musoma, Kigoma Ujiji, Lindi na Tabora kurasimisha makazi **3,000** kwa kila Halmashauri. Hadi tarehe 15 Mei, 2017 jumla ya makazi **4,333** kati ya **6,000** yalirasimishwa na uchongaji wa barabara zenye urefu wa kilomita **9.1** ulifanyika katika kata ya Kimara katika Manispaa ya Ubungo.

65) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17 Wizara yangu iliahidi kuendelea kuratibu utekelezaji wa Programu ya Taifa ya Kurasimisha Makazi na Kuzuia Ujenzi Holela Mijini (2013- 2023). Ili kufikia dhamira ya Programu hii, Serikali imetoa elimu na kugawa miongozo ya urasimishaji kwa wataalam **97** wa sekta ya ardhi katika Halmashauri **12** za Musoma, Mwanza, Kigoma Ujiji, Tabora, Lindi, Nzega, Singida, Iringa, Mbeya, Tunduma, Sumbawanga na Mtwara. Aidha, michoro ya urasimishaji kutoka halmashauri mbalimbali yenye

jumla ya vipande vya ardhi **53,764** iliidhinishwa (**Jedwali Na.11**). Pia utafiti wa awali uliofanyika katika halmashauri sita (**6**) za Musoma, Kigoma Ujiji, Singida, Tabora, Sumbawanga na Lindi umeonesha maeneo yenye jumla ya makazi **50,200** yanaweza kurasimishwa chini ya mradi wa *Private Sector Competitiveness Project* (PSCP).

### Upangaji wa Makazi ya Vijiji

66) **Mheshimiwa Spika**, upangaji wa makazi vijijini unalenga kudhibiti ukuaji holela wa maeneo hayo ambayo yanatarajiwa kuwa miji ya baadaye. Katika mwaka wa fedha wa 2017/18, Wizara itaendelea kuzijengea uwezo Halmashauri za wilaya tano katika uandaaji wa mipango kina ya makazi na vituo vya biashara. Halmashauri hizo ni Kilombero, Ulanga, Malinyi, Mbeya na Iringa.

### Utengaji wa Maeneo ya Ujenzi wa Viwanda

67) **Mheshimiwa Spika**, katika kushiriki kutimiza azma ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda, jumla ya ekari **83,080** zimeainishwa katika maeneo ya mipango kabambe katika halmashauri **14** nchini kwa ajili ya ujenzi wa viwanda (**Jedwali Na.12**). Hili ni ongezeko la ekari **19,050** ikilinganishwa na maeneo yaliyoainishwa katika mwaka wa fedha 2015/16. Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara itaendelea kuhimiza halmashauri zinazoandaa mipango kabambe kuendelea kutenga maeneo zaidi kwa ajili ya viwanda.

### Wakala wa Uendelezaji Mji Mpya wa Kigamboni (KDA)

68) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2016/17 Wizara kupitia KDA iliahidi kuendelea kuandaa mipangokina ya matumizi ya ardhi katika eneo lote la mpango, kuanisha na kupima maeneo ya miundombinu na huduma za umma, kufanya uthamini na kulipa fidia, kukamilisha mpango mkakati wa KDA wa miaka mitano (2016/17-2020/21). Hadi tarehe 15 Mei, 2017, mipangokina **28**

yenye viwanja **4,500** vya matumizi mbalimbali ya ardhi imeandaliwa na kuidhinishwa tayari kwa upimaji wa viwanja husika. Pia barabara kuu zenye urefu wa kilomita **59.8** zimepimwa na kusimikwa mawe ya mpaka. Vilevile, hatimiliki **256** zimetolewa katika eneo la Mji mpya wa Kigamboni na vibali vya ujenzi **15** zimetolewa kwa waendelezaji wa ardhi. Rasimu ya Mpango mkakati wa Wakala wa miaka mitano iliandaliwa (2017-2022).

69) **Mheshimiwa Spika**, pamoja na juhudi zinazofanywa na KDA katika kuendeleza mji wa Kigamboni, kumekuwa na maoni ya baadhi ya wadau kwamba majukumu ya KDA yatekelezwe na Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni. Hivyo, Serikali inayafanyia kazi maoni haya pamoja na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ili kuona namna bora zaidi ya kusimamia uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni.

### **Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji**

70) **Mheshimiwa Spika**, jukumu kubwa la Bodi ya Wataalam wa Mipangomiji ni kusajili wataalam na makampuni na kudhibiti utendaji wa wataalam na makampuni katika fani hii. Vilevile, Bodi hii ina jukumu la kusimamia weledi na kutoa adhabu stahiki kwa wataalam na makampuni yanayokiuka taratibu na sheria zinazosimamia upangaji miji na vijiji. Shughuli hii inafanywa kulingana na Sheria ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji Na. 7 ya Mwaka 2007. Katika mwaka wa fedha 2016/17, Bodi ilisajili jumla ya wataalam **31** na kufanya idadi ya wataalam waliosajiliwa kufikia **306**. Kadhalika katika kipindi hicho, Bodi ilisajili makampuni **8** na kufikisha jumla ya makampuni **40** ya mipangomiji na vijiji. Aidha, Bodi ilifuta usajili wa wataalam **16** na kutoa onyo kwa mtaalam mmoja (**1**). Katika mwaka wa fedha 2017/18 Bodi itaendelea kusajili wataalam na makampuni yatakayokidhi vigezo na kuchukua hatua stahiki kwa wataalam wasio waadilifu na makampuni yasiyofuata taratibu kwa mujibu wa sheria.

### FUNGU 03: TUME YA TAIFA YA MIPANGO YA MATUMIZI YA ARDHI

71) **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Na.6 ya mwaka 2007. Sheria hiyo inaipa Tume mamlaka ya kupanga matumizi ya ardhi yote nchini kwa azma ya kutumia vizuri rasilimali zote za ardhi ili kuondoa umaskini na kuleta maendeleo endelevu.

#### Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi (2013 – 2033)

72) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara yangu kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi iliendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi kwa kufanya uhamasishaji wa Mpango na kutoa mafunzo kwa watendaji (Timu za Usimamizi wa Ardhi za Wilaya) wa Halmashauri za Wilaya **24**. Mafunzo hayo yalihusu mbinu shirikishi za uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji. Halmashauri hizo ni Mbeya, Ulanga, Kilombero, Kisarawe, Kilwa, Chamwino, Urambo, Geita, Bahi, Kongwa, Kilolo, Mufindi, Madaba, Njombe, Ludewa, Makete, Mbinga, Nyasa, Mvomero, Tanganyika, Serengeti, Liwale, Newala na Tarime.

73) **Mheshimiwa Spika**, Tume kwa kushirikiana na Taasisi ya *Ujamaa Community Resource Team*, Jumuiiko la Maliasili Tanzania, HakiArdhi, Umoja wa Waandishi wa Habari za Ardhi na Mazingira na mashirika ya kimataifa ya *Care International* na *Oxfam*, iliendelea kutoa elimu kwa umma juu ya malengo na umuhimu wa Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi, utekelezaji wake na mchango wake katika kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi nchini. Elimu hii ilitolewa kupitia vyombo vya habari ambapo jumla ya vipindi maalum **8** vilirushwa hewani kupitia televisheni na radio.

74) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Tume itafanya mapitio ya Programu za Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi 2013- 2033. Lengo likiwa ni kuhuisha na kujumuisha masuala ya maendeleo ya viwanda nchini ili

kuendana na azma ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda.

### **Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya na Vijiji**

75) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara yangu iliahidi kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya wilaya **5** na vijiji **1,500** kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Hadi kufikia tarehe 15 Mei 2017, Tume imewezesha kuandaliwa kwa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **91** katika Wilaya **23**. Kazi hii imefanyika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo USAID, DFID, SIDA, DANIDA, Mradi wa Misitu ya Asili (PFP), Halmashauri za Wilaya ya Geita, Wilaya ya Kilwa, Chuo cha Mipango Dodoma, Taasisi za *LECIDE, PELUM Tanzania, African Wildlife Foundation (AWF)* na *Frankfurt Zoological Society*.

76) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Tume itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuongeza kasi ya kupanga matumizi ya ardhi nchini na kufikia lengo la Vijiji **1,500** na Wilaya **5** kwa mwaka. Ili kuweza kufikia lengo hili na kutatua changamoto mbalimbali zinazokabili upangaji, utekelezaji na usimamizi wa matumizi ya ardhi nchini, Tume kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeandaa mkakati na mpango kazi ambao utatekelezwa na wadau wote ili kufikia lengo hilo. **Natoa rai kwa sekta binafsi na wadau mbalimbali wa maendeleo washirikiane na Tume ili kuongeza kasi ya upangaji wa matumizi ya ardhi ya vijiji na wilaya ili kuondoa migogoro ya ardhi.**  
**MAENDELEO YA SEKTA YA NYUMBA**

77) **Mheshimiwa Spika**, sekta ya nyumba hutoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi kwa kuwapatia wananchi siyo tu makazi bali pia inaongeza fursa za ajira na kupunguza umaskini, kuchangia mapato ya Serikali na kuongeza pato la Taifa. Ili kuwezesha sekta hii kufikia malengo hayo, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa kurahisisha upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya upatikanaji wa mikopo ya nyumba. Pia Wizara yangu imekuwa ikihimiza Shirika la Nyumba la Taifa, taasisi za Serikali, sekta binafsi na

wadau wengine kuongeza kasi ya uwekezaji katika sekta ya nyumba ili kupunguza uhaba mkubwa wa nyumba uliopo nchini.

78) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara imeendelea kufuatilia maendeleo ya sekta ya nyumba nchini. Mwamko wa taasisi za fedha wa kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba unaongezeka mwaka hadi mwaka. Hadi sasa jumla ya benki **28** zimeshatoa mikopo ya nyumba yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni **416**. Serikali imekuwa ikitoa fedha kupitia taasisi ya *Tanzania Mortgage Refinancing Company* (TMRC) ili kuziwezesha benki kutoa mikopo ya nyumba kwa wananchi. Hadi sasa zaidi ya wananchi **1,210** wamefaidika na mikopo yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni **126**. Vilevile, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania inatoa mikopo ya nyumba kwa taasisi ndogondogo za fedha (*microfinance*) ili zitoe mikopo ya uendelezaji wa nyumba yenye masharti nafuu kwa wananchi wa kipato cha chini. Hadi sasa wananchi wapatao **574** wamefaidika na mikopo hiyo ambayo jumla yake ni zaidi ya shilingi bilioni tisa (**9**).

79) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara yangu imeendelea kukusanya taarifa za waendelezaji milki na kuingizwa katika kanzidata. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017, kanzidata hiyo ina jumla ya waendelezaji milki **127** na nyumba **17,813**. Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara yangu kupitia mradi wa *Housing Finance Project* unaosimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania itaboresha kanzidata ya nyumba nchini kwa kujumuisha taarifa za soko la nyumba kama vile bei za nyumba na kodi ya pango la nyumba. Aidha, Wizara yangu itaratibu uandaaji wa mwongozo na viwango vya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu (*Guidelines and Standards for Affordable Housing*) lengo ni kuwa na viwango vya ujenzi wa nyumba za watu wa kipato cha chini nchini.

## **Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali**

80) **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inasimamia Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali ulioanzishwa kupitia Waraka wa Serikali Na. 8 wa mwaka 1992. Lengo la Mfuko huo ni kuwawezesha watumishi kupata mikopo ya kujenga, kukarabati ama kununua nyumba. Katika mwaka wa fedha 2016/17 watumishi wa Serikali **80** wamepatiwa mikopo ya jumla ya shilingi milioni **743**. Vilevile, katika kipindi hicho Wizara imekusanya marejesho ya jumla ya shilingi milioni **500.6**. Katika mwaka 2017/18 Wizara yangu itaendelea kupokea na kushughulikia maombi mapya na kukusanya marejesho kulingana na taratibu za mfuko.

## **Ushirikiano na Taasisi za Makazi za Kimataifa**

81) **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inaratibu ushirikiano wa kimataifa katika masuala ya makazi. Katika mwaka wa fedha 2016/17 Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ya makazi nchini iliadhimisha siku ya makazi duniani mnamo tarehe 3 Oktoba, 2016. Katika maadhimisho hayo, Wizara ilitumia fursa hiyo kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kutekeleza lengo la 11 la Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Maendeleo Endelevu. Lengo hili linahusu kuwa na Miji na Makazi Salama, Imara na Endelevu. Aidha, Wizara ilishiriki katika Mkutano Mkuu wa III wa makazi ulioandaliwa na Shirika la Makazi la Umoja wa Mataifa (UN-Habitat) mjini Quito, Ecuador, Oktoba, 2016. Ajenda Mpya ya Makazi Duniani (*New Urban Agenda*) ilipitishwa kwa ajili ya kutekelezwa na nchi wanachama kama dira ya uendelezaji makazi kwa kipindi cha miaka 20 ijayo (2016-2036).

## **Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi (NHBRA)**

82) **Mheshimiwa Spika**, Wakala umeendelea kufanya utafiti wa vigae vya kuchoma kwa ajili ya kuelekea vinavyotokana na udongo wa mfinyanzi, matofali ya kuchoma yanayofungamana, uboreshaji wa nyumba za

udongo na matofali ya udongo, ujenzi wa sakafu (*suspended floor*) na utafiti wa kiasi cha nishati kinachotumika katika ujenzi wa nyumba.

83) **Mheshimiwa Spika**, utafiti mwingine uliofanywa ulihusu mashine ya kufyatua matofali mawili kwa nguvu za kunyonga baisikeli (*Tricycle Bricks Making Machine*) na mashine ya kufyatua matofali mawili inayoendeshwa kwa kutumia dizeli (*Hydraulic brick making machine*), kwa kushirikiana na taasisi ya NYUMBU. Utafiti mwingine ni kutengeneza fremu za milango na madirisha kwa kutumia zege, matofali ya saruji yanayofungamana yenye kuhitaji kiasi kidogo cha plasta na matofali ya kufungamana ya kujengea matenki ya mvingo ya kuhifadha maji.

84) **Mheshimiwa Spika**, ili kusambaza matokeo ya tafiti hizo, hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017 jumla ya mashine **133** za kufyatulia matofali ya kufungamana na vigae **53,389** vilitengenezwa na kuuzwa kwa wateja mbalimbali wa Wakala. Aidha, Wakala kwa kushirikiana na kampuni ya *Green Resources Ltd* uliendesha mafunzo ya vitendo kuhusu ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu kwa wananchi **173** kutoka wilaya mbalimbali. Vilevile, Wakala ulishiriki katika maonesho mbalimbali ili kusambaza matokeo ya tafiti yaweze kuwafikia wananchi walio wengi. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wakala utaendelea kufanya tafiti mbalimbali na kusambaza matokeo ya tafiti hizo kwa wananchi.

## SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA

### Miradi ya Ujenzi wa Nyumba

85) **Mheshimiwa Spika**, Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) liliendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Na. 2 ya mwaka 1990 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2005. Shirika limeendelea kutekeleza majukumu yake ili kumudu ushindani wa kibiashara katika ujenzi wa nyumba za kuuza na kupangisha ikijumuisha nyumba za gharama nafuu. Katika mwaka wa fedha 2016/17, Shirika liliahidi



kuendelea kukamilisha miradi iliyopo katika mikoa mbalimbali pamoja na kuendelea kujenga nyumba za gharama nafuu.

86) **Mheshimiwa Spika**, katika Hotuba ya bajeti ya Wizara ya mwaka wa fedha 2016/17 suala la ujenzi wa nyumba za gharama nafuu liligusa hisia za Waheshimiwa Wabunge wengi na waliitaka Serikali kuangalia upya suala hili. Wizara yangu imeendelea kulihimiza Shirika la Nyumba kuweka kipaumbele katika ujenzi wa nyumba za gharama nafuu na kuzihamasisha Halmashauri kulipatia Shirika ardhi nafuu ya kujenga nyumba hizo. Aidha, taasisi na halmashauri zimeshaelekezwa na Serikali kuweka miundombinu ya umeme, maji na barabara katika maeneo yanayojengwa nyumba na NHC ili kupunguza gharama za ujenzi wa nyumba hizo.

87) **Mheshimiwa Spika**, hadi sasa Shirika limekamilisha ujenzi wa miradi **29** kati ya miradi**54** iliyokuwa inatekelezwa. Miradi hiyo ni ya nyumba za gharama nafuu, gharama ya kati na juu, majengo ya biashara na majengo ya matumizi mchanganyiko na ina jumla ya nyumba **1,686**. Jumla ya miradi ya nyumba za gharama nafuu ni **14** na ina idadi ya nyumba **492**; miradi **10** ni ya nyumba za gharama ya kati na juu na ina jumla ya nyumba **881**; miradi **4** ni ya nyumba za biashara na ina nyumba **229** na jengo moja (1) ni la matumizi mchanganyiko na lina nyumba **84**. Aidha, jumla ya miradi **25** yenye jumla ya nyumba **4,126** inaendelea kujengwa. Kati ya hiyo, miradi **14** ni ya nyumba za gharama nafuu na ina jumla ya nyumba **1,002**; miradi **3** ni ya nyumba za gharama ya kati na juu na ina nyumba **760**; miradi **5** ni ya nyumba za biashara na ina nyumba **203**; na miradi 4 ni ya nyumba za matumizi mchanganyiko na ina nyumba **2,161**.

88) **Mheshimiwa Spika**, katika kuunga mkono uamuzi wa Serikali wa kuhamishia rasmi Makao Makuu Dodoma, Shirika limetoa kipaumbele katika ujenzi wa nyumba za makazi kwa ajili ya watumishi na wananchi wengine watakaohamia Dodoma. Katika mwaka wa fedha 2016/17 Shirika limeendelea kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa nyumba **300** katika eneo la lyumbu, Dodoma.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2017/18 Shirika litaendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa nyumba katika eneo la lyumbu na kukamilisha taratibu za kupata ardhi ya kujenga nyumba mjini Dodoma.

### **Mauzo na Makusanyo ya Kodi ya Pango la Nyumba**

89) **Mheshimiwa Spika**, hadi tarehe 15 Mei, 2017 Shirika lilikuwa limekusanya jumla ya Shilingi bilioni **39** kutokana na mauzo ya nyumba. Aidha, katika mwaka wa fedha 2016/17 Shirika lilitarajia kukusanya kodi ya pango kiasi cha shilingi bilioni **86.59**. Hadi tarehe 15 Mei, 2017 makusanyo ya kodi ya pango yalifikia shilingi bilioni **88.28** ambayo ni sawa na asilimia **102** ya lengo la mwaka. Katika mwaka 2017/18 Shirika linatarajia kukusanya kodi ya pango kiasi cha shilingi bilioni **95.10** (Jedwali 13).

### **Uendelezaji wa Vitovu vya Miji**

90) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Shirika liliendelea kutekeleza miradi ya Vitovu vya Miji (*Satellite Cities*) kama Mwendelezaji Mkuu katika maeneo ambayo Shirika linamiliki ardhi. Miradi hii ni pamoja na Kawe ambapo mpangokina upo katika hatua za mwisho za kuidhinishwa na ujenzi wa nyumba unaendelea; Safari City ulioko Arusha ambako ujenzi wa nyumba **10** za mfano na uuzaji wa viwanja unaendelea; ujenzi wa nyumba **300** katika eneo la lyumbu Dodoma na Usa River ambapo mpangokina umepitishwa na mkandarasi wa kujenga nyumba za mfano amepatikana. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Shirika litaendelea kupanga na kuendeleza maeneo ya vitovu vya Kunduchi Rifle Range, Songwe, Ruvu, Pembamnazi, Chato na Kibondo.

### **Ardhi kwa ajili ya Ujenzi wa Nyumba**

91) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Shirika liliongeza akiba ya ardhi kiasi cha ekari **112.74**. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Shirika kwa kushirikiana na halmashauri za miji na wilaya na wadau wengine katika

kutekeleza agizo la Serikali litahakikisha kuwa ardhi yake inawekewa miundombinu ya umeme, barabara na maji kabla ya kuanza kwa ujenzi. Hatua hii itachangia kwa kiasi kikubwa kupunguza gharama za nyumba hususan nyumba za wananchi wa kipato cha chini.

## HUDUMA ZA KISHERIA NA SERA

### Huduma za Kisheria

92) **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kusimamia sekta ya ardhi kwa kuzingatia sheria zilizopo. Katika mwaka 2016/17, Wizara iliahidi kuandaa mapendekezo ya kutunga na kuhuisha sheria mbalimbali zinazohusu sekta ya ardhi. Kazi zilizofanyika katika kipindi hiki ni kutunga Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini Na. 7 ya mwaka 2016 ambayo ilianza kutumika rasmi tarehe 1 Januari, 2017 baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 1 la tarehe 6 Januari, 2017. Aidha, ili kusimamia na kuendeleza sekta ya milki, kuhuisha utaratibu wa utwaaji ardhi na kusimamia mawakala wa ardhi, Wizara yangu imeandaa rasimu za miswada ya Sheria ya Usimamizi wa Uendelezaji Milki, Sheria ya Utwaaji Ardhi na Fidua na Sheria ya Mawakala wa Ardhi.

93) **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara imeandaa rasimu ya Marekebisha ya Sheria ya Mipangomiji Na. 8 ya mwaka 2007 ili kusogeza huduma za mipangomiji katika ngazi ya Kanda. Kadhalika, imeandaa rasimu ya Kanuni za Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini na kutunga kanuni za Mitihani kwa Maafisa wa Mipangomiji za mwaka 2016 zilizotangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 277 la tarehe 5 Agosti, 2016. Kanuni hizi zinatumiwa na Bodi ya Usajili wa Maafisa Mipangomiji wakati wa kusajili wataalam hao. Aidha, rasimu ya tafsiri ya Kiswahili ya Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Na. 2 ya mwaka 2002 imeandaliwa. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara itakamilisha rasimu za miswada ya Sheria ya Usimamizi wa Uendelezaji Milki, Sheria ya Utwaaji Ardhi na Fidua, Sheria ya Mawakala wa Ardhi na Kanuni za Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini.

## Mapitio ya Sera

94) **Mheshimiwa Spika**, Wizara imekamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 na kuandaa Rasimu ya marekebisho ya Sera hiyo kwa kushirikiana na wataalam washauri kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu Ardhi na sekta binafsi. Kwa ujumla, madhumuni ya mapitio ya Sera hiyo ni kuweka misingi ya kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995. Lengo la marekebisho hayo ni kuimarisha usalama wa milki, kuboresha mazingira ya uwekezaji katika sekta ya ardhi, kudhibiti migogoro ya matumizi ya ardhi pamoja na kuhakikisha kwamba kila kipande cha ardhi kinapangwa, kupimwa na kumilikishwa.

95) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara iliahidi kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 na kuandaa Sera ya Nyumba. Wizara kwa kutumia wataalaam washauri kutoka Chuo Kikuu Ardhi inaendelea na mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 ili kuihuisha na kutayarisha rasimu ya Sera ya Nyumba. **Natoa wito kwa wadau wote kujitokeza kutoa maoni ili tuweze kupata sera zitakazokidhi mahitaji ya sasa na baadaye.**

## Elimu kwa Umma

96) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17 Wizara iliahidi kuendelea kuelimisha umma kuhusu sera, sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia sekta ya ardhi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa elimu kwa umma ilitolewa kupitia vyombo mbalimbali vya habari ikiwemo luninga (vipindi 23), redio (vipindi 28) pamoja na machapisho, vipeperushi na jarida la Wizara ambapo nakala **2,500** zilichapishwa na kusambazwa. Aidha, elimu ilitolewa kupitia tovuti ya Wizara, mitandao ya kijamii, matangazo, mahojiano, makala maalum magazetini saba (7), taarifa kwa umma, mikutano 17 na semina mbili (2). Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara itaendelea kuelimisha umma kuhusu sera, sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia sekta ya ardhi.

## HUDUMA ZA UTAWALA NA RASILIMALI WATU

97) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara yangu iliahidi kuendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa kuweka mifumo bora zaidi ya utendaji kazi na mazingira bora ya ofisi kwa lengo la kuleta ufanisi katika kazi. Pia Wizara iliahidi kuwapatia mafunzo watumishi 150 wa kada mbalimbali. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017 Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya ofisi kwa kununua vitendea kazi na kukarabati majengo ya ofisi. Vilevile Wizara iliandaa ofisi za Makao Makuu yake Mjini Dodoma. Aidha, jumla ya watumishi **491** wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara inatarajia kuwapatia mafunzo watumishi **70** na kuajiri watumishi **291**. Pia Wizara itaendelea kupanua na kuboresha ofisi zake ili kuwezesha watumishi wengi zaidi kuhamia Dodoma.

98) **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kupitia Kituo cha Huduma kwa Mteja (*Customer Service Centre*) kilichopo katika Kanda ya Dar es Salaam. Kituo kimeweza kuwahudumia jumla ya wananchi **88,400** ambao ni sawa na wastani wa wateja **2,210** kwa wiki na wateja **442** kwa siku ikilinganishwa na wastani wa wateja **420** kwa siku katika mwaka 2015/16 waliofika kupata huduma mbalimbali zitolewazo na kituo. Dhamira ya Wizara ni kuwa na vituo vya huduma kwa mteja kwa kila ofisi ya kanda.

99) **Mheshimiwa Spika**, ufanisi kazini unategemea watumishi wenye afya bora. Katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara yangu imeendelea kuwaelimisha na kuwasisitiza watumishi kupima afya zao ili kujikinga na janga la UKIMWI na magonjwa mengine. Aidha, Wizara imeendelea kuwawezesha watumishi na familia zao wanaoishi na Virusi vya UKIMWI ambapo watumishi **20** wamewezeshwa kupata dawa na lishe.

## Vyuo vya Ardhi Tabora na Morogoro

100) **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea kuviimarisha vyuo vya Morogoro na Tabora kwa kuendelea na ujenzi wa maktaba katika Chuo cha Ardhi Tabora, kuweka mfumo wa kielektroniki wa usajili wa wanafunzi na kununua vifaa na mitambo ya kufundishia na kujifunzia kwa vitendo ili kuwawezesha wanachuo kupata ujuzi unaokidhi viwango katika taaluma zao. Idadi ya wahitimu katika vyuo vya ardhi vya Morogoro na Tabora iliongezeka kutoka **495** mwaka 2015/16 hadi **559** mwaka 2016/17 (**Jedwali Na. 14**). Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara itaendelea na ujenzi wa maktaba katika Chuo cha Ardhi Tabora na ununuzi wa samani kwa ajili ya maktaba ya Chuo cha Ardhi Morogoro.

## C: CHANGAMOTO NA MIKAKATI YA KUKABILIANA NAZO

101) **Mheshimiwa Spika**, licha ya juhudi zilizotekelezwa na Wizara katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara bado inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i) Uratibu wa sekta ya ardhi kwa kuwa inasimamiwa na mamlaka zaidi ya moja;

ii) Uhaba wa wataalam na vitendea kazi vinavyohitajika ili kukidhi utoaji wa huduma katika sekta ya ardhi;

iii) Kasi ya ongezeko la idadi ya watu na mifugo ikilinganishwa na upatikanaji wa ardhi iliyopangwa na kupimwa;

iv) Ucheleweshaji wa ulipaji wa fidia stahiki kwa ardhi iliyotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo; na

v) Uelewa mdogo wa wananchi kuhusu sera na sheria za ardhi.

102) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, hotuba yangu imeainisha mikakati mbalimbali

itakayotekelezwa ili kukabiliana na changamoto hizo. Katika kuimarisha usalama wa milki pamoja na kuongeza kasi ya kupima na kupanga ardhi, Wizara imekamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya mwaka 1995 kwa kushirikiana na wadau mbalimbali nchini.

103) **Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla, madhumuni ya mapitio ya Sera hiyo ni pamoja na kuziba mianya au viashiria vya migogoro ya matumizi ya ardhi baina ya watumiaji nchini, kuongeza kasi ya upimaji, upangaji na umilikishaji wa kila kipande cha ardhi na kuwawezesha wananchi wasio na ardhi vijijini kumiliki ardhi kwa shughuli za kilimo na ufugaji na kujenga mazingira bora yanayovutia uwekezaji nchini. Aidha, katika kuimarisha na kuendeleza sekta ya milki, Wizara kwa kushirikiana na wataalam washauri kutoka Chuo Kikuu Ardhi inapitia Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 kwa lengo la kuihuisha zaidi kwa kuzingatia mazingira ya sasa ya mahitaji ya jamii ya makazi na nyumba.

104) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu uhaba wa wataalam na vitendea kazi, Wizara inaendelea kuishirikisha sekta binafsi katika utekelezaji wa majukumu yake. Hadi 15 Mei, 2017 jumla ya kampuni binafsi za kupanga **38** na kupima ardhi **67** zilikuwa zimesajiliwa. Aidha, Wizara imepeleka vitendea kazi muhimu kwenye kanda ili kuimarisha utoaji wa huduma za ardhi karibu na wananchi yakiwemo magari.

105) **Mheshimiwa Spika**, Wizara inatekeleza programu ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na halmashauri itaendelea kuhakiki viwanja na mashamba ambayo hayajaendelezwa kwa muda mrefu, kufuta milki na kuyapangia matumizi mengine. Vilevile, ili kupunguza au kudhibiti migogoro inayosababishwa na ucheleweshaji wa ulipaji wa fidia stahiki na kwa wakati, Serikali imeunda Bodi ya Mfuko wa Fidia ya Ardhi kwa ajili ya kuratibu masuala yote ya fidia nchini yakayofanywa na wizara na taasisi za mbalimbali. Aidha, Serikali inaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu sheria, kanuni, taratibu na miongozo inayotawala sekta ya ardhi.

## D: SHUKRANI

106) *Mheshimiwa Spika*, kwa niaba ya Wizara yangu, naomba kumalizia hotuba yangu kwa kuwashukuru kwa dhati wadau wote wa sekta ya ardhi ikiwa ni pamoja na Serikali za Vijiji, Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji. Vilevile napenda kuishukuru Benki ya Dunia na nchi wahisani zikiwemo Uingereza, Denmark, Sweden, Japan, China, India, Korea ya Kusini na Marekani. Wizara yangu inatambua na kuthamini michango inayotolewa na wadau wote wa sekta ya ardhi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

107) *Mheshimiwa Spika*, kwa mara nyingine napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Dkt. Angelina Sylvester Lubala Mabula (Mb), kwa kunisaidia katika kutekeleza majukumu yangu. Pia napenda kumshukuru Katibu Mkuu Dkt. Yamungu Kayandabila na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Moses Kusiluka kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa. Nawashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Wakuu wa Taasisi zilizochini ya Wizara pamoja na watumishi wote wa sekta ya ardhi katika ngazi zote kwa kunisaidia kutimiza majukumu yangu.

## E: HITIMISHO

108) *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri zote kutayarisha mipango ya kuendeleza miji na vijiji, kusimamia upangaji, upimaji, urasimishaji, umilikishaji na usajili wa hati ili kuwezesha kuwepo kwa usalama wa milki. **Natoa rai kwa mamlaka na asasi mbalimbali pamoja na wadau wote wa sekta ya ardhi kutoa ushirikiano ili kuhakikisha kuwa ardhi inaziwezesha sekta zote kufikia malengo ya kumletea Mtanzania maendeleo na kuondokana na umaskini.**



**F: MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2017/18**

**Makadirio ya Mapato**

109) *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara inatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 112,050,000,000/=** kutokana na kodi, tozo na ada mbalimbali zinazotokana na shughuli za sekta ya ardhi kwa kutekeleza mikakati ambayo imeainishwa katika hotuba.

**Makadirio ya Matumizi**

110) *Mheshimiwa Spika*, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu niliyoyaeleza katika hotuba hii kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Fungu **48**: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu **03**: Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kama ifuatavyo:-

**Fungu 48: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

AINA	MAPATO/MATUMIZI	SHILINGI
A	Mapato ya Serikali	<b>112,050,000,000</b>
B	Matumizi ya Kawaida	
	Matumizi ya Mishahara	18,484,916,852
	Matumizi Mengineyo	24,770,166,074
	<b>Jumla Ndogo</b>	<b>43,255,082,926</b>
C	Matumizi ya	
	Fedha za Ndani	16,400,000,000
	Fedha za Nje	9,000,000,000
	<b>Jumla Ndogo</b>	<b>25,400,000,000</b>
	<b>JUMLA KUU (B+C)</b>	<b>68,655,082,926</b>

Jumla ya matumizi ya kawaida na maendeleo  
**Shilingi 68,655,082,926**

**Fungu 03: Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

AINA	MATUMIZI	SHILINGI
A	Matumizi ya Mishahara	1,135,550,000
B	Matumizi Mengineyo	979,821,822
	<b>Jumla</b>	<b>2,115,371,822</b>

Jumla ya matumizi ya kawaida ni **Shilingi 2,115,371,822/=**.

111) **Mheshimiwa Spika**, jumla kuu ya fedha zote zinazombwa kwa Wizara (Fungu 48 na Fungu 03) ni Shilingi **70,770,454,748/=**.

112) **Mheshimiwa Spika**, pamoja na hotuba hii yapo majedwali ambayo yanafafanua kwa kina utekelezaji wa majukumu, Randama na pia nimeambatisha vitabu viwili (2) vya taarifa za utekelezaji wa majukumu ambavyo ni sehemu ya hotuba yangu. Naomba taarifa hizo zichukuliwe kuwa ni vielelezo vya hoja hii. Hotuba hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Wizara kwa anuani ya [www.ardhi.go.tz](http://www.ardhi.go.tz).

113) **Mheshimiwa Spika**, mwisho natoa shukrani zangu za dhiti kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

114) **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na hoja imeungwa mkono. Pia nashukuru kwa hotuba yako ambayo imeweza

kufafanua baadhi ya maeneo muhimu, naamini Waheshimiwa Wabunge wameipokea na wameikubali.

Tunaendelea na sasa tunamkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii ili aweze kuja kusoma taarifa yake.

**MHE. SILAFU J. MAUFI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Utalii, naomba nisome na kuikabidhi kwa Waheshimiwa Wabunge Taarifa kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ufinyu wa muda, napenda kuwasilisha taarifa hii kwa muhtasari. Kwa mantiki hiyo basi, naomba taarifa yote ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii iingie kwenye *Hansard*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 98(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka sharti la Kamati za Kisekta ikiwemo Kamati hii kufanya ukaguzi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kisha kuchambua bajeti ya Wizara inayoisimamia. Naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Wizara kwa mwaka 2016/2017 na kuchambua Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inahusisha Mafungu mawili; Fungu la 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu Namba 03 - Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa majukumu yaliyotekelezwa katika Wizara; sehemu hii inajelekeza katika kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali kwa mtiririko ulioelezwa katika kipengele namba mbili cha sehemu ya pili kwa namna ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukusanyaji wa maduhuli katika bajeti ya 2016/17; Wizara ilitarajiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 111.77 kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato yanayotokana na sekta ya ardhi. Hadi kufikia Februari, 2017, Wizara ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 57.91 ambayo ni sawa na asilimia 52 ya kiwango kilichokadiriwa kukusanywa kwa mwaka. Katika makusanyo hayo, shilingi bilioni 51.4 sawa na asilimia 88.19 ya makusanyo zinatokana na kodi ya mapango ya ardhi. Kamati inaona kuwa endapo mfumo wa *Land Rent Management System* utakuwa kwa Halmashauri zote hapa nchini ni dhahiri kuwa lengo katika makusanyo linaweza kufikiwa kwa uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 61,873. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 25.531 zilikuwa kwa ajili ya matumizi mengineyo, shilingi bilioni 16.342 kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 20 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo shilingi bilioni kumi ni fedha za ndani na shilingi bilioni 10 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2017 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 28.414. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 9.994 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 10.793 kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 3.626 ni fedha zilizopelekwa kwa ajili ya miradi ambazo ni sawa na asilimia 38 ya bajeti ya mwaka 2016/2017. Kwa ujumla fedha zilizopelekwa hadi

Februari, 2017 ni sawa na asilimia 46 ya fedha zilizotengwa. Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa Wizara ilifanyiwa uhamisho wa fedha za nje toka fungu 48 shilingi bilioni 3.3 kwa ajili ya kulipa deni la uandaaji wa mipango kabambe ya Miji ya Arusha na Mwanza. Jumla ya shilingi bilioni 4.2 ni fedha za ndani ikijumuisha fedha zilizofanyiwa uhamisho wa bilioni 3.4 ni fedha za nje. Kwa ujumla, hadi kufikia Februari, 2017, Wizara ilikuwa imepokea asilimia 39.2 ya fedha za matumizi mengineyo. Asilimia 69.7 fedha za mishahara na asilimia 38 fedha za maendeleo ambapo uwiano wa tengo la fedha za maendeleo na fedha za matumizi ya kawaida ni asilimia 32.3, fedha za miradi ya maendeleo na asilimia 67.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya utoaji wa fedha inaendelea kuwa ya kusuasua. Kushindwa kutoa fedha kwa wakati na kwa kiasi kinachotarajiwa, huahirisha kiwango kikubwa kutekeleza shughuli za Wizara hali inayochangia ongezeko la migogoro ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Fungu 48 hadi mwezi huo iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 13 kwa ajili ya mradi namba 4943 unaojulikana kama *Land Tenure Support Programme* ambao ni mradi wa umilikishaji ardhi na kutekelezwa kwa majaribio katika Wilaya ya Ulanga, Kilombero na Malinyi, Mkoani Morogoro. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni tatu ni fedha za ndani na shilingi bilioni kumi ni fedha za nje. Mradi huu unatekelezwa chini ya kifungu 2001- Utawala wa Ardhi katika Fungu namba 48.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya ukaguzi; Kamati ilibaini kuwa mradi huu uko kwenye hatua za utekelezaji. Hadi Februari, 2017 Wizara ilipokea jumla ya shilingi bilioni 3.8 sawa na asilimia 29.2 ya fedha zilizotengwa ambapo kati ya fedha hizo shilingi milioni 400 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 3.4 ni fedha za nje. Kamati ilijionea utekelezaji wa mradi huu ambapo kazi ya kupima mipaka ya vijiji imepunguza kwa kiasi kikubwa migogoro ya mipaka iliyokuwepo kwa muda mrefu. Programu hii imekuwa ikishirikisha wanakijiji na wanashiriki kikamilifu kwa utekelezaji. Kamati ilishuhudia utatuzi wa mgogoro wa muda mrefu kati ya kijiji cha Nkanu

na Kanoro ambao ulipitia katika program hii, mgogoro huu sasa umekamilika kabisa. Kamati inaiona hii ni hatua muhimu katika kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji kwa kuwa mafanikio ya mradi huu tayari yameshaonekana kwa maeneo yaliyofikiwa. Kamati inashauri Serikali kutenga fedha za kutosha ili kuweza kufikia maeneo mengi zaidi nchini ili kumaliza kabisa migogoro ya ardhi inayoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi huu unaonesha kuwa Serikali imechukua ushauri wa Kamati na kuongeza fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka asilimia 4.78 ya bajeti yote kwa mwaka 2015/2016 hadi asilimia 32.3 kwa bajeti yote ya Wizara kwa mwaka 2016/2017. Pamoja na ongezeko hilo, Kamati hadi ilipofikia kufanya uchambuzi kuna miradi ambayo pamoja na kutengewa fedha haikupelekewa fedha kabisa. Hali hii ya fedha kutotolewa kabisa inasikitisha na ni wazi kuwa uwezekano wa Serikali kufikia malengo iliyojiwekea ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/17; kutokana na ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati imebaini kuwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ilipanga kutekeleza miradi mitano lakini ilitengewa fedha za nje kwa ajili ya mradi mmoja tu wa *Land Tenure Support Programme*. Kutokana na hali hiyo, Kamati ina maoni yafuatayo:-

(a) Miradi yote ambayo inatengewa fedha za nje upatikanaji wa fedha umekuwa wa kusuasua ambapo wakati Kamati inafanya uchambuzi huu mwezi Machi, 2017 miradi mitatu kati ya mitano haikuwa imepelekewa fedha zozote. Hali hii inazorotesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwani inaonekana kama vile miradi mingine sio kipaumbele kwa Serikali.

(b) Pamoja na kuwa Mradi wa Umilikishaji Ardhi umetengewa fedha nyingi, kiasi kikubwa cha fedha hizi ni fedha za nje. Jambo hili linazorotesha utekelezaji wa mradi kwa kuwa utoaji wa fedha za nje ni mgumu, huambatana

na masharti magumu. Serikali haina budi kutenga fedha za ndani za kutosha ili kutekeleza programu hii kwa ufanisi na kwa kasi zaidi tofauti na ilivyo sasa.

(c) Kutopatikana kwa fedha kwa wakati kunachangia kuzorotesha utekelezaji wa miradi yetu.

(d) Kuendelea kutoa fedha kwa kusuasua kwa miradi ya maendeleo inaongeza gharama zaidi ya miradi hiyo hapo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2016/2017; wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuboresha utekelezaji wa kazi za Wizara. Baadhi ya ushauri umezingatiwa na kutekelezwa. Kwa mfano, Kamati iliridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Serikali kupunguza gharama ya nyumba zinazojengwa na Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) kwa kuwezesha miundombinu ya maji, umeme na barabara ambapo hapo awali Shirika lilikuwa linabeba gharama hizo na kufanya bei ya nyumba kuwa ya juu kwa kutokuwasaidia wananchi wa kipato cha kati na kipato cha chini ambao ndiyo walengwa wa mradi huu. Mfano mzuri wa utekelezaji huu ni nyumba zilizojengwa eneo la Iyumbu, Dodoma ambapo Serikali kupitia iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu - Dodoma (*CDA*) watajenga miundombinu ya barabara na maji. Kamati inaamini utekelezaji huu utaendelezwa na Mamlaka iliyochukua nafasi ya *CDA* baada ya kufutwa kwa amri ya Rais. Hatua hii itapunguza kwa kasi kubwa gharama ya nyumba na kupanua wigo mkubwa kwa wananchi walengwa kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua katika Mradi wa Uendelezaji wa Mji mpya wa Kigamboni kwa kuhamishia Ofisi ya *KDA* kwenye Ofisi ya Kanda ya Dar es Salaam ili kupunguza gharama ya pango iliyokuwa inapanga wakati mradi wenyewe haujaanza kufanya kazi. Ni maoni ya Kamati kuwa Serikali

itazingatia ushauri wa kutenga fedha kwa ajili ya mradi huu ambao umechukua muda mrefu bila kuchukua hatua yoyote ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine, Kamati haikuridhishwa na uanzishwaji wa Mabaraza ya Ardhi ya Nyumba katika Wilaya zote nchini. Kila Wilaya inatakiwa iwe na Baraza la Ardhi na Nyumba kwa mujibu wa Sheria ya Mabaraza Na. 2 ya mwaka 2002. Ni jambo la kusikitisha kuwa hadi sasa jumla ya Mabaraza 100 yaliyoanzishwa ni Mabaraza 53 tu yanatoa huduma wakati Mabaraza 47 hayajaanza kutoa huduma kutokana na changamoto ya upatikanaji wa rasilimali watu na fedha. Hali hii inapelekea msongamano wa mashauri ya ardhi na kusababisha mashauri kuchukua muda mrefu kupata suluhu. Kamati inaishauri Serikali kutoa kipaumbele cha bajeti kwenye uanzishwaji wa Mabaraza haya ili kuongeza tija katika kuwapunguzia wananchi adha ya kusafiri umbali mrefu kufuata huduma na kupunguza migogoro ya ardhi isiyo ya lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imezingatia ushauri wa Kamati wa kutunga Sheria ya Uthamini wa Usajili wa Wathamini Na. 7 ya mwaka 2016 ambayo kwa kiasi kikubwa itarekebisha mapungufu ya utoaji wa maeneo bila kulipia fidia stahiki na kwa wakati. Sambamba na hilo, Serikali imeunda Bodi ya Mfuko wa Fidia ambao utakuwa na jukumu la kujiridhisha kuwa fedha za fidia zipo kabla ya uthamini kuweza kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2017/2018; uchambuzi wa makadirio na mapato; katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara inatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 112.50 ikiwa ni ongezeko la asilimia 0.3 ikilinganishwa na mapato ya mwaka 2016/2017 ya shilingi bilioni 111.77. Mapato haya yanatokana na tozo mbalimbali za sekta ya ardhi huku ada ya ardhi (*land rent*) ikiingiza mapato zaidi ikilinganishwa na vyanzo vingine. Ongezeko la mapato linachangiwa kwa kiasi kikubwa na mfumo wa kielektroniki yaani *Land Rent Management System*. Ni maoni ya Kamati kuwa Serikali



itahakikisha mfumo wa *Land Rent Management System* unatumiwa na Halmashauri zote nchini ili kuongeza mapato yatokanayo na ada ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo ambalo Serikali inapata mapato ya uhakika pamoja na mapato yatokanayo na tozo za ardhi iliyorasimishwa na ile iliyopimwa. Mpaka sasa ardhi ambayo imepimwa na kurasimishwa ni asilimia 15 tu ambayo ni ndogo sana. Serikali iongeze fedha kwa ajili ya kupima na kurasimisha ardhi na pia iingie ubia na makampuni binafsi kwa lengo la kupima na kurasimisha ardhi kwa wingi zaidi kwa lengo la kuongeza thamani ya ardhi, kuondoa migogoro na kuongeza pato kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018; kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inaomba Bunge lako Tukufu liidhinishhe makadirio ya mapato na matumizi ya Fungu namba 48 kiasi cha shilingi 68,655,082,926; kati ya hizo, shilingi 43,255,082,296 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 25,400,000,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla bajeti ya mwaka 2017/2018, imeongezeka kwa asilimia 10.9 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2016/2017. Kuongezeka huku kumekwenda sambamba na kuongezeka kwa bajeti ya maendeleo kutoka shilingi bilioni 20 mwaka 2016/2017 hadi shilingi 25,400,000,000 mwaka 2017/2018. Ongezeko hili linatokana na Serikali kuongeza fedha katika miradi ya maendeleo. Aidha, Serikali imetenga shilingi 16,400,000,000 fedha za ndani na shilingi bilioni tisa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa mwaka 2017/2018 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishhe makadirio ya mapato na matumizi ya Tume ya Taifa ya Mipango na Matumizi ya Ardhi - Fungu namba 03 jumla ya shilingi bilioni 2.115. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 1.135 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi milioni 979.82 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Kamati inaipongeza Serikali kwa kuonesha juhudi ya wazi katika kutenga fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati; katika nchi yenye mipaka inayotambulika kisheria, ni dhahiri kuwa ardhi yake haiongezeki tena baada ya kuwekewa mipaka. Kutokuongezeka kwa ardhi hakumaanishi ya kuwa watu wake pamoja na mali zao haziongezeki. Uwiano huu wa ardhi isiyoongezeka na watu ambao wanaongezeka kwa kasi, unahitaji umakini mkubwa katika kupanga matumizi ya ardhi kwa kuwa ni rasilimali muhimu ambayo shughuli zote za kijamii, kiuchumi na kimaendeleo zinafanyika juu yake. Aidha, ardhi ni rasilimali adimu ambayo hushindaniwa na watu kwa ajili ya shughuli mbalimbali hivyo inafanya iwe na thamani kubwa. Kwa sababu hiyo ardhi inatakiwa kumilikiwa kwa kufuata sheria na taratibu za nchi yetu.

Mheshimwa Mwenyekiti, mapendekezo. Kwa kuwa sekta ya ardhi inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo za migogoro ya ardhi, ujenzi holela, kukosekana kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi na kwa kuwa changamoto hizo zinachangia kwa kiasi kikubwa kuzorotesha uchumi, nguvu kazi za Taifa na Utaifa, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza masuala 15 yafuatayo:-

(i) Kuipatia Tume ya Matumizi ya Ardhi rasilimali watu na fedha za kutosha kutekeleza majukumu ipasavyo ili Taifa lipunguze ama liepukane kabisa na migogoro ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini. *(Makofi)*

(ii) Kuongeza kasi ya kutoa elimu kwa umma juu ya matumizi ya ardhi kulingana na mipaka yake ili kupata uelewa wa pamoja juu ya ardhi na kukomesha kabisa uvamizi wa ardhi ambao umekithiri nchini. *(Makofi)*

(iii) Kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuanzisha Mabaraza ya Ardhi katika Wilaya zote nchini kwa mujibu wa sheria na kuwezesha yale Mabaraza ambayo yameanzishwa

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

lakini hayajaanza kutoa huduma kutokana na upungufu wa rasilimali watu na rasilimali fedha ili wananchi wasilazimike kwenda umbali wa muda mrefu. *(Makofi)*

(iv) Kuendelea kuwezesha mfumo wa kielektroniki wa kuhifadhi kumbukumbu za ardhi ili kasi ya kupeleka huduma hii kwenye Halmashauri iongezeke na kuongeza ufanisi katika utawala wa ardhi hapa nchini kwetu. *(Makofi)*

(v) Kutenga fedha za ndani za kutosha na kuzipeleka kwenye miradi kwa wakati ili kutekeleza miradi kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, mwisho lakini si kwa umuhimu nawapongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge hili. Mungu awajalie afya njema, hekima na busara katika kutekeleza wajibu huu mkubwa mliokabidhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Lukuvi, Naibu wake Mheshimiwa Angeline Mabula pamoja na Katibu Mkuu Dkt. Yamungu Kayandabila na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Moses Kusiluka, Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Wizara ambao wameipa Kamati ushirikiano wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano walionipa wakati wa kujadili na kuchambua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018, naomba niwatambue wote kwa ujumla wao.

Pia napenda kutoa shukrani za dhati kwa Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashillah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athumani Hussein, Makatibu wa Kamati Ndugu Gerald Magili, Ndugu Elieka Saanya, Ndugu Elihaika Mtui na Msaidizi wa Kamati hiyo Ndugu Jane Ndulesi kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha

taarifa hii kwa wakati. Aidha, nawashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, sasa naomba Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Fungu namba 48 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 jumla ya shilingi 68,655,082,926 na Fungu namba 03, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi jumla ya shilingi 2,115,371,822.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja, ahsante kwa wakati wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Silafu Maufi kwa niaba ya Mwenyekiti.

**TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**MAJUKUMU YA KAMATI NA MUUNDO WA TAARIFA**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

## 1.1 Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Fasili ya 7 (1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 inataja majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuwa ni:-

(a) Kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi;

(b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge chini ya wizara;

(c) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za wizara ; na

(d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara [ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Bajeti ya Wizara, Fungu 48 (Wizara) na Fungu 03 (Tume ya Matumizi ya Ardhi)]

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 98(1), (2), ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka sharti la Kamati za Kisekta, ikiwemo Kamati hii kufanya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kisha kuchambua bajeti ya wizara inazosisimamia. Naomba kutoa Taarifa kuwa Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kuchambua bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inahusisha Mafungu mawili: **Fungu 48** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na **Fungu 03** Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

## 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inafafanua mambo yafuatayo:-

**1. SEHEMU YA KWANZA**

Sehemu hii inahusu utangulizi

**2. SEHEMU YA PILI**

**1.1** Uchambuzi wa Majukumu Yaliyotekelezwa

**1.2** Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**1.3** Uchambuzi wa Taarifa Kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli.

**1.4** Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina.

**1.5** Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka 2016/2017.

**1.6** Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

**1.7** Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**1.7.1** Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2017/2018

**1.7.2** Uchambuzi wa Makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018

**3. SEHEMU YA TATU**

Sehemu hii inahusu Maoni na Ushauri wa Kamati; na Hitimisho

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA MAJUKUMU YALIYOTEKELEZWA KATIKA WIZARA

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu hii inajielekeza katika kutoa ufafanuzi wa masuala mbali mbali kwa mtiririko ulioelezwa katika kipengele 2.0 cha sehemu ya pili kwa namna ifuatayo;

#### 2.1 UKUSANYAJI WA MADUHULI KATIKA BAJETI YA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ilitarajiwa kukusanya jumla ya shilingi **billioni 111.77** kutokana na vyanzo mbali mbali vya mapato yanayotokana na sekta ya ardhi. Hadi kufikia Februari, 2017, Wizara ilikusanya jumla ya shilingi **bilioni 57.91** ambazo ni sawa na **asilimia 52** ya kiwango kilichokadiriwa kukusanywa kwa mwaka. Kati ya makusanyo hayo, shilingi **bilioni 51.04** sawa na **asilimia 88.19** ya makusanyo zinatokana na kodi ya pango la ardhi. Kamati inaona kuwa, endapo mfumo wa **Land Rent Management System** utatumiwa na Halmashauri zote nchini ni dhahiri kuwa lengo katika makusanyo linaweza kufikiwa kwa uhakika.

#### 2.2 UPATIKANAJI WA FEDHA KUTOKA HAZINA KATIKA BAJETI YA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/2017 Wizara iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 61,873,949,000/=**. Kati ya fedha hizo **shilingi 25,531,158,000/=** zilikuwa kwa ajili ya matumizi mengineyo, **shilingi 16,342,791,000/=** kwa ajili ya Mishahara na **shilingi 20,000,000,000/=** kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo **shilingi 10,000,000,000/=** ni fedha za ndani na **10,000,000,000/=** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2017, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi 28,414,164,022/=**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 9,994,249,148/=** zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi 10,793,695,560/=** kwa ajili ya

mishahara na **shilingi 7,626,219,314/=** ni fedha zilizopokelewa kwa ajili ya miradi ambazo ni sawa na **asilimia 38** ya bajeti ya mwaka 2016/2017. Kwa ujumla fedha zilizopokelewa hadi Februari, 2017 ni sawa na **asilimia 46** ya fedha zilizotengwa. Aidha uchambuzi unaonesha kuwa wizara ilifanyiwa uhamisho wa fedha nje ya fungu 48 **shilingi bilioni 3.3** kwa ajili ya kulipa deni la uaandaaji wa mipango kabambe ya majiji ya Arusha na Mwanza. Jumla ya **Shilingi bilioni 4.2** ni fedha za ndani ikijumuisha fedha zilizofanyiwa uhamisho na **shilingi bilioni 3.4** ni fedha za nje. Kwa ujumla, hadi kufikia Februari, 2017 Wizara ilikuwa imepokea **asilimia 39.2** ya fedha za matumizi mengineyo, **asilimia 69.7** fedha za mishahara na **asilimia 38** fedha za maendeleo ambapo uwiano wa tengeo la fedha za maendeleo na fedha za matumizi ya kawaida ni **asilimia 32.3** fedha za miradi ya maendeleo na **asilimia 67.7** fedha za matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, hali ya utoaji fedha lmeendelea kuwa ya kusuasua. Kushindwa kutoa fedha kwa wakati na kwa kiasi kilichoidhinishwa kunaathiri kwa kiwango kikubwa utekelezaji wa shughuli za Wizara hali inayochangia ongezeko la migogoro ya ardhi nchini.

### **2.3 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KATIKA BAJETI YA 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Fungu 48 iliidhinishwa jumla ya shilingi **13,000,000,000/** - kwa ajili ya mradi namba 4943 unaojulikana kama **Land Tenure Support Programme** ambao ni Mradi wa Umilkishaji Ardhi na unatekelezwa kwa majaribio katika Wilaya za **Ulanga, Kilombero** na **Malinyi** Mkoani **Morogoro**. Kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 3** ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 10** ni fedha za nje. Mradi huu unatekelezwa chini ya Kifungu 2001-Utawala wa Ardhi (*Land Administration*) cha Fungu 48.

#### **2.3.1 Matokeo ya Ukaguzi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa mradi huu uko kwenye hatua za utekelezaji. Hadi februari, 2017 Wizara



ilipokea jumla ya **shilingi bilioni 3.8** sawa na **asilimia 29.2** ya fedha zilizotengwa ambapo kati ya fedha hizo **shilingi milioni 400** ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 3.4** ni fedha za nje. Kamati ilijionea utekelezaji wa mradi huu ambapo kazi ya kupima mipaka ya vijiji imepunguza kwa kiasi kikubwa migogoro ya mipaka iliyokuwepo kwa kuwa programu hii imekuwa shirikishi na hivyo wanakijiji wanashiriki kikamilifu kwenye utekelezaji. Kamati ilishuhudia utatuzi wa mgogoro wa muda mrefu kati ya kijiji cha **Nkanu** na **Kanoro** ambao kupitia programu hii mgogoro huo umemalizika kabisa. Kamati inaiona hii kama hatua muhimu katika kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji. Kwa kuwa mafanikio ya mradi huu tayari yameshaonekana kwa maeneo yaliyofikiwa, Kamati inashauri Serikali kutenga fedha za kutosha ili kuweza kufikia maeneo mengi zaidi nchini ili kumaliza kabisa migogoro ya ardhi inayoendelea.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi huu unaonesha kuwa Serikali imechukua ushauri wa Kamati wa kuongeza fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka **asilimia 4.78** ya bajeti yote kwa mwaka wa fedha 2015/2016 hadi **asilimia 32.3** ya bajeti yote ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Pamoja na ongezeko hilo, Kamati hadi ilipofanya uchambuzi kuna miradi ambayo pamoja na kutengewa fedha haikupelekewa fedha kabisa. Hali hii ya fedha kutotolewa kabisa inasikitisha na ni wazi kuwa uwezekano wa Serikali kufikia malengo iliyojiwekea ni mdogo.

### **2.3.2 Maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati imebaini kuwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ilipanga kutekeleza **miradi mitano (5)** lakini ilitenga fedha za nje kwa ajili ya mradi mmoja tu wa **Land Tenure Support Programme**. Kutokana na hali hiyo Kamati ina maoni yafuatayo:-

a) Miradi yote ambayo haikutengewa fedha za nje upatikanaji wa fedha umekuwa wa kusuasua ambapo

wakati Kamati inafanya uchambuzi huu mwezi Machi, 2017, miradi mitatu (3) kati ya mitano haikuwa imepelekewa fedha zozote. Hali hii inazorotesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwani inaonekana kama vile miradi mingine sio kipaumbele cha Serikali;

b) Pamoja na kuwa mradi wa Umilikishaji Ardhi (LTSP) umetengewa fedha nyingi, kiasi kikubwa cha fedha hizi ni fedha za nje. Jambo hili linazorotesha utekelezaji wa mradi kwa kuwa utoaji wa fedha za nje ni mgumu huambatana na masharti magumu. Serikali haina budi kutenga fedha za ndani za kutosha ili kutekeleza programu hii kwa ufanisi na kwa kasi zaidi tofauti na ilivyo sasa;

c) Kutopatikana kwa fedha kwa wakati kunachangia kuzorotesha utekelezaji wa miradi; na

d) Kuendelea kutoa fedha kwa kusuasua kwa miradi ya maendeleo kunaongeza gharama za mradi.

## **2.4 UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa Fedha 2016/2017, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuboresha utekelezaji wa kazi za Wizara. Baadhi ya Ushauri umezingatiwa na kutekelezwa.

Kwa mfano, Kamati inaridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Serikali kupunguza gharama za nyumba zinazojengwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kwa kuwekeza kwenye miundombinu ya **maji, umeme na barabara** ambapo hapo awali shirika lilikuwa linabeba gharama hizo na kufanya bei ya nyumba zake kuwa juu na hivyo kutowasaidia wananchi wa kipato cha kati na cha chini ambao ndio walengwa wa mradi huu. Mfano mzuri wa utekelezaji huu ni nyumba zitakazojengwa eneo la **lyumbu Dodoma** ambapo Serikali kupitia iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA) watajenga

miundombinu ya barabara na maji. **Kamati inaamini kuwa utekelezaji huu utaendelezwa na mamlaka iliyochukua nafasi ya CDA baada ya kufutwa kwa amri ya Rais. Hatua hii itapunguza kwa kiasi kikubwa gharama za nyumba na kupanua wigo wa wananchi walengwa kunufaika.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua katika mradi wa Uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni kwa kuhamishia ofisi ya KDA kwenye ofisi ya Kanda ya Dar Es Salaam ili kupunguza gharama ya pango ilipokuwa imepanga wakati mradi wenyewe haujaanza kufanya kazi. **Ni maoni ya Kamati kuwa Serikali itazingatia ushauri wa kutenga fedha kwa ajili ya mradi huu ambao umechukua muda mrefu bila kuchukua hatua za utekelezaji.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, Kamati haikuridhisha na kasi ya uanzishwaji wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba katika wilaya zote nchini. Kila wilaya inatakiwa iwe na Baraza la Ardhi na Nyumba kwa mujibu wa Sheria ya Mabaraza Na. 2 ya mwaka 2002. Ni jambo la kusikitisha kuwa hadi sasa jumla ya **mabaraza 100** yaliyoanzishwa ni **mabaraza 53** pekee yanatoa huduma wakati mabaraza mengine **47** hayajaanza kutoa huduma kutokana na changamoto ya upatikanaji wa rasilimali watu na fedha. Hali hii inapelekea msongamano wa mashauri ya ardhi na kusababisha mashauri kuchukua muda mrefu kupata suluhu. **Kamati inaishauri Serikali kuweka kipaumbele cha bajeti kwenye uanzishwaji wa mabaraza haya ili kuongeza tija itakayowapunguzia wananchi adha ya kusafiri umbali mrefu kufuata huduma na kupunguza migogoro ya ardhi isiyo ya lazima.**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imezingatia ushauri wa Kamati kwa kutunga sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini Na. 7 ya mwaka 2016 ambayo kwa kiasi kikubwa itarekebisha mapungufu ya utwaaji wa maeneo bila kulipa fidia stahiki na kwa wakati. Sambamba na hilo Serikali imeunda Bodi ya Mfuko wa Fidia ambao utakuwa na jukumu la kujiridhisha kuwa fedha za fidia zipo kabla ya uthamini kufanyika.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla pamoja na nia njema ya Wizara kutekeleza ushauri wa Kamati bado changamoto kubwa ya fedha, vitendea kazi na rasilimali watu vimekuwa kikwazo kikubwa katika utekelezaji wa shughuli za wizara. **Ni maoni ya Kamati kuwa Serikali italipa kipaumbele suala la kuongeza bajeti kwa sekta hii ili kupambana na changamoto zinazoikabili.**

## **2.4 MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

### **2.4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara imepanga kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

a) Kugharamia majukumu muhimu ya wizara ikiwa ni pamoja na kununua vitendea kazi muhimu vya ofisi,  
b) Kugharamia malipo ya pango za ofisi za wizara zilizoko Dodoma, Makao makuu ya kanda nane (8) pamoja na taasisi zake,

c) Kugharamia huduma za intaneti, umeme, maji na simu kwa ofisi na taasisi zake zilizoko makao makuu ya wizara mjini Dodoma na ofisi za kanda,

d) Gharama za undeshaji magari ikijumuisha matengenezo na mafuta,

e) Kulipia stahili za watumishi ikiwa ni pamoja na kulipia stahili za likizo, na

f) Gharama za kuhamasisha ukusanyaji wa mapato.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na malengo yaliyowekwa na Wizara kwani yakitekelezwa kwa ukamilifu

yatachangia kupunguza migogoro ya ardhi na ujenzi holela mijini, na katika miji inayokua.

## 2.5 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara inatarajia kukusanya jumla ya shilingi **112, 050, 000,000/=** ikiwa ni ongezeko la **asilimia 0.3** ikilinganishwa na mapato ya mwaka 2016/2017 ya **shilingi bilioni 111.77**. Mapato haya yanatokana na tozo mbalimbali za sekta ya ardhi huku ada za ardhi (Land Rent) ikiingiza mapato zaidi ikilinganishwa na vyanzo vingine. Ongezeko la mapato linachangiwa kwa kiasi kikubwa na mfumo wa kielektroniki yaani *Land Rent Management System*. **Ni maoni ya Kamati kuwa Serikali itahakikisha mfumo wa *Land Rent Management System* unatumiwa na Halmashauri zote nchini ili kuongeza mapato yatokanayo na ada ya ardhi.**

**Mheshimiwa Spika**, katika eneo ambalo Serikali inapata mapato ya uhakika ni pamoja na mapato yatokanayo na tozo za ardhi iliyorasimishwa na ile iliyopimwa. Mpaka sasa ardhi ambayo imepimwa na kurasimishwa ni asilimia 15 tu ambayo ni ndogo sana. Serikali iongeze fedha kwa ajili ya kupima na kurasimisha ardhi na pia iingie ubia na makampuni binafsi kwa lengo la kupima na kurasimisha ardhi kwa wingi zaidi kwa lengo la kuongeza thamani ya ardhi, kuondoa migogoro na kuongeza pato kwa Serikali.

## 2.6 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inaomba Bunge lako Tukufu liidhinishhe makadirio ya mapato na matumizi ya fungu 48 kiasi cha **shilingi 68,655,082,926/=**. Kati ya fedha hizo, shilingi **43,255,082,926/=** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **25,400,000,000/=** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kwa ujumla bajeti ya mwaka 2017/2018 imeongezeka kwa asilimia 10.9 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2016/2017. Kuongezeka huku kumekwenda

sambamba na kuongezeka kwa bajeti ya maendeleo kutoka **shilingi 20,000,000,000/** mwaka 2016/2017 hadi shilingi **25,400,000,000/** mwaka 2017/2018. Ongezeko hili linatokana na Serikali kuongeza fedha katika miradi ya maendeleo. Aidha, Serikali imetenga **shilingi 16,400,000,000/** fedha za ndani na **shilingi 9,000,000,000/=** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishhe makadirio ya mapato na matumizi ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi **Fungu 03** jumla ya **shilingi 2,115,371,822/=**. Kati ya fedha hizo **shilingi 1,135,550,000/=** ni kwa ajili ya mishahara na **shilingi 979,821,822/=** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuonesha juhudi za wazi katika kutenga fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, katika nchi yenye mipaka inayotambulika kisheria, ni dhahiri kuwa ardhi yake haiongezeki tena baada ya kuwekewa mipaka. Kutoongezeka kwa ardhi hakumaanishi kuwa watu wake pamoja na mali zao haviongezeki. Uwiano huu wa ardhi isiyoongezeka na watu wake ambao wanaongezeka kwa kasi, unahitaji umakini mkubwa katika kupanga matumizi ya ardhi kwa kuwa ni rasilimali muhimu ambayo shughuli zote za kijamii, kiuchumi na kimaendeleo zinafanyika juu yake. Aidha, ardhi ni rasilimali adimu ambayo hushindaniwa na watu kwa ajili ya shughuli mbalimbali hivyo kuifanya iwe na thamani kubwa. Kwa sababu hiyo ardhi inatakiwa kumilikiwa kwa kufuata sheria na taratibu za nchi yetu.

**Mheshimwa Spika**, kwa kuwa asilimia 80 ya wananchi wa vijijini wanategemea ardhi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi, na kwa kuwa mara nyingi viongozi wa vijiji huingia mikataba tofauti na taratibu na wawekezaji, ni dhahiri

kwamba Serikali inatakiwa kuwa makini katika suala la umilikishwaji ardhi kwa wawekezaji kwa kutoa elimu kwa viongozi wa vijiji na wananchi kwa ujumla ili kupunguza migogoro isiyo ya lazima.

### **3.1 MAPENDEKEZO**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa Sekta ya Ardhi inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo za migogoro ya ardhi, ujenzi holela, kukosekana kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi na kwa kuwa changamoto hizo zinachangia kwa kiasi kikubwa kuzorotesha uchumi, nguvu kazi na utaifa, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza masuala kumi na tano (15) yafuatayo:

a) kuipatia Tume ya Matumizi ya Ardhi rasilimali watu na fedha za kutosha kutekeleza majukumu yake ipasavyo ili Taifa lipunguze ama liepukane kabisa na migogoro ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini;

b) Kuongeza kasi ya kutoa elimu kwa umma juu ya matumizi ya ardhi kulingana na mipaka yake ili kupata uelewa wa pamoja juu ya ardhi na kukomesha kabisa uvamizi wa ardhi ambao umekithiri nchini;

c) Kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuanzisha mabaraza ya ardhi katika wilaya zote nchini kwa mujibu wa sheria na kuyawezesha yale mabaraza ambayo yameanzishwa lakini hayajaanza kutoa huduma kutokana na upungufu wa rasilimali fedha ili wananchi wasilazimike kwenda umbali mrefu kutafuta huduma;

d) Kutekeleza kwa ukamilifu sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini ya mwaka 2016 ili kusimamia utaratibu wa kutotwaa ardhi ya wananchi kwa matumizi ya serikali au wawekezaji bila ya Mthamini Mkuu kujiridhisha kwamba fedha za kulipa fidia zipo tayari;

e) Kusimamia sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini ipasavyo kwa lengo la kutatua migogoro ya

matumizi ya ardhi inayoendelea kuibuka kwa kasi hapa nchini ambayo hutokana na baadhi ya wathamini kutozingatia maadili ya uthamini;

f) Kuendelea kuuwezesha mfumo wa kielektroniki wa kuhifadhi kumbukumbu za ardhi (ILMIS) ili kasi ya kupeleka huduma hii kwenye halmashauri iongezeke na kuongeza ufanisi katika utawala wa ardhi aidha,;

g) longeze kasi ya kubatilisha umiliki wa mashamba yote ambayo yalimilikishwa kwa wawekezaji lakini hayajaendelezwa ili kuyabaini kwa lengo la kuyapangia matumizi upya na kuendelea kutatua migogoro inayosababishwa na upungufu wa ardhi;

h) Kupitia Hazina izihimise halmashauri zote zilizokopa kwa ajili ya upimaji viwanja kurejesha fedha hizo ili ziweze kukopeshwa kwa Halmashauri zingine na hivyo kufanya zoezi la upimaji kuwa endelevu;

i) Kusimamia na kutekeleza Sheria ya Mipango miji kwani mbali ya changamoto ya ukuaji wa kasi wa miji, kumekuwepo pia na usimamizi hafifu wa sheria unaopelekea uvunjifu wa sheria zilizopo na ujenzi holela wa makazi;

j) Mpango kabambe wa mipango miji usiishie tu kupanga miji mikubwa bali ipanue wigo hadi kwenye miji inayokua ili ikue na uwiano mzuri wa Majiji na miji iliyopangwa vizuri;

k) Kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya kuwezesha Taasisi za Utafiti zinazojishughulisha na Utafiti wa Vifaa vya Ujenzi na Nyumba bora. Mfano mzuri ni Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na vifaa vya ujenzi wa nyumba bora kwa bei nafu. Lengo ni kuwawezesha kufanya tafiti nyingi zaidi na kuwafikia wananchi wengi zaidi;

l) Kuiwezesha Bodi ya Mfuko wa Fidua ya ardhi ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ;



m) Kutenga fedha za ndani za kutosha na kuzipeleka kwenye miradi kwa wakati ili kutekeleza miradi kwa ufanisi;

n) Wizara iendelee kufanya kazi kwa pamoja na wadau wengine wa ardhi:- TAMISEMI, sekta ya Maliasili, sekta ya Kilimo na Mifugo ili kwa pamoja ipatikane mikakati endelevu ya kukabiliana na migogoro kati ya watumiaji wa ardhi hususan wakulima na wafugaji; na

o) Wadau wote ambao ni wasimamizi na watekelezaji wa sheria za ardhi wahakikishe Sheria za ardhi zinaboreshwa na kusimamiwa kikamilifu kwa lengo la kuondoa kabisa migogoro baina ya watumiaji wa ardhi.

#### 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini si kwa umuhimu, nawapongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kulingoza Bunge hili. Mungu awajalie afya njema, hekima na busara katika kutekeleza wajibu huu mkubwa mliokabidhiwa.

**Mheshimiwa Spika**, napenda na kumshukuru Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhe. William V. Lukuvi, (Mb) na Naibu Waziri Mhe. Dkt. Angelina Lubala. Mabula, (Mb), pamoja na Pamoja na Katibu Mkuu Dkt. Yamungu Kayandabila na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Mosses Kusiluka, Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na wafanyakazi wa Wizara wote ambao wameipa Kamati ushirikiano wa kutosha.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano walionipa wakati wa kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

- |                                |   |              |
|--------------------------------|---|--------------|
| 1. Mhe. Atashasta Nditiye, Mb  | - | Mwenyekiti   |
| 2. Mhe. Kemirembe J. Lwota, Mb | - | M/Mwenyekiti |

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

3. Mhe. Fredy Atupele Mwakibete, Mb	-	Mjumbe
4. Mhe. Devota Minja , Mb		"
5. Mhe. Grace Sindato Kiwelu, Mb		"
6. Mhe. Jaffar Sanya Jussa, Mb		"
7. Mhe. Joshua Samweli Nassari, Mb		"
8. Mhe. Khalifa salim Suleimani, Mb		"
9. Mhe. Dkt Godwin Aloyce Mollel, Mb		"
10. Mhe. Magdalena Hamis sakaya, Mb		"
11. Mhe. Mary Pius Chatanda, Mb		"
12. Mhe. Musukuma Joseph Kasheku, Mb		"
13. Mhe. Lucy Fidelis Owenya, Mb		"
14. Mhe. Pauline Philipo Gekul, Mb		"
15. Mhe. Risala Kabongo, Mb		"
16. Mhe. Shabani Omari Shekilindi, Mb		"
17. Mhe. Silafu Jumbe Maufi, Mb		"
18. Mhe. Yussuf Haji Khamis, Mb		"
19. Mhe. Yussuf Salim Hussein, Mb		"
20. Mhe. Zainabu Nuhu Mwamwindi, Mb		"
21. Mhe. Sebastian Simon Kapufi, Mb		"
22. Mhe. Richard Mganga Ndassa, Mb		"
23. Mhe. Omari Abdallah Kigoda, Mb		"
24. Mhe. Salma Mohamed Mwasu, Mb,		"
25. Mhe. Neema Willium Mgaya, Mb		"
26. Mhe. Nape Moses Nnauye, Mb		"

**Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Didimu Kashiilillah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussen, Makatibu wa Kamati Ndugu Gerald Magili, Ndg. Elieka Saanya na Ndg Elihaika Mtui, Msaidizi wa Kamati Ndg Jane Ndulesi kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha Taarifa hii kwa wakati. Aidha, nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi **Fungu 48** kwa mwaka **2017/2018** jumla

ya shilingi 68,655,082,926/= na Fungu 03 Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi jumla ya shilingi 2,115,371,822/=.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Eng. Atashasta J. Nditiye, (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII**

Mei, 2017

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, karibu. *(Makofi)*

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu kwa neema za Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2017/2018 na kwa sababu ya urefu wa hotuba yenyewe, naomba hotuba nzima na kwa bahati nzuri hajapigwa panga, iwekwe yote katika *Hansard*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukurani kwa uongozi mzima wa Kambi ikiongozwa na Mheshimiwa Freeman Mbowe kwa kuendelea kutuamini mimi na Mheshimiwa Salma Mwassa kuisimamia na kuisemea Wizara hii. Mungu aendeleo kuwapa nguvu na uvumilivu ya kuyakabili yote na naamini kwa nguvu za Mungu tutavuka na kuvishinda vikwazo vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo mkunjufu niendeleo kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Bukoba Mjini *(Bukoba Town)* kwa ushirikiano wanaonipa kwa kuwawakilisha na kuliongoza Jimbo lao. Kwa dhati kabisa

nimshukuru Mstahiki Meya wa Manispaa ya Bukoba, Chief Kalumuna, Madiwani wote wa Manispaa ya Bukoba bila kujali tofauti zao za kivyama, Mkurugenzi na Watendaji wake wote, Mwenyekiti wa Chadema Bukoba Mjini Jenerali Victor Sherejey na Kamati yake ya utendaji kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa. Ushirikiano ninaopata kutoka kwa viongozi wenzangu unalifanya Jimbo la Bukoba Manispaa kuwa sehemu ya kuigwa ambapo figisu na tofauti za kivyama haviwi kikwazo cha kuwaletea wananchi maendeleo wanayoyahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee naomba niishukuru familia yangu yote ambayo inaendelea kunipa moyo katika kazi hii ambayo inaninyima muda mwingi wa kuwa nao muda mwingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pole kwa wote waliopatwa na majanga mbalimbali tetemeko, njaa, mafuriko, ukame, ajali mbaya, ugumu wa maisha na kadhalika. Kubwa ni kuwa na subira na kuyaombea na kuyaunga mkono yale tunayoyaainisha kama sababu na kikwazo cha maisha na maendeleo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi nchini. Itakumbukwa kuwa tarehe 01 Novemba, 2013 Bunge lako Tukufu liliunda Kamati Teule kwa ajili ya kuchunguza chanzo cha migogoro ya ardhi nchini. Hoja ya kuundwa kwa Kamati Teule iliridhiwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati Teule ya Bunge iliyoundwa iliwasilisha taarifa yake Bungeni tarehe 06 Februari 2015; pamoja na mambo mengine taarifa ya Kamati ilieleza aina ya migogoro ya ardhi nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ingependa kurejea baadhi ya masuala muhimu yaliyoibuliwa na Kamati Teule ya Bunge wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati Teule iliainisha migogoro ya wakulima na wafugaji, migogoro kati ya wakulima na wawekezaji, migogoro kati ya wafugaji na wawekezaji, migogoro kati ya wakulima/wafugaji dhidi ya

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

maeneo ya hifadhi na migogoro kati ya wananchi na Serikali. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaongeza mgogoro mwingine ambao ni mgogoro unaotokana na mipaka ya maeneo ya utawala kama vile vijiji/mitaa na hata ngazi zingine za maeneo ya utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati Teule ya Bunge iliweka bayana kuwa hali ya migogoro imekuwa ya muda mrefu pamoja na kuwa Serikali imekuwa ikileta mipango, sera na hata sheria mbalimbali kukabiliana na tatizo hili. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaunga mkono kauli ya Kamati Teule ya Bunge kuwa hali ya migogoro ya ardhi nchini isipotafutiwa ufumbuzi inaweza kuhatarisha amani na mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilieleza sababu ambazo ni chanzo cha migogoro ya ardhi nchini kama ifuatavyo:-

(i) Kutokutengwa kwa maeneo mahususi ya kilimo na ufugaji;

(ii) Kutokupimwa na kutokubainishwa kwa mipaka ya vijiji;

(iii) Watu wachache kumiliki maeneo makubwa ya ardhi;

(iv) Wawekezaji kutokuzingatia na kufuata sheria za uwekezaji kwenye ardhi;

(v) Rushwa miongoni mwa watendaji wa Serikali;

(vi) Kutowalipa wananchi fidia kamilifu na kwa wakati; na

(vii) Tofauti ya Sera ya Ardhi na Sera ya Mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watu wachache kumiliki maeneo makubwa ya ardhi, Kambi Rasmi ya Upinzani

Bungeni ingependa kwa mara nyingine kuikumbusha Serikali juu ya Hoja Binafsi ya aliyekuwa Waziri Kivuli wa Ardhi, Mheshimiwa Halima Mdee katika kipindi cha mwaka 2010-2015 ambaye alieleza kwa undani juu ya uwekezaji kwenye mashamba makubwa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuleta Bungeni taarifa ya ukaguzi wa mashamba makubwa nchini ili ijadiliwe na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tuliweka bayana orodha ya watu wanaomiliki mashamba makubwa na kusababisha uhaba wa ardhi kwa wananchi. Orodha ya wanaohodhi mashamba makubwa wapo pia wanasiasa (vielelezo tumeviambatanisha). *(Makofi)*

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda Serikali kutoa kauli juu ya mashamba hayo ambayo yalionekana ni muhimu kurudishwa Serikalini kama agizo la Bunge limeshatekelezwa. Katika hili tuomba tofauti za kiitikadi ziwekwe pembeni, wasiwepo baadhi ya wanasiasa wanaoshughulikiwa na baadhi ya wanasiasa wanaotoka chama fulani hawashughulikiwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wawekezaji kukodisha mashamba kwa wananchi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kueleza kuwa tatizo hilo bado lipo na Serikali inashindwa kuchukua hatua hata baada ya kushauriwa hivyo na Kamati Teule ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata baadhi ya kauli na matendo ya viongozi wa Serikali inakuwa pia chanzo cha migogoro. Itakumbukwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam aliutangazia umma kuwa amekabidhiwa ardhi kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda. Waziri mwenye dhamana naye akatangaza wazi kuwa mwekezaji huyo sio mmiliki wa ardhi, maana yake Mkuu wa Mkoa aliingizwa kwenye choo cha watu fulani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa viongozi wa Serikali ambao

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

hawahusiki na masuala ya ardhi kuacha kutafuta umaarufu kupitia ardhi ya Watanzania. Aidha, Kambi Rasmi inahoji kama utaratibu wa viongozi wa Serikali hiyo hiyo na chama hicho hicho kushindania umaarufu kwenye vyombo vya habari kama unatupeleka sehemu salama kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya muda mfupi ya Kamati Teule kwa Serikali. Baadhi ya mapendekezo ambayo Kamati ilipendekeza ni kama ifuatavyo:-

(i) Serikali iharakishe usuluhishi wa mgogoro Wilayani Kiteto;

(ii) Kupima ardhi ya Mkoa wa Morogoro kama mpango wa dharura;

(iii) Serikali ifute na kuyapima upya mashamba ya wawekezaji ambayo yametelekezwa;

(iv) Serikali ipime upya maeneo ya vijiji vyenye migogoro;

(v) Serikali iangalie upya uamuzi wa kupanua mipaka ya maeneo ya hifadhi ili makazi na shughuli za kiuchumi za wananchi zipanuliwe;

(vi) Serikali itwae maeneo ambayo yalibinafsishwa bila kuzingatia mipaka; na

(vii) Serikali ilete Bungeni marekebisho ya sheria kwa ajili ya kuweka vigezo vya usajili wa vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaikumbusha Serikali kuhusu ahadi ya Waziri Mkuu aliyoitoa Bungeni kuwa Serikali italetta taarifa ya utekelezaji wa Maazimio mbalimbali ya Bunge. Tunaomba taarifa ya utekelezaji wa Kamati Teule ya Bunge kuhusu masuala ya migogoro ya ardhi iletwe Bungeni haraka. Ni muhimu taarifa ya Serikali ikaletwa Bungeni ili ijadiliwe kwa sababu hadi sasa

tunavyozungumza hapa bado Kiteto kuna mgogoro, Kilosa kuna mgogoro, kwani mkulima mmoja Ndugu Augustino Mtitu wa Jimbo la Mikumi alipigwa mkuki na wanaodaiwa kuwa wafugaji. Mkulima mwingine Ndugu Rajab Ayoub wa Mbigiri, Wilayani Kilosa alijeruhiwa kwa sime akiwa shambani mwake na wanaodaiwa kuwa wafugaji. Aidha, yapo matukio kadhaa ya mifugo kupewa sumu au kujeruhiwa moja kwa moja na wanaodaiwa kuwa ni wakulima. Hii ni ishara kuwa matukio haya yanazidi kutokea kwa sababu Serikali imeyafungia Maazimio ya Bunge kabatini bila kuchukua hatua za dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi yetu inazo taarifa kuwa moja ya sababu za migogoro katika Mkoa wa Morogoro ni baadhi ya viongozi wa vijiji na mitaa kuuza ardhi mara mbili kwa wakulima na wafugaji. Aidha, baadhi ya wakulima huuza ardhi kwa wafugaji na baadaye kukana mikataba/makubaliano ya awali. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwachukulia hatua kali za kisheria viongozi na watu wote ambao wamekuwa sehemu ya migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu (*property tax*); mwaka wa fedha unaokwisha mwezi Juni 2017, Serikali iliweka utaratibu wa kisheria wa kuziondoa Halmashauri kwenye mamlaka ya kukusanya kodi ya majengo (*property tax*) na kuikabidhi kazi hiyo TRA, huku Serikali ikijua kuwa hiki ni chanzo muhimu kwa mapato ya Halmashauri zetu nchini.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ililiona jambo hili kama mkakati wa Serikali kupunguzia/kuzinyima mapato Halmashauri zetu hasa zinaongozwa na Kambi ya Upinzani na kuongozwa na UKAWA. Ieleweke kuwa Halmashauri zimekuwa zikikusanya mapato kwa ajili ya kuendesha miradi ya maendeleo.

Kwa hiyo, Kambi inaona kwamba haukuwa uamuzi sahihi kutunga sheria ya kuondoa vyanzo hivi kwenye Halmashauri. Kufutwa kwa kifungu kilichokuwa kinazipa Halmashauri jukumu la kukadiria na kukusanya kodi za



mapato kimeziyumbisha sana Halmashauri zetu kwani chanzo cha kodi ya majengo kilikuwa ni mojawapo ya chanzo kikubwa cha mapato ya Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mjadala wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI tulieleza wazi kuwa taarifa ya Serikali inaonyesha kuwa kodi iliyokusanywa na TRA ni shilingi milioni 4,762 kati ya zilizokuwa zimetarajiwa milioni 29,000 sawa na aslimia 17 tu ambayo ilitarajiwa kukusanywa na TRA. Kwa takwimu hizi TRA imeonyesha wazi haina uwezo. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuleta tena marekebisho ya sheria hii ili ifanyiwe marekebisho chanzo hiki kirudishwe katika Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali bado inang' ang'ania chanzo hiki, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri majengo yagawanywe kwenye madaraja kama vile majengo makubwa ya kibiashara, *residential apartments*, na majengo mengine makubwa kama itakavyoamuliwa ili kodi hizo zikusanywe na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) lakini majengo madogo ya biashara na nyumba za makazi kodi yao ikusanywe na Halmashauri ili kuongeza ufanisi wa TRA katika ukusanyaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi ya ardhi. Ni takwa la kisheria kupitia kifungu cha 22 cha Sheria ya Ardhi kuwa ardhi yoyote inayomilikiwa kwa mujibu wa sheria kulipiwa kodi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina tatizo na hatua zinazochukuliwa na Wizara kuhakikisha kuwa kila mwenye miliki ya ardhi nchini analipa kodi kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa. Waziri mwenye dhamana ya ardhi alitoa maelekezo mwezi Aprili mwaka huu kuwa wananchi wote wanaomiliki ardhi iwe imepimwa au haijapimwa wanatakiwa kulipia ardhi hiyo na hapa amezungumza na kusesitiza.

Ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuwa agizo hilo la Waziri ni kinyume na Sheria ya Ardhi kwa kuagiza kodi kulipwa kwa ardhi ambayo haijasajiliwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kusitisha agizo hilo kwa sababu

wanakwepa jukumu la kupima ardhi badala yake wanatoa maelezo ambayo ni kinyume cha sheria. Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kuwa kama Serikali inaona uamuzi wa kutoa maagizo hayo ni tija kwake ni vema ikaleta marekebisho ya sheria hapa Bungeni kuliko kuendelea kufanya hivyo kinyume na taratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapenda kusisitiza kuwa tamko hili la Waziri linakiuka Sheria ya Ardhi Na. 4 na Na. 5 ya mwaka 1999 inayotaka kodi ya ardhi ilipwe kwenye maeneo yaliyopimwa. Tunataka Serikali na Waziri atakapokuja hapa atoe ufafanuzi juu ya suala hilo la maeneo ambayo hayajapimwa, je, yatalipishwaje kodi na kwa utaratibu upi kwani watu hao hawana nyaraka zozote za umiliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatakiwa kuwekeza katika kusimamia upimaji maeneo yote ambayo hayajapimwa ili kutoa miliki kwa wahusika kwani kwa kufanya hivyo itapanua wigo wa mapato, itapandisha thamani ya ardhi, itapunguza au kuondoa migogoro, itawapa fursa wananchi kutumia ardhi kama dhamana, itavutia uwekezaji, itasaidia utunzaji bora kumbukumbu za ardhi na itaweka hata mandhari nzuri za maeneo yetu.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa tamko hilo la Serikali ni kukimbia jukumu lake la msingi la kuhakikisha inapima ardhi yote. Kama Serikali itatumia njia hii, ni maoni ya Kambi ya Upinzani Bungeni kuwa itazalisha migogoro ya ardhi lukuki hasa kwenye Miji, Manispaa na Majiji kwa sababu udanganyifu utakuwa mkubwa. Ieleweke kabisa kuna watu matapeli watumia sababu za kulipia kodi ya ardhi kama sehemu ya kutaka kupewa miliki ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watumishi wa ardhi Katika Halmashauri. Wakati wa Bunge la Kumi, Mheshimiwa George Simbachawene aliyekuwa Waziri alitoa ahadi ya kwamba Serikali ingewahamishia watumishi walioko katika Halmashauri kuwa chini ya Wizara moja kwa moja ili kupunguza malalamiko ambayo yalikuwa yanatolewa. Tunaamini Serikali haikutoa ahadi hiyo kwa bahati mbaya.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepigwa na butwaa kwa sababu Serikali ya Awamu ya Nne ilikuwa chini ya CCM na Serikali ya Awamu ya Tano ipo chini ya CCM, lakini tunashangazwa na sababu zilizotolewa za kushindwa kuanzisha mchakato wa kuhamisha ajira ya watumishi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia randama ya Wizara imeeleza kuwa Serikali inaendelea na kutekeleza dhana ya kugatua madaraka (*Development by Devolutions*) kwenda katika ngazi za msingi. Hivyo, utaratibu wa kuhamisha ajira za watendaji wa sekta ya ardhi kutoka Halmashauri utakinzana na dhana hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni ishara kuwa ahadi na *commitment* za Serikali zilizopita zilikuwa ni hewa. Kwa hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako Tukufu sababu za ziada zilizopelekea kutotekeleza ahadi yake ya awali iliyoitoa hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuundwa kwa Mamlaka ya Kusimamia Sekta ya Milki nchini; mwaka 2011 wakati wa mkutano wa kwanza wa Bajeti wa Bunge la kumi, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni alishauri umuhimu wa kuundwa kwa mamlaka ambayo itasimamia sekta ya ujenzi hasa ujenzi wa majengo makubwa. Katika randama za Wizara hii kwa mwaka huu, Serikali imesema italeta Muswada utakaounda Mamlaka ya Sekta ya Miliki nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaunga mkono kuundwa mamlaka hiyo kama ilivyokuwa imeshauri miaka iliyopita lakini inapata mashaka na nia ya Serikali ya kuendelea kuchelewa kuleta Muswada huo Bungeni.

Aidha, kupitia randama za Wizara, Serikali imeeleza kuwa tayari imekamilisha maandalizi ya utungwaji wa Sheria

ya Mawakala wa Ardhi (*Real Estate Agents Act*) na tunashauri sheria iwe moja ambayo itakuwa inasimamia sekta ya miliki na mawakala kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya fidia kwa wananchi; kwa niaba ya wananchi wa Bukoba, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Waziri na Naibu Waziri wa Maji na uongozi pamoja na wasimamizi wa BUWASA (*Bukoba Urban Water Supply*), kwa kutimiza ahadi iliyotolewa katika Mkutano wa Bunge la Bajeti hapa nilipokamata shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushukuru kwa kuwa wananchi hao sasa wamelipwa, ingawa bado wanadai riba kwa sababu malipo yale yalichelewa. Mimi nashukuru kwa upande wa Bukoba, lakini bado kuna matatizo katika baadhi ya maeneo mengine mengi nchini yanayolalamikia kutolipiwa fidia naomba yalipwe haraka kwa mujibu wa sheria zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 20 Mei, 2015, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa maelekezo ya Rais ilitoa ahadi ya kuwalipa fidia watu wa Dar es Salaam katika eneo la Mloganzila. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepitia vitabu vya bajeti na kubaini kwamba hakuna fedha zozote zilizotengwa. Tunataka kujua hawa watu watalipwa kutoka fungu lipi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bomoabomoa ya Kimara - Kiluvya Jijini Dar es Saalam; katika miaka 1970, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya utawala wa Baba wa Taifa ilitekeleza sera za Chama cha *TANU* na ilianzisha Vijiji vya Ujamaa katika kutekeleza mpango kabambe wa Operesheni Vijiji. Katika Mkoa wa Dar es Salaam miongoni mwa vijiji vya ujamaa vilivyoanzishwa na kupewa usajili kando ya barabara ya Morogoro ni pamoja na Kijiji cha Kimara, Kijiji cha Mbezi, Kijiji cha Kibamba na Kijiji cha Kiluvya.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uthibitisho wa kwanza kwa upana wa hifadhi ya barabara ya Morogoro kwa eneo la Ubungo hadi TAMCO Kibaha ni mita 22.85 tu na siyo hadi mita 121.92 zinazozungumzwa sasa. Ndiyo maana wakati wa ujenzi wa barabara ya Morogoro mwanzoni mwa miaka ya 1970 nyumba za wananchi zilizoangukia ndani ya mita 22.85 ndiyo zilizotakiwa kuondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uthibitisho wa pili, pale Serikali ilipowahamishia wananchi katika vijiji vilivyotajwa hapo juu, ikawajengea majengo ya huduma mbalimbali za kijamii kama vile shule ya msingi pale Mbezi, zahanati ya Kibamba, hospitali na nyumba za watumishi katika kijiji cha Kibamba. Majengo haya yalijengwa nje kidogo ya mita 22.85 toka katikati ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka 2000, majengo ya wananchi, majengo ya Serikali yaliyoko ya mita 22.85 yamekuwa yanapigwa alama ya X. Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuhoji hivi kweli Serikali inaweza kuvamia hifadhi za barabara na kujenga majengo kwa shughuli zingine za maendeleo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uthibitisho wa tatu, taasisi ya kiserikali Halmshauri ya Jiji na Maafisa Ardhi wa Wilaya waliwapimia wananchi waliogawiwa wakati wa Operesheni Vijiji kwa kuacha hifadhi ya barabara ya upana wa mita 22.85 na ambazo zinaendelea kulipiwa kodi ya ardhi hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uthibitisho wa nne, mkazi mmoja wa Kimara aitwaye Ndugu Joseph Marwa aliiandikia barua Wizarani Kumb.Na TRM/0.10/9/47 na kajibiwa na barua iliyowekwa saini na Ndugu A. K. Fuko kwa niaba ya Katibu Mkuu ikimwambia kwamba yeye nje ya barabara kwa mita kumi, hivyo hahusika na fidia na hupaswi kuondoka pale alipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inajiliza licha ya uthibitisho wote huu na mambo yote tuliyoyaanisha hapa, upana ambao unahalalishwa ni upana wa mita 22.8 huu upana wa mita 121 unatoka wapi? Kwa nyakati tofauti kuanzia mwaka 2000 hadi 2004 wananchi wanaoishi pembezoni mwabarabara ya Morogoro kati ya Ubungo na TAMCO Kibaha wamejikuta na sintofahamu juu ya hatma ya mali na maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mambo yote tuliyoyazungumza tunaomba kupitia kwa Serikali itakapokuwa inajibu tueleze mita sahihi za pale Ubungo hadi Kibaha ni mita ngapi ambazo zinakubalika kwa mujibu wa sheria? Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kuwa kuna shauri lililopo Mahakamani lakini tunaomba ufafanuzi utolewe hapa kwa mita halali ni zipi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeeleza ya migogoro ya ardhi ya Pugu Kajungeni bado kuna migogoro pale ambako watu wameingiliwa, kuna migogoro ambayo bado imeendelea kutokea uwanja wa ndege watu waliohamishwa bado hawana amani kwa sababu hawajakabidhiwa ardhi na wengine ambao walichukuliwa maeneo yao hawajalipwa fidia, tunaomba Serikali itoe maelezo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna migogoro mingine ambayo bado ipo ya vijiji na hifadhi ya wanyama. Huko Serengeti bado kuna sintofahamu, kumekuwa na migogoro kati ya kumekuwa na mgogoro kati ya hifadhi ya Serengeti na Vijiji vya Merenga, Machochwe, Nyamakendo, Mbalibali, Tamkeri, Bisarara, Mbilikiri na Bonchugu, tunaomba Serikali itoe maelezo migogoro hii itaisha lini? Itigi nako bado kuna migogoro kati ya wawekezaji na wananchi wanaoishi maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakuu wa Wilaya na Mkoa kuingilia majukumu ya Mabaraza ya Ardhi, kumekuwa na mchezo wa Wakuu wa Wilaya na Mkoa wanaingilia Mabaraza ya Ardhi. Katika gazeti la Nipashe, Mkuu wa Mkoa wa Kigoma wakati huo aliamuru kumtoa ofisini Mwenyekiti

wa Baraza la Ardhi la Wilaya ya Kigoma Mheshimiwa Kimm kwa kuwatumia Usalama wa Taifa na Polisi. Kama hiyo haitoshi Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni na yeye alinukuliwa na kituo cha Radio akiingilia maamuzi ya Baraza, tunaomba maelezo yatolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NHC* na nyumba za bei nafuu; Shirika letu la Nyumba la Taifa limeshindwa kabisa na inabidi likiri kwamba limeshindwa kuwapa wanafunzi nyumba za bei ya nafuu. Tunaomba kwa kuwashauri tu waingie kwenye *google* sasa hivi dunia ukiingia kwenye *google* kuna nchi zilizoendelea na ambazo za uchumi wa kati zinafyatua nyumba za bei nafuu hata za Dola 4500 sasa wao nyumba za 40,000,000 hatuamini kama ni nafuu kwa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kuwezesha umilikishaji wa ardhi, mradi huu ambao unafadhiliwa kwa pesa za nje tunaona zimeshindwa kutengewa fedha za kutosha na nashukuru Kamati imeweza kuliona hilo na imetoa ufafanuzi mbalimbali. Miradi ya urasimilishaji kutokana na changamoto za kibajeti Wizara imeshindwa kuhudumia miradi hii ya urasimishaji kama vile mradi wa Dar es Salam maeneo ya Kimara ambao ulikuwa wa majaribio pamoja na Waziri kusema kwamba hakuna matatizo, sisi tunafikiri anaficha mambo, hii ni kuficha ugonjwa lakini kifo kinaweza kumuumbua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani tunashukuru na kuyapongeza maeneo yote ambayo yamekuwa na mwamko katika utekelezaji wa mpango wa urasimishaji na tunampongeza Mheshimiwa Waziri kwamba amekuwa anahudhuria hafla za kuzindua. Tunapongeza Mji wa Bukoba *Town* umeanza programu hii, Karagwe huko Kyaka Misenyi, Wilaya ya Ilemela na Nyamagana wamekuwa na mradi huu, tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa Wizara iingilie kati kuhakikisha mradi huu wa kurasimisha unakwenda kwa kasi. Watu wanaofanya shughuli hii tunaomba wapewe

msaada kuhakikisha wanapewa usaidizi na makampuni yanayohusika yapewe msaada kwani watendaji ndani ya Halmashauri wameonekana kuwanyanyapaa watu hawa kwa sababu inaaminika wamewaingilia kwenye ulaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hati za kimila bado hazijatoa matumaini kwa wananchi wenye nazo kwani hawakopeshwi, tunataka Serikali ituletee takwimu ni watu wangapi ambao wameweza kukopeshwa na ni benki gani zinatoa mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa watumishi wa sekta ya ardhi; tunataka kuileza Serikali bado kuna upungufu mkubwa wa watumishi katika Halmashauri. Mfano, Ngara hakuna mtumishi hata mmoja wa ardhi, sasa tunategemea hii sekta ya ardhi itaendeshwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matatizo ya mashamba ya ushirika, mfano, Garagagua Siha, kuna matatizo kweli kweli. Mashamba ambayo *KNCU* iliyatoa kama *collateral*, matokeo yake yakachukuliwa, tunaomba Serikali iingilie kati ili wananchi waweze kupata ardhi kwani tatizo la ardhi Wilaya ya Hai ni kubwa mno. Pia kumekuwa na matatizo ya mashamba mengine ya ushirika yaliyoko katika Wilaya ya Hai, Mkoani Kilimanjaro ambapo baadhi ya Vyama vya Msingi wameyatumia kwa muda mrefu kuyakodisha kwa wananchi kila msimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba mashamba haya yapimwe na kupewa wananchi ambao kimsingi wana matatizo makubwa ya ardhi. Tunaomba pia Serikali eneo la sehemu ya Kiwanda cha *Mashine Tools* ambacho kwa sasa hakizalishi, tunaomba ardhi hii ipewe Halmashauri ya Hai ambayo inaweza kuruhusiwa kujenga Mji Mdogo wa Hai ambao itakuwa ni sehemu ya kuendeleza biashara za wananchi na pia kujenga kituo cha Polisi kwani matukio ya uhalifu yamekuwa makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ilitengewa jumla ya



Sh.61,000,000,000/= mpaka sasa imeishia kupewa asilimia 39.2 ya bajeti iliyopitishwa na Bunge. Sasa sijui kutafanyika maajabu gani kwa pesa alizozungumza Mheshimiwa Waziri hapa. Mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh.68,000,000,000/= na matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, imekuwa dhamira na dira yetu ya Kambi Rasmi ya Upinzani kutochoka kutimiza haki na jukumu letu la Kikatiba na Kisheria kukosoa na kuishauri Serikali ya CCM japo tunapata masimango, mabezo, dharau na kadhalika, tunaamini Mungu anaona na anawaona na siku moja atatenda, kama siyo leo kesho vizazi vyetu vijavyo vitatoa hukumu ni yupi alikuwa kikwazo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba zetu za miaka ya nyuma tumekuwa tukiishauri na tunaendelea kushauri kwamba tukae kama Taifa kujipanga upya kutengeneza dira kupitia Katiba mpya inayozungumzia namna ya kusimamia na kugawa rasilimali ardhi. Ni vema pia Wizara hii na Serikali kwa ujumla ikapanga katika bajeti zake mambo machache ya kufanyiwa kazi kwa kuangalia vipaumbele, kuliko utaratibu wa sasa wa kujirundikia majukumu mengi ambayo kwa ufinyu mkubwa wa mapato ya Serikali, yamekuwa yanatekelezwa kwa uhafifu na hivyo kuonekana kama ghillba kwa wananchi. Kama tulivyoshauri tungekamilisha mfumo unganishi wa kuhifadhi kumbukumbu za ardhi tungepunguza au kuondoa kabisa migogoro ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara na Taasisi zake; Serikali ijitazame upya juu ya utaratibu wa kugawa maduhuli yake kwa ofisi, Wizara na taasisi zake. Je, inatoa kwa uwiano ulio sawa au inatolewa kwa mfumo wa utaratibu wa mwenye kisu kikali ndiye mla nyama. Kama hatujalionga hilo la kujipanga upya na kuendelea kufanya kazi kimazoea kwa kutegemea umahiri au zaidi mitazamo ya mtu mmoja aliyeko katika nafasi ya kimaamuzi kwa wakati huo, ni wazi marathoni yetu ya utatuzi wa kero za ardhi haitakuwa na mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa staili hii namalizia kusema kwamba, tutaendelea kubadilisha chupa lakini mvinyo utaendelea kuwa ni uleule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lwakatare, Waziri Kivuli wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI  
BUNGENI KATIKA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA  
MAENDELEO YA MAKAZI MHESHIMIWA WILFRED MUGANYIZI  
LWAKATARE (MB) AKIWASILISHA MAONI YA KAMBI RASMI  
YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU BAJETI YA WIZARA HIYO  
KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

(Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016)

---

**1. Utangulizi**

**Mheshimiwa Spika**, nasimama tena mbele ya Bunge lako tukufu kwa neema za Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa shukurani kwa uongozi mzima wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na Wabunge wote wa Kambi ikiongozwa na Mheshimiwa Freeman A. Mbowe (Mb) kwa kuendelea kutuamini mimi na Mheshimiwa Salma Mwaswa (Mb) kuisimamia na kuisemea Wizara hii kwa kipindi chote hiki. Mungu aendelee kuwapa nguvu na uvumilivu ya kuyakabili yote na naamini kwa nguvu zake yeye TUTAVUKA na kuvishinda vikwazo vyote.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa moyo mkunjufu niendeleo kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Bukoba Mjini (Bukoba Town) kwa ushirikiano wanaonipa kwa kuliwakilisha na kuliongoza Jimbo lao. Kwa dhati kabisa nimshukuru Mstahiki Meya wa Manispaa ya Bukoba, Chief Karumuna, Madiwani wote wa Manispaa ya Bukoba bila kujali tofauti zao za kivyama, Mkurugenzi na Watendaji wake wote, Mwenyekiti wa Chadema Bukoba Mjini Victor Sherejey na Kamati yake yote ya utendaji kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa.

**Mheshimiwa Spika**, ushirikiano ninaopata kutoka kwa viongozi wenzangu unalifanya Jimbo la Bukoba na Manispaa kwa ujumla kuwa sehemu ya kuigwa ambapo figisu na tofauti za kivyama haziwi kikwazo cha kuwaletea wananchi maendeleo wanayoyahitaji kutoka kwetu tuliochaguliwa kuwaongoza na kusimamia shughuli zao za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Mshikamano wetu ndio utaendelea kuwa chimbuko la kuipata na kuiona Bukoba Mjini waitakayo. Kipekee naomba niishukuru familia yangu yote ambayo imeendelea kunipa moyo katika kazi hii ambayo inaninyima muda mwingi wa kuwa nao.

**Mheshimiwa Spika**, Nitoe pole kwa wote waliopatwa na majanga mbalimbali tetemeko, njaa, mafuriko, ukame, ajali mbaya, ugumu wa maisha n.k kubwa ni kuwa na subira na kuyaombea na kuyaunga mkono yale tunayoyaaainisha kama sababu na kikwazo cha maisha na maendeleo yao.

## **2. Migogoro ya Ardhi Nchini**

**Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kuwa tarehe 01 Novemba mwaka 2013 Bunge lako tukufu liliunda Kamati Teule kwa ajili ya kuchunguza chanzo cha migogoro ya ardhi nchini na hatimaye kuja na mapendekezo ili Bunge liazimie na kuielekeza serikali kwa ajili ya mustakabali wa taifa letu kwa ujumla. Hoja ya kuundwa kwa Kamati Teule iliridhiwa na Bunge baada ya malalamiko ya muda mrefu yaliyokuwa

yanawasilishwa Bungeni na Wabunge kwa niaba ya wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati Teule ya Bunge iliyoundwa iliwasilisha taarifa yake Bungeni tarehe 06 Februari 2015. Pamoja na mambo mengine taarifa ya Kamati ilieleza aina ya migogoro ya ardhi nchini, uchambuzi wa mipango, sera na sheria zinazohusiana na masuala ya ardhi, uchunguzi wa Kamati pamoja na mapendekezo ya muda mfupi, kati na muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ingependa kurejea baadhi ya masuala muhimu yaliyoibuliwa na Kamati Teule ya Bunge wakati huo;

**(a) Aina ya Migogoro**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati Teule ilianisha aina kadhaa za migogoro ya ardhi nchini kuwa ni migogoro ya wakulima na wafugaji, migogoro kati ya wakulima na wawekezaji, migogoro kati ya wafugaji na wawekezaji, migogoro kati ya wakulima/wafugaji dhidi ya maeneo ya hifadhi na migogoro kati ya wananchi na serikali. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inakubaliana na uainishaji huo wa migogoro lakini ingependa kuongeza mgogoro mwingine ambao ni mgogoro unaotokana na mipaka ya maeneo ya utawala kama vile Vijiji/Mitaa na hata ngazi zingine za maeneo ya utawala.

**(b) Hali ya Migogoro**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati Teule ya Bunge iliweka bayana kuwa hali ya migogoro ya ardhi nchini baina ya wakulima na wafugaji au baina ya makundi hayo na wawekezaji imekuwa ya muda mrefu pamoja na kuwa serikali imekuwa ikileta mipango, sera na hata sheria mbalimbali kukabiliana na tatizo hili. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaunga mkono kauli ya Kamati Teule ya Bunge kuwa hali ya migogoro ya ardhi nchini isipotafutiwa ufumbuzi inaweza kuhatarisha amani na mustakabali wa nchi yetu.

**(c) Sababu ya Migogoro**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati Teule ya Bunge ilieleza sababu nyingi ambazo ni chanzo kinachosababisha migogoro ya ardhi nchini ambapo pamoja na sababu zingine ni kama ifuatavyo;

- (i) Kutokutengwa kwa maeneo mahususi ya Kilimo na Ufugaji.
- (ii) Kutokupimwa na kutokubainishwa kwa mipaka ya Vijiji
- (iii) Watu wachache kumiliki maeneo makubwa ya ardhi
- (iv) Wawekezaji kutokuzingatia na kufuata sheria za uwekezaji kwenye ardhi
- (v) Rushwa miongoni mwa watendaji wa serikali
- (vi) Kutowalipa wananchi fidia kamilifu
- (vii) Tofauti ya sera ya ardhi na sera ya mifugo

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu watu wachache kumiliki maeneo makubwa ya ardhi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ingependa kwa mara nyingine kuikumbusha serikali juu ya hoja binafsi ya aliyekuwa Waziri Kivuli wa Ardhi Mheshimiwa Halima Mdee (2010-2015) ambaye alieleza kwa undani juu ya uwekezaji kwenye mashamba makubwa nchini ambao utaleta tishio la uhaba wa ardhi na pia serikali kushindwa kusimamia uwekezaji wenye tija katika sekta ya ardhi. leleweke kuwa serikali ilikubali kufanya ukaguzi kwenye mashamba makubwa nchini na kuleta taarifa yake Bungeni, hata hivyo mpaka leo taarifa hiyo haikuwahi kujadiliwa ndani ya Bunge lako tukufu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuleta Bungeni taarifa ya ukaguzi wa mashamba makubwa nchini ili ijadiliwe na Bunge na pia kuzingatia ushauri kama ulivyotolewa na Kamati Teule ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa nyakati tofauti tuliweka bayana orodha ya watu wanaomiliki mashamba makubwa na kusababisha uhaba wa ardhi kwa wananchi. Ukiangalia kwa makini orodha ya wanaohodhi

mashamba makubwa ambayo hata hivyo imeonekana wanashindwa kuyaendeleza wapo pia wanasiasa (vielelezo vimeambatanishwa). Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda serikali kutoa kauli juu ya mashamba hayo ambayo yalionekana ni muhimu kurudishwa serikalini kama agizo la Bunge limeshatekelezwa. Katika hili tofauti za kiitikadi ziwekwe pembeni vinginevyo serikali itakuwa ikifanya kazi zake kwa upendeleo na kwa hila.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu wawekezaji kukodisha mashamba kwa wananchi kinyume na taratibu za kisheria za kubinafsishwa ardhi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kueleza kuwa tatizo hilo bado lipo na serikali inashindwa kuchukua hatua hata baada ya kushauriwa hivyo na Kamati Teule ya Bunge. Ieleweke kuwa hata baadhi ya waheshimiwa Wabunge wametoa malalamiko kwa niaba ya wananchi juu ya tabia za wanaoitwa wawekezaji kuwakodisha ardhi wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, hata baadhi ya kauli na matendo ya viongozi wa serikali zimekuwa zikichangia kutozingatiwa na kuheshimiwa kwa taratibu na sheria za ardhi nchini ambapo inakuwa pia chanzo cha migogoro ya ardhi. Itakumbukwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam aliutangazia umma kuwa amekabidhiwa ardhi kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda lakini baada ya muda mfupi Waziri mwenye dhamana akatangaza wazi kuwa mwekezaji huyo sio mmiliki wa ardhi ambayo imetangazwa kutolewa kwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa viongozi wa serikali ambao hawahusiki na masuala ya ardhi kuacha kutafuta umaarufu kupitia ardhi ya watanzania. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashangaa na kuhoji kama utaratibu wa viongozi wa serikali hiyohiyo na Chama hichohicho kushindania umaarufu kwenye vyombo vya habari kama unatupeleka sehemu salama kama taifa.

**(d) Mapendekezo ya muda mfupi ya Kamati Teule kwa serikali**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mapendekezo mengi ya Kamati kuhusu masuala ya utatuzi wa migogoro ya ardhi, baadhi ya mapendekezo ya muda mfupi ambayo yalipendekezwa na Kamati Teule ya Bunge ni kama ifuatavyo;

(i) Serikali iharakishe usuluhishi wa mgogoro baina ya wakulima na wafugaji wanaogombania maeneo Wilayani Kiteto.

(ii) Kupima ardhi ya Mkoa wa Morogoro kama mpango wa dharura ili kupunguza migogoro ya wakulima na wafugaji

(iii) Serikali ifute na kuyapima upya mashamba ya wawekezaji ambayo yametelekezwa na wawekezaji ili ardhi hiyo wapatiwe wananchi.

(iv) Serikali ipime upya maeneo ya Vijiji vyenye migogoro ya mipaka

(v) Serikali iangalie upya uamuzi wa kupanua mipaka ya maeneo ya hifadhi na kuangalia upya maeneo ambayo kwa sasa yamepoteza hadhi ya kuitwa hifadhi ili makazi na shughuli za kiuchumi za wananchi zipanuliwe.

(vi) Serikali itwae maeneo ambayo yalibinafsishwa bila kuzingatia mipaka na hivyo wawekezaji kuingilia ardhi ya wananchi.

(vii) Serikali ilete Bungeni marekebisho ya Sheria kwa ajili ya kuweka vigezo vya usajili wa Vijiji ambapo pamoja na mambo mengine Kamati iliitaka pia serikali kuzingatia historia na uwepo wa ardhi ya kutosha.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaikumbusha serikali kuhusu ahadi ya Waziri Mkuu aliyoitoa Bungeni wakati akijibu swali la Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuwa serikali italeta taarifa ya utekelezaji

wa maazimio ya Bunge. Kamati Teule ya Bunge kuhusu maula ya migogoro ya ardhi inapaswa kuletwa Bungeni haraka.

**Mheshimiwa Spika**, ni muhimu taarifa ya serikali kuhusu maazimio ya Bunge kuhusu migogoro ya ardhi ikaletwa Bungeni ili ijadiliwe kwa sababu toka maazimio haya yatolewe ndani ya Bunge lako tukufu tumeshuhudia mgogoro wa Kiteto ukiwa bado haujapatiwa ufumbuzi, huko Kilosa Mkoani Morogoro Mkulima mmoja Ndugu Augustino Mtitu wa Kitongoji cha Upangwani, Kijiji cha Doma Isanga, Kata ya Masanze, Jimbo la Mikumi Wilaya ya Kilosa alipigwa mkuki na wanaodaiwa kuwa wafugaji. Kama hiyo haitoshi baada ya muda mfupi mkulima mwingine Ndugu Rajab Ayoub wa Kijiji cha Mbigiri Wilayani Kilosa alijeruhiwa kwa sime akiwa shambani mwake na wanaodaiwa kuwa ni wafugaji. Aidha yapo matukio kadhaa ya mifugo ya wafugaji kupewa sumu au kujeruhiwa moja kwa moja na wanaodaiwa kuwa ni wakulima.

**Mheshimiwa Spika**, Ni ishara kuwa matukio kama haya ya mauaji yanayotokana na migogoro ya ardhi yanazidi kutokea kwa sababu serikali imeyafungia maazimio ya Bunge kabatini bila kuchukua hatua za dharura kama ilivyokuwa imeazimiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa kuwa moja ya sababu za migogoro ya ardhi hasa kwa Mkoa wa Morogoro ni baadhi ya viongozi wa serikali za Vijiji na Mitaa ambao sio waaminifu kuuza ardhi mara mbili kwa wakulima na wafugaji na hivyo kuchochea migogoro. Aidha baadhi ya wakulima huuza ardhi kwa wafugaji na baadae kuikana mikataba/makubaliano ya awali waliyofanya na wafugaji.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuwachukulia hatua kali za kisheria viongozi na watu wote ambao wamekuwa sehemu ya migogoro ya ardhi kwa kufanya mambo ambayo hayana uadilifu na kusababisha migogoro isiyoisha ndani ya jamii.



### 3. Kodi ya Majengo (Property Tax)

**Mheshimiwa Spika**, Mwaka wa fedha unaokwisha mwezi Juni 2017 serikali iliweka utaratibu wa kisheria kuondoa mamlaka ya Halmashauri kukusanya kodi ya majengo (property tax) na kuipa haki hiyo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) huku serikali ikijua kuwa kodi hiyo ilikuwa sehemu muhimu sana ya mapato ya Halmashauri nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ililiona jambo hili kama mkakati wa kuondoa mapato kwa Halmashauri ili kuzipunguzia nguvu Halmashauri nyingi za Majiji ambazo zinaongozwa na Wapinzani. Ieleweke kuwa halmashauri hapa nchini zimekuwa zikikusanya mapato kwa ajili ya kuendesha miradi yake ya maendeleo na shughuli nyingine za kawaida kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato kwa mujibu wa sheria ya fedha ya Halmashauri (Local Government finance Act, 1982) Haukuwa uamuzi sahihi kutunga sheria ya kuondoa chanzo cha mapato cha kodi ya majengo kutoka katika halimashauri nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kufutwa kwa kifungu kilichokuwa kinazipa Halmashauri jukumu la kukadiria na kukusanya kodi za majengo na kulihamishia TRA kupitia sheria ya fedha ya mwaka 2016, kifungu cha 38 baada ya kufanya marekebisho kwa kuvifuta vifungu vya 31A na 31B vya sheria ya fedha ya Serikali ya Mitaa sura 290 kumeziyumbisha sana halimashauri katika kutekeleza majukumu yake kutokana na ukweli kwamba chanzo cha kodi ya majengo kilikuwa ni mojawapo ya chanzo kikubwa cha mapato ya Halmashauri.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wakati wa mjadala wa Ofisi ya Rais TAMISEMI tulieleza wazi kuwa taarifa ya Serikali inaonyesha kuwa kodi ya Majengo iliyokusanywa ni shilingi milioni 4,762.37 kati ya mllioni 29,004 sawa na asillmia 17.4 tu ambayo ilitarajiwa kukusanywa na TRA.

**Mheshimiwa Spika**, kwa takwimu ambazo nimerejea katika hotuba hii, ni ishara kwamba hoja niliyoielezea mwaka jana

katika Bunge hili ilikuwa ni muhimu kuzingatiwa na serikali kwa sababu ni wazi kuwa TRA haina uwezo wa kufanya kazi ya kukusanya chanzo hiki cha mapato. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kulieleza Bunge hili sababu za kuipa TRA mamlaka ya kukusanya kodi ya majengo wakati haikuwa imejipanga kimikakati na kimfumo kufanya kazi hiyo, aidha Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuleta tena marekebisho ya Sheria ya Fedha ili kurudisha chanzo hiki cha mapato katika ngazi ya Halmashauri kama ilivyokuwa awali.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa kuwa baada ya kuziondolea Halmashauri haki ya kutoza kodi ya majengo, Halmashauri nyingi hasa za Vijijini zimeanza kutoza kodi ya majengo kwa wananchi huko vijijini jambo ambalo limekuwa kero kwa wananchi wetu ambao kwa waliowengi hawana vipato vizuri.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kupitia Wizara hii kulieleza Bunge lako tukufu, ni kwa nini wameondoa kodi ya majengo kama chanzo cha mapato na kuruhusu Halmashauri kuanza kuwatoza wananchi wa vijijini kodi ya majengo yao.

**Mheshimiwa Spika**, Kama serikali bado inang'ang'ania chanzo hiki, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri majengo yagawanywe kwenye madaraja kama vile majengo makubwa ya kibiashara, *residential apartments*, na majengo mengine makubwa kama itakavyoamuliwa kodi zao zikusanywe na Mamlaka ya Kodi Tanzania (TRA) lakini majengo madogo ya biashara na nyumba za makazi kodi yao ikusanywe na Halmashauri ili kuongeza ufanisi wa TRA katika ukusanyaji.

#### 4. Kodi ya Ardhi

**Mheshimiwa Spika**, ni takwa la kisheria kupitia kifungu cha 22 cha Sheria ya Ardhi sura 113 kuwa ardhi yoyote inayomilikiwa kwa mujibu wa sheria kulipiwa kodi ya ardhi kama sehemu ya masharti ya miliki ya ardhi nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalitambua jukumu hili kwa

sababu imekuwa ikilipigia kelele kwa miaka mingi sasa kuwa wamiliki wengi wa ardhi hasa wanaomiliki mashamba makubwa wamekuwa hawalipi kodi ya ardhi wala kuendeleza ardhi ambazo wamemilikishwa kwa mujibu wa sheria.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina tatizo na hatua zinazochukuliwa na Wizara kuhakikisha kuwa kila mwenye miliki ya ardhi nchini analipa kodi kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa. Itakumbukwa kuwa Aprili mwaka huu 2017 Waziri mwenye dhamana ya ardhi alitoa maelekezo kuwa wananchi wote wanaomiliki ardhi iwe imepimwa au haijapimwa wanatakiwa kulipa ardhi.

**Mheshimiwa Spika**, ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuwa agizo hilo la Waziri linaenda kinyume na sheria ya ardhi kwa kuagiza kodi hiyo kulipwa kwa ardhi ambayo haijasajiliwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kusitisha agizo hilo kwa sababu wanakwepa jukumu la kupima ardhi badala yake wanatoa maelezo ambayo ni kinyume cha sheria. Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kuwa kama serikali inaona uamuzi wa kutoa maagizo hayo ni tija kwake ni vema ikaleta marekebisho ya sheria hapa Bungeni kuliko kuendelea kufanya hivyo kinyume na taratibu.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunapenda kusisitiza kuwa tamko hilo la Waziri linakiuka sheria ya ardhi Na. 4 na Na. 5 ya mwaka 1999 inayotaka kodi ya ardhi ilipwe kwenye maeneo yaliyopimwa na kumilikishwa kwa kipindi maalum (miaka 33, 66 na 99) tunataka Serikali itoe ufafanuzi juu ya maeneo ambayo hayajapimwa yatalipishwaje kodi na kwa utaratibu upi kwani watu hao hawana nyaraka zozote za umiliki.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuacha kutafuta njia za mkato za kuwakamua wananchi pesa badala yake serikali inatakiwa kuwekeza katika kusimamia maeneo yote ambayo hayajapimwa ili kutoa miliki kwa wahusika kwani kwa kufanya hivyo:-

- (i) Itapanua wigo wa mapato ya Serikali
- (ii) Itapandisha thamani ya ardhi
- (iii) Itapunguza au kuondoa kabisa migogoro ya ardhi
- (iv) Itawapa fursa wananchi kutumia ardhi zao kama dhamana katika Taasisi za kifedha
- (v) Itavutia Uwekezaji
- (vi) Itasaidia utunzaji bora kumbukumbu za ardhi
- (vii) Itaweka mandhari nzuri za maeneo husika na mpangilio mzuri wa matumizi yote ya ardhi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa tamko hilo la serikali ni kukimbia jukumu lake la msingi la kuhakikisha ardhi yote inapimwa na badala yake wanatafuta njia ya mkato ya kuongeza mapato. Kama njia hii itatumiwa na serikali ni maoni ya Kambi Rasmi Upinzani Bungeni kuwa itazalisha migogoro ya ardhi lukuki hasa kwenye Miji, Manispaa na Majiji nchini kwa sababu udanganyifu utakuwa mkubwa na matapeli watatumia sababu za kulipia kodi ya ardhi kama sehemu ya kutaka kupewa miliki ya ardhi.

## 5. Watumishi wa Ardhi Katika Halmashauri

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa Bunge la kumi serikali kupitia kwa Naibu Waziri wa Ardhi wakati huo Mheshimiwa George Simbachawene alitoa ahadi ya serikali kuwa kutokana na malalamiko mengi ya wananchi pamoja na tuhuma na vitendo vya rushwa vinavyofanywa na watumishi wa idara ya ardhi ya Halmashauri nchini, serikali itahakikisha kuwa watumishi hao wanapokea maelekezo ya moja kwa moja kutoka serikalini na watakuwa wanapokea malipo kama watumishi wa Wizara ili iwe rahisi kupokea maelekezo na usimamizi moja kwa moja kutoka Wizarani pamoja na kuendelea kufanya kazi katika Halmashauri zetu.

**Mheshimiwa Spika**, serikali haikutoa ahadi hiyo kwa bahati mbaya, hiyo ilitokana na hoja za waheshimiwa Wabunge kuwa hakuna uhusiano wa moja kwa moja katika Wizara na watumishi wa idara ya ardhi katika Halmashauri mbalimbali nchini jambo linalopelekea watumishi wa ardhi

katika ngazi ya Halmashauri kutokuwa na ufanisi na kujihusisha na vitendo visivyo vya uadilifu wakati wa kutoa huduma kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepigwa na butwaa kwa sababu serikali ya awamu ya nne ilikuwa chini ya CCM na serikali ya awamu ya tano ipo chini ya CCM lakini kwa utendaji wa serikali ya awamu ya tano inaonekana kama vile imeshuka kutoka mwezini. Hii ni kutokana na sababu zilizotolewa za kushindwa kutekeleza ahadi ya serikali ya kushindwa kuanzisha mchakato wa kuhamisha ajira ya sekta ya ardhi kutoka serikali za mitaa kwenda Serikali kuu.

**Mheshimiwa Spika**, serikali kupitia randama ya Wizara imeeleza yafuatayo kuhusu kutekeleza ahadi hii;

**“Serikali inaendelea na utekelezaji wa dhana ya kugatua madaraka (Development by Devolutions) kwenda katika ngazi za msingi. Hivyo, utaratibu wa kuhamisha ajira za watendaji wa sekta ya ardhi kutoka Halmashauri utakinzana na dhana hii”**

**Mheshimiwa Spika**, hii ni ishara kuwa ahadi na commitment za serikali wanazozitoa Bungeni wanazitoa kwa ajili ya kuwashawishi waheshimiwa wabunge kupitisha bajeti na mipango mingine ya serikali tu na si kuzingatia wanachoahidi mbele ya Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, Wabunge waliishauri serikali kutokana na uzoefu wa masuala wanayokumbana nayo katika utekelezaji wa shughuli zao majimboni na Waheshimiwa Wabunge walitoa ushauri huo wakizingatia kuwa ipo dhana na mfumo wa D by D na kwa upande wa serikali walitoa ahadi hiyo wakijua kuwa mfumo huo wa utawala upo. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kulieleza Bunge lako tukufu sababu za ziada zilizopelekea kutotekeleza ahadi yake iliyoitoa katika Bunge hili.

**6. Kuundwa kwa Mamlaka ya kusimamia Sekta ya Milki nchini (Real Estate Regulatory Authority)**

**Mheshimiwa Spika**, mwaka 2011 wakati wa mkutano wa kwanza wa Bajeti wa Bunge la kumi, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni alishauri umuhimu wa kuundwa kwa mamlaka ambayo itasimamia sekta ya ujenzi hasa ujenzi wa majengo makubwa ambayo inaweza kuwa chanzo kikubwa cha mapato ya serikali ikiwa serikali itakitumia vizuri.

**Mheshimiwa Spika**, hoja hiyo ilitolewa kwa sababu ya hali ya wakati huo iliyoonesha kuwa kulikuwa na ongezeko kubwa la majengo makubwa hasa katika miji mikubwa nchini lakini pamoja na ukuaji huo bado sekta hiyo ilionekana kutochangia fedha za kutosha katika pato la taifa.

**Mheshimiwa Spika**, katika randama za Wizara hii kwa mwaka wa fedha uliopita , serikali iliahidi kuwa mwaka wa fedha 2016/2017 muswada utakaounda mamlaka ya sekta ya miliki nchini ungeletwa Bungeni na hatimaye kuundwa kwa mamlaka hiyo. Aidha randama za Wizara kwa mwaka huu zinaonesha kuwa muswada huo wa sheria utaletwa kwa mwaka ujao wa fedha. Kambi Rasmi ya Upinzani inaunga mkono kuundwa mamlaka hiyo kama ilivyokuwa imeshauri miaka iliyopita lakini inapata mashaka na nia ya serikali ya kuendelea kuchelewa kuleta muswada huo Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuacha ahadi za mara kwa mara za jambo hilo na sasa ifanye kwa vitendo ili jambo hilo lifike mwisho.

**Mheshimiwa Spika**, aidha kupitia randama za Wizara serikali imeeleza kuwa tayari imekamilisha maandalizi ya utungwaji wa Sheria ya Mawakala wa Ardhi (Real Estate Agents Act). Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza Sheria hiyo ihuishwe ili masuala ya msingi ya sheria hiyo yaunganishwe na Sheria ya Real Estate Regulatory Authority na kuwa sheria moja ambayo itakuwa inasimamia sekta ya miliki na mawakala kwa ujumla.

## 7. Malipo ya fidia kwa wananchi

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya wananchi wa Bukoba napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Waziri na Naibu Waziri wa Maji na uongozi pamoja na wasimamizi wa BUWASA (*Bukoba Urban Water Supply*), kwa kutimiza ahadi iliyotolewa katika Mkutano wa Bunge la Bajeti wa mwaka uliopita wakati nilipoomba ufafanuzi kwenye mshahara wa Waziri ili serikali ianze kulifanyia kazi suala la fidia kwa wananchi wa Kata ya Kahororo waliopisha mradi wa mfumo wa maji taka walipwe fidia zao na serikali.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kushukuru kwa kuwa wananchi hao walilipwa fidia zao ingawa bado wanadai riba za ucheleweshaji malipo ambazo nazo Naibu Waziri wa Maji ameahidi kufuatilia ili walipwe. Napenda kumkumbusha Waziri kuhusu ahadi hii ya serikali ya kulipa riba ya fidia yao ili kumaliza kabisa malalamiko yao dhidi ya serikali.

### (a) Malipo ya Fidia ya Hisani kwa Wananchi wa Mloganzila

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu mgogoro wa toka kabla ya mwaka 2004 kati ya wananchi wa Mloganzila waliohamishwa kupisha ujenzi wa MUHAS Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wakati ikijibu swali la Mbunge wa Kibamba John Mnyika tarehe 3 Februari 2017 ilieleza kuwa Serikali pia ililipa kiasi cha Sh. 8,067,904,700 kwa ajili ya fidia ya maendelezo katika ardhi kwa wananchi 1,919 katika kipindi cha mwaka 2008 mpaka 2010. Aidha ilijibu kuwa mwaka 2011 Serikali ilitenga kiasi cha sh. 1,610,374,700 kwa ajili ya fidia ya wananchi 619 waliosalia. Hata hivyo, kwa kipindi chote Serikali imekataa kuwalipa wananchi hao fidia ya ardhi pamoja na wananchi hao kupewa ardhi hiyo na Serikali yenyewe na kupatiwa hati ya kijiji cha Kwembe.

**Mheshimiwa Spika** Tarehe 20 Mei 2015 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa maelekezo ya Rais ilitoa ahadi ya kuwalipa wananchi hao fidia ya hisani au mkono wa kwaheri ya shilingi milioni mbili kwa kila

mwananchi ahadi ambayo miaka miwili imepita bila ya kutekelezwa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepitia vitabu vya bajeti na kubaini kwamba hakuna fedha zozote zilizotengwa kwa ajili ya kufanya malipo hayo. Serikali itoe maelezo ni kiasi gani kwa sasa kinatarajiwa kutolewa kwa wananchi, ni kwanini hakuna fedha zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na ni lini malipo hayo yanatarajiwa kufanyika?

**(b) Bomoa Bomoa ya Kimara- Kiluvya Jijini Dar es Saalam**

**Mheshimiwa Spika**, Katika miaka 1970, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya utawala wa Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Nyerere ikiwa inatekeleza sera za chama cha TANU ilianzisha Vijiji vya Ujamaa katika kutekeleza mpango kabambe wa “Operesheni Vijiji” ambapo wananchi waliondolewa pasipo hiari yao toka ardhi, mashamba na makazi yao na kuhamishiwa katika vijiji vya ujamaa vilivyoanzishwa na kisha halmashauri za vijiji zilizokuwa na mamlaka kisheria ya kugawa ardhi, kuwagawia ardhi kwa ajili ya makazi na kilimo kuanzia yalipo mawe yanayoonyesha mwisho wa hifadhi ya barabara ya wakati huo yaliyokuwa mita 22.85 tu toka katikati ya barabara, pande zote mbili.

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mkoa wa Dar es Salaam miongoni mwa vijiji vya ujamaa vilivyoanzishwa kando kandao ya barabara ya Morogoro ni pamoja na:-

- 1) **Vijiji vya Kimara A na B**
- 2) **Kijiji cha Mbezi kilichokuwa na hati ya usajili namba DSM/VIJ/08.**
- 3) **Kijiji cha Kibamba kilichokuwa na hati ya usajili namba DSM/VIJ/36**
- 4) **Kijiji cha Kiluvya, ardhi yake ilipimwa na kijiji kupatiwa hati miliki ya kijiji yenye namba 34125 iliyotolewa tarehe 2 Julai 1988.**

**Mheshimiwa Spika**, Uthibitisho wa kwanza kuwa upana wa hifadhi ya barabara ya Morogoro kwa eneo la Ubungo hadi



TAMCO Kibaha ni mita 22.85 tu na sio hadi mita 121.92 ni kitendo cha, Wizara iliyokuwa na dhamana ya usimamizi wa barabara kupanda mawe yaliyoonyesha mwisho wa hifadhi ya barabara mita 22.85 na sio hadi 121.92 toka katikati ya barabara, pande zote mbili. Hatua hiyo iliashiria kuwa Serikali kupitia Wizara hiyo ilikamilisha utwaaji wa ardhi kwa upana wa mita 22.85 tu kati ya 121.92 zilizokuwa zimetambuliwa awali kwa ajili ya kutwaliwa kupitia Government Notice 161 ya 5/5/1967 kwa kulipia fidia.

**Mheshimiwa Spika**, Ni kutokana na ukweli huo, ndio maana wakati wa ujenzi wa barabara ya Morogoro mwanzoni mwa miaka ya 1970 nyumba za wananchi zilizoangukia ndani ya mita 22.85 ndio zilizotakiwa kuondolewa, baadhi yao kutakiwa na mamlaka za serikali kujenga upya nyumba zao nje ya mita 22.85 hadi leo baadhi ya wananchi hao bado wapo hai.

**Mheshimiwa Spika**, Uthibitisho wa pili, pale Serikali ilipowahamishia wananchi katika vijiji vilivyotajwa hapo juu, ikawajengea majengo ya huduma mbali mbali za kijamii kama vile Shule ya Msingi ya Mbezi katika Kijiji cha Mbezi. Zahanati ya Kibamba Hospitali na nyumba za watumishi katika Kijiji cha Kibamba n.k. Majengo haya yalijengwa nje kidogo ya mita 22.85 toka katikati ya barabara.

**Mheshimiwa Spika**, Hivyo basi ujenzi na uwepo wa majengo ya Serikali ndani ya eneo ambalo baadaye toka mwaka 2000, lilianza kudaiwa ni sehemu ya hifadhi ya barabara ya Morogoro ni uthibitisho kuwa hifadhi ya barabara halali kwa barabara ya Morogoro kwa eneo la Ubungo hadi Tamco Kibaha ni mita 22.85 tu, toka katikati ya barabara, pande zote mbili.

**Mheshimiwa Spika**, Kuanzia mwaka 2000, sambamba na makazi na majengo ya wananchi, majengo ya Serikali yaliyoko nje ya mita 22.85 toka katikati ya barabara yamekuwa mara kwa mara yakipata misukosuko ya kuwekewa alama za X na hata kubomolewa kwa madai eti yako ndani ya hifadhi barabara ya Morogoro.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuhoji hivi kweli Serikali inaweza kuvamia hifadhi za barabara na kujenga majengo ya shughuli zingine za maendeleo? Na kwanini Serikali ifanye hivyo wakati Tanzania bado ina ardhi tele?

**Mheshimiwa Spika**, Uthibitisho wa tatu, ni taasisi za kiserikali yaani Halmshauri ya Jiji la Dar es Salaam, na maafisa ardhi wa Wilaya na Jiji kuwapimia wananchi wa vijiji vilivyotajwa katika hotuba hii ambapo ardhi waliyogawiwa wakati wa operesheni vijiji kwa kuacha hifadhi ya barabara ya upana wa mita 22.85 tu; na Wizara hii yenye dhamana ya masuala ya ardhi kutoa hati miliki ambazo zinaendelea kulipiwa kodi ya ardhi hadi sasa. Hii ni licha ya kuanzia mwaka 2000, kuwepo madai kutoka Wizara yenye dhamana ya barabara kuwa hifadhi ya barabara kwa eneo hilo ni mita hadi 121.92 toka katikati ya barabara, pande zote mbili kwa eneo hilo.

**Mheshimiwa Spika**, Uthibitisho wa nne, Mwaka 1985, mkazi mmoja wa Kimara aitwaye Ndg Joseph Marwa aliiandikia barua Wizara ya Mawasiliano na Ujenzi akitaka kufahamu kama amejenga ndani ya eneo la hifadhi ya barabara ya Morogoro, na kujibiwa kwa barua yenye Kumb. Na TRM/0.10/9/47, kutoka Wizara ya Mawasiliano na Ujenzi ya Tarehe 20 Agosti 1985 iliyowekwa saini na Ndg A.K Fuko kwa niaba ya Katibu Mkuu iliyosema kuwa "Mnamo tarehe 14/08/1985 Tumetuma vijana toka ofisi ya Chief Engineer Matengenezo kwenda kupima na kubaini wewe upo mita 33 toka katikati ya barabara hivyo upo nje ya hifadhi ya barabara kwa mita kumi {10.m} hivyo hukuhusika na fidia na hupaswi kuondoka".

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inajuliza licha ya uthibitisho wote huu wa nyaraka, matendo ya wizara, idara na taasisi mbalimbali za kiserikali kutambua kuwa upana halali wa hifadhi ya barabara ya Morogoro kwa eneo la Ubungo hadi TAMCO Kibaha ni mita 22.85 tu, pande zote mbili na sio hadi 121.92.

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na mazingira maalum ya kutaka kulinda umiliki wa ardhi ya wananchi waliohamishiwa

katika vijiji vya ujamaa, mwaka 1999 Serikali iliwasilisha muswada wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na 5 ya 1999, ambao ulipitishwa na bunge na kuridhiwa na Rais Benjamin Mkapa tarehe 15 Mei 1999.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa nyakati tofauti kuanzia mwaka 2000 hadi 2004 wananchi wanaoishi pembezoni mwa Barabara ya Morogoro kati ya Ubungo na TAMCO Kibaha ndipo wamejikuta katika sintofahamu juu ya hatma ya mali na maisha yao baada ya mkandarasi kutumwa kupanda mawe na miti ili kuonyesha mwisho wa hifadhi ya barabara ni mita 121.92 kutoka katikati ya barabara, badala ya mita 22.85 bila kulipwa fidia stahilifu. Aidha yaliwekwa pia mabango yakuonyesha hivyo, huku mawe yaliyopandwa na COMWORKS miaka ya 1970 yanayoonesha hifadhi ya barabara hiyo ni 22.85 kutoka katikati ya barabara, ambayo hadi leo yapo na yanapuuza.

**Mheshimiwa Spika**, Kutoka wakati huo nyumba za wananchi wanyonge zikaanza kukosa wapangaji, wamiliki wa ardhi wakashindwa kuendeleza ardhi zao, wawekezaji mbali mbali wakashindwa kuwekeza n.k. Ni kutokana na vitendo hivi vya ardhi ya wananchi kutwaliwa isivyo halali na pasipo wamiliki kulipwa fidia yoyote kwa kupandwa mawe, na mabango ya barabara eneo lote toka Ubungo mwisho hadi Kiluvya, hakuna huduma ya kijamii kama vile mabenki, maduka makubwa [Shopping malls] wala shughuli kubwa za kiuchumi zinazofanyika, na hivyo kuleta athari mbaya za kijamii na kiuchumi kama vile kukosekana kwa ajira na njia za wananchi kujikimu kimaisha.

**Mheshimiwa Spika**, Kibaya zaidi zoezi la upandaji mawe na mabango husika wakati huo halikuheshimu ardhi inayomilikiwa kwa hati miliki na zinazolipiwa hadi na Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, Ardhi hizo ziliingiliwa isivyo halali na wamiliki wake wamekuwa wakizuiwa kuendeleza maeneo yao wanayoyalipia. Yote haya yamekuwa yakifanyika isivyo halali kwa njia za vitisho vya kubomolewa. Idadi kubwa sana

ya makazi ya wananchi yamebomolewa isivyo halali kwa madai kuwa yako katika hifadhi za barabara, kitu ambacho si kweli.

**Mheshimiwa Spika**, Tatizo lingine linalojitokeza ni utekelezaji wa kibaguzi wa Sheria ya barabara Namba 13 ya 2007 na Kanuni zake, Sheria na Kanuni hizo ziko wazi kuwa hifadhi ya barabara ya Morogoro ni kama ifuatavyo:-

- a) Jengo la Umoja wa Mataifa (la Zamani) hadi Km 10 (Dar es Salaam) ni Mita 60
- b) Km 10 hadi 16 ni mita 90
- c) Km 16 hadi 37 ni mita 120 (Mbezi hadi Tamco baada ya barabara ya (TAMCO -Vikawe-Mapinga)
- d) Km 37 hadi Km 69 mita 60
- e) Km 69 hadi Km 70 ni mita 60 (Ruvu darajani) na inayobaki kwenda Morogoro ni mita 60

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kurejea kwa urefu kuhusu mgogoro wa kuongeza upana wa barabara hiyo wakati huo ukiwa ni wa mita 22.8 na kuongezwa hadi 121.9, hivi karibuni Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) Mkoa wa Dar es Salaam ilitoa notisi ya siku 28 kwa wakazi wa Kimara hadi Kiluvya kuwataka kubomoa nyumba na kuondoa mali ambazo inadaiwa kuwa majengo na mali hizo yapo katika hifadhi ya kipande hicho cha barabara ya Morogoro.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na notisi hiyo kutolewa kwa wananchi ieleweke kuwa Wizara hii ilishatoa hati za miliki ya ardhi na leseni mbalimbali za makazi kwa wananchi hao toka miaka ya 70, 80 na 90. Aidha TANROADS imeongeza upana wa barabara kutoka mita 60 katikati ya barabara kila upande hadi 121.9. Hii maana yake ni kuwa upana wa barabara ya Morogoro kutoka Kimara hadi Kiluvya itakuwa mita 240 kutoka 121.9 za awali.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kuwa kuna shauri lililopo Mahakamani kuhusu jambo hili lakini ingependa serikali ieleze Bunge lako tukufu kuwa ni upana upi hasa wa barabara ya Morogoro ambao

upo kwa mujibu wa sheria unaotambuliwa na serikali zaidi ya ule ambao nimeurejea katika hotuba? Hii ni kutokana na upana wa barabara hii kubadilika mara kwa mara jambo ambalo linaathiri makazi na shughuli za kiuchumi za wananchi.

**(c) Migogoro ya Ardhi ya Pugu Kajiungeni, Kipawa na UVKIUTA**

**Mheshimiwa Spika**, mgogoro mwingine wa ardhi upo pia katika Mkoa wa Dar es Salaam, Jimbo la Ukonga, kata Pugu eneo la Pugu Kajiungeni. Hili lilikuwa eneo la wazi ambalo lilikuwa linatumwa kwa matumizi ya mnada na michezo kwa vijana wa Pugu. Hata hivyo jambo la kushangaza ni kuwa eneo hilo limeuzwa kinyemela na huku ikifahamika kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri aliwapa wajasiliamali wadogo vijana na akina mama ili waweze kufanya biasharaza ndogo ndogo.

**Mheshimiwa Spika**, jambo ambalo limewastua wananchi wa eneo hilo ni uvamizi wa usiku wa manane ambao ulipelekea kuvunjwa kwa mabanda yote ya wafanyabiashara ndogondogo na hadi sasa mali za waliokuwa wanafanya biashara eneo hilo zimepotea. Mgogoro huo umekuwa mkubwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dae Es Salaam inazo taarifa za mgogoro huu lakini mpaka sasa hakuna hatua zozote zilizochukuliwa.

**Mheshimiwa Spika**, mgogoro mwingine wa ardhi ni wa wananchi wa Kipawa ambao walihamishwa kupisha upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere. Baada ya wananchi kuhamishwa katika eneo hilo walipelekwa maeneo ya Zavala, Kinyamwezi Nyeburu na Kipawa mpya kwenye Kata ya Buyuni. Waliohamishwa kutoka Kipawa kupisha ujenzi wa ndege hawakulipwa na wala kupewa maeneo mapya na kule walikopelekwa baadhi yao wamepewa maeneo ya watu wa Buyuni. Huu ni mgogoro mkubwa na hadi sasa hakuna majibu ya serikali na wananchi wanaendelea kugombania ardhi.

**Mheshimiwa Spika**, kuna mgogoro mwingine mkubwa wa tangu 1998, maarufu kama UVKIUTA. UVKIUTA ulikuwa ni Umoja wa Vijana wa Kikristo Tanzania ambao wanahusisha Kata za Chamazi Wilaya ya Temeke na Kivule Wilaya ya Ilala.

**Mheshimiwa Spika**, UVKIUTA wanalalamikiwa na wananchi kuwa wameongeza eneo ambalo awali hawakuwahi kuwa nalo ambapo baada ya kuongeza eneo lao limewaathiri wananchi wa Mtaa wa Magole Mkombozi katika Kata ya Kivule ambao awali eneo lao halikuwa la UVKIUTA.

**Mheshimiwa Spika**, Eneo hili anayetajwa kuhusika na mgogoro huo ni anayedaiwa kuwa mlezi wa UVKIUTA ambaye pia ni Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Ndg Jordan Rugimbana. Wananchi walipewa eneo wakati wa Mwalimu Nyerere lakini Ndugu Rugimbana na timu yake wameongeza kwa nguvu eneo hili kwa kuchukua maeneo ya wananchi na kwa sasa nguvu kubwa imekwisha tumika na kuvunja nyumba zaidi ya 700.

**Mheshimiwa Spika**, Ndugu Rugimbana ambaye alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni kwa ujanja ujanja anadai eneo hilo liko Wilaya ya Temeke lakini wananchi katika eneo hilo walipiga kura zao Kata ya Kivule wilaya ya Ilala. Lakini kwenye suala hili la uporaji wa ardhi yao inadaiwa kuwa eneo hilo liko Temeke hali inayopelekea Mbunge wa Ukonga na Mwenyekiti wa mtaa wa Kivule Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara ashindwe kutetea maslahi ya watu wake. Aidha, zipo taarifa kuwa hata UVKIUTA yenyewe kwa sasa haipo kitaasisi bali ni ujanja wa watu wachache.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri kuangalia ni jinsi gani atawarudishia imani wananchi wa maeneo hayo kwa kuwa Serikali ipo na kimsingi inatakiwa kusimamia sheria kwa kuwa hakuna mtu aliyepo juu ya sheria na haki za wananchi zinalindwa.

**(d) Mgogoro wa Mipaka kati ya Vijiji na Hifadhi ya Wanyama ya Serengeti**

**Mheshimiwa Spika**, Hifadhi ya Wanyama ya Serengeti ilianzishwa mwaka 1968 kwa mujibu wa sheria za nchi huku mipaka ya Hifadhi hiyo ikitajwa na kuwekwa wazi kwenye gazeti la serikali lililoanzisha rasmi mbuga huyo.

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na mgogoro kati ya Hifadhi ya Serengeti na Vijiji vya Merenga, Machochwe, Nyamakendo, Mbilibali, Tamkeri, Bisarara, Mbilikiri na Bonchugu kutokana na Hifadhi hiyo kuhamisha mipaka mara kwa mara tanga Hifadhi hiyo ianzishwe.

**Mheshimiwa Spika**, ipo ramani mpya ya mwaka 2008 ambayo imelalamikiwa na wanachi kwa kuwa ramani hiyo inapingana na mipaka ya awali ambayo iliwekwa kuonesha mipaka ya Hifadhi jambo ambalo linafanya maeneo makubwa ya Vijiji hivyo kuwa sehemu ya hifadhi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kuwa serikali iliunda Tume inayohusisha Wizara tano lakini cha kushangaza Halmashauri za Vijiji wala Wilaya hazikuhusishwa wakati Tume ikitafuta suluhisho la mipaka ya hifadhi na Vijiji. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuhakikisha kuwa inaunda Tume nyingine huru kushughulikia mgogoro huu na ambayo itawahusisha viongozi wa Vijiji na Halmashauri ili kupata suluhisho la mgogoro na wananchi waweze kuendelea na shughuli zao.

**(e) Mgogoro wa Mipaka kati ya Mitaa ya Kisopwa, King'azi na Mloganzila**

**Mheshimiwa Spika**, kwa muda mrefu kabla hata ya kuundwa kwa Manispaa mpya ya Ubungo katika Mkoa wa Dar es Salaam kumekuwa na mgogoro wa mipaka katika Mitaa ya Kisopwa, King'azi na Mloganzila ambapo pamoja na taarifa kuhusu mgogoro huo kuwasilishwa na Mbunge wa Ubungo wakati huo Mheshimiwa John Mnyika bado kuna hali

ya sintofahamu kuhusu mipaka ya Mitaa ambapo mamlaka za serikali za mitaa hiyo zimekuwa zikigombania mpaka kukusanya mapato kutoka kwa wananchi huku suala la mipaka likiwa bado halijaamuliwa.

**Mheshimiwa Spika**, Manispaa ya Kinondoni wakati huo pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe zilishindwa kufikia muafaka kuhusu mipaka ya Mitaa hiyo mpaka leo ambao imeundwa Manispaa mpya ya Ubungo. Aidha ieleweke kuwa wananchi waliowengi wa Mitaa wameandikishwa kupiga kura katika Jimbo la Kibamba katika Manispaa ya Ubungo na iliyokuwa Manispaa ya Kinondoni ilijenga huduma za kijamii ikiwemo shule, zahanati na kulipa fidia katika maeneo hayo. Hata hivyo linapokuja suala la kukusanya tozo mbalimbali Halmashauri ya Kisarawe hukusanya tozo hizo na kuleta mgogoro. Aidha, utata mkubwa zaidi unaibuka baada ya ujenzi wa Chuo na Hospitali ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishu cha Muhimbili (Muhimbili University of Health and Allied Science-MUHAS) ambapo hulazimika kuwajibika kwa halmashauri mbili tofauti.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani imeshangazwa na serikali kuchukua muda mrefu kupata suluhu ya tatizo hili la muda mrefu huku serikali yenyewe kupitia TAMISEMI ikiwa ndiyo inaratibu suala la kutangaza maeneo ya utawala nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kuwa kuna Kamati iliyoundwa na Naibu Waziri wa Ardhi kwa ajili ya kuchunguza na kushauri serikali kuhusu mgogoro huo wa mipaka ya maeneo ya utawala. Kambi Rasmi ya Upinzani inashangwaza na hatua hiyo ya Serikali kutaka ushauri upya wakati ambapo aliyekuwa Rais Jakaya Kikwete na aliyekuwa Waziri Mkuu Mizengo Pinda walishatoa majibu ya kwamba maeneo hayo yalipaswa kuwa Manispaa ya Kinondoni ambayo sasa imegawanywa na kuzaliwa Manispaa ya Ubungo.



**(f) Mgogoro kati Wananchi na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi**

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa za mgogoro kati ya Wananchi wa Vitongoji vya Nzuguu, Nzegamila na Milumbi vilivyopo Kata ya Idodyandole Wilaya mpya Itigi ambapo wanamlalamikia Mkurugenzi wa Halmashauri kuamua kuwaondoa wananchi katika Viitongoji vyao ili eneo hilo litumike kwa ajili ya uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na malalamiko mengine dhidi ya Mkurugenzi wao Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeona ni vema iwasilishe jambo hili ili ikiwezekana serikali ichukue hatua za kuona njia bora za kufuatilia malalamiko haya kabla mgogoro haujawa mkubwa. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kuwa ofisi ya Waziri Mkuu imeandikiwa kwa kina mgogoro huu na kwa hiyo inaamini hatua stahiki zitachukuliwa. Taarifa zinaonesha kuwa takribani kaya 250 zimeamriwa ziondoke katika Vitongoji hivyo ili kupisha mwekezaji.

**8. Wakuu wa Wilaya na Mikoa kuingilia majukumu ya Mabaraza ya Ardhi**

**Mheshimiwa Spika**, Mabaraza ya Ardhi yameanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 167(1) cha Sheria ya Ardhi namba 4 ya mwaka 1999 na kifungu cha 62 (2) cha Sheria ya Ardhi ya Kijiji Namba 5 ya mwaka 1999 ambapo vifungu hivyo vimeelekeza namna ya kuundwa kwa Mahakama za ardhi.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 22 cha Sheria ya Usuluhishi wa Migogoro ya Ardhi kinampa mamlaka Waziri kuunda Mabaraza ya ardhi kwa ajili ya usuluhishi wa migogoro ya ardhi.

**Mheshimiwa Spika**, leleweke kuwa ukiachia Mahakama Kuu kitengo cha Ardhi na Mahakama ya Rufaa kama zilizotajwa kwenye sheria nilizorejea, Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya, Baraza la Kata na Halmashauri ya Kijiji zina hadhi ya Mahakama (quasi-judicial) katika kushughulikia migogoro ya ardhi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Mabaraza ya Ardhi kupewa mamlaka hayo ya kisheria kushughulikia utatuzi wa migogoro ya ardhi nchini kumekuwa na tabia ya Wakuu wa Wilaya na Mikoa kuingilia mamlaka za Mabaraza ya ardhi kwa kauli au kutoa maelekezo kwa Wenyeviti ambao wamepewa mamlaka ya kuamua masuala ya migogoro.

**Mheshimiwa Spika**, tabia hii ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuingilia Mabaraza ya Ardhi haijaanza hivi karibuni, Gazeti la Nipashe la tarehe 17 April 2010 liliripoti kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma wakati huo aliamuru kumtoa ofisini Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi la Wilaya ya Kigoma Mheshimiwa R.J Kim kwa kuwatumia Usalama wa Taifa na Polisi.

**Mheshimiwa Spika**, sababu za Mkuu wa Kigoma kutoa amri ilidaiwa kuwa ni kitendo cha Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi kukiuka maelekezo ya Mkuu wa Mkoa mara kwa mara.

**Mheshimiwa Spika**, tabia hiyo ya wakati huo haijaachwa kutokana na Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuendelea kuingilia utendaji wa Mabaraza ya Ardhi kwa kauli au kwa kutoa maelekezo. Hivi karibuni Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni alinukuliwa akitoa maelezo ya kupinga maamuzi ya Baraza la Wilaya la Kinondoni kwenye moja ya hukumu za Baraza hilo akijua kuwa njia ya kupinga maamuzi hayo ni kwa njia ya rufaa.

**Mheshimiwa Spika**, aidha Mkuu wa Wilaya ya Morogoro mwezi Aprili mwaka 2017 alinukuliwa na kituo cha radio cha Abood cha Mkoani Morogoro akiwataka wananchi wa Wilaya hiyo kuwa wanaweza kupeleka taarifa za migogoro kwake kabla ya kuiwasilisha kwenye Mabaraza ya Ardhi.

**Mheshimiwa Spika**, ieleweke kuwa hata Bungeni inakatazwa kuzungumzia mwenendo wa mashauri yaliyopo Mahakamani. Aidha serikali imekuwa ikitoa sababu za mashauri kuwa Mahakamani au kwenye Mabaraza ya maamuzi na kukataa kujibu hoja mbalimbali. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kutoa kauli hapa Bungeni kama

kwa sasa Wakuu wa Wilaya wamekuwa sehemu ya Mabaraza ya Ardhi nchini. Aidha Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kupitia waraka wa TAMISEMI kama ilivyoazimiwa na Bunge kutolewa kuweka wazi kwa Wakuu wa Wilaya na Mikoa kutoingilia utendaji wa Mabaraza ya Ardhi waache utaratibu wa rufaa ufuatwe.

## 9. NHC na Nyumba za Bei Juu

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kuwa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) linafanya kazi zake kibiashara na hivyo ni lazima shirika hilo litengeneze faida kutokana na mauzo au upangishaji wa nyumba zake nchini kote.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani ilishotoa maoni hapa Bungeni kuitaka serikali kuondoa baadhi ya kodi kwenye nyumba za NHC ili kuiwezesha NHC kujenga nyumba za bei nafuu na kuwawezesha wananchi wengi zaidi kumiliki nyumba bora na hivyo kupunguza changamoto ya wananchi kuwa na makazi duni nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inakumbushia ushauri wake mwingine iliyotoa katika Bunge la kumi kuhakikisha kuwa serikali inashusha kodi ya vifaa vya ujenzi na kupunguza bei ya vifaa hivyo ili kuwezesha wananchi wenyewe kujenga nyumba zao kuliko kutegemea nyumba za NHC ambazo kimsingi hazimngusi mwananchi wa hali ya chini.

**Mheshimiwa Spika**, Ikumbukwe kuwa hivi karibuni baadhi ya vyombo vya habari viliripoti kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la wananchi hasa wa mijini kukosa makazi na wengine kulala mitaani kwa sababu ya kushindwa kulipa pango la nyumba. Kambi Rrasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kulieleza Bunge lako tukufu ni hatua gani ambazo wamezichukua kuhakikisha kuwa wanapunguza kodi kwenye vifaa vya ujenzi.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ya CCM inapaswa kutambua kuwa kuna ukuaji wa kasi wa Sayansi na Teknolojia. Leo hii ukitafuta taarifa kupitia mtandao wa *google* utapata taarifa nyingi juu ya uwepo makampuni mengi katika nchi zinazoendelea na za uchumi wa kati yanayojenga nyumba za bei ya thamani hata dola 4500 zenye kutumia teknolojia ya vifaa nafuu lakini nyumba imara na maridadi.

**Mheshimiwa Spika**, Kama NHC upeo wao ni hizo nyumba wanazozilita za bei nafuu (milioni 40) ambazo watanzania masikini hawawezi kuzimudu, kwanini Seriklai isiruhusu hayo Makampuni yakaja hapa Tanzania na kupata fursa ya kuonesha namna wanvyoweza kujenga nyumba za bei nafuu?

**Mheshimiwa Spika**, Na kwa kuanzia kama *Pilot Study* hizo kampuni ziruhusiwe zije Bukoba kwa gharama za watu wenyewe, ili ziwajengee wananchi walioathiriwa na tetemeko na kwani bado baadhi yao wanalala kwenye maturubai kwa kukosa uwezo wa kuzijenga upya au kuzikarabati nyumba zao.

## 10. Mradi wa Kuwezesha Umilikishaji wa Ardhi (Land Tenure Support Programme)

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu ambao unafadhiliwa kwa pesa za nje (Billioni 15) na za ndani (Billioni 2) ulioanza kutekelezwa Mkoani Morogoro (Ulanga, Malinyi na Kilombero) unasuasua sana kutokana na ukosefu wa fedha. Bajeti ya 2016/2017 ulitengewa shilingi bilioni 13 fedha za ndani na shilingi bilioni 10 fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, Jambo la kustaajabisha ni kuwa hadi kufikia Februari, 2017 fedha za ndani zilizotolewa ni milioni 400 tu ambazo ni sawa na 29.2% na fedha za nje ambazo ni bilioni 3.4. Kambi ya Upinzani inapenda kujua hivi kwanini Serikali inaendela na mambo yake ya kujipangia mambo makubwa isiyokuwa na uwezo wa kugharamia au kuyafanya?

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa tabia hii ya kutenga fedha nyingi wakati fedha hazitolewi kwa ukamilifu wake ni kuwaghilibu wananchi. Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji serikali, ni kwa nini isijipangie mambo machache na kwa priorities (vipaumbele) yanayoendana na mapato halisi ya kifedha? Hii tabia imeendelea kutupeleka kwenye usemi wa "mtaka vyote hukosa kwa pupa vyote" tunatawanya kidogo tulichonacho au tunachopata pasipo ufanisi wowote.

## **11. Kufutwa kwa Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu (CDA)**

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inashukuru hatimaye CDA imefutwa kwa tamko la Mheshimiwa Rais baada ya mapambano ya muda mrefu ya wananchi wakiongozwa na Viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na UKAWA kwa ujumla. Lakini lazima tuyajua matatizo yaliyoachwa na CDA ili wale waliokabidhiwa (Manispaa ya Dodoma) wayajue wayaepuke na yaliyopo ili ufumbuzi kama ifuatavyo;

(i) Wapo wananchi takribani 1000 ambao hawana makazi baada ya nyumba zao kuvunjwa bila fidia. Maeneo hayo ni pamoja na Njedengwa nyumba 270, Msangalale nyumba 35, Itega nyumba 200, Amani nyumba 107, Kisasa nyumba 5, Chinyoza nyumba 63, Mkabama nyumba 10 na Mbuyuni nyumba 37. Serikali ituambie inaelekeza nini Manispaa ya Dodoma kulitatua hili?

(ii) CDA ilishindwa kusimamia kwa haki upimaji wa viwanja na kulipa fidia stahiki kwa wananchi wenye mashamba yao yaliyoingiliwa.

(iii) CDA iliviruhusu au kufumbia macho baadhi ya maofisa wake kufanya ufisadi wa viwango vya juu na baadhi ya Maofisa kujimilikisha viwanja lukuki. Je Serikali inaelekeza nini Manispaa ya Dodoma kukabiliana na mambo hayo?

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka

serikali kuhakikisha kuwa inaielekeza Manispaa ya Dodoma kufanya tathmini ya miradi ya iliyotekelezwa na CDA kwa ujumla ili kuona namna ya kutatua mapungufu yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu yao. Aidha, Manispaa ya Dodoma ihakikishe kuwa inawashirikisha wananchi wa Dodoma wakati wa utekelezaji wa majukumu yake ya kusimamia ardhi ili kuepuka migogoro ya ardhi (nimeambatanisha baadhi ya migogoro ya CDA na wananchi kama ilivyoelezwa na Kamati Teule ya Bunge).

## 12. Miradi ya Urasimishaji

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na changamoto za kibajeti Wizara imeshindwa kuhudumia miradi ya urasimishaji kama vile Mradi wa Dar es Salaam maeneo ya Kimara ambao ulikuwa wa majaribio (pilot area) ili baadaye uende nchi nzima.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huo umekwama kwa kukosa fedha. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri Serikali kuongeza nguvu kwa utaratibu wa kutumia sekta binafsi kuwezesha huo urasimishaji kwa mfumo wa (PPP). Aidha, tunashauri Serikali iweke utaratibu wa kuingia ubia na Sekta binafsi katika mpango wa PPP ili kuja kurejesha gharama za washirika kupitia kodi zitazokusanywa baada ya urasilimishaji huo.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na wananchi wengi kuhangaika na kujibana kununua ardhi na wengine kupenda kujenga nyumba na hata kuitikia wito wa kurasimisha mashamba na makazi kwa kutumia wapimaji wa Makampuni binafsi, wengi wanakwazwa kupata hati miliki kutokana na gharama kufikia huko kuwa juu sana hasa gharama ya kitu kinachoitwa "*premium*" Mfano mwananchi anaweza kununua ekari moja ya ardhi kwa shilingi Milioni 2 akajigharamia upimaji lakini Serikali ikamtoza gharama za kuandaa hati kwa zaidi ya milioni 2.5.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani pamoja na kuitaka Serikali kuangalia upya viwango mbalimbali vya tozo zinazotowza katika kuipata Hati miliki. Pia tunashauri Serikali

uweke utaratibu unaoainisha bei elekezi kwa Makampuni binafsi yanayofanya shughuli za upimaji na gharama hizo za shughuli ya upimaji kuwekwa wazi kwa wananchi ili kuweka uwiano ulio sawa wa bei kwa maeneo yote ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha tunashauri makampuni haya binafsi yapewe ushirikiano mzuri na ofisi za Serikali na hasa Halmashuri kwani imethibitika wapo Maafisa wa Serikali hasa Idara za ardhi ambao wanaziona Kampuni hizi zimeingia kuzuia maslahi yao waliyokuwa wamezoea hapo kabla.

**Mheshimiwa Spika**, Misimamo na ushindani wa itikadi za kisiasa nao umeonekana kuwa kikwazo kwa badhi ya maeneo. Mfano mzuri ni Mji mdogo wa Katoro Geita ambapo ramani imeandaliwa tangu mwaka 2015 ambapo Mtaa wa California ulipimwa na kupatikana viwanja 1462 ikapelekwa wizarani na ikarudi. Kazi iliyokuwa imebaki ilikuwa ni kupima kwa maana ya kuweka *becons*.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kazi hizo zote kugharamiwa na kampuni binafsi iliyopewa kazi hiyo na Halmashauri ya Wilaya ya Geita kwa mkataba pale Katoro siasa za vyama za ushindani zimechukua nafasi kubwa kuliko kazi inayopaswa kufanyika.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuyatolea tamko maeneo kama hayo ambayo Viongozi waliopewa dhamana ya kusimamia mambo wanakuwa sehemu ya kukwamisha michakato ya urasimishaji makazi kwa wananchi kwa sababu ya itikadi kisiasa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani tunayashukuru na kuyahimiza maeneo yote ambayo yamekuwa na mwamko katika utekelezaji wa mpango huu wa urasimishaji ili waendeleo kwa kasi zaidi, kwa mfano Kata mbalimbali za Bukoba Town, Karagwe Mtaa wa Katome- Ruzinga, Kyaka Wilaya ya Misenyi, Mwanza Wilaya ya Ilemela na Nyamagana na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Morogoro.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha tunatoa shukurani kwa Waziri wa Ardhi kwa hamasa ambayo amekuwa akiitoa katika zoezi hili la urasimishaji wa makazi na hata kuhudhuria yeye binafsi kwenye hafla mbalimbali za kukabidhi hati. Tunaendelea kusisitiza kuhusu Wizara kuendelea kutoa hamasa na elimu kwa wananchi ili waweze kushiriki kikamilifu katika kurasimisha makazi na ardhi zao.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuondoa ukiritimba na kero ambayo imejitokeza kwa baadhi ya Wilaya zinazowataka watu waliopima maeneo yao kufuata hati zao ofisi za Kanda wao wenyewe. Tunashauri maafisa wa ardhi ndani ya Halmshauri wawe wakizifuatilia hati hizo kwenye Ofisi za Kanda ili wananchi waweze kuzichukua kwenye ofisi za Halmshauri zao.

### 13. Hati za Kimila

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kutambua umuhimu wa hati za kimila hasa kwa wananchi wa Vijijini lakini Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa zoezi hili linasuasua na haliendi kwa kasi inayotakiwa na sehemu nyingi utoaji wa hati hizi umesimama. Serikali ilieleze Bunge hili ni kwanini zoezi hili haliendelei kama inavyopaswa?

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona sababu mojawapo inaweza kuwa ni kutothaminiwa kwa hati hizo katika taasisi nyingi za kifedha zinazotoa mikopo kama zilivyo hati za kawaida. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunaitaka Serikali ndani ya muda muafaka ilete ndani ya Bunge takwimu zinazoonyesha ni hati za kimila ngapi na maeneo zilizopo na ni wa mabenki gani zimetumika kuchukulia mikopo. Na mikopo hiyo ni ya kiasi gani cha fedha.

**Mheshimiwa Spika**, takwimu hizo zitasaidia wananchi kuona umuhimu wa kuwa na hati hizo lakini pia kuwafanya Waheshimiwa Wabunge kuendelea kutoa hamasa kwa wananchi kuunga mkono zoezi hili na hatimaye kujipatia hati zao kwa ajili ya shughuli zao za kiuchumi.



#### 14. Upungufu wa Watumishi wa Sekta ya Ardhi

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri nyigni zinakabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi wa Sekta ya Ardhi kitu kinachofanya huduma za ardhi yaani kupanga Miji na kufanya uthamini na kutoa Hati Miliki kuwa duni.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kutoa mfano mmoja tu wa Halmashauri ya Ngara ambayo haina mtaalam yeyote wa Sekta ya Ardhi. Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kuwa tatizo hili liko katika Halmashauri nyingi nchini jambo ambalo linarudisha nyuma shughuli mbalimbali za sekta ya ardhi nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuhakikisha kuwa inakuwa na mpango endelevu wa kuhakikisha Halmashauri zote zinakuwa na Watumishi wenye utaalamu wa masuala ya ardhi ili kurahisisha huduma kwa wananchi lakini pia kuepuka migogoro isiyo ya lazima kutokana na kukosekana wataalamu hao.

#### 15. Mashamba ya Ushirika Yarudishwe kwa Wananchi

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kutambua kuwa masuala ya ushirika yanashughulikiwa na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi lakini Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuweka wazi msimamo wake kuwa kwa kuwa miliki ya ardhi nchini husimamiwa na Wizara hii ni vema tukaonesha japo kwa ufupi masuala ya ardhi yaliyopo chini ya Ushirika ili serikali ichukue hatua za dharura.

**Mheshimiwa Spika**, Lipo shamba la Garagagua lilipopo Wilaya ya Siha Mkoani Kilimanjaro ambalo lina ekari takribani 3400 ambalo awali lilikuwa chini ya Chama cha Ushirika cha Mkoa wa Kilimanjaro (KNCU). Kutokana na ushirika huo kushindwa kulipa deni la mkopo uliotolewa na Benki ya CRDB, Benki hiyo ililazimika kuliuzwa kwa mnada kwa mwekezaji ambae pia ni mmiliki wa mashamba ya Kifufu maarufu kwa kilimo cha maparachichi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na tuhuma hizo za ufiadini kutoka kwa vyama vya msingi dhidi ya KNCU wananchi wa maeneo yanayozunguka shamba hilo wana uhitaji mkubwa wa ardhi na wameiomba serikali hata kabla ya shamba hilo kupigwa mnada ili serikali iweze kupima shamba hilo na kuwamilikisha baada ya KNCU kushindwa kuliendeleza na kuitumia kama collateral kupata mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha. Taarifa kuhusu shamba hili na ufiadini wote uliofanyika zinajulikana katika ngazi zote za serikali kwa sababu ni za muda mrefu zikiwemo idara ya Usalama wa Taifa na TAKUKURU.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuchukua hatua dhidi ya waliohusika na sakata la mali za KNCU ikiwemo waliohusika na kuhujumu shamba la Garagua na kuona namna gani wanaweza kuzungumza na mwekezaji aliyezuwa Shamba hilo kwa mnada kama anaweza kuachia wananchi shamba hilo.

**Mheshimiwa Spika**, mashamba mengine ya ushirika ni yale yaliyopo Wilaya ya Hai Mkoani Kilimanjaro ambapo baadhi ya vyama vya msingi wameyatumia kwa muda mrefu kuyakodisha kwa wananchi kila msimu wa kilimo kwa maslahi binafsi na sio kwa manufaa ya ushirika. Kwa kuwa kuna uhaba mkubwa wa ardhi kwa wananchi wa Jimbo la Hai, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kuwa serikali iyachukue mashamba hayo na kuyapima na kuwapa wananchi hasa wenye kipato cha chini ili wayamiliki kihalali kuliko kuyaacha kuwa sehemu ya mapato kwa viongozi wachache wa vyama vya msingi. Aidha, mashamba haya yanaweza kutumiwa na wananchi kuzalisha kwa wingi kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji na kuwa chanzo cha mali ghafi za viwanda vinavyoshughulika na mazao ya kilimo.

**Mheshimiwa Spika**, Waziri anatambua maombi ya muda mrefu ya wananchi wa Hai kupitia kwa Halmashauri ya Wilaya kuomba sehemu ya ardhi ya Kiwanda cha Machine Tools ambacho kwa sasa hakizalishi. Msingi wa maombi ya wananchi ni kutaka sehemu ya ardhi ijengwe ofisi za Mji Mdogo wa Hai ambao utakuwa ni sehemu ya kuendeleza

biashara za wananchi lakini kikubwa zaidi ni ujenzi wa Kituo cha Polisi ambacho kitaimarisha ulinzi katika eneo hilo ambalo limekuwa likiathiriwa kwa kiasi kikubwa na matukio ya ujambazi. Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuhoji kama maombi hayo Wizara imeyafanyia kazi.

## **16. Mapitio ya Bajeti ya Mwaka 2016/2018 na Mwelekeo wa Bajeti ya Mwaka 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2016/17 Wizara ilitengewa jumla ya shilingi 61,873,949,000/= kati ya fedha hizo, miradi ya maendeleo ilitengewa shilingi 20,000,000,000/= ambazo shilingi 10,000,000,000/= zikiwa fedha za ndani na shilingi 10,000,000,000/= . Fedha za matumizi mengineyo zilizotengwa ni shilingi 25,531,158,000/=

**Mheshimiwa Spika**, takwimu za wizara zinaonesha kuwa hadi mwezi februari, 2017, fedha za matumizi mengineyo (OC) zilizopokelewa ni shilingi 9,994,249,148/- sawa na asilimia 39.2 ya bajeti iliyopitishwa na Bunge. Aidha kwa miradi ya maendeleo fedha zilizokuwa zimepokelewa ni shilingi 7,626,219,314/= sawa na asilimia 38, lakini katika hizo fedha za maendeleo kuna shilingi 3,301,058,684.65 kwa ajili ya kulipia deni la Mkandarasi aliyeandaa Mipango Kabambe ya Majiji ya Arusha na Mwanza,

**Mheshimiwa Spika**, kwa hali hiyo ni kwamba fedha halisi zilizopokelewa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kipindi cha bajeti ya mwaka 2016/17 ni shilingi 4,325,160,629.4 tu sawa na asilimia 21.62 pekee.

**Mheshimiwa Spika**, mwaka wa fedha 2017/18 Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 68,030,880,526/- kwa ajili ya kutekeleza kazi zake. Kati ya fedha hizo shilingi 21,470,166,074/- ni matumizi mengineyo, ikiwa ni pungufu ya shilingi 4,060,991,926/- kwa kulinganisha na maombi ya mwaka jana kwa matumizi mengineyo. Fedha za maendeleo zinaombwa jumla ya shilingi 25,400,000,000/-

**Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri kuwa wizara hii bado inao

uwezo wa kukusanya mapato mengi, lakini haiwezi kufanya hivyo kama uwekezaji hautafanyika. Hii inaonekana wazi kwa kuangalia kiasi kilichotengwa mwaka jana na kilichotolewa. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri fedha za maendeleo ziongezwe ili upimaji wa ardhi na umilikishwaji ufanyike kwa haraka ili kodi ya ardhi ikusanywe. Uwezi kuvuna usipowekeza!!

## 17. Hitimisho

**Mheshimiwa Spika**, imekuwa dhamira na dira yetu ya Kambi Rasmi ya Upinzani kutochoka kutimiza haki na jukumu letu la kikatiba, kisheria na kikanuni la kuikosoa na kuishauri Serikali ya CCM japo tunapata masimango, mabezo, dharau n.k Tunaamini Mungu anaona na siku moja atatenda. Na kama sio leo au kesho vizazi vyetu vijavyo vitatoa hukumu ni yupi alikuwa kikwazo.

**Mheshimiwa Spika**, hotuba zetu za miaka ya nyuma tumekuwa tukishauri na tunaendelea kushauri kuwa:

1. Tukae kama Taifa kujipanga upya kutengeneza dira kupitia katiba mpya inayozungumzia namna ya kusimamia na kugawa rasilimali Ardhi.
2. Ni vyema Wizara hii na Serikali kwa ujumla ikapanga katika bajeti zake. Mambo machache ya kufanyiwa kazi (Kwa kuangalia vipaumbele) kuliko utaratibu wa sasa wa kujirundikia majukumu mengi ambayo kwa ufynyu mkubwa wa mapato ya Serikali yamekuwa yanatekelezwa kwa uhaffu na hivyo kuonekana kama ghilba kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, kama tulivyoshauri, tungelikamilisha mfumo unganishi wa kuhifadhi kumbukumbu za ardhi (Integrated land Management of land information system) tungelipunguza au kuondoa kabisa migogoro ya ardhi nchini. Pia Serikali ijitazame upya juu ya utaratibu wa kugawa maduhuli yake kwa ofisi, Wizara na taasisi zake; je inatoa kwa uwiano ulio sawa au inatolewa kwa mfumo wa utaratibu wa "mwenye kisu kikali ndiye mla nyama".

**Mheshimiwa Spika**, kama hatujaliona hilo la kujipanga upya na kuendelea kufanya kazi kimazoea kwa kutegemea umahiri au zaidi mitizamo ya mtu mmoja aliyeko katika nafasi ya kimaamuzi kwa wakati huo, ni wazi marathoni yetu ya utatuzi wa kero za ardhi haitakuwa na mwisho.

**Mheshimiwa Spika**, kwa staili hii, ni kwamba tutaendelea kubadilisha chupa lakini mvinyo utaendelea kuwa ni uleule.

---

WILFRED MUGANYIZI LWAKATARE (Mb)  
**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI  
NA WAZIRI KIVULI WA ARDHI, NYUMBA NA  
MAENDELEO YA MAKAZI  
25 Mei 2017**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza na mjadala wetu, tutaanza na Mheshimiwa Faustine Ndugulile atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka baadaye atafuatia Mheshimiwa Maftaha Nachuma.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa ya kwanza ya kuwa mchangiaji katika hotuba ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Nianze kwa kumpongeza sana Waziri Mheshimiwa William Lukuvi, Naibu Waziri Mheshimiwa Angeline Mabula, Katibu Mkuu Dkt. Kayandabila na safu yake kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaendelea kuifanya katika Wizara ya Ardhi. Kwa mara ya kwanza nitaanza kuiongelea vizuri Wizara ya Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mitano ambayo nimekuwa Mbunge katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sijawahi kuunga mkono bajeti ya Wizara ya Ardhi, inawezekana leo ikawa ndiyo mara yangu ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la kwanza ambalo nilitaka niligusia ni suala la *premium*. Mheshimiwa

Waziri ameongea katika hotuba yake kwamba amepunguza *premium* kutoka 7.5 *percent* kwenda asilimia 2.5. Tunatoa pongezi nyingi sana kwa Serikali, lakini bado tunaamini kwamba kiwango hiki bado ni kikubwa sana. Waende wakaliangalie tena. Katika suala la mashamba makubwa ambayo wamekuwa wanayahimiza wananchi wayapime, kikwazo kimoja cha kupanga Miji na upimaji imekuwa ni *premium*. Kwa hiyo, naomba waende wakaiangalie upya ili kama ikiwezekana tuiunguze zaidi na itatoa hamasa kwa wananchi kupima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni viwango vya *land rents*; kodi za ardhi nazo bado kuna wakati walipandisha, nadhani sasa wamefanya marekebisho. Suala hapa siyo kupandisha viwango, suala hapa ni kuhamasisha wananchi waweze kuwa wanalipia. Tukiongeza viwango vikawa vikubwa sana, ulipaji nao utakuwa ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nataka sana Wizara nayo itusaidie, asilimia 30 ya mapato yale ya *land rent* yanayotakiwa kurudishwa katika Halmashauri, mpaka wakati tunatengana na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke tulikuwa tunaidai Wizara ya Ardhi takribani Sh.3,000,000,000/=. Ni fedha nyingi sana ambazo zingeweza kutusaidia katika maendeleo ya Halmashauri zetu. Sasa nadhani ifike mahali kama inashindikana fedha ile kwenda na wao wakaturejeshea 30 *percent*, kwa nini sasa tusipitishie sheria tufanye mabadiliko tu-*retain* ile 30 *percent* na sisi tuwapatieni ile hela nyingine iliyobaki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo nataka kuligusia ni *master plan* ya Mkoa wa Dar es Salaam. Dar es Salaam inakuwa kwa kasi kubwa sana, lakini utengenezaji wa *master plan* umekuwa unakwenda muda mrefu sana. Nimeona katika ripoti yao wanaongelea mwezi Agosti, naamini Agosti itakuja nayo itakwisha. Tungependa kuona ifikapo mwisho wa mwaka huu tuwe na *master plan* ya Dar es Salaam, ujenzi holela unatapakaa kwa kasi kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nne ambalo ninataka kuligusia ni mradi wa viwanja 20,000 katika Jimbo langu la Kigamboni, hususan katika eneo la Kibada. Wananchi walionunua viwanja vile, walilipa *premium* ambayo inaendana na utengenezaji wa miundombinu. Mpaka sasa hivi tunavyoongea kuna wananchi wa Kibada wanaelea, kuna viwanja wamewapa kwenye mabonde, sasa hivi kuna wananchi wa Kibada wanashindwa kufika majumbani kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kibada hawana miundombinu ya kufika katika makazi yao na nitamwomba sana Mheshimiwa Waziri baada ya bajeti yake twende Kibada akawaone wananchi wale ambao walilipa fedha na wanalipa kodi ya ardhi, wanaishi kwa shida sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ambalo nataka kuliongelea ni suala la Kigamboni. Serikali ilikuja na mpango wa Kigamboni mwaka 2008 tunavyoongelea sasa hivi ni mwaka wa tisa, wananchi wale hawajengi, hawakarabati, hawauzi wala hawakopesheki. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri tangu ameingia katika Wizara ile, tumeweza kufanya kazi kubwa sana mimi na yeye na namshukuru sana chini ya uongozi wake, yale ambayo wananchi wa Kigamboni tuliyokuwa tumesimamia, ameweza kuyasimamia na kuyatekeleza kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana yeye na safu nzima ya Wizara yake. Hatua tuliyofikia ni nzuri sana na ndiyo maana mnaona Mbunge wa Kigamboni sasa hivi ametulia, la sivyo siku za nyuma hapa pangukuwa hapatoshi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kuna lile ombi ambalo tumeleta kwenu Serikalini na ambalo nashukuru Mheshimiwa Waziri ameligusia kwa kidogo. Kuwepo mamlaka mbili za kupanga mji inaleta kero na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuvunja *CDA*. Sisi pia sasa

tunasema *KDA* hatuitaki. Tunaomba mradi ule uletwe chini ya Halmashauri mpya, chini ya uongozi mpya wa Kigamboni ili sisi wenyewe tukausimamie. Mheshimiwa Waziri akiweza kulitekeleza hilo, tutakuwa marafiki wa kudumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, machache nakushukuru sana na kwa mara ya kwanza naunga mkono bajeti ya Wizara ya Ardhi. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Mwakasaka.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa pili katika Wizara hii. Nami kama Msemaji aliyetangulia nianze kwanza kupongeza kwa jinsi ambavyo Mheshimiwa Lukuvi pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Angelina Mabula wanavyokwenda na kasi ya kuweza ku-*so/ve* migogoro mbalimbali ya ardhi katika nchi hii, kitu ambacho tulikuwa hatujazoea kukiona mara kwa mara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lukuvi amekwenda sehemu nyingi sana na pengine kama alivyosema Mheshimiwa Ndugulile, kwa kawaida alikuwa anapinga mambo mengi ya ardhi lakini leo anaunga mkono hoja, basi na mimi nianze kwa kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo kuna changamoto chache ambazo nyingi tumeshazifikisha ambazo zinahusiana na Mkoa wetu wa Tabora na hasa Tabora Manispaa. Tabora Manispaa sijui niseme ina bahati mbaya au nzuri, lakini kwa ulinzi ni bahati nzuri kwamba tumezungukwa kwa kiwango kikubwa na Kambi za Jeshi. Sasa kumekuwa na mwingiliano mkubwa sana baina ya wanajeshi pamoja na wananchi na hili mara kwa mara nimekuwa nikilizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na migogoro mikubwa ambayo tayari imeripotiwa mara nyingi,



ningemwomba Mheshimiwa Waziri watafute utaratibu wa Wizara ya Ardhi pamoja na Jeshi kwa maana ya Ulinzi ili kuweza kutatua migogoro ile kwa sababu inahatarisha amani. Maeneo mengi ambayo ni ya Jeshi kwa madai yao, wameweka zile *beacon* ambazo wanazitambua wao, lakini wananchi sehemu nyingi hasa maeneo ya Usule, Kata za Mbugani, Tambukareli, Cheyo, Mtendeni na Malolo wanazo *beacon* za muda mrefu ambazo walipimiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Jeshi wanapokuja na wao wanasema wana alama zao, hili suala limekuwa na mgogoro wa muda mrefu, naomba Wizara iweze kulishughulikia suala hilo ili wananchi pamoja na Jeshi wasiwe na mgogoro na kwa kuzingatia kwamba Jeshi mara nyingi hawatumii maeneo yale, wananchi wamekuwa wakiyatumia kwa kilimo. Sasa wale wananchi waweze kupewe ruhusa, tunaongelea kilimo, sasa Jeshi eneo kubwa hawalimi kabisa na wananchi wamekuwa wakilima muda mrefu basi watatue hili suala ili wananchi waweze kuyatumia maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo lenyewe sitalizungumzia kwa undani ila kwa kuwa nimesikia hapa pia yupo Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi Dkt. Yamungu, tuna Chuo cha Ardhi pale Tabora Mheshimiwa Waziri cha Ardhi kina changamoto nyingi sana, kuna upungufu mwingi ikiwemo na vitendea kazi. Chuo hiki cha Ardhi ni cha miaka mingi na changamoto zile walimwakilishia Dkt. Yamungu akiwa ni mgeni rasmi kwenye mahafali ya Chuo cha Ardhi yaliyopita ambayo na mimi nilihudhuria, nina imani kama hajamfikishia Mheshimiwa Waziri changamoto zile basi amfikishie rasmi, kwa sababu yuko hapa waliorodhesha changamoto nyingi, basi nisiziorodheshe sasa hivi yeye atampatia ili aweze kuzifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu nije kwenye hivi viwango maalum wanavyolipa wamiliki wa nyumba na majengo. Tabora Manispaa ndiyo peke yake ambayo imekuwa inalipa Sh.25,000/= kwa mwaka ilikuwa ni *flat rate*. Tofauti kabisa na Manispaa na Halmashauri zingine ambazo

nyingi zilikuwa zinalipa kwa mfano, Morogoro Sh.10,000/=, Temeke Sh.15,000/=; Mwanza Sh.10,000/=; Manispaa ya Songea Sh.12,500/=, lakini Tabora Mjini Sh.25,000/=. Sasa sijaelewa ni vigezo gani pamoja na kwamba kitu kinachotumika wanadai kwenye ile *valuation* wanatumia ile 0.25 thamani ya nyumba wana *calculate* kwa hiyo 0.25 kupata thamani au tozo ambayo anayotakiwa kutozwa huyu mmiliki wa nyumba au jengo. Hata hivyo, katika sehemu nyingi imekuwa ni Sh.10,000/=, haijafika Sh.20,000/= kwa nini Manispaa ya Tabora ni Sh.25,000/= ? Naomba Mheshimiwa Waziri hilo aweze kuliangalia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne naomba nizungumzie nyumba zinazojengwa na *National Housing*. Nia ni njema kwamba waweze kuzikopesha nyumba hizi kwa watu mbalimbali na hasa wanyonge pia ikiwezekana, lakini kuna mchezo mchafu unafanyika kwenye hizi nyumba. Kuna wenzetu ambao wana uwezo mkubwa wa kifedha huwa wanazinunua hizi nyumba wao, wanazinunua kwa wingi na wakati mwingine kwa majina mbalimbali halafu wanakuja kuzipangisha. Sasa naomba wafanye uchunguzi watu wa namna hiyo waweze kudhibitiwa ili kweli lile lengo la kwamba watu wapate nyumba nafuu liweze kutimia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niongelee hili suala la Wathamini wa Ardhi (*Valuers*) wamekuwa hawawatendei haki wananchi wengi hasa wanyonge, siyo wote lakini baadhi yao. Wanapofanya *valuation*, hapa kwenye *valuation* huwa ndiyo kuna harufu hapa ya rushwa. Unaweza ukakuta kwa mfano kiwanja ambacho labda au nyumba ambayo ingekuwa na thamani ya Sh.50,000,000/= huyu *Valuer* kwa sababu hajaongea kwa matamshi ambayo angeyataka yeye ana-*value* ile labda kwa Sh.2,000,000/=. Sasa yule mnyonge anashindwa afanye nini kwa sababu huyu mtu wa *valuation* ndiye anayetambulika kisheria kwamba akifanya *valuation* basi hiyo ndiyo itafuatwa. Mheshimiwa Waziri naomba hawa *Valuers* siyo wote lakini baadhi yao siyo waaminifu na eneo hilo lina mambo mengi ya rushwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kuongelea suala la Sheria ya Mabaraza ya Ardhi Namba mbili (Na.2) ya mwaka 2002. Ni kweli uanzishwaji wake ulikuwa ni wa muhimu kwa sababu kila Wilaya ikiwa na Baraza la Ardhi angalau migogoro mingi ya ardhi itapungua. Naiomba Wizara fedha ambayo inatakiwa kwa ajili ya kuanzisha Mabaraza ya Ardhi kila Wilaya ipelekwe kwa wakati unaotarajiwa ili sehemu nyingi kuwe na Mabaraza haya ya Ardhi kwa ajili ya kuweza kutatua migogoro mingi ya ardhi katika sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache, narudia kuunga mkono hoja na nasema ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwakasaka, tunaendelea na Mheshimiwa Maftaha Nachuma.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia. Kwanza kabisa naomba nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanah Wataala* ambaye ameendelea kunijalia afya njema na leo hii niweze kuzungumza machache niliyokuwa nayo, pili nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi asubuhi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba wakati nachangia bajeti ya Wizara ya Maji, nilizungumza hapa kwamba Mtume Mohammed alisema Karne ya Sita kwamba *Man laa yashkur nnasa, laa yashkur Allah*, kwamba mtu yeyote ambaye hashukuru binadamu wenzake kwa wema wanaofanya basi hata Mwenyezi Mungu kwa neema alizompa hawezi kumshukuru pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee kabisa naomba nikiwa kama mzalendo wa Taifa hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kitendo kikubwa alichokifanya jana, kwa maamuzi magumu aliyoyafanya jana, kuhakikisha kwamba wale wanaotorosha madini yetu kwenda nje ya nchi

wanachukuliwa hatua kwa kunyang'anywa yale madini. Tunampongeza kweli na ni kitendo cha kishujaa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze tu kwamba nchi hii kama hatuchukui maamuzi magumu tutaendelea kuwa maskini mpaka kiama. Wenzetu walioendelea duniani kupitia sekta hii ya madini, nchi ndogo kama Botswana ni kwa sababu wanachukua maamuzi magumu. Nimwombe Mwenyezi Mungu aendeleo kumpa afya njema Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania achukue maamuzi magumu zaidi, Tanzania tuondokane na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mimi ninayezungumza hapa kama siyo kufanya maamuzi magumu nisingekuwa Mbunge leo hii, mimi nilikuwa Mwalimu, nikaandika barua kuomba likizo isiyokuwa na malipo ili niweze kugombea Jimbo la Mtwara Mjini, lakini kulikuwa na ujanja ujanja ulifanyika wakaninyima ruhusa nikamua kuacha kazi masaa 24 ili niweze kugombea Ubunge na leo hii nazungumza ni Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Jimbo la Mtwara Mjini ni kwa sababu ya maamuzi magumu. Kwa hiyo, hii nchi kama tunahitaji maendeleo lazima tuwe na Viongozi wanaochukua maamuzi magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwa namna ya kipekee kabisa, niishukuru Wizara hii ya Ardhi, siku kadhaa zilizopita nilikuwa Mtwara nikiwa na Mheshimiwa Waziri hapa tulienda kuzindua mpango kabambe ambao unaitwa *master plan* kwa mara ya kwanza tangia Serikali hii ya Awamu ya Tano mpango wa kwanza kuzindua ni mpango wa *master plan* wa Mtwara Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kufanya kazi kubwa sana na wananchi wa Mtwara sasa kwa sababu hii *master plan* ambayo tumeizindua juzi ndiyo mwarobaini ya migogoro yote ya ardhi pale Manispaa ya Mtwara Mikindani. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na namshukuru sana, Mungu ambariki

aendelee kutatua migogoro mingine ambayo ipo katika maeneo mbalimbali ya nchi hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, wakati nafanya kampeni 2015 niliweza kuzungumza mambo mengi sana yanayohusu ardhi, kwa sababu Mtwara Mjini kulikuwa na changamoto nyingi sana za ardhi. Miongoni mwa mambo mengi ambayo nilikuwa nayahutubia na wananchi wangu wakanituma nije kueleza katika Bunge hili, ilikuwa ni suala la urasimishaji wa ardhi. Mheshimiwa Waziri hapa wakati anazungumza kwamba maeneo kadhaa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hivi sasa urasimishaji unaendelea ikiwemo Jimbo la Mtwara Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara hii na namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa kubariki Mtwara Mjini, lakini pia kutuletea Wataalam ambao tunashirikiana nao katika suala hili la urasimishaji wa ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wito wangu kwa Madiwani wa Jimbo la Mtwara Mjini, wahamasishe wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini ili zoezi hili liweze kukamilika kwa wakati. Kwa namna ya kipekee kabisa nawashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Mtwara Mjini kwa kuendelea kuwa na imani na Mbunge wao na nawaambia kwamba naendelea kupambana, nitawatetea kipindi chote cha miaka yote iliyobaki na Mtwara Mjini sasa ni Mtwara kuchele kweli kweli, siyo kama kauli za kubeza za miaka ya nyuma kulivyokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani hizo za dhati kabisa naomba nizungumze suala moja ambalo hivi sasa pale Mtwara Mjini, nimwombe Mheshimiwa Waziri atusaidie katika hili. Mtwara Mjini kuna eneo linaitwa Mangowela, sasa hivi wamebatiza jina panaitwa Libya, hili eneo lilikuwa linamilikiwa na Wazee Nane wa Mji wa Mtwara, na hapa nina majina yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niyasome haya mbele ya Bunge lako hili Tukufu, wamiliki wa eneo hili ni Mzee Mohammed Saidi Mussa, Mussa Ismail Selemani, Ndugu Karama Akidi Ismail, Ndugu Abdallah Mfaume Mkulima, Ndugu Fatu Mchimwamba, Ndugu Abubakari Zarali Mohammed, Ndugu Musa Saidi na Ndugu Ashiraf Makuti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee hawa ni wazee ambao wamezaliwa miaka 1920 huko nyuma, walikuwa wanamiliki eneo hili la Mangowela, lakini hivi sasa linaitwa eneo la Libya, lakini jambo la ajabu sana ambalo lilifanyika miaka ya 2000 wameamka asubuhi wakakuta *beacon* zimewekwa, walivyoulizwa hizi *beacon* zilizowekwa katika eno hili la Libya ni za nini, wanaambiwa kuwa hili eneo limeuzwa na wamiliki wa eneo hili. Wakashangaa sana, kwamba wamiliki wa eneo hili ni watu wa aina gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, huu mgogoro ni mgogoro ambao ni mkubwa sana hivi sasa Mtwara, naipongeza Wizara hii kwamba jana niliuliza swali hapa juu ya mgogoro wa Mji Mwema na kwamba tayari wameshamaliza na fidia ile inaenda kulipwa mwisho wa mwezi huu, tunashukuru sana kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri mgogoro huu wa Mji wa Libya, naomba sana wananchi hawa wamekuja Ofisini kwangu zaidi ya mara nne, wametembea maeneo yote kudai haki yao, lakini mpaka leo wanaambiwa lile eneo limeuzwa na wao wameuzwa bila wao kuelezwa. Hata hao waliouza wanasema kwamba walipewa na watu fulani, lakini hakuna *documents* zozote kwamba lile eneo lilikuwa ni la kwao, wamiliki wa eneo hili la Libya ni hawa wazee ambao nimewasoma hapa, kwa hiyo tunaomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja atusaidie katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kuzungumza Mbunge mmoja kaongea hapa kuhusu shirika la *NHC* (Shirika la Nyumba Tanzania), kwa kweli linafanya kazi kubwa sana

ya kuhakikisha wanaboresha makazi ya Watanzania, wanajenga majumba maeneo mengi, lakini nyumba hizi ambazo zinajengwa kwamba eti ni nyumba za maskini, kimsingi siyo nyumba za maskini. Mfano tu hata nikiwa Mwalimu pale Lindi, mwaka 2007, kuna nyumba zilijengwa pale Lindi, lakini zile nyumba mimi nilienda kuomba kama Mwalimu, Mwalimu ambaye nilikuwa nachukua mshahara 940,000 wakati ule, nikaambiwa kwamba zile nyumba wewe kama Mwalimu huwezi kuzinunua ni nyumba ambazo zinaanzia Sh.50,000,000/= na Sh.60,000,000/= huko na kuendelea. Sasa hizi kweli ni nyumba za bei nafuu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba Waziri ahakikishe kwamba hii *NHC* kweli ijenge nyumba za bei nafuu ili Watanzania wengi maskini waweze kupata hizi nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze pia suala hili la kucheleweshwa hati, Mheshimiwa Waziri ana mpango mzuri sana hapa, kazungumza vizuri sana, kwamba ametoa maagizo kwa Taasisi zote, kwa Halmashauri zote, wahakikishe kwamba tunaenda kama Wabunge kukagua Masjala za Halmashari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe atoe agizo lingine kwamba ucheleweshaji wa hizi Hati unafanywa na Watendaji wa Halmashauri na watu wa ardhi wa Halmashauri na wale ambao wataendelea kukiuka agizo lako Mheshimiwa Waziri, basi hawa watu aweke hatua za kuchukuliwa mara moja ili sasa tatizo hili la kuchelewesha Hati Tanzania liweze kwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri ambayo tumeifanya kuanzia asubuhi hadi mchana sasa hivi, Mungu awabariki sana. Kabla sijasitisha shughuli za Bunge naomba nitaje majina ambayo yataanza kuchangia jioni ya leo.

Tutaanza na Mheshimwa Richard Ndasa, atafuatiwa na Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa Stanslaus Mabula, Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mheshimiwa Martha Umbulla na Mheshimiwa Salma Mwassa.

Waheshimiwa Wabunge baada ya kutaja majina hayo nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11 jioni ya leo.

*(Saa 6.52 Mchana, Bunge lllisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Tunaendelea na majadiliano yetu na kama nilivyowataja mchana, tunaendelea sasa tuko na Mheshimiwa Ndassa, baadae Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Stanslaus Mabula wajiandae.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nami niungane na wachangiaji wenzangu waliopita kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kwa kazi nzuri sana wanayofanya katika Wizara hii ya Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lukuvi ni Waziri wa mfano na hili wala halina kificho, kwa hiyo nimwombe tu Waziri Mheshimiwa Lukuvi pamoja na timu yake basi ile *speed* ambayo wanayo ikiwezekana waongeze kwa sababu ardhi ndiyo kila kitu, maeneo mengi inatakiwa watu wapimiwe ili wakae kwenye makazi salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais. Kitendo alichokifanya jana cha kuwaonesha Watanzania na dunia kwa ujumla katika sakata kubwa la usafirishaji wa mchanga. Kazi ile imefanywa kitaalam na niwaombe Waheshimiwa Wabunge wote, wa vyama vyote, hata mdogo wangu pale Mheshimiwa Ester Bulaya, kwa sababu bahati nzuri wenzetu upande wa kule mlikuwa kila siku mkisema kwamba



tunaibiwa sasa ule ni mwarobaini, sasa tumuunge mkono Mheshimiwa Rais kwa hatua hii ambayo ameichukua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nimpungeze pia Mheshimiwa Rais kuhusu kuivunja CDA. Mheshimiwa Lukuvi mimi ni mmoja wa wahanga niliyedhulumiwa kiwanja changu na bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu, nafikiri kwa hali ya sasa tutakwenda vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara mwaka huu imepanga kukusanya maduhuli, tozo shilingi bilioni 112, nilikuwa najaribu kuangalia ile *trend*, mwaka 2015/2016 Mheshimiwa Waziri alipanga kukusanya bilioni 70, akakusanya bilioni 74, mwaka uliopita 2016/2017 alipanga kukusanya milioni 111.7 mpaka Mei ana bilioni 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu najua yeye pamoja na timu yake ni wachapakazi wazuri na mimi kama Mjumbe wa Kamati hiyo tungependu zaidi ile bajeti ambayo wameipanga wakaitekeleze, kwa sababu ili apate fedha za kuweza kufanyia kazi kwenye maeneo ambayo ameyapanga lazima makusanyo, ikiwemo na tozo ziweze kupatikana. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake *speed* iongezeke, lakini pia kuzuia mianya ya pesa zinazotumika vibaya kwa sababu bila kuzuia mianya hawezi akakusanya vizuri. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri aliangalie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nimwombe, Halmashauri zetu huko tuliko bila kuficha Mheshimiwa Waziri hatuna uwezo wa pesa wa kupima kila kitu, tunayo Miji, lakini nianzie upande wa taasisi za Serikali, shule za msingi, shule za sekondari, zahanati, vituo vya afya, tukiacha kwa jinsi ilivyo sasa taasisi za Serikali zinavamiwa, inawezekana hata kwa Mheshimiwa Waziri zipo shule za msingi na shule za sekondari zinavamiwa na watu, wanajenga karibu na shule. Unakwenda kujenga karibu na shule ya sekondari pale kuna wasichana, kuna vijana, kuna nyumba ya makazi pale, kwa

hiyo mtajikuta kwamba hakuna kitakachokuwa kinaendelea kwa sababu mji na shule ni vitu viwili tofauti. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri hili alitazame vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, nimejaribu kuangalia kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri mipaka ya Kimataifa na anasema kwa mwaka 2017/2018 Wizara itaendelea na uimarishaji wa mpaka wa Tanzania na Kenya ikiwa ni pamoja na utengenezaji wa ramani za msingi pamoja na kupima kipande cha mpaka kuanzia Ziwa Victoria hadi ziwa Natron. Akaendelea, Majadiliano kati ya Tanzania na Zambia, Tanzania na Uganda kwa ajili ya uimarishaji wa mipaka yanaendelea.

Mheshimiwa Waziri, Watanzania tunaweza sisi tukawa watulivu lakini huwezi ukajua nchi zingine kwenye mipaka yetu hiyo, nakumbuka vizuri kwenye mpaka wetu wa Zambia lakini bado tuna tatizo na Kenya na Uganda. Nashauri kwamba, najua kuna kazi nzuri inafanywa tusiishie tu kwenye maneno, twende kwenye vitendo zaidi, ni vizuri tukaainisha mipaka yetu inaishia hapa. Tukiacha wenzetu wanaweza kwa sababu huwezi kujua anaweza akaja Rais mwenye mfano huo unaofanana na wengine huko, akasema hili ni eneo la kwangu akalazimisha, kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri hili alitazame vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni huduma za upangaji Miji. Tuna utaratibu wa kujisahau tunaacha miji inajengwa, inakua bila kupimwa na baadaye ndiyo tunakwenda kupima, kinachofanyika ni kwenda kuweka "X" kwenye nyumba za wananchi, kitendo hiki sio kizuri sana. Kwa nini sasa kusiwe na uratibu mzuri wa kupima na kuweka mipango miji ikakaa vizuri iliyopimwa ili kusudi watu waweze kukaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Malya, Sumve, Kabila, Nyambiti, Nhungumalwa, Mvomero, maeneo haya Mheshimiwa Waziri ni maeneo yanayokua. Mheshimiwa Naibu Waziri wewe anafahamu pale Sumve ni Mji unaokua, sasa tusipoupima leo na tukisema tutegemee Halmashauri,

Halmashauri hazina kitu, nafikiri zote ukiachia labda zile za mjini, lakini ukisema Magu iende ikapime yenyewe, Kwimba, Mvomero hatuwezi kutimiza yale ambayo Mheshimiwa Waziri ameamdika humu. Kwa hiyo, nimwombe sana kwenye maeneo mengine kule kama Halmashauri zenye uwezo zikafanye lakini Halmashauri ambazo hazina uwezo kwa kweli nimwombe sana Mheshimiwa Waziri ziweze kusaidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nipongeze utendaji kazi mzuri wa Shirika letu la Nyumba *National Housing*, niwaombe sana kwa sababu wanafanya kazi nzuri na mimi kama Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili kwa kweli kazi yao ni nzuri sana, tuwatie moyo, kazi wanayofanya ni nzuri sana, bahati nzuri na mimi niliishawahi kuwa Mjumbe wa Bodi wa Shirika la Nyumba kazi tuliyoiacha sisi ndiyo wanayoiendeleza, naomba moto tuliouacha basi mwendeleze lakini niwatakie kila la kheri katika shughuli zenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri upande wa mipaka ya Tanzania nimelisema hili nalirudia tena, tunaweza tukalionga kama ni jambo dogo, lakini mbele ya safari lina athari kubwa tukiliacha. Nasema tena tukiacha tukasema kwamba kwa sababu majirani zetu ni wazuri mno wanaweza wakafika mahali wakatugeuka. Nimshauri sana Mheshimiwa Waziri hili kwa sababu ameshalianza, naomba waendeleo nalo, nawatakia kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ndassa. Sasa namkaribisha Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Awali ya yote nitumie nafasi hii kumpongeza Waziri na timu yake kwa kazi nzuri ambayo amefanya Jimboni kwangu, anajua mimi siyo mtu wa kusifia sifia lakini pale ambapo mtu anakuwa anaonesha kitu cha maana lazima tumpe *credit* zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyozungumza eneo la Chasimba ambalo lilizungumzwa sana Bunge hili, sasa hivi wananchi wameshapimiwa, Wataalam wa Wizara walikaa pale siku 30 wameweka kambi, hawakulipwa posho, walikuwa wanapika kama vile wako shuleni. Kwa hiyo kwa kweli nashukuru sana na wananchi wa Chasimba, Mtaa wa Basihaya wana-*appreciate* kazi nzuri mliyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sifa hizo ambazo nimezitoa Jimbo la Kawe bado lina changamoto nyingi sana, kuna migogoro ya ardhi mingi bado na Mheshimiwa Waziri nimpongeze kwa sababu hotuba yake ime-*reflect* maoni ya Waziri Kivuli wa miaka mitano iliyopita. Naona anachokifanya hapa ndicho kile ambacho tulikuwa tunamshauri afanye na ndiyo maana anapewa *credit* kwa sababu alijua kwamba Tanzania inajengwa na watu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namwomba katika muktadha huo huo wa kuchukua mawazo yetu kwenye masuala ya kuchukulia hatua watu ambao wanamiliki maeneo makubwa ya ardhi na hawayaendelezi asiwe na *double standard*. Kama kuna kada wa CCM haendelezi achukue, kama kuna kada wa CUF haendelezi achukue, kama kuna kada wa CHADEMA haendelezi achukue. Asipofanya hivyo na sisi tutakuja hapa tutamsulubu kwa ubaguzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi yalizungumzwa masuala ya migogoro ya wakulima na wafugaji, tunategemea Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hapa, atatueleza kwa sababu Wizara yake ndiyo Mama, hizi Wizara nyingine zinategemea yeye katika kuonesha mwelekeo. Kwa hiyo, tunatarajia majibu yake yeye yatatoa mwelekeo wa Taifa kwa kushirikiana na Wizara zingine, ili tujue tunaendaje kutatua migogoro hii kwa kuhakikisha tunaweka ama tunapanga matumizi bora ya ardhi. Kwa hiyo, nategemea atakuja na hayo majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanja 20,000 ama mradi wa viwanja 20,000. Nasisitiza kama ambavyo nilisisitiza miaka

kadhaa iliyopita, tunaomba ifanyike *audit* ya vile viwanja, kwa sababu tunajua sekta ya ardhi ilikuwa imegeuzwa sehemu ya wajanja wachache kujinufaisha kwa maslahi yao. Tukiweza kufanya *audit* katika hivi viwanja, tutajua nani anamiliki nini, tutajua viwanja vya wazi ni vipi na tutajua viwanja vya huduma za jamii ni vipi. Kuanzia hapo tutaweza kujua Serikali iliweza kufanikisha ama ilishindwa na turekebishe nini. Kwa hiyo, naomba sana atueleze kama hiyo *audit* itaanza kufanyika na ifanyike lini, atagundua madudu mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulizungumza suala la migogoro ya Jimboni kwangu, eneo la Nyakasangwe, Kata ya Wazo. Huu mgogoro ni wa muda mrefu, utatuzi wa huu mgogoro ulishaanza kufanyiwa kazi toka mwaka 1998 na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mheshimiwa Makamba. Kuna nyaraka zote tumezipeleka Wizarani kwake na barua ya mwisho tumepeleka tarehe 20 Januari, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro huu unahusu wananchi wasiopungua 4,000, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, tulimaliza hatua mbalimbali za kisiasa na za kitaalam, tukafikia hatua ya kuanza kutambua wananchi kwa kushirikiana na MKurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni, kwa sababu tunajua yeye ndiyo mamlaka yenye uwezo wa kushughulika na masuala ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunataka kufikia mwisho, hawa Viongozi vijana mnaowateua teua hawa wanaopenda kuuza sura, Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, akaja akataka kuvuruga mambo wakati Ofisi ya Mkurugenzi na Viongozi waliopita wote wa Mkoa na Wilaya tulikuwa tumeanza kufika sehemu ya mwisho. Sasa yule dogo sishughuliki naye kwa sababu siyo saizi yangu, mimi nakwenda kwa Mheshimiwa Waziri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mimi na Mkurugenzi tumeshafika sehemu nzuri na wananchi, tumekaribia kumaliza tulete Wizarani, dogo anataka

kuingilia, sasa tumemwandikia barua tarehe 20 Januari, 2017 tumeambatanisha nyaraka zote, tunaomba Ofisi yake ilitafutie ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunataka kulimaliza, juzi amekuja mtu ama Mtaalam Mshauri anazunguka eneo la Nyakasangwe, Kampuni ya Nari, anasema yeye ametumwa na Kiwanda cha Wazo na kwamba Kiwanda cha Wazo kilipewa mamlaka ya kufanya utafiti ama leseni ya kufanya utafiti na kwamba lile eneo inasemekana lina madini, kwa hiyo wameanza kufanya *survey* na kuweka alama na kuzua taharuki kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili suala nimeshakabidhi Wizara ya Nishati na Madini. Kwa hiyo, wakati Mheshimiwa Waziri ananipa majibu yake kama Waziri wa Ardhi natarajia vilevile Waziri wa Nishati na Madini anayekaimu ambaye ni Naibu sasa, atatoa majibu ili wananchi wangu waache kuishi kwa taharuki, hilo la Nyakasangwe nimemaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Boko kwa Somji, nimesema leo naenda Kijimbo jimbo zaidi kwa sababu wananchi wa Kawe ndiyo wananiweka mjini. Suala la eneo la Boko na lenyewe liko Wizarani kwake ni mgogoro wa muda mrefu sitataka kuongea kwa kina hapa, lakini tokea mchakato wa upatikanaji wa hili eneo, toka kipindi kile cha sheria za Mkoloni, taratibu hazikufuatwa. Nitampelekea Mheshimiwa Waziri kabrasha ili aweze kulifanyia kazi kwa sababu kuna matapeli pale wanazunguka, wanasema ooh, tunataka tulipwe fidia, sisi ni wamiliki halali wakati mmiliki halali alishakufa, wakati Serikali iliishataifisha eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namwamini Mheshimiwa Waziri katika kufanya maamuzi wala sina shaka katika hilo na ardhi ni mali ya umma, tusiruhusu wajanja wachache ambao walitumia ombwe lililokuwepo, wakati watu wengine wanaongoza Wizara ya Ardhi kuweza kuvuruga mustakabali wa wananchi. Kwa hiyo, naomba

suala la Boko kwa Somji tulimalize ili basi kama ambavyo tulivyopima Chasimba, tupime Nyakasangwe, tupime Boko kwa Somji maisha ya wananchi wangu yaende kuwa mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana tulikuwa tunazungumza kuhusiana na suala la ardhi, umiliki wa ardhi na nafasi ya mwanamke katika umiliki wa ardhi, nimwombe Mheshimiwa Waziri wanawake wanatengeneza asilimia zaidi ya 80 ya *labour force* ya kilimo, tunaomba sheria zinazowakandamiza hawa wanawake, zisipofanyiwa marekebisho Sheria za Kimila, hata kama tuwe na sheria nyingine nzuri kwa kiwango gani hawa wanawake hatutawasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba kwa dhati, kweli Sheria ya Ardhi Namba 4 inasema haki, Sheria Namba 5 inasema haki, lakini sheria zetu zinatambua Sheria za Kimila. Sasa kama haya mambo ambayo yanamilikiwa kimila yasiipokuwa *formalized*, tutakuwa tunafanya biashara kichaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, tuangalie haya mambo kwa kina, tusaidie wanawake ili tuweze kujenga Taifa letu kwa usawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, leo nimekuwa mpole kidogo, nashukuru na nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi anayoifanya. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Halima Mdee. Tunaendelea na Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi jioni hii. Nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunipa afya, kwa sababu ya muda naomba nami kwa uchache sana nichangie Wizara hii muhimu kabisa, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa kazi

nzuri wanayoifanya, katika kuhakikisha Tanzania ambayo tunatamani kuona imepangwa basi angalau wameanza na miji kadhaa ambayo kwa kweli kama tutafanikisha, tunaweza tukafikia hatua nzuri sana, kwa sababu tunafahamu upangaji wa ardhi unaendana na uimarishaji wa uchumi bora kwa maisha ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli uisiofichika kwamba ardhi kubwa ya Tanzania bado haijapangwa sawa sawa na miji mingi tuliyonayo karibu miji yote hata Mji wa Dodoma ambao ulikuwa umeshaanza kupangwa kwa namna fulani, sasa hivi tunakoelekea kama hakutakuwa na usimamizi mzuri, tutegemee Miji aina ya Manzese na hapa Dodoma itakuwepo mingi sana na maeneo mengine mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu tena nirudie kumshukuru Mheshimiwa Waziri, nakumbuka mwaka 2014, moja ya Miji ambayo ilikuwa imetengewa mkakati wa kupanga Mipango Miji Kabambe, Mji wa Mwanza ulikuwa ni moja kati ya miji karibu 14. Fedha nyingi sana ya Serikali imetumika pale katika kuweka mkataba na kampuni moja SULBANA *International* wa zaidi ya dola milioni tano za Kimarekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa sababu kwa mwaka huu peke yake, ndiyo mwaka ambao kazi kubwa sana imefanyika. Hivi tunavyozungumza karibu asilimia 90 ya kazi hii na timu hii kwa kweli ndugu Waziri naomba niipongeze sana timu aliyoikabidhi kazi hii kwa sababu inafanya kazi nzuri sana. Matarajio yangu ni kwamba kazi hii itakapokuwa imekamili kwa sababu Mwanza ndiyo inaonekana kuwa ya kwanza, kwa namna Watendaji na Watumishi hawa walivyojitoa kufanya kazi hii usiku na mchana itakuwa imetuzalishia matunda makubwa zaidi na itapunguza kero nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko shida moja tu Mheshimiwa Waziri lazima tukubaliane kwamba mipango hii kabambe ya uboreshaji wa miji, pamoja na jitihada nyingi



hizi ambazo inafanya kama tutaiacha, kama baada ya kukamilika hatutaona umuhimu wa kuipeleka kwa haraka ili ikamilike, tunakusudia miaka 20 itakuwa imetosha kabisa kuhakikisha kazi hii imekamilika na *projection* zake ziko wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema miaka 20 sasa hivi kwa Mwanza na llemela kwa maana ya Nyamagana na llemela ukitafuta makazi yako zaidi ya laki moja na sitini lakini wataalam wanatuambia miaka 20 ijayo tutakuwa na makaazi zaidi ya 520 wakati nyumba moja peke yake kuna wakaazi wasiopungua watano. Kadri miaka inavyokwenda watakuwa wanashuka kwa sababu tunaamini uchumi utakuwa umekua, elimu itakuwa imekua kubwa sana na kuzaliana kutapungua sana tofauti na sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, wito wangu kwenu ili hili liweze kufanikiwa vizuri ni lazima tuhakikishe, katika miji yote huu ndiyo mji wenye *square metres* za mraba 472 peke yake unaotakiwa kwenda kufanyiwa kazi, siamini kama unaweza kutuchukulia muda mrefu sana kuutengeneza Mji wa Mwanza ukawa ni moja kati ya Miji bora kabisa Tanzania kuliko ilivyo sasa. Tunaita Mji wa pili kwa ukubwa lakini ni kwa maandishi tu kutokana na uchangiaji wa uchumi siyo kwa muonekano wa mji kiuhalisia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo sasa, tunafahamu kwamba kwa nini sasa hivi tunalazimisha na tunasisitiza sana urasimishaji wa makazi. Utakubaliana na mimi kwamba tunahimiza urasimishaji wa makazi kwa sababu muda mrefu tuliacha ujenzi holela ukatokeza sana. Urasimishaji wa makazi tafsiri yake, tunataka tutoke kwenye makazi holela tuje sasa kuyafanya makazi haya yawe rasmi. Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi, pamoja na jitihada zote hizi tunazofanya, namshukuru sana siku chache zilizopita amefanya ziara Mwanza, pale ametema cheche kali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza na Mheshimiwa Waziri tayari *invoice* 19,000 zimeshaandaliwa na

zaidi ya 3,000 zimeshakwenda kwa wananchi na 800 wameshalipa. Inaonekana kulikuwa na uzembe mkubwa. Kwa hiyo, tuendeleo kutoa nafasi, lakini tuendeleo kurudisha fedha hizi ambazo zinatokana na malipo ya ardhi, zitasaidia sana kuhakikisha kazi hizi zinakwenda haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunataka kuimarisha makazi yetu vizuri tunaondoa makazi holela, liko tatizo moja kubwa na tatizo hili ndilo linaloikabili nchi nzima. Katika maeneo ipo michoro ilishaandaliwa miaka 10, 20 au 30 iliyopita lakini hayajawahi kuelekezwa sawasawa na mwananchi hajawahi kupata elimu vizuri kwamba hii michoro ikishapita huruhusiwi kujenga chochote humu ndani. Matokeo yake maeneo yamevamiwa na leo ukitaka kwenda kumwondoa mwananchi ambaye ulimfanyia mchoro miaka 20 iliyopita na hukumpa utaratibu unakwenda kuonekana ni mvamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na urasimishaji makazi haya tunaulizana, ninayo maeneo kwenye Jiji la Mwanza na Jimbo la Nyamagana, ukichukua maeneo ya Mtaa wa Ibanda, Mtaa wa Swila, Mtaa wa Bukaga, Mtaa wa Kasese kwenye Kata za Nyegezi, Kata ya Igoma na Kata ya Mkolani, yako zaidi ya makazi elfu mbili, wapo wananchi wengi, walishajenga siku nyingi, michoro imetengenezwa. Hakuna namna tunaweza kuwasaidia wananchi hawa pamoja na kutaka kupanga Mji wa Mwanza vizuri kama hatutafumbua tatizo hili kubwa. Kinachoonekana leo ili tuweze kufumbua tatizo hili ni kwenda kuvunja makazi ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutaendana na kasi ya Mheshimiwa Rais anayoizungumza, hatutaendana na kauli ya Mheshimiwa Rais ya kuwasaidia wanyonge. Sasa ni lazima tumsaidie Mheshimiwa Rais, ni lazima tuoneshe njia watalaam huku wanasema, kwa mfano miaka karibu 25 iliyopita eneo la Mkolani, Mtaa wa Kasese kuanzia kona ya Nyegezi pale Nyegezi, unakuja Butimba, unakuja Mkolani watu walishapima miaka mingi, Halmashauri wanasema

mchoro wao unaonesha barabara ni mita 100, *TANROADS* wanasema barabara yetu ni mita 60. Nani anaingia katikati hapa kutatua mgogoro huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo watu kwenye mita zaidi ya 40, Halmashauri inasema hii ni *buffer zone* na watu wana miaka dahari mle ndani, leo wanatakiwa wavunjiwe nyumba zao, zaidi ya watu 1,600. Mheshimiwa Waziri najua yeye ni mtu wa huruma na hata akienda kwenye eneo hili mwenyewe anaweza kushangaa na akashangaa watalaam tulionao, kwa nini hawawezi kuchukua maamuzi mpaka wakubwa wafike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, nimeshazungumza na mama yangu, jirani yangu, dada yangu Mheshimiwa Angelina, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, amesema wataliangalia kwa makini na nimeshazungumza na Mheshimiwa Waziri vizuri na najua ameshanisaidia sana. Kwa hiyo, naendelea kuwaomba tunao wajibu wa kuwasaidia Watanzania. Mwanza tunayotaka kuitengeneza leo uwe mji wa mfano hatutaonesha kama ni mji wa mfano kama hatutatatua changamoto hizi, badala yake tutaendelea kujaza kero kwa wananchi na hii itakuwa siyo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia tu nizungumze suala moja ambalo amelizungumza Ndugulile hapa asubuhi. Bado hakuna elimu hata kwa watalaam wetu kule chini, tunazungumza asilimia 30 ya fedha za kodi ya ardhi zinazokusanywa, leo ukitaka kuuliza, hata Watendaji hawajui kama zile fedha hazitakiwi kurudi tena lakini watendaji wenyewe wanajua bado tunadai fedha nyingi. Fedha hizi zikija zitasaidia kumaliza kero ya kupima ardhi kwenye maeneo mengi ambayo tumeshindwa kupima mpaka leo, hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri waliangalie. Kama ilishaamriwa hivyo na Bunge hili likapitisha sheria, uende waraka kule chini kwa Watendaji kwenye

Halmashauri walifahamu hili, kwamba fedha hizi wanazolipa mpaka leo Halmashauri ya Jiji la Mwanza imeshakusanya kodi ya ardhi zaidi ya bilioni moja na milioni mia tisa thelathini na mbili, lakini tunategemea asilimia 30 ya fedha zile iweze kutusaidia kukamilisha shughuli nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana hata zoezi la urasimishaji makazi kuna wakati lilikwama kwa sababu vifaa vilikuwa hakuna. Mheshimiwa Waziri alivyoondoka hatujui fedha zilipatikana wapi, *computer* zikanunuliwa, kila kitu kikawekwa na kazi hii niliyomwambia zaidi ya wananchi 800 wameshafanyiwa malipo, ndiyo matokeo ya matumizi ya fedha. Lazima tukubali kutumia fedha ili tujenge miji yetu na *plan* hizi tulizonazo ziweze kufanikiwa. Hatuwezi kufanikiwa kama hatujaona umuhimu wa ardhi na matumizi ya ardhi haya ni lazima tuyafanye *for public consumption*, tukifanya ni ya kwetu binafsi hatuwezi kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, wananchi wa Jiji la Mwanza na Jimbo la Nyamagana wanayo masikitiko makubwa, yako maeneo yao wamekuwemo kwa muda mrefu lakini leo wanaonekana wavamizi, kwa sababu tu hatukuchukua hatua mapema, hatukutoa elimu mapema. Tutoe elimu, tuwaoneshe wananchi wapi panastahili na wapi pasipostahili, tutafanikiwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya. Tuendeleo kujenga Tanzania na wananchi wanyonge wapate tiba. Ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.  
(*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mabula. Sasa namkaribisha Mheshimiwa Allan Kiula, baadaye Mheshimiwa Martha Umbulla na Mheshimiwa Salma Mwassa wajiandae.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwa mara ya kwanza katika kikao hiki cha Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya, wanasema mwenye macho haambiwi tazama. Yapo mabadiliko makubwa ambayo Waziri aliahidi alivyoingia kwenye Wizara hii kwamba atafanya mabadiliko makubwa katika Wizara yake na tunayaona. Jambo kubwa zaidi ni kwamba wananchi wanachotarajia ni kuona matokeo chanya, kuona mabadiliko na kupata huduma ambazo zinatolewa na Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kwa makini hotuba ya Waziri imeainisha mikakati mbalimbali na mipango mbalimbali ambayo wanakwenda kutekeleza katika mwaka ujao wa fedha tutakapopitisha bajeti hii. Nami kabla sijasonga mbele zaidi niseme kabisa naunga mkono hotuba ya Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hotuba ya Waziri, yapo mambo ambayo lazima tuyazungumze kwa sababu sisi ni Wawakilishi wa Wananchi. Japan wanayo *management system* ya *Gemba Kaizen*. *Gemba Kaizen* maana yake unatakiwa uende kwenye eneo la kazi/tukio. Sasa suala la migogoro Wabunge wote tunasimama hapa kuzungumza migogoro ya mipaka. Hilo ni jambo kubwa sana, tunatarajia kabisa kwamba watendaji wa Wizara wafike kwenye mipaka hiyo na wafike kwa haraka na migogoro iweze kutatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilichangia na mwaka huu nimekuwa nikimsumbua Waziri, hata juzi nilikuwa ofisini kwa Waziri na Naibu Waziri nimefika, kumweleza matatizo tuliyonayo wananchi wa Mkalama. Imekuwa ni adha kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lililopita nilimwonesha Waziri picha ya mwananchi aliyekakwa panga kwa sababu

ya mgogoro wa ardhi. Hii migogoro ya mipaka inatakiwa ipate mwarobaini wake. Nilimweleza Waziri kwamba tuna mgogoro kati ya Iramoto na Hydrom, Eshgesh, Singa 'A' na Singa 'B', Kikonda na Singida Vijijini, Lukomonyeri na Singida Vijijini, Iguguno na Singida Vijijini, Mpambala na Bukundi ambako ni Simiyu. Sasa migogoro ya mipaka haiishii watu kupigana mapanga tu hata shughuli za maendeleo wananchi sasa wamekuwa wanakwepa kuzifanya maana mtu mwingine anasema yuko Mkalama, mara anasema yuko Hydrom, mara anasema yuko Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la mipaka ni muhimu likawekwa wazi na likatatuliwa. Naamini kabisa kwa kasi ya Waziri na Naibu Waziri, jambo hili halitakiwi kuchukua muda na linatakiwa lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ofisi zetu hasa za Wakuu wa Wilaya tumezifanya kama Mahakama vile, kwa sababu kila siku watu wako pale wanazungumzia suala la migogoro ya mipaka kati ya Wilaya na Wilaya na kati ya Mkoa na Mkoa, jambo hili tunaomba lipewe kipaumbele. Pia namshukuru Waziri alishaahidi kwamba atalifanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni upimaji wa Miji na Vijiji. Suala hili na lenyewe ni muhimu sana kwa sababu ziko Halmashauri mpya zimeanzishwa na zilivyoanzishwa kata kadhaa zilitolewa na vijiji vilianzishwa. Hata hivyo, sasa wahusika hawajaenda kuoneshwa mipaka yao. Kwa hiyo, imeanza kuleta migogoro kati ya vijiji na vijiji. Hilo ni tatizo, na lenyewe ni kubwa ambalo linaleta usumbufu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba humu limezungumzwa suala la Hati za Kimila, maeneo mengine ambayo sisi hatujaanza kufika hatua ya juu kwa nini tusipate Hati za Kimila kama wanavyofanya wenzetu wa Kiteto na maeneo mengine, kwa sababu Hati za Kimila inaonekana zinaweza kusaidia kupunguza migogoro hii. Hilo ni jambo muhimu, nawakumbusha tena Wizara, naomba waweze kulisimamia kwa ukaribu kabisa ili tuweze kuishi kwa amani katika Tanzania yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni suala la Baraza la Ardhi. Kwenye hotuba ya Waziri nimeona suala la Baraza la Ardhi na tumeona Halmashauri zingine Mabaraza ya Ardhi yameanzishwa. Hata hivyo, ukiangalia hotuba ya Kamati nanukuu ukurasa wa 18:

*“Kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuanzisha Mabaraza ya Ardhi katika Wilaya zote nchini.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri wenzetu Kamati wameliangalia hili jambo na wameliona kwa uzito wake na sisi kama Wabunge tunalileta hapa kwa uzito wake. Nieleze masikitiko yangu makubwa. Miezi sita iliyopita Wataalam walikuja Mkalama, wakaja pale wakatuambia masharti yao, wakasema tuwaoneshe jengo, wakaoneshwa jengo wakalikubali lile jengo, lakini toka walivyoondoka hakuna *feedback*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kunapokuwa hakuna *feedback* ndipo uhasama unaanza kati ya wananchi na Wizara pasipo sababu yoyote ile. Kama Rais anatumbua watu, kuna tatizo gani kutumbua hao watu waliokuja miezi sita halafu hawajarudisha *feedback*? Nafikiri Waziri atachukua hatua na nafikiri wakati wa kuhitimisha atanipa majibu ya kuniridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachukulia hiyo kwamba ni dharau, tumedharaulika. Kama mtu anakuja unampa jengo halafu hafanyi kitu chochote ina maana ametudharau na sisi hatuwezi kudharauliwa kwa sababu mimi ni Mbunge wa Jimbo, nawakilisha wananchi wa Mkalama hapa. Kwa hiyo, nasi tuna haki kama ambavyo majimbo mengine yana haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, sisi ni Watanzania. Wananchi wangu wanapata huduma Baraza la Ardhi Kiomboi ambako ni mbali, kwanza kwenda kule lazima ulipe nauli na ukifika kule labda kesi inaahirishwa au unalala kule. Pia humu ndani kuna akinamama wengi, akinamama wengi wamedhulumiwa ardhi, wajane wamedhulumiwa ardhi,

hawapati haki yao. Sasa jambo hilo ni muhimu lazima liangaliwe, kama Baraza linaweza kuanzishwa, kwa nini lisianzishwe watu wapate huduma mahali ambapo ni karibu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne, nimpongeze Waziri kwa kualika taasisi zake mbalimbali. Tumeona hapa ndani kuna Watumishi *Housing, National Housing* na mimi nilipata bahati ya kutembelea Watumishi *Housing* na niliweza kutembelea *National Housing*, wanafanya kazi kubwa sana. Kwa sababu na wenyewe wako hapa, Wilaya mpya zinazoanzishwa tayari kuna *potential* ya uwekezaji wa nyumba za wafanyakazi. Kwa hiyo, Wilaya mpya kama Mkalama inahitaji uwekezaji wa namna hiyo iwe *National Housing* au Watumishi *Housing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Mkalama Mjini chumba peke yake choo kwenda nje shilingi 50,000. Sasa kama ni shilingi 50,000 hiyo ni *potential market*, lakini watumishi wanakaa kwenye *substandard house* na mtumishi haendi mahali kwa sababu ya mshahara peke yake, mtumishi anakwenda kuangalia na mazingira ya kazi. Kwa hiyo, tunatumaini hizi taasisi zinaweza kutusaidia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa watumishi wa Serikali. Mfuko huo ulianzishwa na Sheria ya mwaka 1992. Tunajua umefanya kazi kubwa, ukisoma kwenye bajeti ya Waziri tunauona kama ule Mfuko uko *under funded, funding* zinazokwenda pale hazitoshi. Tunaomba *fund* hizo ziweze kuongezwa ili watumishi wengi waweze kupata mikopo na waweze kujenga nyumba pia tuangalie marejesho waliokwishapata urejeshaji wake uko vipi? Ningependa kufahamu Mfuko huu tangu uanzishwe ni watumishi wangapi wamekwishapata hiyo mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine namba sita ni kuhodhi ardhi. Kama alivyosema Waziri hilo jambo ni la kusema hapana, watu wengi wamehodhi ardhi, wananchi wanaongezeka na mtu mwingine anakuwa na ardhi kubwa, kazi yake haitumiii yeye anakodisha watu kulima tu na hiyo



iko sana kule Kidarafa, iko sana Mwanga, sasa huo ni unyonyaji, ardhi ya kwetu wewe kazi yako ni kukodisha watu. Nafikiri ni muda muafaka sasa Wizara kuchukua hatua na kuwachukulia hatua wale watu kwa kuwanyang'anya ardhi hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la saba ni ardhi *versus* ongezeko la wananchi. Wizara hii ni Wizara nyeti, Taifa zima linategemea Wizara hii. Nafikiri Wizara inatakiwa ije na *strategic plan* ya kuonesha ukubwa wa ardhi na ongezeko la watu *plus economic activities*, mifugo, kilimo, madini, hilo ni jambo muhimu sana. Hata migogoro ambayo ilikuwa inazungumzwa jana kwenye Wizara ya Utalii yote hii inagusa rasilimali ardhi, watu hatujapangwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni jukumu la Wizara hii kuweza kutupanga vizuri na uamuzi unatakiwa utolewe sasa hivi kwa sababu tunapochelewa kutoa uamuzi tunatengeneza bomu ambalo baada ya miaka mingi hatuwezi kulihimili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja nafikiri ujumbe utakuwa umefika mahali pake. Tuna imani na Wizara hii na tuna imani na Mheshimiwa Waziri na Naibu wake. Tunatumaini kwamba Tanzania itakuwa Tanzania mpya na watafanya kazi kubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Allan Kiula. Tunaendelea na Mheshimiwa Martha Umbulla, baadaye Mheshimiwa Salma Mwassa ajiandae.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa fursa hii niweze kuchangia hoja iiyopo mbele yetu. Nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa ofisi yake kwa kazi nzuri wanayoifanya nchi yetu. Kipekee

Mheshimiwa Waziri amekuja Mkoani kwetu Manyara, ametusaidia migogoro mingi na kwa kweli Mungu aendelee kumwongoza na kumpa afya njema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite kwenye sekta ya ardhi, rasilimali ardhi hakuna asiyejua umuhimu wake na uhitaji wake sasa hivi katika nchi yetu. Uhitaji wa ardhi miaka 30 iliyopita na leo, mwaka huu tuliopo na miaka 30 ijayo ni tofauti kabisa kuashiria kwamba nchi yetu inanyemelewa na ufinyu wa ardhi. Hili ni jambo la hatari kama hatutaweka mipango madhubuti katika kuiweka ardhi yetu iweze kutusaidia katika mipango yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana jioni tulikuwa na mjadala mzito baina ya Wabunge wanaotetea wakulima na wengine wanaolaumu wafugaji, lakini hakuna mshindi hata wangetumia lugha namna gani kusema kwamba wafugaji ni wabaya, wakulima ni wabaya wanafanya hivi na vile kwa sababu wakulima ni Watanzania wale wale na wataishia kuwa Watanzania na wataendelea kulima na wafugaji hali kadhalika ni Watanzania wataendelea kufuga na wataendelea kuwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la maana ni kuhakikisha kwamba tunabuni mipango madhubuti ili kuhakikisha kwamba jamii zote mbili hizi na hata watumiaji wengine wa ardhi wanaishi vizuri katika nchi yao bila kuwa na migogoro ya hapa na pale na bila ya kuwa na migogoro ya kuvamia ardhi na kusababisha maafa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa ninaloona ni kubadilisha *mindset*, ni lazima tubadilishe *mindset* yetu. Huwa natumia mfano wa mkoa mdogo wa Kilimanjaro kulinganisha na Mkoa wetu wa Manyara, ukiangalia Mkoa wa Kilimanjaro mnisamehe wananchi wa Kilimanjaro na Wabunge wa huko. Mkoa wa Kilimanjaro una eneo dogo sana lakini una watu wengi, Mkoa wa Manyara una eneo kubwa sana watu ni wachache, lakini utakuta katika eneo dogo hilo hakuna migogoro inayolingana na migogoro iliyoko Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini inakuwa hivyo? Ni kwa sababu wananchi wa Kilimanjaro toka mwanzo waliona kwamba ardhi yao ni finyu kwa hiyo lazima waweke mikakati madhubuti, wameweka *mindset* yao kwamba ni lazima ardhi yao finyu wanaitumia kwa busara ili iweze kukidhi mahitaji ya wananchi wao. Kwa hivyo eneo kubwa linaleta udanganyifu kwamba bado ardhi yetu ni kubwa kwa hiyo tunaweza tukavamia hapa tukaitumia kwa ajili ya matumizi ya mashamba au kufuga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni lazima tubuni kama nilivyoeleza, kwamba ardhi inanyemelewa na ufinyu wa ardhi na ongezeko kubwa la watu, kwa hivyo lazima kuwe na ubunifu. Jana nilikuwa nasoma mipango ya miaka mitano yaani 2015/2016 na 2016/2017. Tuna mipango mizuri sana, tuna mipango madhubuti kuhusu sekta ya ardhi, lakini cha kushangaza bado hatuwezi kutamba leo kusema mipango tuliojiwekea imeweza kuleta *impact* hii hasa katika sekta ya ardhi, hivyo bado tuna safari ndefu kuhakikisha mipango yetu tunayopanga lazima iwe *real*, iende sambamba na hali halisi, kama kuna ongezeko kubwa la watu ni lazima ardhi yetu iende sambamba na ongezeko kubwa la watu na kuhakikisha kwamba inatumika madhubuti na inatutosha kwa matumizi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tujizatiti na matumizi bora ya ardhi. Naishauri Serikali kwamba *to pull resources* zote sasa hivi kwa sababu kilio hiki ni kikubwa. Tangu niingie Bungeni hapa kilio cha wakulima na wafugaji kiko pale pale, sijaona tofauti, kilio kinazidi kila siku na kwa kilio hicho, tukiangalie sasa mipango yetu iweze kutupa ahueni. Tuhakikishe *resources* tulizonazo tuweze kuweka mipango bora ya matumizi ya ardhi yetu ili tuondoe kilio cha wakulima wetu na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali pia kutoa elimu hasa kwa jamii ya wafugaji. Jamii yetu ya wafugaji bado hawajawa na upeo wa uelewa katika matumizi ya ardhi. Sheria ni jambo ambalo lazima tujizatiti nalo liweze kusaidia katika kuhakikisha ardhi yetu tunaiwekea mikakati

madhubuti ili liweze kwenda kusaidia wananchi wake na hatimaye tuweze kuwa na maisha bora na *harmony* baina ya jamii zetu za watumiaji wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna migogoro ya wakulima na wafugaji lakini na watumiaji wengine wa ardhi kama wawindaji, warina asali, waokota matunda, nao itafika mahali watahitaji ardhi ya kuitumia. Tumeweka mipango madhubuti ya kupanua kilimo chetu bila kuzingatia kwamba kilimo hicho hicho kinahitaji ardhi madhubuti ambayo tutakwenda kuitumia kupanua kilimo ili tuweze kupata malighafi kwa ajili ya viwanda vyetu na kadhalika ili tuweze kuinua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la sheria ni suala muhimu sana katika kudhibiti matumizi bora ya ardhi, naomba kutoa mfano wa Wilaya ya Kiteto katika Mkoa wa Manyara. Wilaya ya Kiteto ilivamiwa na wakulima toka nje ya Wilaya na hii ni kwa sababu ilionekana kwamba Wilaya ile ilikuwa na ardhi *prime*, haina mwenyewe sana, kwa hiyo walikuja wakulima kutoka nje wakapasua pori wakalima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimu mmoja ambaye amekuja kama kibarua, msimu unaofuata hawi tena kibarua anafyeka pori anakuwa yeye ndiye mmiliki wa shamba. Kwa hiyo, anafika mahali anawaita watu wengine 200 zaidi, analima msimu mmoja kama kibarua msimu unaofuata anawaleta 200, kwa hiyo ni 200 x 200x 200 ardhi inakuwa imekwisha kulimwa kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleze kwamba, sheria huwa inafanya kazi kwa sababu wavamizi wote waliovamia mbuga mbalimbali katika Wilaya yetu tuliweza kuwaondoa kwa kutumia sheria. Kwa hiyo, sheria inafanya kazi kuhakikisha kwamba tunadhibiti matumizi bora ya ardhi kama ambavyo tumefanya kule Kiteto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri, bado Kiteto kuna matatizo kadhaa. Kwa bahati

mbaya Tume mbalimbali ambazo zimeundwa ili zituletee majawabu tuweze kufanyia kazi, bado hatujapata majawabu yake, naomba basi tuweze kupata maelekezo ili wananchi nao wapate utulivu katika Wilaya yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano, kwa nini naipongeza hasa Mawaziri wake? Wakati nikiwa Kiteto kama kiongozi miaka yangu mitatu ambayo nimekuwa nikipambana kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji, hakuna ambaye hajasikia Kiteto kulikuwa na mauaji ya wakulima na wafugaji lakini bahati mbaya wala simteti mtu, hakuna Waziri aliyekanyaga kusaidia kutatua migogoro ile ama kuona ni namna gani tunaisaidia Serikali kuhakikisha kwamba migogoro inakwisha na watu wanaacha kupigana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Serikali ya Awamu ya Tano imejitahidi. Hapa Mvomero wamekatwakatwa ng'ombe usiku, asubuhi Mheshimiwa Mwigulu yupo pale, alipokuwa Waziri wa Kilimo na Mifugo, nampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia migogoro ya ardhi, Awamu hii Mheshimiwa Lukuvi ametembelea pale mara nyingi, sikumwona Waziri wa Ardhi wala wa Kilimo na Mifugo wakati ule kwa miaka yote mitatu na ndiyo maana naipongeza Serikali ya Awamu ya Tano wakiongozwa na Jemedari wao Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli katika kutatua migogoro ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti nimeona nichangie haya machache katika sekta ya ardhi, naunga mkono hoja na ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Martha Umbulla. Tunaendelea na Mheshimiwa Salma Mwasa na baadaye Mheshimiwa Shangazi na Mheshimiwa Shaabani Shekilindi wajiandae.

**MHE. SALMA M. MWASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niseme ardhi toka dunia iumbwe haiongezeki, lakini watu wanaongezeka, shughuli za binadamu zinaongezeka, kwa hiyo angalia adha wanayoipata wafanyakazi wa ardhi au wasimamizi wa ardhi kwamba unapewa usimamie jukumu ambalo *demand* yake ipo juu lakini ongezeko lake hallongezeki, kwa hiyo wanapata tabu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme kabisa tusiwaangalie wafanyakazi wa sekta ya ardhi kwa *negative way* kama tunavyowaangalia sasa hivi, kwamba wanaonekana ni majambazi, ni wanyang'anyi na kila kitu siyo kweli, tuwaangalie kwa mtazamo ambao wanafanya kazi kwa juhudi kabisa na ndiyo maana wanamwezesha Mheshimiwa Waziri ku-*perform* katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri amefanya mambo mazuri kabisa lakini kwa kusaidiwa na timu ambayo ni kali, anayo timu nzuri sana. Kwanza kabisa tukianza na Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Moses Mpogole, huyo ni Mwalimu wangu sina tatizo na utalaam wake, yupo vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile analo gwiji wa Uthamini, Dada yangu Ndugu Evelyn Mgasha yupo vizuri. Pia anaye Kamishna ambaye ni makini Mary Makondo Mheshimiwa Waziri ana timu nzuri akianzisha kipenga mpira anaupiga huku hadi huku, hakuna mgogoro wowote. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri arasimisha, apime na kupanga amalize mgogoro hakuna kitu kingine hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la maslahi duni ya Wafanyakazi wa Umma. Wafanyakazi wa Umma kwa kweli wana maslahi ambayo hayaeleweki, hawapandishwi madaraja, maslahi yao duni, kwanza kabisa ukiangalia hasa hawa wafanyakazi wa ardhi mnawasakama hapa bure,

wafanyakazi hawa wana mazingira magumu sana. Ukiangalia vitendea kazi hawana, unakuta Idara nzima ina gari moja, huyo Afisa Ardhi ataendaje kukagua kiwanja ili aweze kuthibitisha kwamba hiki kiwanja mchoro huu ni sahihi au la!

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hawana hata kompyuta wala nini ya kuweza kusema kwamba hii itawasaidia wao katika kazi zao. Kwa hiyo mazingira yao ni duni, hakuna mbadala, mishahara yao ni midogo. Ukiangalia sekta ya ardhi, hivi mtu unampa akutunzie bilioni moja, kitu cha thamani halafu unamwambia mshahara wake laki mbili, laki tatu, huyu mtu si unamtia kwenye majaribu. Kwa hiyo, hapa ndiyo maana mnawaangalia kwenye mazingira ambayo ni wanyang'anyi, siyo kweli. Waandalieni mazingira wafanye kazi, watumishi wa ardhi wana mazingira mabovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye uhaba wa fedha, Wizara hii pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri amejipamba hapa, anayo hela sijui nini, lakini nikisoma kwamba bajeti ya 2016/2017 aliidhinishiwa bilioni 61 lakini zilizomfikia mpaka Januari ni bilioni 28 tu. Sasa nashindwa kuelewa kwamba je, wamtengee fedha kwa sababu anakusanya sana kwenye kodi, kwenye nini, makusanyo yake siyo mabaya, lakini mbona haletewi hela kwa wakati, yaani hana hela hapa zinazoeleweka. Shilingi bilioni 28 kati ya 61 anafanyaje kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingi ya maendeleo kutegemea fedha za nje, kwanza twende kwenye ule mradi wa *Land Tenure Support Program* uliopo kwenye Wilaya za Malinyi na Ulanga. Mradi ule umetengewa bilioni tatu hela za ndani, bilioni 10 hela za nje, mpaka tunaenda kukagua ule mradi tunakuta kabisa hela za ndani kati ya bilioni tatu zimepelekwa milioni 400 tu na fedha za nje kati ya bilioni 10 zimepelekwa bilioni 3.4, sasa kama kweli urasimishaji ni tatizo la kuondoa migogoro, kama hiyo miradi haipelekewi fedha kwa wakati na uhaba wa fedha unaoikumba, tunamalizaje hiyo migogoro? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kwenye Mabaraza ya Ardhi. Mabaraza ya Ardhi haya sheria yake imepitwa na wakati, tunaomba Mheshimiwa Waziri alete hapa sheria tena kwa sababu mabaraza haya yanasema kwamba yasiongelee mali ambayo inapita milioni hamsini, kwa Mabaraza ya Wilaya lakini Mabaraza ya Kata wanasema yasiongelee kitu chenye thamani inayozidi milioni tatu, sasa eneo kama la Dar es Salaam, nyumba ya milioni 50 unaipata wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, hali hii inasababisha mlundikano mkubwa kwenye Mahakama hizi za Ardhi, Mahakama Kuu tu, haya Mabaraza yamekuwa kama mapambo kwa sasa, hii sheria yake imepitwa na wakati, tunaomba Mheshimiwa Waziri ailete hapa Bungeni tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niongelee kwenye miradi ya ujasiriamali; kuondoa hii migogoro ya ardhi Mheshimiwa Waziri lazima apime na kupanga ardhi. Kwa ufinyu wa bajeti kama ninavyouona hapa ina maana kupima kama kupima Mheshimiwa Waziri hataweza gharama ni kubwa, kurasimisha pia itakuwa ni jibu lake sahihi. Kwa hiyo, kama ndiyo hivyo basi, huu urasimishaji kwenye hii miradi iliyoanza usiende kwa kusuasua kama ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ameutaja hapa mradi wa Kimara, lakini mradi ule unaenda kwa kusuasua sana. Mimi mwenyewe natembelea pale mara kadhaa, mradi ule watu wale hawana magari ya kwenda *site*, hawana mafuta, hawana *beacons*, wale wafanyakazi hawajalipwa, wengine hata vibarua wameshasusa kwenda hata *site*. Mheshimiwa Waziri ananiambia kwamba mradi huu unaendelea vizuri, naomba tu autembelee au kama vipi tuongozane twende tukautembelee, kwa sababu naona anaupamba bure wakati mradi huu umekwama, naomba twende tukatembelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niongelee, Tume ya umiliki wa ardhi, ile Tume ya kupanga ardhi. Tume ya



Matumizi Bora ya Ardhi ni Tume ambayo nayo inatakiwa iwekwe kipaumbele lakini mpaka sasa toka mwaka jana Tume hii inapangiwa pesa ndogo sana, sielewi kama hawaitaki, kama hawaitaki basi waifute tuelewe. Sasa mbona wanaipangia bilioni mbili, bilioni mbili watafanya nini hawa? Kama hii Tume ingeshirikiana na Wizara hii vizuri, ungekuwa ni mwarobaini wa hili tatizo, migogoro yote ingekwisha na tungeelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee pia mambo ya kodi ya ardhi, kodi ya ardhi inavyoonekana kwenye Wizara hii ndiyo uti wa mgongo wa maduhuli yote, lakini hiyo kodi ya ardhi inapatikana wapi kama eneo halijapimwa na kupangwa? Naomba kabisa Mheshimiwa Waziri urasimishaji huo apange hela nyingi apeleke huko ili aweze kupata kodi ya ardhi, asing'ang'anie kutoza kwenye maeneo yasiyopimwa, anakiuka Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 Na. (5) na (4), huwezi kutoza kodi kwenye maeneo ambayo hayajapimwa, atakuwa anatoza kwa kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atueleze kabisa akihitimisha kwamba anavyotuambia kwamba anatoza kodi kwenye maeneo yasiyopimwa kivipi? Wale watu hawana nyaraka kwanza anajuaje, kwa sababu kodi ya ardhi ni Mthamini anathamini lile eneo, akishathamini ndiyo anakwambia kwamba hili eneo kulingana na *location* yake basi inatakiwa itozwe kodi kiasi fulani. Sasa hapo ananiambia kwamba anatoza kodi kwenye maeneo ambayo hayajapimwa kwa vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri asikwepe jukumu lake, apime, apange, arasimishe akiona vipi mambo yamemwendea vibaya aombe hela hata huko nje, kama hivi anavyotegemea hela za nje halafu yeye mwenyewe za ndani amebana, sasa sijui itakuwaje!  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niongelee mambo ya uthamini, kuna Mbunge mmoja hapa alikuwa anasema

kabisa mambo ya uthamini, ooh, *Valuers* ni wadanganyifu, sijui kwenye mali ya bilioni moja anasema milioni mbili. Hao siyo Wathamini waliosoma Chuo cha Ardhi, hao watakuwa ni *Valuers* wa mtaani anawajua yeye huyo Mbunge, *Valuers* makanjanja na *Valuers* ambao wamesoma Chuo cha Ardhi hawawezi kuongea udanganyifu, wao wanatumia *opinion* yao wanatumia kanuni, sheria na taratibu walizofundishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Valuers* ni watu waliosoma muda mrefu, hawawezi kufanya *cheating* za hovyoye, yeye aangalie vizuri huyo aliyethamini mali ya bilioni moja kuja kuirudisha milioni mbili, amuulize vizuri alitoka wapi, inawezekana hao ndiyo vishoka kwenye hiyo taaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siamini kabisa kwamba *Valuers* aliyefundishwa na Walimu makini na Walimu wenyewe mnawaona walivyo makini mpaka wameenda kumteua Naibu Katibu Mkuu kule na wameona umakini wake anaouonesha leo aende akamfundishe *Valuer* anaye-*cheat* haiwezekani! Huyo siyo *Valuer* aliyefundishwa Chuo cha Ardhi ni kanjanja sijui alipotoka ni wapi mpaka akakutana naye. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa niendeleo kusema ukosefu wa wataalam au upungufu wa wafanyakazi kwenye hii Wizara ya Ardhi au kwenye sekta ya ardhi. Kwa kweli mpaka sasa kuna upungufu mkubwa wa wafanyakazi kwenye sekta ya ardhi, zaidi ya asilimia 70 kuna upungufu, wafanyakazi waliopo ni wachache sana, sasa hivi unakuta Afisa Ardhi mmoja anafanya kazi za Maafisa Ardhi 10 mpaka 20, mtu mmoja, halafu bado mnamsonga na maneno, bado sijui mwizi, siju nini, bado mshahara wake mdogo, hana *over time*, naomba mtoe kibali cha kuajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Salma. Tunaendelea na Mheshimiwa Shangazi na Mheshimiwa Shaabani Shekilindi dakika tano tano na baadaye Mheshimiwa Abdallah Chikota na Mheshimiwa Anna Lupembe wajiandae.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami naomba nitumie fursa hii kumpongeza Waziri mwenye dhamana pamoja na Naibu wake, wanafanya kazi nzuri sana, kazi ambayo haiwezi ikatiliwa shaka na Mbunge yeyote makini humu ndani.

Vilevile naomba nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara ndugu yangu Kayandabila nae anafanya kazi nzuri sana, tumeona jinsi tatizo la ardhi katika nchi yetu linavyozidi kutatuliwa siku hata siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo kuna tatizo kidogo katika eneo langu la Halmashauri ya Lushoto, kuna Mwekezaji mmoja wa nchi jirani ya Kenya amemilikishwa mashamba matatu lakini ameshindwa kuyaendeleza.

Sasa katika Halmashauri yetu tuna uhaba mkubwa sana wa ardhi na ardhi hii hekari 4,019 zimekaa tu *domant*. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, kwamba huyu Mwekezaji anapita na anatoa lugha za kashfa mitaani kiasi kwamba anajifananisha kwamba yeye mmoja ni sawa na Watanzania watano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa tafsiri rahisi ya yeye mmoja na Watanzania watano ni kwamba hapo kuna Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Waziri mwenye dhamana na Mbunge. Kwa hiyo, sisi watano ni yeye mmoja. Sasa naomba nimwachie hilo Mheshimiwa Waziri aangalie namna gani tunafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shamba la kwanza lina hati namba 41/44, hekari 562; shamba la pili ni hati namba 17/146, hekari 1188; shamba la tatu ni namba 11/247, hekari 2,442; na tumeshatoa *notice* ya *revocation* kuanzia tarehe 14 Julai, 2016 na hakujibu na tarehe 9 Desemba, *file* limeshafika kwa Kamishna wa Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Kamishna wa Ardhi Kanda ya Kaskazini kwa masikitiko makubwa yule mama ambaye alikuwa pale kabla hajahamishwa amekalia *file* na kila tukiuliza analeta sababu ambazo siyo za kiofisi. Jambo lolote la kiofisi linapaswa kujibiwa kwa nyaraka za kiofisi, lakini mama huyu kila wakati ukiuliza anatoa majibu kwamba *file* halijakamilika, sijui *notice* zimekosewa. Sasa haya ni mambo ya *technical* ambayo wananchi hawapendi kuyasikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kwenye barua yetu Afisa Mteule wa Ardhi ameandika wazi kwenye hitimisho, mwekezaji katika mashamba ya katani Mnazi ameshindwa kwa kiasi kikubwa kuyaendeleza mashamba anayoyamiliki. Katika hekari 4,192 ni hekari 500 tu ndizo ambazo ameziendeleza kwa kupanda mkonge na kuvuna, hekari 1,942 mkonge uko porini kwenye vichaka hautunzwi kabisa. Hekari 1023 ni msitu mtupu ambao unatumiwa na wafugaji wa kijamii ya kimasai kwa malisho ya mifugo yao. Pia mmiliki huyu hajalipa kodi ya ardhi tangu 2004/2005 mpaka sasa na anadaiwa zaidi ya shilingi milioni 42.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wawekezaji kama hawa kwa kweli sidhani kama wana nafasi katika Serikali hii ya Awamu ya Tano. Namsihi sana Mheshimiwa Waziri tuchukue hatua stahiki. Wananchi hawa wa Lushoto kama nilivyotangulia kusema wana uhaba mkubwa wa adhi. Kwa hiyo ardhi hii ndio angalau tukipata na sisi tunaweza tukaingia na wenzetu hawa kuingia katika *economic zone* tukapata angalau mahali pa kuwekeza. Kwa hiyo, namsihi sana, namwamini Mheshimiwa Waziri, sijawahi kutilia shaka uwezo pamoja na mama yangu pale Angelina Mabula nawapongeza sana, ahsanteni sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shangazi. Tunaendelea na Mheshimiwa Shaban Shekilindi na Mheshimiwa Ana Lupembe na Mheshimiwa Gibson Meiseyeki wajiandae.

**MHE. SHABANI O. SHELIKINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie hotuba iliyoko mbele yetu. Kwanza nimpongeze Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya kwani Watanzania wanaiona kazi yao kubwa lakini sisi hatuna cha kuwalipa ila Mwenyezi Mungu mwenyewe ndio atajua cha kuwalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite moja kwa moja kwenye ujenzi wa nyumba za bei nafuu. Mimi niko kwenye Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii, tulitembelea wakala wa kuuza vifaa vya ujenzi na ujenzi wa nyumba za bei nafuu. Kwa kweli inasikitisha sana kama kweli Serikali ina nia ya dhati kujenga nyumba za bei nafuu basi wawezeshe wakala wale, kwani wakala wale vifaa vyao wanauza bei nafuu sana, *just imagine* kigae kimoja kinauzwa Sh.500/= halafu ukiuliza unaambiwa bado wako kwenye utafiti. Kwa nini sasa Serikali isitenge mafungu ya kutosha kuwawezesha wakala wale ili wakasambaa kwenye mikoa hadi wilayani sambamba na hayo waendeleo kufundisha vijana wetu ili waweze kupata elimu na kujijiri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna huu mtandao wa *ILMIS*. Huu mtandao ni mzuri sana lakini nimuombe Mheshimiwa Waziri Lukuvi huu mtandao usiishie Dar es Salaam tu, huu mtandao uende kwenye majiji makubwa kama Mwanza, Arusha, Tanga, Mbeya na majiji mengineyo hapa Tanzania, kwani mpango huu ni mzuri ambao utarahisisha kabisa hata ile kazi ya kupata hati au kubaini kiwanja cha mtu. Pia ikiwezekana nimwombe Mheshimiwa Lukuvi kwa heshima na taadhima mtandao huu hebu auzambaze kwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie kwenye upimaji wa ardhi. Kama Mheshimiwa Rashid Shangazi alivyosema

kwamba Lushoto kuna uhaba sana wa ardhi na watu wa Lushoto wako tayari kupimiwa ardhi lakini wanapohitaji kupimiwa ardhi basi kunakuwa na figisufigisu nyingi sana. Nashindwa kuelewa tatizo liko wapi? Ukizingatia Wilaya ya Lushoto pamoja na kwamba ni ya milima, milima lakini ina watu wengi sana ambao wana uhitaji, wanahitaji hati ili waweze kukopa benki, wanahitaji pia na hati za kimila. Kwa hiyo tatizo liko wapi Mheshimiwa Lukuvi kwa wananchi wa Lushoto? Hivi kwa nini wanapata tabu kiasi hicho? Wanapohitaji kupimiwa au kupata hati inakuwa ni shida kubwa sana kiasi kwamba mpaka wawapigie watu magoti? Nashindwa kuelewa kwa ajili gani inakuwa hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo huyu mtu wa shamba, mwekezaji shamba la Mnazi, huyu mtu anasema ameishika Serikali kwa hiyo hatambui viongozi zaidi ya yeye na pesa zake. Kwa hiyo nimuulize Mheshimiwa Lukuvi tatizo liko wapi hapa na yeye ameshikwa? Eeh tunataka kujua kwa sababu mtu huyu anatusumbua sana kiasi kwamba sijui yeye anajiamini vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Lukuvi, nawaamini sana na dada yangu Mheshimiwa Mabula, naamini hii ni *issue* ndogo sana mpaka kesho naamini taarifa hii tutaipata. Tunataka mtu huyu tumjue ni nani na ana uwezo gani katika nchi hii? Mheshimiwa Lukuvi najua kazi yake, natambua uwezo wake naamini hili sasa limefika kwake sasa. Tunahitaji ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo wananchi wa Lushoto kama Mheshimiwa Shangazi alisema kwamba wanahitaji sana kupima ardhi lakini kunakuwa na tabu moja kubwa sana. Sasa sijajua kwamba pale hakuna vifaa au wataalam hakuna? Mheshimiwa Lukuvi mimi ndiyo maana nikampongeza sana kwa sababu naamini kazi yake na sidhani kabisa kwamba kazi hii itamshinda. Naomba sasa wananchi wa Lushoto waweze kupata hati kwa mapema na wapimiwe kwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Chikota, baadaye Mheshimiwa Anna Lupembe na Mheshimiwa Gibson ajiandae.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami niungane na Wabunge wenzangu kuwapongeza Mawaziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Lukuvi na Naibu Waziri Mheshimiwa Mabula kwa kazi nzuri wanazozifanya na kwa kweli wanastahili pongezi, tunawapongeza sana. Pia nimpongeze Ndugu yangu Katibu Mkuu Dkt. Yamungu Kayandabila na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Kusiluka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunashuhudia mabadiliko makubwa sana kwenye Wizara hii. Zamani tulikuwa na urasimu mkubwa sana wa kutoa huduma. Ukifika pale Wizarani sasa hivi unaona kabisa mabadiliko ambayo yamefanywa. Kwanza kuna sehemu imeandaliwa kwa ajili ya watu kupewa huduma na eneo lile sehemu kubwa tatizo la mteja linashughulikiwa kidigitali, kwa hiyo tunapongeza sana Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunaona jinsi Wizara hii inavyozingatia ugatuaji. Wamepunguza shughuli nyingi makao makuu wamepeleka kwenye ngazi ya kanda na ugatuaji kwenye ngazi ya kanda si wa madaraka tu wamepeleka na fedha na rasilimali watu, kwa hiyo nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kwenye Wizara hii sasa tunaona jitihada ambazo zinafanywa kuziwezesha Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Waziri amesema nini atakifanya kuziwezesha mamlaka ya Serikali za Mitaa waweze kuandaa hati wao wenyewe. Mheshimiwa Waziri tunampongeza na tunamwombea kwamba awe na nguvu zaidi na hekima ili aweze kutuletea mazuri zaidi ya hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo nina mchango ufuatao mwingine. Kwanza kuhusu suala la usimamizi wa ardhi na huduma za upangaji miji na vijiji. Suala hili ni mtambuka na suala hili ni muhimu. Pamoja na mazuri yote yanayofanywa katika ngazi ya Wizara bila kuwa na watendaji wa kutosha katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa haya mazuri yote ambayo yamekuwa yameandaliwa na Wizara kule chini hayataonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto kubwa ya watumishi wa sekta hii kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kama nilivyosema suala hili mtambuka na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ina nafasi kubwa sana katika utekelezaji wa yale ambayo yamepangwa Wizarani. Ili shughuli ya ardhi ishughulikiwe vizuri kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa ina vitengo vitano, lazima kuwe na mthamini (*valuer*), lazima kuwe na mpima (*surveyor*), lazima kuwe na afisa ardhi vile vile kunahitajika mrasimu ramani na *town planner*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya watumishi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni ya kutisha. Kwenye jimbo langu la Nanyamba kwenye hao wote walioorodheshwa hapa hawapo. Kuna *surveyor* msaidizi tu ndiye anayeendesha ile idara. Sasa utakuta yote yanayoamuliwa na baraza huyu mtu peke yake hawezi kutekeleza na mwezi Agosti anastaafu. Kwa hiyo, akistaafu mwezi Agosti ile ofisi tunafunga kabisa. Kwa hiyo nashauri, huko nyuma Serikali iliona tatizo la wahasibu kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Wizara ya Fedha ikaomba kibali cha jumla ikaajiri wahasibu wengi ikapeleka kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa iliipelekewa wahasibu watano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba Wizara ya Ardhi iombe kibali cha jumla cha kuajiri watumishi watakaopelekwa kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa ili kibali hiki kikipatikana waajiriwe vijana ili wapelekwe kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Vijana wasomi wapo mitaani, kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri aombe kibali cha jumla ili watumishi wapatikane, ili haya mazuri ambayo anayafanya kwenye ngazi ya Wizara yakafanywe kule kwenye Mamlaka



ya Serikali za Mitaa. Tusipofanya hivi itakuwa kule juu mnafanya vizuri lakini huku chini kuna malalamiko mengi na kama anavyoona kwamba gharama za watu binafsi au kampuni binafsi (*private sector*) bado ni za juu na wananchi wetu bado hawawezi kuwatumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili unahusu urejeshaji wa fedha za kodi ya matumizi ya ardhi (*retention*) kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya LAAC, hoja hii imesimama kwa muda mrefu sana. Nina taarifa hapa ya CAG ya 2015/2016, CAG anasema vizuri kabisa kwamba asilimia 80 ya makusanyo ya kodi ya matumizi ya ardhi hayakurudishwa kwa halmashauri husika shilingi bilioni 6.7. Taarifa ya CAG inasema hivyo, na CAG ali-*test* kwenye halmashauri 71 akakuta bilioni 6.7 hazijarejeshwa. Je, kwenye halmashauri zilizokaguliwa 171 kuna shilingi ngapi ambazo hazijarejeshwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri afanye jitihadi za makusudi kwa sababu ukiangalia ile Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982 inasema miongoni mwa vyanzo vya mapato vya halmashauri ni pamoja na kodi hii hapa. Vile vile kuna waraka ulitolewa na TAMISEMI kuhusu asilimia 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama kuna maelekezo mapya, kama hizi fedha hazitolewi basi waraka utolewe ili kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa wasiweke kama vyanzo vya mapato. Kwa sababu sasa hivi kuna maelezo mengi, ukiuliza unaambiwa kwamba Wizara haipewi fedha kutoka Hazina, lakini pili kuna maelezo mengine yalitoka katikati pale kwamba Mamlaka ya Serikali za Mitaa haziwezi kupewa mpaka ilete mpango wa matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inashangaza kwa sababu Mamlaka ya Serikali za Mitaa wakati inapoandaa bajeti kuna kitu kinaitwa *Medium Term Expenditure Frame Work (MTEF)* inaonyesha *activities* zote ambazo zitafanywa na *council* kwa mwaka husika na fedha ambazo zitahusika. Kwa hiyo,

sioni sababu ya kuwaambia Mamlaka ya Serikali za Mitaa walete tena mpango wa matumizi wakati kuna *MTEF* wa halmashauri husika. Kwa hiyo naomba hizi fedha wapewe ili waweze kutekeleza majukumu yao ambayo yapo kisheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la *CDA*. Nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa maamuzi mazito aliyoyafanya ya kuivunja *CDA*, lakini pia kufutwa kwa hati miliki ya *CDA* na kupeleka majukumu yake kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo awali nikiwa mtumishi niliwahi kufanya kazi Manispaa ya Dodoma na Mheshimiwa Waziri wakati huo alikuwa Mkuu wa Mkoa wangu, aliona jinsi ambavyo *CDA* ilikuwa inaendeshwa kwa ubabe, ilikuwa inatengeneza kero. Tulikuwa tunatafuta eneo la kujenga sekondari lakini kuna siku alituita Mheshimiwa Lukuvi ofisini kwake tukakaa masaa matano, *CDA* hawataki kutoa eneo kwa ajili ya ujenzi wa sekondari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wa Dodoma sasa hivi wanahangaika wanakwenda shule ya Mnadani, Shule ya Lukundo, ile Shule ya Sechelela mbali kabisa na nje ya Dodoma. Kata ya Kilimani hii hapa Uzunguni ikaamuliwa kwamba shule ya sekondari ya kata ijengwe Ntyuka watoto wale wanaumia kila siku kupanda ule mlima lakini kwa ubabe wa *CDA* kwamba hawawezi kutoa lile eneo na maeneo ambayo sisi tuliona kama Manispaa kwamba ijengwe sekondari wamepewa watu wengine tu wamejenga mahoteli na shughuli zingine. Kwa hiyo, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake wa kuivunja *CDA* na nashauri sasa Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma ichukue majukumu hayo mazito na iyatekeleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nina ushauri wa aina mbili kwa Wizara. Kwanza wale watumishi wa *CDA* wote wasirundikwe Manispaa, watakuwa na *subortage* kwa Mkurugenzi wa Manispaa ili aonekane kwamba hafai.

Naomba watumishi wale wasambazwe kwenye Mamlaka zingine za Serikali za Mitaa na *cream* iletwe Dodoma ili waweze kuchapa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini na sasa hivi Mamlaka ya Manispaa ya Dodoma iwezeshwe kutekeleza yale majukumu kwa sababu tukiwalaumu tu kwamba hawawezi wale kwa muda mrefu hawajafanya shughuli za ardhi, shughuli hizi walikuwa wanafanya *CDA*, kuna madeni, kuna viwanja ambavyo hawajapewa wenyewe waliolipia. Kwa hiyo shughuli hii sasa itafanywa na Manispaa. Kwa hiyo lazima tuwape muda manispaa waweze kuchukua majukumu hayo; tuwawezeshe, tusiwalaumu mapema ili waweze kutekeleza majukumu haya mazito kwa urahisi na hatimaye tuweze kuendeleza makao makuu ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuunga mkono hoja na nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Lupembe.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuzungumza jioni hii. Kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye aliyetupa uzima na uhai, ametupa muda mwingine tena wa kuweza kumtumikia. Pili, naomba nimpongeze Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri ambayo aliyofanya jana kwa ajili ya kulitumikia Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa nzuri ambayo anaifanya katika Wizara hii pamoja na Naibu Waziri. Wanafanya kazi kubwa ambayo inaonekana kihalisia, tunaomba tuwapongeze sana na Mungu aendelee kuwasimamia ili waweze kufanya kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na Mkoa wangu wa Katavi nikiongelea kuhusu masuala ya Wilaya mpya ya Tanganyika. Wilaya ya Tanganyika ina vijiji vingi sana

ambavyo mpaka leo havijafikiwa kupata hati miliki ya kimila. Wananchi wengi wanaoishi maeneo haya hawana faida na rasilimali zao walizonazo. Kwa sababu tumeona Wizara hii ni sikivu, tunaomba basi wanavijiji wale wa Wilaya ya Tanganyika, Mkoa wa Katavi wafikiwe ili waweze kupata hati miliki za kimila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 70 ya Mkoa wa Katavi ni pori, asilimia 30 ndiyo maeneo wanayoishi wananchi; na siku hadi siku ndani ya Mkoa wetu wa Katavi wananchi wanaongezeka na maeneo yetu ya kufanyia shughuli za kibinadamu ni machache. Naomba Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii; kwa kuwa Wizara ya Maliasili wana sehemu kubwa sana ya hifadhi; na ukizingatia sasa hivi siku hadi siku tunazaana. Sasa binadamu tumeongezeka, mapori yamekuwa makubwa mno, tunaomba Wizara hizi zitutazame kwa hali ya ukaribu zaidi Mkoa wa Katavi kuweza kutupunguzia maeneo ili tuweze kupata sehemu ya kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta kata nyingine hawana kabisa sehemu za kulima, wakiingia tu wanaingia kwenye hifadhi, wakienda huku mapori ambayo yanahifadhiwa na Serikali, sasa wanashindwa jinsi gani ya kufanya shughuli za kibinadamu. Tunaomba Wizara hii ya Ardhi pamoja na Maliasili waweze kutuona kwa ukaribu zaidi kwa ajili ya kutuongezea maeneo ili wananchi wa Mkoa wa Katavi waweze kupata maeneo ya kufanyia shughuli zao kibinadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya yangu ya Mpanda Manispaa ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri, alifika katika Wilaya ya Mpanda, alijionea mwenyewe hali halisi. Katika Wilaya ya Mpanda Kata yetu ya Kashaurili ambayo ndiyo Makao Makuu ya Wilaya ya Mpanda katika zile nyumba za wenyeji hakuna mtu mwenye hatimiliki mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama Wizara itusaidie kutokana na hali halisi. Kwa upande wa ardhi

Manispaa hatuna kabisa wafanyakazi. Wafanyakazi ni wachache sana; wafanyakazi ambao wameajiriwa ni watatu tu, wengine wote ni vibarua. Sasa wale vibarua wanakuwa hawafanyi kazi yao kimakini kwa sababu, wanajua wenyewe ni vibarua. Sasa naomba kama Wizara itusaidie sasa kutuletea watumishi ambao wameajiriwa ili waweze kufanya kazi vizuri pale Manispaa, Mpanda Mjini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi katika Wilaya ya Mpanda. Katika Kata ya Ilembo kuna migogoro ya ardhi kati ya wananchi na Jeshi. Najua Mheshimiwa Naibu Waziri alielezwa, basi tunaomba suala hili liweze kufanyiwa kazi haraka iwezekanavyo kwa sababu, wananchi wa Mpanda pale Kata ya Ilembo pamoja na Kata ya Misunkumilo kila wakiingia kidogo tu Jeshi linasema eneo lao. Sasa tunaomba huu mgogoro uweze kwisha, ili wananchi waweze kupata fursa ya kuweza kufanya kazi zao za kijamii wakiwa katika hali ya usalama zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilipongeze Shirika la *National Housing*, limefanya kazi nzuri sana kiasi kwamba hatimaye na sisi wananchi ambao tunaishi katika wilaya mbalimbali tumeona jitihada za *National Housing*. Tunaomba tumpongeze sana Mkurugenzi wa *National Housing*, Mchechu kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika nchi yetu ya Tanzania. Ameweka alama kubwa sana katika nchi yetu, ameweka alama kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Mpanda Mjini tumejengewa nyumba za *National Housing*. Nyumba zikijengwa zinatakiwa zitumike na binadamu, zisipotumika na binadamu zile nyumba zikishafungwa miaka miwili, ama mitatu lazima zinakuwa na ufa. Ina maana kuwa binadamu akiishi ndani ya nyumba zile nyumba zinaendelea kuishi, lakini kama ndani ya nyumba haishi mtu nyumba nayo inapata uharibifu, inaweka ufa matokeo yake inaonekana kama nyumba nzee (iliyozeeka). Sasa pale Mpanda mmetujengea

nyumba nzuri sana, tunaomba tuwashukuru, lakini zile nyumba bado hazijapata wanunuzi, zile nyumba zinakaa bure, zimefungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba, sasa hivi Wilaya ya Mpanda ni Mkoa wa Katavi, kuna wafanyakazi mbalimbali wa kisekta, wa Wizara, wa maeneo mbalimbali wamekuja maeneo yale, hawana sehemu ya kuishi. Tunaomba hizi nyumba ambazo zimejengwa Wilaya ya Mpanda, Ilembu, zipangishwe. Zikishapangishwa hapo badaye wale wafanyakazi wanaweza kuzinunua kuliko kuzifungia, zile nyumba hazina mtu wa kuishi, matokeo yake zinakuwa kama vile maboma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wizara pamoja na Shirika letu la *National Housing* waangalie upya hizi nyumba ambazo hazijaweza kununuliwa basi wazipangishe ili ziweze kupata wanunuzi mbele ya safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niingie tena kwenye masuala ya migogoro ya ardhi. Naiomba Serikali, tunajua Awamu hii ya Tano kusema kweli imejitahidi sana, migogoro ya ardhi imepungua, lakini bado kuna kazi kubwa. Tunaomba Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, migogoro ya ardhi ni mikubwa sana ndani ya maeneo yetu husika. Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema, ifike kipindi sasa tutafute maeneo ya wafugaji na maeneo ya wakulima, maana wengi unakuta wakati mwingine wanatetea wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna wakulima ambao nao wanapaswa wapate stahiki yao. Tunaomba Serikali kwa ujumla wake, sasa hivi kifike kipindi cha kuwapangia wafugaji maeneo yao na wakulima maeneo yao, ili nchi yetu ya Tanzania iendelee kuwa na amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana na naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anna Lupembe. Tunaendelea na Mheshimiwa Gibson Meiseyeki na baadaye Mheshimiwa Innocent Bilakwate, Mheshimiwa Balози Adadi na Mheshimiwa Amina Makilagi wajiandae.

**MHE. GIBSON B. OLE-MEISEYEKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na zaidi pia kwa kulipatia jina langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa maombi kwa Mheshimiwa Waziri; nimkumbushe tu kwamba, kuna kile kilio chetu ambacho wananchi wa Kata yangu ya Bwawani walilia mbele ya Waziri Mkuu na wakaahidi kwamba mgogoro ule wa ardhi wangeufanyia kazi na yeye alikuja pale na akaagiza vijana wake waweze kufanya kazi ile. Hata hivyo, mpaka sasa ni zaidi ya miezi sita hatujapata mrejesho wowote. Kwa kweli wananchi wananisumbua sana kuhusiana na mgogoro ule wa ardhi ulioko pale Kata ya Bwawani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna wananchi wangu wa Kata za Oldonyosambu na Olkokola ambao ardhi yao ilitwaliwa na Jeshi na ilikuwa wapewe fidia, lakini baadhi yao hawakupata. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ningeomba badaye atuambie mahali ambapo imefikia, ili tuweze kupata majibu ya kuwapa wananchi wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Arusha DC imezunguka Jiji la Arusha kwa pande zote. Kiukweli, *influx* ya wananchi sasa hivi katika Mji wa Arusha ni kubwa sana na wote asilimia zaidi ya 80 wanakuja Arumeru, hasa Jimbo langu la Arumeru Magharibi. Ardhi kule inazidi kuwa finyu na ninachokiona huko mbele ni migogoro zaidi za ardhi ikiwa kama hakutakuwa na jitihada za makusudi za kuhakikisha kwamba, wananchi wale wanaokuja maeneo yale ama wale wakazi wa maeneo ya Arusha ambao wengi wao ni wafugaji na wanapenda kulima, ardhi inazidi kuwa finyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri kwamba, kuwe na mpango wa kupata mapori au mashamba pori yale

ambayo yapo, hayajaendelezwa, ili vijana hawa ambao wako tayari kufanya kazi za kilimo waweze kutengewa maeneo kule na ikiwezekana taarifa ziweifike maana wako tayari kwenda mashambani popote, maporini kule, kwenda ku-*establish* mashamba ili kujipatia riziki zao. Hata hivyo, ukweli ni kwamba kwa sasa hivi mazingira ni kama vile wanabaniwa sana kiasi kwamba wanashindwa kupata mwelekeo kwamba ni namna gani wanaweza kupata maeneo kwa ajili ya kujiendeleza kwa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tulikuwa kwenye Semina hapa ambayo Mheshimiwa Waziri wa Maliasili alituandalia. Wataalam wale maprofesa walikuja hapa walituambia kuwa nchi hii haina tatizo la ardhi. Hatuna matatizo ya ardhi ukilinganisha kilichopo na idadi ya watu na lilikuwa ni jambo la aibu sana, wamesema hapa tunachokikosa sisi ni mipango. Alilinganisha Tanzania na akina Vietnam jinsi ambavyo wako kwenye eneo dogo, watu wengi na hawana migogoro hii ambayo kama sisi tuliyonayo na wale watu wanazalisha chakula mpaka sisi tunapewa huku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa jana tulikuwa na matatizo ya njaa, nchi yenye ardhi kubwa kama Tanzania halafu watu tunalialia na vibakuli vya kuombaomba chakula? Ifike wakati sasa Waheshimiwa muamue sasa kwamba, mnaipanga hii nchi ili Watanzania wengi ambao wana nguvu za kufanya kazi waweze kupata maeneo ya kufanya kazi za kilimo na mifugo, tena bila kugombana. Kuna nchi nyingi tu ambazo ni ndogo kwa *size*, zina watu wa kutosha, wengi lakini hawana migogoro kama tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningomba, Waheshimiwa Mawaziri, kama tulivyoomba katika bajeti iliyopita wakati ule Mheshimiwa Mwigulu akiwa kwenye kilimo yeye akiwapo hapo na Mheshimiwa Maghembe pale, kwamba washirikiane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mizengwe mingi sana katika nchi hii; yametengwa kwa ajili ya kilimo lakini maeneo hayo yana misitu, kuna miti lakini watu wananyimwa kukata



miti, eneo la kulima utalimaje sasa kwenye miti, si lazima uikate? Likishakuwa *declared* kwamba ni eneo la maendeleo ya kilimo na mifugo basi Wizara ya Maliasili na Utalii isiende tena kupeleka pale wataalam wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale watu wana chokocho nyingi sana, wako *aggressive* na wakati mwingine wanafanya biashara ambazo ni kichaa kule kwenye mashamba. Kwa hiyo, Waheshimiwa Mawaziri ningewaomba washirikiane. Maeneo ya kilimo kama kuna misitu, kama kuna miti huko na tayari wamesha-*declare* ni eneo la kilimo na ufugaji basi watu wa maliasili wasiwe wanaingia sana kule, hii mizozano hii inaleta *fracas* kwa wananchi wanashindwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningewaomba wakae pamoja ili wananchi waweze ku-*explore* na ku-*enjoy* matunda ambayo nchi hii inaweza ikawapa. Tuna ardhi kubwa, maeneo ni mengi, hakuna sababu ya sisi kugombana. Viongozi ama tuseme watu wanapokaa kwenye madawati yao wasiwe wanakaa pale wanakuwa kama *obstacles*, watu wamekaa tu! Mtu akishakaa anakuwa bwanyenye kazi yake ni kuzuia watu wengine wasi-*develop*, wanakosa nafasi ya kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kila mmoja kwenye nafasi yake awe ni chachu ya mtu mwingine kunufaika na chochote ambacho kinapatikana kwenye nchi hii na asikae pale anakuwa kama kizingiti kuzuia mtu. Kuna wivu sana wa kimaendeleo kwenye nchi hii. Kwa hiyo tusaidiane, vijana wapewe nafasi na vijana wako wengi na hawana kazi, tutengeneze ajira ili watu waweze kuzipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Mheshimiwa Waziri ni Shirika la Nyumba na Mheshimiwa Angela Kairuki hapa inaweza ikamhusu pia. Tunawapeleka Walimu, Madaktari, na Manesi vijijini; maeneo yetu mengine kwa kweli ni maeneo ambayo si mazuri kwa maisha ya binaadamu. Kule hakuna nyumba, hakuna maji. Kuna kata zangu nyingine kwa kweli

ni za ajabu sana, hakuna barabara, hakuna umeme, hakuna maji, Kata za Bwawani, lakini bado kuna shule kule, kuna zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumwomba Mheshimiwa Waziri Shirika lako la Nyumba, ikiwezekana lifanye makubaliano, sisi Halmashauri ya Arusha *DC* tuko tayari kama ataruhusu tuingie mikataba, watujengee nyumba nzuri kwa ajili ya wafanyakazi kwenye maeneo yale, halafu sisi kwa kutumia vyanzo vyetu vya ndani tuweze kuwa-*fund*, kuwalipa kama ni kodi, kama ni kulipa *instalment* ya kununua zile nyumba, pengine baada ya miaka 10 kadhaa hivi tutakuwa tumeshazinunua na wafanyakazi wanakuwa wako *comfortable* kule vijijini. Maana sasa hivi huwezi kumchukua mtu ana *degree* yake nzima, nzuri safi tu, hajachakachua cheti wala nini halafu unampeleka kwenye nyumba za udongo, nyingine hazina madirisha, hakuna umeme, hakuna *solar*, hakuna kitu halafu unataka afundishe shule yetu ya kata iliyoko kule! Kwa hiyo, wanapata shida sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri Serikali iangalie utaratibu badala ya kujenga majumba tu mijini huku ambako tayari watu binafsi wamewekeza na nyumba bado si tatizo sana, tukawekeze hizi nyumba kwenye maeneo ambayo yana *challenges* nyingi ili nyumba ziwe nzuri, wataalam angalau wawe *comfortable* kwenda kufanya kazi vijijini na huduma ziweze kutolewa ambazo zinaeleweka kwenye vijiji vyetu. Kwa hiyo, naomba hilo lizingatiwe pia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba kwamba, miingiliano ile ya kwenye Wizara kidogo iwe *controlled* ili tuweze ku-*enjoy*matunda ambayo yako kwenye nchi hii. Kwa hiyo kwa leo niseme tu Mheshimiwa Waziri ningefurahi sana kama akinijibu yale maombi yangu ya Kata yangu ya Bwawani na wale ambao wanahitajika kufidiwa katika eneo ambalo jeshi limechukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana na ningefurahi siku moja nisimame hapa nimsifu kama

alivyosifiwa na akina Mheshimiwa Mdee; mimi bado hajanigusa, kwa hiyo naomba na mimi aniguse ili nikija hapa Bunge Ijalo na mimi nimsifie kidogo. Arumeru tuna shida sana, nikimpa nafasi Mheshimiwa Nassari hapa ataongea mpaka asubuhi, ni kwa sababu ya ongezeko kubwa la wananchi katika Mkoa wa Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tu watutanue, mapori yako mengi ambayo hayana hata mipango mingine hamna...

**MBUNGE FULANI:** Awatanue?

**MHE. GIBSON B. OLE-MEISEYEKI:** Yes! Tutanuliwe kule, kwamba yale maeneo ambayo yako wazi yanafaa kwa kilimo...

**MBUNGE FULANI:** Mtanuliwe!

**MHE. GIBSON B. OLE-MEISEYEKI:** ...kwa sababu kiukweli hata sehemu za kuzikia siku hizi ni tatizo. Katika viunga vya Mji wa Arusha sasa hivi tunakwenda kuzikana Manispaa kwa sababu, ardhi imekuwa ni finyu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo tu machache kwa leo. Nakushukuru sana kwa kunipa fursa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Gibson. Tunaendelea na Mheshimiwa Innocent Bilakwate.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa afya na nguvu kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa na ninachowaahidi sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia Wizara hii kwanza kipekee nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya. Kwa kweli ameonesha huyu ni

mtetezi wa wanyonge. Ninachowaomba Waheshimiwa Wabunge na Watanzania, Mheshimiwa Rais anafanya kazi ambayo anahitaji msaada wa Mungu pekee ili ampe ulinzi. Hili jambo si la kawaida na halikuwahi kusikika kwenye masikio ya Watanzania, naomba tumwombe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara ya Ardhi kwa kazi nzuri wanayoifanya. Ingawa kwa upande wangu kwenye Jimbo la Kyerwa bado hajafika lakini nasikia kwingine anafanya vizuri, kwa hiyo nampongeza; na naamini huko Kyerwa atafika, kwa sababu yanayojiri huko Kyerwa anayajua na anayafahamu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee Jimbo langu la Kyerwa. Kwa kweli, tunayo matatizo ambayo ni makubwa kutokana na kwamba ile Wilaya bado ni mpya. Mheshimiwa Waziri bado hatujapata watendaji wa kutosha wa kuweza kupima maeneo ya wananchi, hasa yale maeneo ambayo ni ya Mji ule wa Rubwela na miji mingine midogo ambayo tumeitenga. Naamini wananchi wangu hawa watakapopimiwa ardhi yao tutaweza kuinua uchumi wao, wataweza kwenda kukopa. Pia maeneo haya yakipimwa naamini hata uchumi wa Taifa utainuka kwa sababu watakapopata pesa watafanya shughuli ambazo zitawapatia kipato na Serikali itapata sehemu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna watumishi wachache pale kwenye halmashauri yetu, kwa hiyo niombe Mheshimiwa Waziri aliangalie. Hata hivyo, si watumishi wachache tu, Idara ya Ardhi hawana hata gari, hawana hata pikipiki na jioografia ya wilaya yangu kwa kweli si nzuri. Kwa hiyo, hili tuliangalie, tusiwapeleke tu kule watumishi halafu tukawa-*dump* kule, hawana vitendea kazi halafu tutegemee hatimaye wanaweza wakawapimia wananchi ardhi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo Mheshimiwa Waziri naomba alisikilize ni kwamba, bado maeneo ya vijijini wananchi wanalalamika wanasema

gharama za upimaji ni kubwa. Tuliangalie hili, tusije tukalinganisha na maeneo ambayo ni ya mijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo ambalo mimi nimekuwa nikishangaa sana na nimekuwa nikijiuliza maswali mengi. Mara nyingi hapa Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tukiongelea migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji, lakini nimejiuliza jambo moja, hivi vipindi vyote ambavyo vimepita Serikali haikutenga maeneo kwa ajili ya wafugaji na wakulima? Nimejiuliza sana, lakini hatimaye katika kufuatilia kwangu nimegundua Serikali ilitenga maeneo kwa ajili ya wafugaji lakini maeneo haya kwa sababu ya viongozi ambao wamejaa tamaa, viongozi ambao hawawezi kusimamia majukumu yao maeneo haya wameyagawa, watu wengine wameingia na hatimaye tunasababisha migogoro mikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kule kwangu Kyerwa. Kuna eneo ambalo lilitengwa kwa ajili ya wafugaji mwaka 87. Eneo hili lilitangazwa kwenye Gazeti la Serikali likapewa *GN Number 620*, lakini eneo hilo leo watu wameingia kiholela bila kufuata utaratibu, wamegawana hovy hovy. Sasa unajiuliza hili eneo ambalo lilitangazwa na Serikali bila kutolewa tangazo lingine la kubadilisha matumizi, leo unaweza kuingizaje watu wengine waweze kujimilikisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri; hili najua ugumu wake na mimi kama Mbunge nimetumwa na wananchi kwa ajili ya kuwatetea, hivyo sitanyamaza wala sitatulia katika hili, lazima tuondoe hii migogoro ambayo hatimaye inaleta uadui kati ya wakulima na wafugaji. Mheshimiwa Waziri nakuomba sana, jambo hili siwezi kulinyamazia wakati linaendelea kuleta mgogoro mkubwa kati ya wakulima na wafugaji, lazima litolewe ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo mengine kule kwangu, kwa mfano Kata ya Nkwenda, kuna Kijiji kimoja cha Nyarutuntu; maeneo ya vijiji yanachukuliwa hovy na

wanakijiji hawana msaada, wanapofuatilia hawapati msaada. Naomba Mheshimiwa Waziri aandike, kwenye Kata ya Mgwenda, Kijiji cha Nyarutuntu kuna mgogoro. Huyu bwana amekuwa akiwatumia viongozi wakubwa kwa ajili ya kuteka ile ardhi ambayo ni ya wananchi; hivi vitu ndivyo vinaleta shida kubwa kwa wananchi wetu, naomba tuyafuatilie hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kwenye Mabaraza ya Ardhi. Haya Mabaraza ya Ardhi ni mazuri lakini maeneo mengine yamekuwa kero, hawatendi haki. Kwa mfano maeneo ya vijijini hawana elimu ya kutosha ili waweze kutimiza majukumu yao. Nimwombe Mheshimiwa Waziri tusishie mijini hebu twende na huko vijijini tuweze kuwapa elimu ili wawatendee haki Wanakyerwa na Watanzania ambao hawajatendewa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina mengi ya kusema lakini naomba nirudie, namwomba sana Mheshimiwa sana afike Kyerwa kama anavyofika katika maeneo mengine ili aweze kutatua migogoro ya ardhi ili yule anayestahili haki akapewe haki yake na hatimaye tuweze kukaa vizuri na wakulima na wafugaji wetu kama ndugu na kama marafiki kama ilivyo siku zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, baadaye Mheshimiwa Amina Makilagi ajiandae.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata fursa hii ya kuweza kuchangia hoja hii ambayo ni muhimu sana ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naungana na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hatua ambayo ameichukua, hatua ambayo imedhihirisha madini

yetu yalikuwa yanatoroshwa sana na yalikuwa yanaibiwa sana na ni hatua ambayo inadhihirisha kauli yake kwamba nchi hii ina mali nyingi sana. Kwa hiyo, ningependa kumpongeza sana kwa hatua hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ningependa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na Katibu Mkuu pamoja na Wakurugenzi wote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Viongozi hao wamedhihirisha kwamba kweli wana nia ya kuondoa malalamiko mengi ya ardhi ambayo yalikuwa yamejaa kwenye nchi hii; wamezunguka takribani nchi mzima. Mheshimiwa Waziri amekuja Muheza takribani mara mbili, yote ni kwa ajili ya kutatua matatizo ya ardhi pale wilayani Muheza. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ardhi ni suala muhimu sana. Katika wiki iliyopita tulikuwa na hoja ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Katika hoja hiyo *issue* ya ardhi ndiyo ambayo wawekezaji wote wanataka wakija hapa nchini wakute ardhi iko sawasawa. Sasa vituo vyetu vya *TIC* na *EPZA* vina matatizo makubwa sana ya ardhi na sina uhakika kama Wizara hii imeweza kuwasaidia kwa kiwango gani ili waweze kuwa na ardhi pale waweze kuwa na *land bank* ili wawekezaji wanapofika wasipate matatizo yoyote. Kama hawajawa-*approach* ni vizuri wakati wanagawa ardhi kwa kweli kuangalia hivi vituo viwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TIC* na *EPZA* ni kitovu cha wawekezaji na ni kitovu cha maendeleo. Mwekezaji akija anahitaji hoteli, anahitaji kuweka viwanda lakini lazima awe ardhi. Hatutaki wawekezaji waje hapa na waanze kusumbuka kuanza kutafuta ardhi wao, wanatakiwa wakute ardhi ipo hapo. Kwa hiyo ni vizuri wakiwasiliana na Mawaziri wanaohusika ili kuhakikisha kwamba kwa kweli ardhi inakuwepo na wakati wanagawa ardhi Wizara hii kweli vituo hivyo visikose ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amekuja Muheza na alikuja mara mbili. Mara ya kwanza kukabidhi

mashamba ambayo yamefutiwa hati, takribani mashamba saba na mara ya pili akaja tena kwa suala hilo hilo kwa sababu kulikuwa na shamba moja ambalo lilisahaulika la Kibaranga na akaja akatukabidhi hati, kwamba Mheshimiwa Rais amefuta hati ya hayo mashamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba yale, ukichukulia hili shamba la mwisho la Kibaranga, tulikuwa tumewawekea tunataka kuwahamisha wanakijiji takribani 1,128 ambao walikuwa kwenye hifadhi ya Amani kule Delema; ilitakiwa tuwahamishie pale na tumeshawaamisha pale sehemu kwenye hilo shamba la Kibaranga. Tatizo ambalo linajitokeza ni kwamba wananchi wa pale Kibaranga wanahoji kwamba utawapaje ardhi hawa kabla ya sisi wakazi wa hapa hamjatugawia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulileta malalamiko hayo pamoja na mipango yote ya mashamba yote namna tutakavyogawa sehemu mbalimbali za wawekezaji, hospital, ofisi, shule na kila kitu, na barua hiyo nilimkabidhi Mheshimiwa Waziri. Ni muhimu sana barua hiyo iweze kujibiwa kwa sababu sasa hivi tumeanza kupata wawekezaji na tumeanza kuwaonesha maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunategemea kwamba baada ya kupata majibu ya barua hiyo tutaanza kupanga na kutekeleza namna tutakavyogawa mashamba hayo kwa wananchi, wawekezaji na namna tutakavyoweza kupanga mambo mbalimbali ya maendeleo katika Wilaya ya Muheza. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri namwomba sana, kwamba tukipata majibu ya barua yetu hiyo itatusaidia sana sisi kuweza kupanga mipango yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kwamba, sisi ardhi tunayo sasa hivi hatuna shida ya ardhi, tuna shida tu ya kutafuta wawekezaji Muheza. Hata hivyo, tatizo kubwa ni kwamba tuna upungufu sana la Wapima Ardhi; wapimaji hakuna; tuna mpimaji mmoja ambaye sasa hivi amekwenda kusoma. Sasa kila tukitaka kufanya mipangilio inabidi tuombe Mkoani Tanga.



Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimwomba Mheshimiwa Waziri kwamba *at least* atusaidie wapimaji wawe pale ili tuweze kukamilisha hii kazi ya upimaji pale wilayani ambayo tunaamini kwamba kwa kiasi kikubwa sana itaweza kutusaidia kuweza kupima na kuweza kupanga (*master plan*) ya pale wilayani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho nataka kuongelea suala la *National Housing*. *National Housing* wamefanya kazi nzuri sana na wanaendelea kufanya kazi nzuri sana, wamejenga majengo mengi sana na sasa hivi wako kwenye mikakati ya kujenga nyumba za bei nafuu. Mheshimiwa Waziri naomba; *National Housing* tumewapa eneo pale Muheza la sehemu za Chatuu Kibanda pale, wameshalipia na wananchi wa Muheza walikuwa wanategemea kwamba ujenzi wa hizo nyumba nafuu ungeanza wakati wowote ule. Hata hivyo, mpaka wakati huu hatuoni dalili zozote, tunajuliza hawa *National Housing* vipi, wamesahau kwamba tuliwapa eneo pale Muheza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri kwamba aweke msisitizo ili *National Housing* sasa hivi waje waanze ujenzi pale. Eneo lipo na wananchi wa Muheza wako tayari na wengine wako tayari wanaulizia namna ya ununuzi. Sasa tunamwomba sana aangalie uwezekano wa kuja kusaidia na kuwaamuru *National Housing* waanze kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, yangu leo yalikuwa machache na nakushukuru sana na naomba kuunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Balozi. Mheshimiwa Amina Makilagi sasa ni zamu yake na baadaye Mheshimiwa Anna Gidarya, Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Selasini wajiandae kwa dakika tano tano.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia. Awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kumshukuru

Mwenyezi Mungu muweza wa yote aliyenipa fursa ya kuweza kusimama na kuweza kutoa mchango wangu katika sekta hii muhimu sana ya ardhi ambayo baba wa Taifa aliasisi akasema ili nchi iendelee inahitaji mambo manne na suala la ardhi alilipa kipaumbele cha kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijakwenda kwenye hoja zangu naomba kwanza niseme naunga mkono hoja hii kwa sababu jana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefanya kazi nzuri sana ya kutukuka ambayo sisi Watanzania na hasa wanawake hatuna cha kumlipa zaidi ya kumwomba kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumpa nguvu na kumsimamia aendelee kutekeleza kile alichokiahidi alipokuwa akiomba kura kwa Watanzania na Watanzania wakamwamini na kumpa kura za Urais mpaka 2020. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba kwa kazi aliyofanya Mheshimiwa Rais, maana mimi hapa napokea simu mpaka simu imezima, kama kura zingepigwa leo ushindi wa Chama cha Mapinduzi ungekuwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niunge mkono hoja hii kwa sababu nne zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwanza, kitabu hiki kimeandaliwa vizuri, ni ukweli usiopingika kitabu hiki hakina maneno, kimejeaa *data*, maneno ni ukurasa 1 – 70 lakini kuanzia ukurasa wa 1 mpaka 157 ni *data*. Hongera sana Mheshimiwa Waziri Lukuvi na timu yake kwa kuandaa kitabu hiki vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa sababu Mheshimiwa Waziri, William Lukuvi, Mheshimiwa Naibu Waziri, Angelina Mabula; mimi huwa namwita Sanji, na Katibu Mkuu na timu yote wanafanya kazi nzuri sana na ndiyo maana leo naona kila Mbunge anayesimama muda unamtosha kwa sababu hana cha kuzungumza zaidi kwa sababu mambo mengi yamefanyika katika maeneo yake.

Naomba Mheshimiwa Lukuvi aendelee kufanya kazi, pamoja na timu yake na Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kweli watendaji wa Wizara Ardhi wamebadilika, ameeleza hapo Mheshimiwa Chikota, nimemsikiliza. Siku moja nimewahi kwenda kwenye Wizara fulani tukiwa naye, tulijionea maajabu ambayo yalikuwa hajawahi kutokea; hongereni sana, Mwenyezi Mungu awatie nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naunga mkono hoja hii kwa sababu Wizara ya Ardhi imetatusia migogoro mingi sana iliyokuwa inawakabili wananchi kule Dar- es Salaam, Arusha, Mara, Morogoro na maeneo mbalimbali, nikianza kuyataja tutalala hapa kwa upimaji wa ardhi na maeneo mengine; kwa kweli Lukuvi hatuna cha kumlipa; naomba niungane na wenzangu kusema kwamba Mwenyezi Mungu awatie nguvu na awasimamie katika kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada kuunga mkono hoja hii, sasa naomba nijielekeze katika mambo machache niliyojipanga kuyatilia mkazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, nataka nizungumzie umiliki wa ardhi. Napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Serikali yetu ya CCM kwa kutoa fursa sawa kwa wanawake na wanaume katika kumiliki ardhi. Kwa mujibu wa Sheria ya Mwaka 1979 kifungu cha nne (4) mpaka cha tano (5) kimetoa fursa kwa wananchi wote bila kujali ni mwanamke ama mwanaume kwamba anayo haki ya kumiliki ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi bado yapo matatizo katika jamii ya watu wa Tanzania ambako baadhi ya wanawake hawamiliki ardhi. Kwenye ule utaratibu wa mila baadhi ya makabila mwanamke hamiliki ardhi. Hapa nitatoa mfano wa wajomba zangu kule Kagera ambako mwanamke hana chake, hawezi kumiliki ardhi yeye anamiliki mji tu. Kule Kilimanjaro na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefika wakati kwamba sasa Mheshimiwa Lukuvi sisi tunakuamini...

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilimanjaro tunamiliki ardhi.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Hebu akaangalie taratibu za kimila ambazo ni kandamizi kwa wanawake ili zirekebishwe na wanawake waweze kumiliki ardhi sambamba na wanaume ili wanawake nao wafaidike na matunda ya nchi yao. Wanawake wana fursa, wanawake wana haki ni kwa nini inapofika wakati wa kutoa ardhi eti mila na desturi zinasema wanawake hawana haki? Kwa kweli Mheshimiwa Lukuvi nataka hapa kabla hajahitimisha hotuba atuambie sasa na namwaminia kwa uhodari wake, ana mkakati gani kuhakikisha hizi mila kandamizi zinaweza kuondolewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie migogoro ya wakulima na wafugaji na vile vile migogoro kati ya wananchi na hifadhi. Sitaki nirudie ya wenzangu waliyozungumza. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Serikali lakini bado kuna migogoro mikubwa ya ardhi, bado wananchi wanaishi kwa mashaka, bado wafugaji hawana uhakika, bado mazao ya wakulima yanaliwa na mifugo ya wafugaji; bado hifadhi inawakandamiza wananchi; bado hata wananchi wanakwenda kwenye maeneo ya hifadhi ambako hawaruhusiwi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufike wakati sasa na hapa nataka nije na ushauri, umefika wakati Serikali ya Tanzania ipime ardhi yote ya Tanzania. Naomba nikatae kwamba haiwezekani suala la kupima ardhi kuwaachia Halmashauri, Halmashauri hazina fedha. Serikali itengeneze mkakati maalum wa kutafuta fedha hata kama ni kwa mkopo, hata kama ni kuanzisha mfuko na tuko tayari, zitafutwe hela za kutosha, ardhi ya Tanzania ipimwe yote, wakulima waambiwe ninyi eneo lenu ni hili, wafugaji hapa ni kwenu, wavuvi hapa ni kwenu na Hifadhi ya Taifa ni hapa, ili tuweze kuishi kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumza wenzangu kwamba sasa hivi *population* ya Watanzania imeongezeka, idadi ya mifugo imeongezeka lakini ardhi nayo inaendelea kutumika. Kama hatukujipanga na kuwa na matumizi bora ya ardhi huko baadaye kutakuwa na vita vya watu wanaopigania ardhi. Naomba tusifike huko, hebu Serikali ije na mkakati na mpango. Itengeneze mkakati wa kukopa fedha kwenye vyombo vya fedha ili tuweze kupima ardhi yote ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba niipongeze Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa kazi nzuri sana ya kuendelea kutoa hati kwa Watanzania. Napongeza sasa hivi sekta ya ardhi wameandaa utaratibu mzuri sana, sasa hivi wamefungua ofisi za kanda, ndani ya miezi mitatu mwananchi anapata hati. Zamani ilikuwa ni kero na shida, hongera sana Serikali ya CCM; na ndiyo maana wananchi wanasubiri uchaguzi ufike kwa sababu kazi inafanyika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ushauri, kwamba pamoja na kazi nzuri, lakini zoezi linasuasua. Tumeona kazi nzuri ya Morogoro tumeona kazi nzuri kule Muleba na maeneo mengine ya kupima ardhi mpaka za vijijini. Sasa hivi naomba nishauri Serikali, hebu iongeze kasi ya kupima ardhi, hebu itafute fedha za kutosha, ipeleke kwenye hicho kifungu ili wananchi wote wapimiwe ardhi yao. Kama mwananchi akipimiwa ardhi yake akawa na hatimiliki hata mapato ya Serikali yataongezeka kwa sababu atalipa mapato kwa mujibu wa Sheria badala ambavyo sasa hivi wananchi zaidi ya asilimia 80 wanatumia ardhi lakini hawalipi chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ardhi itamkomboa wananchi na hasa mwanamke aliye kijijini atatumia hati yake kwenda kukopa fedha katika vyombo vya fedha. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Lukuvi na timu yake na Serikali yote kwa ujumla hebu waweke mkakati wa kuhakikisha tunakwenda kupima ardhi. Hapa nataka atakapo-*wind up* hotuba yake Mheshimiwa Lukuvi atuambie ana mkakati gani

wa kuhakikisha kwamba anaharakisha kwenda kupima ardhi na wananchi wote wanapata hatimiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la mipango miji. Ukiwa kwenye ndege ndio utaona hali halisi. Ukienda nchi nyingine utaona ardhi imepimwa vizuri. Afrika Kusini ni mfano na maeneo mengine, kwetu unaona viduku viduku vimekaa. Ufike wakati sasa tuwe na mipango miji, tuwe na *master plan* ya kila mji. Tumechoka kuona miji yetu inajengwa bila kuwa na *master plan*. Sasa hivi tunaanza Jiji la Dodoma, Makao Makuu ya Chama na Serikali, tunataka Mji wa Dodoma upimwe wote, tunataka mikoa mipya na mikoa mingine ipimwe yote na maeneo yote ya halmashauri na miji yetu ili tuwe na miji iliyopangwa kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile niipongeze *National Housing* kwa kazi sana wanayoifanya ya kujenga nyumba. Hongera Mr. Mchechu na timu yako, mmekuwa ni watu waaminifu na waadilifu, mmefanya kazi nzuri sana iliyotukuka ya kujenga nyumba za *National Housing* hapa Tanzania; lakini kama alivyosema Mheshimiwa Lupembe nyumba nyingine hazina watu, tatizo linalowapata nyumba ni ghali. Tunaomba mjaribu kufanya marekebisho. Tafuteni sasa, mkawasaidie na wanyonge hasa wanawake wanaoishi vijijini. Huyu mfanyakazi mdogo mwenye kima cha chini mshahara wake shilingi laki mbili ama laki tatu naye afaidike na mpango huu na inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mr. Mchechu namfahamu, huwa ana mipango; anaweza akatengeneza hata nyumba ya milioni kumi mtu akaishi, anaweza kutengeneza nyumba ya milioni ishirini mwananchi akaishi; ikiwezekana hata ya milioni tano, chumba na sebule ataishi mfanyakazi wa Tanzania na akafaidika kuliko ilivyo sasa milioni mia moja na nyumba ya kima cha chini milioni arobaini kwa kweli inashindikana. Siyo *National Housing* peke yenu hata na ile kampuni ya Watumishi *Housing* pia nao wamefanya nzuri lakini warekebishe hivi viwango. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nipongeze sana mpango wa mashine za kufyatulia matofali kwa vijana, naomba sasa *National Housing*, Mr. Mchechu na wenzake waje sasa na mpango wa kusaidia wanawake. Wanawake nao wanao uwezo wa kufyatua matofali kwa ajili ya kujenga nyumba za bei nafuu, nao...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Amina, muda wako umemalizika...

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** ... nao wakopesheni kupitia vikundi vyao ili nao wanufaike na mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, mchango wangu mwingine nitauwasilisha kwa maandishi, naunga mkono hoja, hongera sana Waziri wa Ardhi, hongera sana Mheshimiwa Dkt.Magufuli Mungu akubariki sana...

**MWENYEKITI:** Heee! Ahsante sana Mheshimiwa, nakushukuru muda wako umemalizika

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:**...kura zikipigwa leo Rais ni wewe. Ahsante sana Kidumu cha Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Anna Gidarya na Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Selasini wajandae kwa dakika tano tano.

**MHE. ANNA J. GIDARYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, hizo dakika zangu mbili zilizoliwa ulinde. Kwanza kabisa naomba niunge mkono Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Hata hivyo kwa kuwa muda ni mchache naomba nijielekeze kwenye hoja mahsus katika Wizara hii. Kwanza kabisa naomba niende kwenye mgogoro wa ardhi katika vijiji vinavyozunguka hifadhi ya Tarangire.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro hii imezungumzwa muda mrefu lakini inavyoonekana hakuna

mafanikio. Nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba leo hii nimekuja na *document* ambayo inaonesha Sheria iliyounda vijiji hivyo na *GN* ya Serikali. Naomba nimkabidhi kitabu hiki ili aende akatatue mgogoro wa Gijedabou, Gedamara na Ayamango. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye shamba la mwekezaji Hamir *Estate* iliyofutwa umiliki wake na Mheshimiwa Rais mwaka 2015, Novemba. Shamba hili lilifutwa na Mheshimiwa Rais tarehe 4 Novemba, 2015, lakini cha kushangaza mwekezaji huyu pamoja na kusitishwa umiliki wa shamba hili bado anaendelea kuitumia shamba hili, jambo ambalo linaibua mgogoro mpya kwa wanakijiji na wananchi wa Bonde wa Kiru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shamba hili wakati Mheshimiwa Rais analifuta, hakukuwa *condition* yoyote iliyowekwa, hakuna maelekezo yaliyoelekezwa kwamba lipelekwe kwa wananchi au liende wapi. Sasa tunaomba Mheshimiwa Waziri hili jambo alifanyie kazi, shamba limefutwa, tujue linakwenda kwa wananchi au linakwenda wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mheshimiwa Waziri mwenye Wizara husika sasa atulettee sheria mpya ya kubadilisha matumizi ya ardhi. Kwa mfano, sasa hivi kumekuwa na sheria inabadilishwa matumizi ya ardhi ya kilimo inakuwa ardhi ya makazi, hii imeleta mgogoro. Kwa mfano Babati Bonga ilikuwa ni matumizi ya kilimo, Arusha Usa River kulikuwa ni matumizi ya kilimo, leo ukikuta ni majumba matupu. Vile vile mfano mzuri, unaweza ukahamisha watu wakakaa jangwani ukawapelekea maji na wanaweza kuishi, lakini huwezi ukapelekwa jangwani ukalima ukaivisha mazao. Sheria hii iletwe hapa iingizwe katika moja ya sheria ya matumizi ya ardhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nyaraka hizi Mheshimiwa Waziri naomba nimkabidhi barua ya ubatilisisho wa umiliki juu ya shamba la huyu mwekezaji Hamir *Estate* kitalu namba 1396 eneo la Bonde la Kiru, Wilayani Babati.



Naomba nimkabidhi nyaraka hizi kwa sababu muda wangu hautoshi ili aone ni jinsi gani yeye anadanganywa. Mgogoro wa Bonde la Kiru umekuwa ni *VICOPA* vya baadhi ya viongozi. Mgogoro huu ni wa tangu mwaka 1998, mwaka 2009 mfanyakazi wa mashamba ya Kiru mchana kweupe saa kumi alikatwa shingo akaletwa Mrara; leo hii tunasema tunashughulikia mgogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namjua Mheshimiwa Waziri anafanya kazi, hata haya matokeo ya hili shamba kufutwa ni pamoja na juhudi zake. Kwa sababu ameanza, aende akamalizie hii ngoma. Amepongezwa sana lakini haimaanishi kwamba mimi simpongezi lakini kuna mambo mengine yanatumiza. Hiki kitabu ukiangalia kuna magofu ya nyumba za watu, watu wanaishi kwenye nyumba za nyasi hawaruhusiwi kuendeleza makazi yao, hawaruhusiwi kulima miaka 11. Hebu ajichukulie sasa, ni miaka 11, wewe ni baba na una watoto sita, chakula chako ni cha kuombaomba, inakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Waziri atakuwa amenisikia kwa haya machache, naomba Mheshimiwa Waziri nimkabidhi hizi nyaraka. Naunga mkono hotuba ya Kambi Rasmi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anna Gidarya. Sasa tunamkaribisha Mheshimiwa Esther Matiko naye dakika tano.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia angalau dakika tano ili niweze kuchangia kwenye Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya dakika tano yale ya kitaifa nitayaandika kwa maandishi, naomba nijielekeze kwenye Halmashauri ya Mji wa Tarime. Kwanza niwapongeze kwa kuanzisha Kanda ya Simiyu ambayo itarahisisha upatikanaji wa huduma ya hati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji wa Tarime kwa kiasi kikubwa sana ardhi yetu haijapimwa. Kwa hiyo ningependa niombe Wizara iweze kuzingatia haya ambayo nitayasema ili waweze kuharakisha na kuhakikisha kwamba tunapata upimaji kwa kiwango kikubwa sana ambapo tukipima ardhi yetu inaongeza thamani na hata wale wananchi wanaweza kuitumia kuweza kukopa na vitu vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna upungufu mkubwa sana wa wafanyakazi, hatuna Afisa Mipango Miji, tuna *surveyor* mmoja tu, hatuna Maafisa Wasaidizi wa Ardhi. Kwa hiyo naomba Wizara, kuna vijana wawili ambao wametoka Chuo cha Tabora wameletwa pale kwenye Halmashauri ya Mji wa Tarime kwa ajili ya ile kazi ya mfumo wa kodi wa ardhi na walikuja kwa mkataba na mkataba unakaribia kwisha; naomba kabisa Mheshimiwa Waziri waweze kuwaajiri wale vijana wabaki katika Halmashauri ya Mji wa Tarime ili kupunguza hii adha ya wafanyakazi na kurahisisha upimaji wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ukosefu wa vifaa vya upimaji. Halmashauri ya Mji wa Tarime tunakodisha vifaa kutoka katika Halmashauri zingine kuja kufanya upimaji. Kwa hiyo naomba Wizara iweze kutupatia angalau *set* moja ya vifaa vya upimaji, kwa mfano *differential GPS* au hata *total stations*, tukipata *set* moja ya hivyo itaturahisishia upimaji katika Halmashauri ya Mji wa Tarime na tuache kukodi kutoka kwenye Halmashauri nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, ningeomba Wizara iweze kutusaidia fedha ili tuweze kuandaa *Master Plan* kwa sababu Halmashauri ya Mji wa Tarime hatuna fedha za kutosha. Tukiandaa *Master Plan* itatusaidia, maana kuna miradi mingine tunaikosa, kwa mfano ya *World Bank*, kama hatuna *Master Plan* hatuwezi kupata hiyo misaada. Kwa hiyo, Wizara ione kwamba ni muhimu sana kutusaidia tuweze kupata. Halmashauri nyingi sana zinakosa miradi ya *World Bank*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo awali kulikuwa na Mfuko ambao ulikuwa unaitwa *Plot Development Revolving Fund (PDRF)*, tulikuwa tunaomba uweze kurejeshwa. Watukopeshe fedha tuweze kuzitumia kupima viwanja ambapo itarahisisha; maana yake kama nilivyosema awali, unakuta Halmashauri zingine hazina fedha za kutosha. Kupitia huo mfuko tunaweza tutakopa fedha, tukapima na kuweza kulipa fidia kwenye viwanja na itasaidia sana kuweza kuweka mji wetu uwe vizuri na hata Bunda nao wana changamoto kama hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho kwa kweli ningependa Wizara ya Ardhi iweze kuingilia ni mgogoro wa ardhi kati ya wananchi wa Tarime wanaotoka Kata ya Nyamisangura na Nkende kwa maana ya Bugosi na Kenyambi na Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Jeshi la Wananchi wa Tanzania walichukua ile ardhi kinyume kabisa na sheria za ardhi; lakini mbaya zaidi tumeshuhudia zaidi ya miaka kumi hawapati fedha za kulipa fidia. Mheshimiwa Waziri ningependa kabisa na kipindi kile cha Wizara ya Ulinzi alisema atakuja Tarime, aje na Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi ili aangalie uhalisia, wale wanajeshi warudi kule kwenye kambi yao na wananchi waweze kurudishiwa ardhi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwa kweli na mimi nichukue fursa hii kuwapongeza *National Housing*, wanajitahidi sana na wanastahili pongezi. Tunaona ni wapi wametoka na wapi walipo kwa sasa hivi. Kuna changamoto ambazo zipo na tumekuwa tukiziongea ambazo kama Wizara au Serikali wakizifanyia kazi tutaweza kupata zile nyumba ambazo tunasema za bei nafuu. Kwa sasa hivi walivyo ni kazi kwa kweli maana Serikali hawawapi ruzuku, wanajiendesha zaidi kama kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna changamoto zingine ambazo tumekuwa tukiongea kwenye kupata ile miundombinu ya kwenda kwenye makazi husika; waweze kupata urahisi kwa hapo maji, umeme na miundombinu ya barabara ambayo itaenda kuwarahisishia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa ndugu zangu wa Mbarali na wenyewe wana mgogoro wa ardhi kati ya hifadhi na wananchi wale wakulima wa Mbarali. Mwaka 2007 walienda wakachukua vijiji 21, sasa hivi tena Serikali imeenda imeongeza *beacon* inachukua Vijiji 32 yaani wale wa Vijiji 21 walihamia kwenye Vijiji vingine na sasa hivi wanaondolewa tena. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri naomba awazingatie na hao watu wa Mbarali nao waweze kupata haki yao ili hatimaye tuondoe hii migogoro ambayo unakuta kwa kweli haina tija na inakatisha tamaa; na tukizingatia wakati wa uchaguzi Chama Cha Mapinduzi kiliahidi kwamba watawajengea barabara ya lami... (*Makofi*)

*(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Matiko, umemaliza muda wako.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:**.. sasa msiwahamishe hapo hawa wananchi. Ahsante sana (*Makofi*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Selasini na baadaye Mheshimiwa Kigua na Mheshimiwa Bulembo ajiandae.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii ndogo ili na mimi nichangie hoja hii. Kama walivyofanya wenzangu, nampongeza Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kazi ambayo wamefanya katika Wizara, ni nzuri ndiyo maana wanapongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya Waziri ukurasa wa 34 kuna hoja hii inayohusu mipaka ya kimataifa, hili ndilo jambo lililonifanya nisimame. Kwanza nimshukuru sana Waziri kwa kuliongelea jambo hili kwa sababu jambo hili limeleta sintofahamu kubwa sana kwa wananchi wangu wa Rombo eneo la Kikelelwa mpaka Nayeme. Wananchi wamewekewa nyumba zao X kwa hoja kwamba wanahamishwa kutoka mpakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa sababu nimefuatilia jambo hili na Waziri ameniweka wazi, kwamba Serikali ya mkoa ina mipango yake ya ulinzi na usalama. Sikatai kuhusu hiyo mipango lakini linapokuja suala linalohusu ardhi ningeomba sana Serikali za Mikoa zihusishe Wizara, kwa sababu sasa hivi wananchi wa Kikelelwa, Tarakea na Nayeme wengine sasa hivi wanaanguka kwa presha, wengine wanawaza kwenda mahakamani kwa sababu ya tishio la kubomolewa nyumba zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na Mheshimiwa Waziri wananchi hawa wameishi katika haya maeneo kabla ya uhuru na kwa sababu hiyo kuwawekea X sasa hivi ni sawa sawa na kuwapa hukumu ya kifo. Naomba ieleweke Rombo hatuna ardhi, hivi sasa hivi tunawaza namna ya kujenga hata taasisi za umma hatuna ardhi, hatuna hata maeneo ya viwanja vya michezo. Kwa hiyo jambo linalohusu ardhi katika Wilaya ya Rombo lisichukuliwe tu kwa mihemko kwa sababu ni jambo hatari na linaweza likasababisha maumivu makubwa sana kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, Mheshimiwa Waziri nashukuru na nimwombe atakapohitimisha hoja yake aseme kitu ambacho kitawapa *comfort* wananchi wa Nayeme, Tarakea na Kikelelwa ili waweze kupata utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze jambo lingine linalohusu ardhi. Mheshimiwa Waziri pale Rombo kuna eneo la Chala. Lile eneo ni ardhi ambayo wazee wanaotoka Kata za Holili, Mahida, Chala, Mengwe, Mamsera na Kata ya Manda walipewa na *Land Board* zamani, wanazo risiti walikuwa wanalipia hiyo ardhi, lakini sasa hivi kuna watu wamepewa ile ardhi kinyemela. Kinachotokea wananchi hata wakiingia katika lile eneo wengine wanapigwa, wengine wanakamatwa na kadhalika. Namwomba Mheshimiwa Waziri aje Rombo tukatembelee lile eneo, aseme kitu cha kuwapa *comfort* wananchi wa maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba pamoja na uhaba wetu wa ardhi tuna Miji ya Tarakea, Mkuu pamoja na Mji wa Holili, ni miji ambayo inapanuka lakini inapanuka hovyoy kwa sababu hatuna fedha kwa ajili ya kulipa fidia. Mnajua matatizo ya ardhi kwetu tunazika katika mashamba yetu humo humo, kwa hiyo ukiamua kumwondoa mtu fidia yake ni kubwa kwa sababu unafidia mpaka makaburi, sasa ile miji inadumaa. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, Halmashauri hawana uwezo lakini wameomba awasaidie bilioni moja kwenye ile taasisi yake wapime, wananchi wapo tayari kununua hivyo viwanja na kurejesha fedha yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize kwa kusema kuhusu migogoro hii ya ardhi. Sisi ambao hatuna ardhi tunaomba hii migogoro iishe kwa sababu tuna hakika ardhi hii ikipimwa kwa sababu na sisi ni Watanzania, vijana wetu wa Rombo nao wanaweza wakapata ardhi katika maeneo mengine. Nilikuwa katika Kamati ya Bunge iliyochunguza migogoro ya ardhi. Wako watu waliopewa mashamba makubwa kwa maana ya uwekezaji, wengine wameyakodisha. Tulienda Kilosa hapa tukakuta Mchina ana shamba anakodisha watu; tumemkuta Mwenyekiti wa Halmashauri hapo ana shamba, anakodisha watu... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Selasini...

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bulaya.

#### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ESTHER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kanuni sitaisoma, kwa jambo ambalo limetokea mapema. Tunajua Mheshimiwa Waziri

Lukuvi ame-*table* hotuba yake leo, ambaye pande zote zimemsifia sana. Sasa naomba mwongozo wako, kwa sababu kwa mujibu wa ratiba hotuba hii ilikuwa inapaswa kuhitimishwa kesho jioni lakini kwa kuzingatia kwamba wenzetu Waislam wanaanza Mfungo wa Ramadhan na wengine wale wanaotoka Zanzibar wanatarajia kusafiri kwa ajili ya kuanza Mwezi Mtukufu na familia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba mwongozo wako sasa, kwa nini kiti chako kisitoe maelekezo kwa Waziri wa Sera, Uratibu na Bunge, Mheshimiwa Jenista Mhagama maana mimi ni kivuli tu, ningekuwa na mamlaka hayo ningefanya; kesho asubuhi atengue kanuni ili sasa baada ya kuhitimisha saa mbili tumalize saa nane mchana ili tutoe fursa kwa wenzetu Waislam waweze kujiandaa na Mfungo wa Ramadhan. Ahsante sana na naamini mwaka 2020 nitakuwa kamili, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Mbona mnaunga mkono kabla sijatoa mwongozo? Nimepokea mwongozo wa Mheshimiwa Esther Bulaya ni kweli jambo alilolitaja limetokea leo asubuhi na limezungumzwa hapa. Imetenguliwa kanuni ili tuweze kuanza saa tatu na kumaliza saa 12 kwa vile Mfungo wa Ramadhani umeingia. Kwa hiyo, kwa kutumia kanuni ya tano kwa mamlaka niliyopewa mwongozo wangu ni kwamba kesho nitamtaka Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu aweze kutengua kanuni ili kesho tumalize Wizara hii saa nane mchana. Huo ndio mwongozo wangu. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Omary Kigua na baadaye Mheshimiwa Abdallah Bulembo na Mheshimiwa Hasunga wajiandae.

**MHE. OMARY M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii jioni ya leo niweze kusema machache juu ya Hotuba ya Wizara ya Ardhi. Nami nitakuwa

ni mnyimi wa fadhila kama sitamshukuru Waziri wa Ardhi, Naibu Waziri pamoja na timu nzima ya Wizara ya Ardhi kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hii nitakuwa na maneno machache sana lakini yatalenga kwenye ushauri zaidi. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Ardhi ikiwezekana alete sheria hapa ambayo itakayozuia maeneo ya kilimo yasitumike kwa ajili ya makazi. Jambo hili tumeliona, kila anayesimama hapa analalamika juu ya migogoro ya ardhi, hakuna kilimo bila mipango bora, kwa sababu tumeruhusu ardhi yenye rutuba tunaanza kujenga. Naona hili haliwezi kufanyiwa kazi bila kuleta sheria hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Ardhi kwamba Bunge litunge sheria ya namna ya kuzuia wananchi wetu wasiuze ardhi; isiwe mtu ana heka, kumi ishirini au zaidi anaamua kuuza tu kwa sababu ya shida yake. Ni kwa nini nasema haya? Hii ni kwa sababu migogoro mingi tunayoiona ya wakulima na wafugaji imesababishwa na wananchi kuuza maeneo yao. Nadhani Mheshimiwa Waziri analo jukumu hilo kuangalia, kupitia kuona ni namna gani tunaweza kupunguza migogoro kwa namna hii ya kuzuia wananchi kutouza ardhi ovyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeliona hili kwa sababu mimi natoka Jimbo la Kilindi ambako kuna migogoro mingi sana. Mtu mwenye pesa yake anatoka Arusha au Manyara huko anauza heka moja anakuja kununua heka 500 kule Kilindi. Sasa hawa wananchi ambao hawana uwezo, mafukara wanauza ardhi wanabakia kuwa vibarua katika ardhi hiyo. Kwa hiyo ili kulizuia hili naomba Mheshimiwa Waziri wa Ardhi alichukue hili aweze kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kuchangia ni juu ya migogoro ya wafugaji na wakulima. Kila aliyesimama hapa anazungumzia migogoro ya wafugaji na wakulima. Katika Jimbo langu la Kilindi nina wafugaji na wakulima wengi sana lakini najiuliza tatizo ni nini? Suluhisho



la kudumu, Mheshimiwa Waziri, ni kupima ardhi. Tupime ardhi hii ili wafugaji wajue maeneo yao ni yapi, wakulima maeneo yao ni yapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini najiuliza zaidi, hivi mimi Wilaya ya Kilindi ambayo ina vijiji 102 tutaweza kuvipima leo kwa muda mfupi hivi? Sasa kama mlianza Morogoro, nadhani muanze na maeneo ambayo yana migogoro ya ardhi Mheshimiwa Waziri anajua, Kilindi ni miongoni mwa maeneo ambayo yana migogoro mikubwa sana ya wafugaji na wakulima, nimwombe baada ya Morogoro aje Kilindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi juu ya mgogoro wa Wilaya za Kilindi na Kiteto ambao umedumu kwa takribani miaka 30. Mheshimiwa Waziri wa Ardhi alikuja mpakani pale, yeye na Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Waziri wa TAMISEMI. Nimshukuru kwa sababu aliweza kutupatanisha mikoa miwili ya Manyara na Tanga pamoja na wilaya hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza, alifanya jitihada kubwa sana na akatenga shilingi milioni mia moja kwa ajili ya kupima. Kwa sababu kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa katika mkutano ule Mheshimiwa Waziri Mkuu aliagiza kwamba ili kutatua mgogoro ule ni lazima tutumie *GN* ya mwaka 1961, *GN* namba 65. Mheshimiwa Waziri wa Ardhi alituma wapimaji, wamefanya kazi nzuri sana na wameweza kuandika ripoti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo hapa ni kwamba Mheshimiwa Waziri alielekeza ziwekwe *beacons*, leo takribani miezi miwili mitatu imeshapita wapimaji hawapo pale. Wananchi wa Jimbo la Kilindi wamenituma, wanajua kwamba yeye ni kiongozi mwadilifu, ameweza kutatua migogoro mingi, hivi tatizo liko wapi? Kwa nini wapimaji wale hawajaweza kuweka *beacons* kwenye mpaka huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa kwenda mbele zaidi, lakini niamini kabisa, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, wananchi wa Wilaya za Kiteto na Kilindi wana imani kubwa sana na Wizara yake, wana imani kubwa na utendaji wake Mheshimiwa Lukuvi. Mimi nimwombe, pale ambapo pamebaki sasa hivi ahakikishe kwamba wapimaji wanaweka mipaka ile ili shughuli za kilimo na ufugaji ziweze kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii nmkwambie, toka wamepita pale, toka Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuja pale wananchi wamekaa kimya wananiuliza Mbunge wao, Mheshimiwa Mbunge tatizo liko wapi, mbona hawa wapimaji wameondoka? Nimwombe Mheshimiwa Waziri, suluhu ya kudumu ni kuweka alama za *beacons* na kufuata maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kwamba *GN* namba 65 ya mwaka 1961 inayogawa Mikoa ya Tanga na Arusha ndiyo alama sahihi, ndiyo *GN* sahihi na mimi nina imani kwamba na wewe utayasimamia hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo machache, nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kigua. Mheshimiwa Abdallah Bulembo.

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami nijielekeze, kama wengine wote walivyosema, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu kwa kazi kubwa wanayoifanya. Wana haki ya kupewa hongera kwa sababu kazi wanafanya na nchi inajua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina mengi sana lakini nina hoja kama tatu. Hoja yangu ya kwanza ni juu ya *National Housing; National Housing* kwa sheria iliyoiunda kwa miaka hiyo mingi iliyopita iliundwa kwa sababu kubwa, watu wa hali ya chini waweze kupata makazi ambayo bei yake ni nafuu. Hata hivyo inawezekana kwa sababu limekuwepo la

muda mrefu tunawapongeza leo wanajenga nyumba nyingi zenye nafasi nyingi lakini zenye uwezo wa watu wakubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijana anayetoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam akaajiriwa kazi mahali fulani hana uwezo wa kupanga nyumba ya *National Housing*, ingawaje pamoja na kwamba msingi wake ulikuwa ni kutoa unafuu kwa wale wanaoanza maisha, wenye kipato cha chini. Ombi langu Mheshimiwa Waziri chini ya *National Housing*, hebu wafanye mara mbili basi, wajenge nyumba zenye uwezo wa watu wa vipato vya juu lakini wajenge nyumba zenye uwezo wa watu wa vipato vya chini. Kwa sababu Watanzania hawa wa vipato vya chini bado wanaishi mijini. Mfano mdogo Dodoma hapa, *TBA* ni Idara ya Serikali, *National Housing* ni idara ya Serikali, ukienda *TBA* nyumba yake, kwa Dodoma, Sh.150,000/= mpaka Sh.250,000/=. Ukienda *National Housing* pale Medeli, Sh.500,000/= mpaka Sh.600,000/=: ni walewale tu, na wote ni Mji huo huo wa Dodoma. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ombi langu kwa *National Housing*, sitaki kuharibu kazi yao kubwa na nzuri wanayoifanya, lakini sisi wanyonge tunakwenda wapi mjini, tutapanga wapi, tunawekwa wapi? Mheshimiwa Waziri hilo anaweza kulifanya, wala halitaki maelezo marefu. Akiamua kufanya... (Makofi)

## TAARIFA

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa mzee wangu, Mheshimiwa Alhaji Bulembo, kwamba nimeona kabisa nia yake njema kabisa ya kutaka wananchi wenye hali ya chini waweze kupata nyumba zenye gharama nafuu. Hata hivyo, akumbuke kabisa kwamba wana wakati mgumu sana wanapojenga nyumba hizi. Wakati mkandarasi anakwenda kuagiza vifaa nje kwa ajili ya kuhakikisha kwamba anajenga nyumba zenye gharama nafuu anatozwa

VAT, lakini pia wakati mkandarasi analipwa fedha pia anadaiwa VAT. Kwa maana hiyo, inashindikana sasa kwamba wangeweza kujenga nyumba zenye gharama nafuu na ndiyo maana nyumba zinakuwa na gharama ya hali ya juu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Alhaji Bulembo aendelee kumshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuhakikisha kwamba masharti mengine ambayo yanapelekwa kwenye taasisi hizo zinazosababisha wajenge nyumba za gharama kubwa yaweze kuondolewa ili Watanzania waweze kupata nyumba zenye gharama nafuu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Huo ni ushauri au taarifa? Mheshimiwa Alhaji Bulembo, unapokea hiyo taarifa?

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei taarifa. Ngoja nimpe faida tu. TBA ni shirika ambalo lipo chini ya hao na *National Housing*. Hebu nenda pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam uone yale majengo ya kulala wanafunzi, amejenga TBA, kwani yeye hakununua saruji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba *National Housing*, basi taarifa yake kama inalenga kule, Mheshimiwa Waziri, pale Dar es Salaam tuna nyumba Upanga, Tabora zipo, Bukoba zipo, tulizorithi mwaka 1967, hazina ukarabati zinaongezekaje bei? Kwa nini? Kwa sababu iko wazi kabisa, zipo nyumba za asili zilizoanzishwa *National Housing* hata ukarabati haufanyiki ingawaje wanazikopea kujenga nyumba nyingine. Kwenye ile mikopo wanayokopa si warudishe na huku ndani basi nyumba angalau ziwe nzuri na wote tunaoshi mjini tunazijua. Kwa hiyo, bado natetea hoja yangu; tunavyosihaji mjini bado kuna watu uwezo wa kupanga ni wa shida lakini wana haki ya kukaa kwenye nyumba za Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili; huyu amenitoa kwenye *mood*; suala la kibenki. Mheshimiwa Waziri, mtu yeyote anapokwenda kukopa benki kwa kawaida lazima apeleke hati benki na anapokwenda kukopa benki, kama ni mke na mume watasaini wanakubali mkopo. Wakishamaliza kukopa, Wizara ya Ardhi inasajili ile hati kwamba hii hati iko benki kwa sababu ya mkopo; tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anashindwa kulipa mkopo wa benki, nyumba inaenda mnadani, watu wanakimbilia mahakamani. Tatizo langu linaponipata, wanatoka tena mahakamani wanakwenda kuweka *caveat* kwenye nyumba ambayo walienda kukopa, benki imeuza, inakuwaje sasa? Kwani ile hati huwa inakwenda pale Ardhi mnahalalisha kwamba ana haki ya kukopa kwa nini? Nyumba ina mkopo, inawezaje tena kwenda kuwekewa *caveat*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili linasumbua benki zisikopeshe watu wanaofanya biashara kwa sababu sasa wanakuwa hawaaminiki. Maana unakopa, kurudisha umeshindwa, mali yako inauzwa unakwenda kuzuia isiuzwe mahakamani, unakwenda kuzuia ardhi na ardhi mnapokea, lakini picha zipo, kila kitu kipo. Kwa nini sasa ardhi hii badala ya kuwalinda benki kama wafanyabiashara inawaingiza kwenye matatizo kwa kutoa hati ya kwanza ya akope na hati ya pili mtu akaweke *caveat*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la tatu, Mheshimiwa Lukuvi, tunaposema kupima, halmashauri zinapima lakini asilimia 30 hairudi kwenye halmashauri hizi. Wakishakusanya ile kodi wawarudishie, kwa sababu wakiwarudishia ile kodi watawapa msingi wa kuendelea kupima ili viwanja viwe vingi. Halmashauri inapima, pesa inalipwa ila asilimia 30 hairudi, sasa hii halmashauri wanaisaidiaje na tunasema tupime maeneo mengi? Wakati mwingine sehemu nyingine hela ya miradi inapatikana, lakini tunazo halmashauri za vijijini ambazo uwezekano wa ku-*expand* kuendelea kupima, hela ile isiporudi hawawezi kupima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo hoja yangu na ushauri wangu katika Wizara hii, kazi kubwa wanafanya, wala haitakiwi kutiwa doa, lakini wawaarudishie hizi halmashauri ili ile asilimia 30 iweze kuwapa nguvu ya kuendelea kupima katika maeneo yao. Nina uhakika suala hili nina imani ataamua, siyo akiamua, anaweza tu, hata akisema kwenye majibu yake kesho watatekeleza tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, niligusia hilo walilosema wengi. Ni kweli tusipokuwa na sababu za kuwa na maeneo maalum ya kilimo na yakalindwa na yakatunzwa yasibadilishwe matumizi, kizazi kinachokuja kulima itakuwa shida sana. Itakuwa shida kwa nini, kama kuna mtu anataka kujenga nyumba si aende maeneo kavu kule ajenge? Hata hivyo, sehemu hii ina maji inaweza kumwagiliwa. Mheshimiwa Waziri, kama walivyosema wengi, hebu aangalie eneo la kisheria fulani. *Otherwise*, kwa sababu hali ya tabianchi inabadilika, mambo yanabadilika, tutakuja kujikuta sehemu ya kulima sasa kwenye mito na nini haipo, watu wamejenga kwa sababu wana hela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie hapo kwa kuunga mkono hoja, nawapongeza kwa kazi kubwa wanayoifanya. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bulembo. Tunaendelea na Mheshimiwa Hasunga na baadaye tutaendelea na Mheshimiwa Ulega na Mheshimiwa Martin Msuha kwa dakika tano tano.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba niungane na wenzangu kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika Wizara hii, kwa kweli hongereni sana. Pia nimpongeze Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania kwa kazi anayoifanya ambayo tunaiona, nampongeza sana na sisi sote tuko nyuma yake, tutaendelea kumuunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze kuzungumzia juu ya upimaji wa ardhi. Katika kupima ardhi, ardhi ndiyo mtaji pekee ambao kila mwananchi wa Tanzania, walio wengi, wanaweza kuwa nao. Ardhi ndicho kitu pekee kinachoweza kutukomboza iwe ni wakulima, wajasiriamali, wanawake au vijana, wote tuna kipande cha ardhi. Pamoja na kazi nzuri abayo Mheshimiwa Waziri amekuwa akiifanya, pamoja na kushusha kodi ya *premium* kutoka asilimia saba kwenda asilimia mbili; ni kazi nzuri, hongereni; lakini hebu tuangalie bajeti ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu tulionao, bajeti ya maendeleo ambayo imekwenda ni asilimia 30 tu, fedha zilizopatikana ni asilimia 30 tu. Hebu tuangalie malengo waliyokuwa nayo. Katika mwaka huu walipanga kwamba wangetoa hatimiliki 400,000, lakini zilizotolewa mpaka tarehe 15, mwezi Mei mwaka huu ni 33,979, sawa na asilimia nane tu ya lengo la mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakuwa na wasiwasi, malengo ni mazuri, nia ni nzuri, tunataka wawekezaji waje hapa kufanya biashara waje kuwekeza, wanawekezaje kwenye ardhi ambayo haijapimwa? Tunainuaje hiyo, tunawasaidiaje wananchi hawa ili waweze kufanya kazi yao vizuri? Hao wawekezaji wakija wanataka kujenga viwanda, ardhi haijapimwa. Nadhani lazima tuwaunge mkono fedha ziende ili wapime, malengo yao yafikie, kinyume cha hapo hatutafika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeangalia miji yetu ilivyo, miji imekuwa ikikua kiholela, nyumba zimekuwa zinajengwa bila mipangilio. Kule Jimboni kwangu Vwawa, Mji wa Vwawa, kuna maeneo yamepangiliwa, kuna maeneo hayajapangiliwa kabisa, maeneo mengi ni *squatters*, ukienda miji mingi maeneo mengi bado ni *squatters*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kupima hayo maeneo tutaendelea kutumia gharama kubwa katika kuendesha nchi hii kwa sababu hata kuwafikia kwenda kutoa huduma hakupo. Sehemu tunazotaka kwenda kujenga huduma za afya, huduma za miundombinu mbalimbali tunashindwa kwa sababu maeneo hayajapimwa. Sasa kasi ya maendeleo ya wananchi ni kubwa ukilinganisha na kasi ya Serikali ya kupima ardhi. Naomba, kama kuna sehemu ya kuwekeza zaidi hili ndilo eneo la kuwekeza, hapo tutakuwa tumepiga dili zuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwekeza kwenye ardhi uka-*plan*, ukaipangilia vizuri, migogoro itapungua, yote itapungua. Nyumba zitakuwa nzuri, kodi zitaongezeka, makusanyo yatakuwa ni mazuri, hata nchi nyingi zinategemea makusanyo ya kodi za nyumba, kodi za viwanja. Sasa kama tusipoipa uzito, tutashindwa. Naomba hilo lipewe uzito unaostahili ili nchi yetu iweze kwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda Mheshimiwa Waziri anipe majibu; pamoja na kazi nzuri aliyoifanya, mimi ni mdau kule Kigamboni, kule Kigamboni alitangaza Mheshimiwa Waziri, alipoingia tu madarakani; akasema ndani ya mwezi mmoja watapata hati, sasa naona amepewa hela kidogo hati hazijatolewa Kigamboni. Mpaka leo wananchi hawana hati, leo hii bado tunahangaika, tunajuliza ule mji, ile *satellite* ipo au haipo na ile ramani Mheshimiwa Waziri ilikuwa nzuri hata mimi mwenyewe niliipenda lakini iko wapi? Hati wananchi hawana, mpaka sasa hivi tunashindwa hata tufanye nini. Naomba, hebu akalifanyie kazi tupate hati, twende kukopa ili tuweze kuwekeza katika maeneo mengine tuinue uchumi wa nchi hii. Mheshimiwa Waziri, nafikiri hilo ni la msingi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu ambayo napenda kuchangia ni kuhusu Shirika la Nyumba. Shirika hili ni kweli linafanya kazi nzuri, limejitahidi sana kuwekeza, limejitahidi sana kujenga nyumba na kuna changamoto kadhaa wanazo. Hata hivyo, nawaomba Shirika la Nyumba,





Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vifaa alivyosema Mheshimiwa Waziri vya kupima ardhi, vile alivyosema atavinunua, najua atakuwa labda hajanunua kwa sababu ya bajeti ndogo, hebu waharakishe vinunuliwe hivyo, vigawiwe kwenye halmashauri zetu vikafanye kazi ya kupima na sisi tutasaidia kusimamia kule ili kazi iwe nzuri, nadhani maendeleo yatapatikana katika nchi hii na kila kitu kitawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sipendi kupoteza muda mwingi, naomba kuunga mkono hoja na naomba kuwapongeza kwa kazi nzuri. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Hasunga. Mheshimiwa Ulega dakika tano.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nachukua fursa hii kukushukuru sana kwa nafasi hii niliyoipata. Pia naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mabula, Katibu Mkuu na Makamishna wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee kabisa, nimpongeze sana rafiki yangu Kamishna Mathew wa pale Dar es Salaam kwa kazi kubwa anayoifanya, halali usingizi, ni kwa sababu ya kuhakikisha migogoro inakwisha Dar es Salaam. Kamishna wangu wa Kanda ya Mashariki, kwa kweli amenisaidia sana katika mgogoro wa vijiji vinne vya Mlamleni, Luzando, Mwanambaya na Mipeko. Amefanya kazi kubwa na natumai kazi hii ataimalizia vizuri hapo mbele. Vile vile, kwa namna ya kipekee, nitambue kazi nzuri anayoifanya Kamishna wetu wa Kanda ya Kusini, kaka yangu Luanda, wote Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichukue fursa hii kurudia tena kusema kwamba kazi hii kubwa wanayoifanya, Mheshimiwa Waziri, tunalo sisi la kujifunza. Kwa sababu Waswahili wanasema, ukiona vyaelea ujue vimeundwa, Mheshimiwa Waziri Lukuvi, kwake yeye kwa kazi

kubwa anayoifanya na Wabunge wote humu tunamsifu, ni kwa sababu tunakwenda kila mahali, tunatatua migogoro na tunafanya vema sana. Hata kwangu Mkuranga migogoro niliyoitaja na mingine ambayo sikuitaja ameifanyia kazi kubwa sana. Namshukuru sana na Mwenyezi Mungu ambariki sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo tatizo katika Kijiji cha Dundani na hili ni tatizo la maeneo mengi linalohusu fidia. Wananchi wanazuiwa kwa ajili ya uendelezaji wa ardhi zile kwa ajili ya uwekezaji, ni jambo jema. Tunapenda uwekezaji, lakini sasa inapofika mahali watu wanasubiri jambo kwa muda mrefu sana inafika miaka mitatu, minne, mitano, maeneo yao yanageuka kuwa mapori, hawawezi kuendeleza chochote katika maeneo yale. Hili linakuwa ni tatizo na linawakatisha tamaa sana wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri, yeye ni *champion*, atusaidie tutoke mahali pa namna hii. Wananchi wanaozuiwa kuendeleza maeneo yao kwa muda mrefu na yanageuka kuwa ni mapori, hawawezi kuvuna nazi zao, hawawezi kulima mihogo pale, hawawezi kufanya maendeleo ya namna yoyote, tuwasaidie. Kama tumeshindwa tutafute namna ya kukaa nao na tuwarejeshee maeneo yao waweze kuendelea na maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nataka nitoe ushauri ni eneo la upimaji na uendelezaji wa ardhi. Hili eneo lina *potentiality* kubwa sana, wazo langu ni kwamba, kwanza nawapongeza sana Wizara, wamekubali kuchukua taasisi na makampuni binafsi kuweza kushiriki katika kazi hizi na hili ni jambo jema, ni lazima tubiasharishe mawazo yetu. Hata hivyo, hapa bado liko tatizo, Wizara ya Ardhi mshirikiane vema hasa na wenzetu wa TAMISEMI, uendelevu wa ardhi kwa kutumia kampuni binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanachukua pesa zao lakini mlolongo unachukua muda mrefu sana, hasa mtu akiwa amekopa pesa yake benki kuweza kufanya marejesho haiwezi kuwa kazi nyepesi tena. Kutoka kununua ardhi

mpaka kufika kuipima, mpaka kufika kuisaidia Serikali kuwauzia wananchi ili sasa papatikane ardhi iliyoendelezwa, inachukua kipindi kirefu sana. Matokeo yake inawakatisha tamaa, Mheshimiwa Waziri aMheshimiwa Mwenyekiti, amefanya kazi nzuri ya kuweka bei elekezi, maana sasa ardhi ilikuwa inafanya *inflation*, kila mtu anajipangia anavyoweza tu, sasa tume-*control* hilo jambo, ni jambo jema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, lazima tuwe na ushirikiano ili hii kazi ya kuipima ardhi yetu ya Tanzania kwa kutumia taasisi binafsi iweze kuwa yenye kuvutia, kazi hii ya kupima Mheshimiwa Waziri peke yake hataweza, tutarudia hapa mwaka hadi mwaka hata miaka mia moja, hatutaweza, ndiyo ile nasema lazima tubiasharishe mawazo yetu. Wizara ya Ardhi na Wizara ya TAMISEMI tushirikiane, milolongo, *bureaucracy* zimekuwa nyingi sana. Ushauri wangu ni huo kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu ya leo na kwa vile muda umemalizika na wamebaki watu watatu hapa, nitaomba hawa wamalizie kesho asubuhi; Mheshimiwa Martin Msuha, Mheshimiwa Yussuf na Mheshimiwa Millya.

Baada ya kusema hayo, kwa vile muda wetu umemalizika kwa siku ya leo, niwatakie kila la heri na jioni njema. Naahirisha Bunge hadi kesho, saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.45 Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 26, Mei, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*